

**BUNGELATANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Ishirini na Mbili – Tarehe 5 Mei, 2020**

*(Bunge lilianza Saa Nane Mchana)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri hiyo Barakoa kiboko kabisa hiyo, umependeza sana. Nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa niaba yake Mheshimiwa Musa Ntimizi.

**MHE. MUSA R. NTIMIZI (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA):**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nimwite Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya Viwanda na Biashara. Hayupo.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

*(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya Mtandao)*

Na. 202

**Kuboresha Miundombinu ya Jiji la Dodoma**

**MHE. RUKIA AHMED KASSIM** aliuliza:-

Kwakuwa Jiji la Dodoma ndio Makao Makuu ya Serikali:

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha miundombinu na shughuli za kijamii katika Jiji la Dodoma kwa miaka mitano ijayo (2020- 2025)?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala yake ya Barabara za Vijijini na Mijini (*TARURA*) imeendelea kuboresha miundombinu ya barabara za Vijijini na Mijini katika Jiji la Dodoma ili kuboresha shughuli za usafirishaji kwa kufanya matengenezo, ukarabati na usanifu wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika kipindi cha miaka mitano 2020 - 2025, Serikali imepanga kufanya yafuatayo ili kuboresha huduma za kijamii katika Jiji la Dodoma; kuunganisha mitaa ya jiji kwa barabara za lami zenye urefu wa kilometa 162.24, kujenga barabara ya mzunguko (*outer ring road*) kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilometa 109, kujenga uwanja mkubwa na wa kisasa wa ndege eneo la Msalato, kujenga bandari kavu eneo la lhumwa, kujenga Hospitali ya Uhuru, Kuipanua Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, kuendelea kutoa huduma za kibingwa katika Hospitali ya Benjamin Mkapa.

Na. 203

**Barabara ya Lokisale - Meserani**

**MHE. JULIUS K. LAIZER** aliuliza:-

Barabara ya Lokisale – Meserani imekuwa kero kwa Wananchi hasa nyakati za mvua:-

(a) Je ni lini Serikali itatenga fedha za kutosha kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha Changarawe?

(b) Je, Serikali ipo tayari kutoa fedha za dharura ili kusaidia matengenezo ya barabara hii iweze kupitika?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI** alijibu-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, Mbunge wa Monduli lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Barabara ya Lokisale - Meserani yenye urefu wa kilometa 52 imetengewa kiasi cha Shilingi 277,280,000.00 kwa ajili ya kufanya matengenezo ya kawaida (*maintenance works*) na matengenezo ya sehemu korofi (*spot improvement*).

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetoa kiasi cha Shilingi milioni 122 kwa ajili ya kurejesha miundombinu iliyoharibiwa na mvua kubwa za masika. Matengenezo hayo yanaendelea.

Na. 204

**Barabara ya Wino – Ifinga Wilaya ya Madaba**

**MHE.JOSEPH K. MHAGAMA** aliuliza:-

Barabara ya Wino–Ifinga katika Halmashauri ya Wilaya ya Madaba yenye urefu wa kilometa 48 imeshindwa kutengenezwa kwa miaka mingi kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Halmashauri na Sasa *TARURA*; jitihada za kupata fedha kupitia vyanzo vingine vya Serikali ikiwemo *TANROADS* zimeshindwa kuzaa matunda hadi sasa:-

Je, ni lini Serikali itasikia kilio cha wananchi wa maeneo hayo kwa kutenga fedha za kutengeneza barabara hii muhimu kwao kiuchumi na kijamii?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Kizito, Mbunge wa Madaba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuifanyia matengenezo barabara ya Wino – Ifinga ambapo katika mwaka wa fedha 2019/2020 barabara hiyo imetengewa kiasi cha shilingi milioni 288 kwa ajili ya matengenezo ya muda maalum (*periodic maintenance*) kipande cha kilometa 15. Tayari mkandarasi ameshapatikana na anasubiri mvua zipungue ili aanze matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mwaka wa fedha 2020/2021, kiasi cha shilingi 300,000,000.00 kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Wino – Ifinga – Luhuji kipande chenye urefu wa kilometa 10 kwa kiwango cha changarawe. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

Na. 205

### **Ahadi ya Umeme–Manyoni Magharibi**

**MHE.YAHAYA O. MASSARE** aliuliza:-

Waziri wa Nishati alipotembelea Jimbo la Manyoni Magharibi aliahidi kuwa Vijiji vyote 16 ambavyo havijaunganishwa na umeme vitaunganishwa kabla ya mwezi Desemba, 2019 lakini hadi leo havijaunganishwa:-

Je, ni lini vijiji hivyo vitaunganishwa ili kutekeleza ahadi hiyo?.

**WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa, Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) na Shirika la Umeme Nchini (*TANESCO*) inaendelea na utekelezaji wa miradi ya kupeleka umeme vijijini nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za mradi katika Wilaya ya Manyoni hususan Jimbo la Manyoni Magharibi inajumuisha kupeleka umeme katika vijiji vyote vilivyobaki vikiwemo vijiji 16 vya Aghondi, Mabonden, Muhanga, Ipande, Damwelu, Ipalalyu, Mitundu, Kitaraka, Kazikazi, Kihanju, Tambukareli, Kalangali, Tulieni, Mnazi Mmoja, Mbugani, Idodyandole, Kintanula, Mwamagembe na Rungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hiyo inajumuisha pia ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 237.8, ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilomita 32, pamoja na ufungaji wa transfoma 16 za KVA 50 na 100 na kuwaunganishia huduma ya umeme wateja wa awali 1,600. Gharama za mradi ni shilingi bilioni 3.6. Kazi za mradi zitakamilika mwezi Juni, 2021.

Na. 206

### **Mgogoro wa Ardhi Kijiji cha Ruhembe**

**MHE. JOSEPH L. HAULE** aliuliza:-

Kumekuwa na mgogoro mkubwa wa siku nyingi wa ardhi ya takribani heka 375 kati ya wananchi wa Kijiji cha Ruhembe na wakulima wakubwa waliopora eneo hilo:-

Je, Serikali itawasaidiaje wananchi hao wanyonge ili wapate haki yao ya ardhi ya kulima waliyoporwa?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Leonard Haule, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, shamba lenye ekari 375 ambalo linamilikiwa na Serikali ya Kijiji cha Ruhembe Kidodi, kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi, Na. 5 ya Mwaka 1999 na

Kanuni zake za Mwaka 2001. Sheria hii imezipa Serikali za Vijiji mamlaka ya kusimamia na kutawala ardhi ya kijiji iliyoko ndani ya mipaka ya kijiji kilichosajiliwa. Serikali inaheshimu maamuzi yaliyotolewa na Kijiji cha Ruhembe kugawa ardhi yenye ekari 375 kwa wananchi kwa makubaliano maalumu ya kutumia ardhi hiyo kwa kilimo lakini itaendelea kumilikiwa na Serikali ya Kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe rai kwa wananchi waliopanda miwa kwenye maeneo hayo kwa makubaliano na kijiji waheshimu makubaliano yao kwa kuchangia katika huduma za jamii pamoja na huduma za kijiji kama ilivyokubalika na mikutano mikuu ya vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto ya ardhi inayowakabili wananchi wa Kijiji cha Ruhembe, Kidodi na Kilosa kwa ujumla. Katika kupatia ufumbuzi suala hili mwaka 1997 Serikali ilitwaa shamba Na. 126 Ruhembe lenye ukubwa wa ekari 3039 na kuligawa kwa wananchi. Serikali inaandaa utaratibu wa wananchi waliogawiwa ardhi ili waweze kuchangia kama sehemu ya gharama kulipia thamani ya shamba hilo ili waendeleo kumiliki ardhi husika na kupunguza uhaba wa ardhi.

Na. 207

### **Barabara ya John Corner – Mtili – Mgololo**

**MHE. MOHMOUD H. MGIMWA** aliuliza:-

Barabara ya Johns Corner – Mtili Mgololo ni barabara muhimu sana kwa uchumi wa Wilaya ya Mufindi na Taifa kwa ujumla na inafanyiwa matengenezo kwa kiwango cha changarawe kila mwaka:-

Je, ni lini Serikali itaijenga kwa kiwango cha lami barabara hii?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mгимwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya *Johns Cornes* – Mtili – Mgololo inajulikana kama barabara ya Mafinga – Mgololo na inasimamiwa na Wakala wa Barabara ya Tanzania (*TANROADS*) Mkoa wa Iringa. Barabara hii ni barabara kuu yenye urefu wa kilometa 81.14. Kati ya kilometa hizo, kilometa 13.59 ni za lami na kilometa 67.55 ni za changarawe. Barabara hii inaunganisha Makao Makuu ya Wilaya ya Mufindi na Kiwanda cha karatasi cha Mgololo na inapita katika maeneo muhimu yenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya misitu, chakula na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia Wakaa wa Barabara (*TANROADS*) inaendelea na kazi ya ujenzi yakinifu, usanifu wa kina na kuandaa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Kazi hii inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Mei, 2020 na Serikali kuanza kutafuta fedha za ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi hizi za Serikali ya Awamu ya Tano, katika mwaka wa fedha 2019/2020, barabara hii imetengewa jumla ya shilingi milioni 350,228,000.00 kwa ajili ya kuifanyia matengenezo mbalimbali yakiwemo; matengenezo ya kawaida matengenezo ya muda maalum, matengenezo ya sehemu korofi pamoja na madaraja saba yaliyoko katika barabara hii.

Na. 208

**Uwanja wa Ndege - Njombe Kuwa Kero kwa Wananchi**

**MHE. LUCIA M. MLOWE** aliuliza:-



Uwanja wa Ndege wa Njombe umejengwa karibu sana na makazi ya wananchi na hivyo kusababisha kero kubwa kwa wananchi ambao hutozwa fedha nyingi kwa kukatiza katika uwanja huo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamisha uwanja huo katika eneo lingine katika Mkoa wa Njombe na eneo la uwanja wa sasa kutumika kwa matumizi mengine?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**  
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, Mbunge viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanja cha Ndege cha Njombe kama ilivyo kwa viwanja vingi vya ndege nchini ilijengwa na Wakoloni kabla ya uhuru mnano miaka ya 1940 na kuanza kutumika mwaka 1945. Aidha, kwa mujibu wa Sheria za Kimataifa za Usalama wa Anga hairuhusiwi kumbe au chombo chochote (watu, magari, wanyama na kadhalika) kukatiza kwenye viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na makazi ya watu kuendelea kusogelea eneo la kiwanja mwaka hadi mwaka tangu kujengwa kwake na kukosekana kwa uzio wa usalama, kumesababisha watu kukatiza katikati ya kiwanja kinyume cha sheria. Ili kuzuia uhalifu huu, hatua kali ikiwa ni pamoja na kutozwa faini zinachukuliwa kwa watu wanaokamatwa wakikatiza kiwanja hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za kuepusha athari hizo, Serikali ilikijumuisha kiwanja hiki katika upembuzi yakinifu na usanifu wa kina uliofanywa na kukamilika mwaka 2017 kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia uliohusisha pia viwanja vya ndege vingine kumi ili kukikarabati kiwanja cha ndege cha Njombe ikiwa ni pamoja na kujenga uzio wa kuzunguka kiwanja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Njombe ni kukiwezesha kukidhi mahitaji ya kiwanja cha mkoa kitakachoweza kupokea ndege za daraja la kati zenye viwango vinavyolingana na vya *Bombardier Q400*. Kazi zitakazohusika katika ukarabari na upanuzi wa kiwanja ni ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege, barabara ya kiungo na maegesho ya ndege kwa kiwango cha lami na ujenzi wa jengo jipya la abiria, Kituo cha Zimamoto, ujenzi wa barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani pamoja na maegesho ya magari na ujenzi wa uzio kuzunguka eneo la kiwanja ambao utasaidia kuzuia wananchi, kiumbe au chombo chochote kukatiza hovy katika eneo la kiwanja hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Serikali inatafuta fedha ili kukarabati kiwanja hiki kwa viwango vinavyokubalika Kimataifa na hivyo Serikali haina mpango wa kukihamisha kiwanja hiki kutoka eneo kilipo kwa vile baada ya kukamilika kwa ukarabati wa kiwanja hiki athari zilizoainishwa na Mheshimiwa Mbunge hazitakuwepo tena.

Na. 209

### **Kuwasaidia Wavuvi Zana za Kisasa – Ziwa Tanganyika**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO** aliuliza:-

Ziwa Tanganyika lina kina kirefu sana. Wavuvi wadogo wanashindwa kuvua mazao ya ziwa kwa kukosa zana za kisasa za uvuvi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wavuvi hao kwa kuwapatia zana za kisasa?

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Suleimani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetoa kipaumbele kwa Sekta ya Uvuvi ili iweze kuwapatia wananchi wake ajira, lise, kipato na kuchangia katika pato la Taifa kwa kuweka mazingira mazuri kwa wavuvi kupata mikopo ya masharti na riba nafuu kutoka katika Benki ya Maendeleo ya Kilimo na kupitia dirisha la Kilimo katika Benki ya Rasilimali (*TIB*). Aidha, Wizara kupitia Dawati la Sekta Binafsi imeviunganisha vyama vya ushirika vya wavuvi na taasisi za fedha ambapo mikopo iliyooombwa na kupitishwa (*Approved*) ni shilingi bilioni 2.6 na mikopo iliyotolewa ni shilingi milioni 323.8. Pia, Wizara imehamasisha Benki ya Posta (*Tanzania Postal Bank - TPB*) kuzindua Akaunti ya Wavuvi (*Wavuvi Account*) kwa ajili ya mikopo na bima mahususi kwa wavuvi hususan wavuvi wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Serikali imefuta Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) kwenye injini za kupachika, nyuzi za kushonea nyavu, nyavu za uvuvi na vifungashio kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2011 na Sheria ya Mamlaka ya Mapato (*VAT Act*) ya Mwaka 2014 ili kuwasaidia wavuvi kupata zana za uvuvi kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wavuvi kufanya uvuvi wenye tija na kuwahimiza wavuvi kujunga katika vikundi na kuanzisha vyama vya ushirika vya msingi, Vyama vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*) na *VICOBA* ili waweze kukopesheka kwa urahisi na Taasisi za fedha na hivyo kujikwamua kiuchumi. Aidha, Serikali inahamasisha Sekta binafsi kujenga viwanda vya kutengeneza boti na zana bora za uvuvi ili kuwezesha wavuvi kuzipata kwa bei nafuu na kwa urahisi.

Na. 210

### **Ujenzi wa Ofisi na Nyumba za Mwakili Nchini**

**MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza:-

Mwakili wa Serikali ambao ni *State Attorney* wapo karibu kila Mkoa nchini lakini sehemu nyingi wamepanga Ofisi

na pia Watumishi hao hawana nyumba za kuishi, wanapanga uraiiani:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga Ofisi za Mwakili wa Serikali kwenye Mikoa yote ya Tanzania?

(b) Je, ni lini Serikali itajenga nyumba za kwisha Mwakili wa Serikali kwenye Mikoa yote Nchini?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Mwakili wa Serikali (*State Attorneys*) wapo karibu kila Mkoa na wanatekeleza majukumu yao chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Mashitaka, baada ya maboresho ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia Hati Idhini Tangazo la Serikali Namba 48, 49 na 50 ya tarehe 13 Februari, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ufinyu wa Bajeti hasa fedha za maendeleo zinazotengwa kwa ajili ya ofisi hizi tatu kumekuwa na changamoto ya kuwa na majengo ya ofisi hizi, hivyo kulazimika kutumia majengo ya taasisi nyingine za Umma au kupanga katika majengo ya watu binafsi. Hata hivyo, jitihada zinaendelea kufanyika ili kuhakikisha kwamba Ofisi zinajengwa kwa awamu katika Mikoa yote kulingana na uwezo wa kibajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa lengo la Serikali ni kuhakikisha inaboresha utendaji kazi wa watumishi wake. Hivyo, pale uwezo wa kibajeti utakapopatikana ujenzi wa nyumba za Mwakili wa Serikali utafanyika kwa awamu ili kutatua changamoto kwa Mwakili hao kupanga nyumba uraiiani. Kwa kufanya hivyo, itasaidia kuboresha utendaji kazi wa Mwakili wa Serikali kwa kiwango kikubwa.

Na. 211

**Mahakama Kutumia Madalali Kuuza Mali za  
Watu Wenye Migogoro**

**MHE. MARIAM K. NASSORO** aliuliza:-

Mahakama zimekuwa zikitumia madalali kuuza au kudai mali za watu walio na mgogoro; Mara nyingi madalali hao hutumia watu wenye nguvu wasiokuwa wastaarabu kuvamia na kuvunja nyumba au kuuza vitu vya watu bila kufuata utaratibu hali inayosababisha wanawake kukosa haki zao:-

(a) Je, Serikali inatoa kauli gani kwa madalali wasiofuata utaratibu?

(b) Je, Serikali inasaidiaje wanawake wanaopeleka mapingamizi Mahakamani ili yasikilizwe kwa haraka ili kuepuka kudhulumiwa haki zao?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Kisangi Nassoro, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uteuzi wa Madalali wa Mahakama hufanyika kwa mujibu wa Kanuni na Tangazo la Serikali (GN) NO. 363 ya 2017 ambalo limeainisha sifa za mtu anayefaa kuteuliwa kuwa Dalali wa Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madalali wanaoteuliwa hutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Kanuni za madalali na endapo atakiuka masharti hayo atakuwa ametenda kosa litakalopelekea moja ya hatua zifuatazo kuchukuliwa; kupewa onyo, kusimamishwa kufanya shughuli za udalali kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja au kufutwa udalali kwa mujibu wa kanuni ya 18 ya GN NO 363/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo dalali yeyote atakiuka utaratibu wa kukamata mali ambayo haikuainishwa katika hati ya ukamataji atakuwa amekiuka utaratibu uliotajwa kwenye Kanuni, hivyo kupelekea kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa Kanuni hizo; na ikithibitika mali husika imekamatwa au kuuzwa kimakosa, mali hiyo itarejeshwa kwa mhusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama kama chombo cha Haki, inapotokea wanawake wanaleta mapingamizi, Mahakama imekuwa ikiangalia mashauri yao sawa na mashauri mengine kwa kuzingatia misingi ya sheria na usawa. Hata hivyo, kwa mashauri yote ambayo yanahitaji kipaumbele cha pekee, Mahakama imekuwa ikiyasikiliza na kuyatolea maamuzi haraka.

**NAIBU SPIKA:** Katibu!

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

#### **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 - Wizara ya Viwanda na Biashara**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimwite Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa ambaye pia leo ni siku yake ya kuzaliwa. *(Kicheko/Makofi)*

Hongera sana Mheshimiwa, nimeambiwa na Mheshimiwa na Mheshimiwa Silafu Maufi pia ni siku yake ya kuzaliwa. *(Makofi)*

Karibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Utangulizi; kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ambayo

ilichambua bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara Fungu 44 na Fungu 60 tarehe 24 na 25 Machi, 2020 Jijini Dodoma, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mipango na Bajeti kwa Mwaka 2019/2020. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hotuba yangu yote iliyowasilishwa kwa Waheshimiwa Wabunge iweze kuingia katika Kumbukumbu za Bunge (*Hansard*) kama ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na baraka katika majukumu niliyokasimiwa. Kwa namna ya pekee namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuiteua kuwa Waziri na kunipa majukumu yanayobeba ajenda kuu ya Serikali ya Awamu ya Tano ya Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda. Nampongeza kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya SADC na namna anavyoshughulikia masuala ya biashara katika nchi za SADC na EAC ikiwa ni pamoja na kuomba kufutiwa madeni kwa nchi za Afrika katika kipindi hiki cha mlipuko wa ugonjwa wa *covid 19*. Nampongeza pia kwa namna anavyotuongoza kwa ujasiri na misingi imara yenye kusheheni uzalendo na mapenzi kwa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Ally Mohammed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi wanavyomsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia ipasavyo misingi ya utafu wetu, kupunguza pengo la walio nacho na wasio nacho, kujenga Tanzania yenye kutua fursa za uhakika za kujiletea maendeleo kwa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Spika kwa umakini wenu katika kuliongoza na kulisimamia Bunge letu. Pia, naipongeza na kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Viwanda, Biashara na Mazingira chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Suleiman Sadiq, Mbunge wa Jimbo la Mvomero, Makamu wake Mheshimiwa Kanali Mstaafu Masoud, Mbunge wa Jimbo la Mfenesini na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati wote. Ushauri na maelekezo yao yamekuwa chachu muhimu sana katika mageuzi ya kifikra na kiutendaji ya Wizara na hivyo kuchochea kasi ya maendeleo ya viwanda na biashara nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee niwashukuru watangulizi wangu Mheshimiwa Charles Mwijage, Mbunge wa Jimbo la Muleba Kaskazini na Mheshimiwa Joseph Kakunda, Mbunge wa Jimbo la Sikonge waliokuwa Mawaziri wa Viwanda na Biashara. Nikiri kuwa misingi waliyoweka inaendelea kuwa chachu muhimu katika kuendeleza Sekta ya Viwanda na Biashara nchini. Aidha, nimshukuru Katibu Mkuu mstaafu Profesa Joseph Buchweshajja kwa kushirikiano alionipa kipindi nilichofanya nae kazi na nimkaribishe Profesa Riziki Shemdoe, Katibu Mkuu wetu mpya. Nampongeza Profesa Shemdoe kwa nguvu na kasi aliyokuja nayo kwenye Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze pia Mheshimiwa Mussa Zungu, Mbunge wa Ilala, Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Mbunge wa Iramba Magharibi kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kuteuliwa kuwa Mawaziri. Naahidi kuendelea kuwapa ushirikiano wa kutosha katika kutimiza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana pia na Waheshimiwa Wabunge kutoa pole kwa familia zilizoondokewa na Wabunge wenzetu ambao ni Mheshimiwa Rashid Akbar aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini; Mheshimiwa Dkt. Getrude Rwakatara, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Richard Ndassa, aliyekuwa Mbunge



wa Sumve; na Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustino Mahiga, aliyekuwa Mbunge wa kuteuliwa na Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii pia kuwashukuru viongozi na watendaji wote wa sekta binafsi kwa michango yao katika kuendeleza Sekta ya Viwanda na Biashara. Nawashukuru *TPSF, CTI, TTCIA, TMDC, CEO Roundtable*, Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania na wengine wengi. Naendelea kuwategemea kama nguzo na mihimili ya kushirikiana katika kuendeleza viwanda na biashara na kuchochea uchumi wetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii ya bajeti ninayowasilisha leo ni matokeo ya uratibu na ushirikiano mzuri wa viongozi wenzangu katika Wizara akiwemo Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, Mbunge wa Jimbo la Nyasa; Katibu Mkuu, Prof. Riziki Shemdo; Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Dovick Nduhiye; Wakuu wa Idara, Vitengo, Taasisi na watumishi wote wa Wizara na Taasisi. Napenda kuwashukuru na kuwapongeza kwa kujituma na kuonesha daima utayari wa kuboresha mbinu na mikakati ya kisekta kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza na kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Karagwe kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu ya kitaifa na ya Jimbo, nawapongeza kwa namna wanavyojibidiisha katika kujiletea maendeleo. Aidha, nawaahidi kwamba nitaendelea kutetea maslahi yao hapa Bungeni na hata nje ya Bunge ili kuhakikisha Karagwe inaendelea kushamiri na kuleta matokeo ya mtu mmoja mmoja, wilaya, mkoa na hatimaye kuongeza mchango wake katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee namshukuru sana mke wangu mpendwa Jenipher Bashi, watoto na familia yangu kwa upendo wao, uvumilivu na maombi yao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu ya kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuomba ushiriki wa dhati kwa kila Mtanzania katika kupambana na virusi vya *corona* ili kulinda nguvu kazi ya Taifa. Naomba sana Watanzania wote kuwa kila mmoja, kila familia, jumuiya zote nchini kutambua kuwa usalama wetu hutegemea jitihada ya kila mmoja kujilinda na kumlinda mwenzake. Katika kukabiliana na janga la ugonjwa wa *corona*, Kampuni ya Kilombero *Sugar* ilichangia jumla ya lita 30,000 za *ethanol* kwa ajili ya kutengeneza vitakasa mikono ambapo Wizara ya Afya ilipewa lita 20,000 na kiasi kilichobaki cha lita 10,000 zilipewa Taasisi za *SIDO* na *TIRDO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa tayari viwanda na makampuni 65 yanazalisha vitakasa mikono vyenye ubora unaokubalika na *TMDA*. Kwa wastani viwanda hivyo vinatumia kiasi cha *ethanol* kwa mwezi kisichopungua lita 2,548,951. Umoja wa Wenye Viwanda vya Dawa na Vifaa Tiba (*TMPA*) kwa ujumla wao viwanda vikubwa vinne vinazalisha vitakasa mikono kwa mwezi lita zipatazo 900,000 na viwanda vya kati na vidogo vipatavyo 61 vinazalisha lita zipatazo 2,745,000 za vitakasa mikono kwa mwezi na kufanya jumla ya uzalishaji vitakasa mikono kuwa lita 3,645,000 kila mwezi. Kati ya hizo, *TIRDO* huzalisha lita 90,000 kwa mwezi na *SIDO* huzalisha lita 18,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tuna viwanda viwili vya kutengeneza barakoa aina ya *surgical masks* ambavyo ni *Pristine na Five Star*. Viwanda hivyo vina uwezo uliosimikwa wa kutengeneza barakao 150,000 kwa siku na uwezo wa uzalishaji kwa sasa ni barakoa 30,000 kwa kiwanda cha *Pristine* na barakoa 40,000 kwa kiwanda cha *Five Star* kwa siku. Aidha, barakoa za vitambaa (*cloth masks*) kwa ajili ya kujikinga tayari jumla ya viwanda 123 vimeitikiwa wito wa kutengeneza barakoa hizo ambapo kati yao viwanda vikubwa ni 13 na viwanda vidogo ni 110. Wizara inaendelea kuhamasisha viwanda vya ndani vya nguo kutengeneza kwa wingi kuwasaidia Watanzania na mapambano ya *corona*. Natoa wito kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya zetu kuhamasisha mafundi vyerehani kwenye kila kijiji kushona

barakoa za nguo kuwasaidia wananchi vijijini. TMDA na TBS, watoe mafunzo kupitia vyombo vya habari na wawape ushirikiano Wakuu wa Mikoa na Wilaya katika majukumu haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya Sekta ya Viwanda na Biashara katika Awamu ya Tano; katika kipindi cha kwanza cha utawala wa Serikali ya Awamu ya Tano, Serikali iliweka nguvu kubwa katika kufanikisha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015/2020. Umakini wa utekelezaji Ilani ya CCM umehamasisha na kuchochea ujenzi wa uchumi wa viwanda ili kufikia malengo ya maendeleo yaliyoainishwa katika Dira ya Taifa ya mwaka 2020/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imejitosheleza katika baadhi ya bidhaa muhimu zinazozalishwa nchini. Saruji, uzalishaji halisi ni tani milioni 7.4 na mahitaji halisi ni tani 4.8. Marumaru; uzalishaji halisi ni mita za mraba milioni 32.4 na mahitaji ya halisi ni wastani wa mita za mraba milioni 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuhamasisha uendelezaji na ujenzi wa viwanda nchini. Kutokana na uhamasishaji huo jumla ya viwanda vipya 8,477 vimeanzishwa kati ya mwaka 2015 mpaka 2019. Viwanda hivyo vinajumuisha Viwanda 201 vikubwa, Viwanda 460 vya kati, Viwanda 3,406 vidogo na Viwanda 4410 vidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara ndogo vimetoa ajira kwa wingi kwa Watanzania ambapo sasa inaajiri zaidi ya Watanzania milioni nane. Ajira hizo zimewezesha Watanzania kujiongezea vipato na kutatua changamoto zao za kijamii na kiuchumi. Hii imetokea kutokana na Serikali ya Awamu ya Tano kuweka mazingira wezeshi, ikiwemo kupunguza Mamlaka za udhibiti na kufanya Watanzania wengi kujiajiri na kutekeleza azma ya ujenzi wa Uchumi wa Viwanda Nchini ambapo takribani asilimia 99 ya viwanda vyote nchini vipo chini ya sekta hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Viwanda vya Dawa na Vifaa Tiba kwa sasa ina jumla ya viwanda 15 ambapo viwanda 12 vinatengeneza dawa za binadamu, viwanda viwili dawa za mifugo na kiwanda kimoja kinatengeneza vifaa tiba. Kwa sasa Viwanda vya Dawa vinazalisha chini ya asilimia 12 ya uwezo wake uliosimikwa na Serikali imekuwa ikiwawekea Wawekezaji mazingira wezeshi ili kufikia asilimia 60 ya uwezo uliosimikwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuweka vivutio vya uwekezaji kwa lengo la kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa kuondoa VAT kwa vifungashio vya dawa zinazozalishwa nje na ndani ya nchi. Kushusha kodi ya mapato kwa asilimia 30 mpaka 20 kwa Mwekezaji mpya ndani ya miaka mitatu ya mwanzo na kuweka upendeleo maalum kwa ununuzi wa dawa zinazozalishwa na viwanda vya ndani kupitia MSD.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makadirio ya uzalishaji wa sukari kwa msimu wa mwaka 2019/2020 yalikuwa tani 345,296 kwa viwanda vya ndani, sawa na asilimia 73.46 ya kiasi cha sukari inayokadiriwa kwa matumizi ya kawaida. Aidha, hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 uzalishaji wa sukari nchini, ulikuwa jumla ya tani 298,949 wakati mahitaji ya sukari kwa mwaka ni wastani wa tani 635,000. Kati ya mahitaji hayo, tani 470,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na tani 165,000 kwa matumizi ya viwandani. Makadirio hayo yametokana na ukweli kwamba mahitaji ya sukari ya matumizi ya kawaida kwa mwezi ni wastani wa tani 38,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu zilizopelekea kupanda kwa bei ni pamoja na mvua nyingi kipindi cha vuli na kupungua kiwango cha sukari kwenye miwa na taratibu za usafirishaji ambazo zimesababisha na ugonjwa wa *corona* ulioenea duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali imetoa tamko kuhusu uuzaji wa sukari. Matamko hayo ni pamoja na sukari iuzwe kwa kuzingatia bei elekezi na endapo

wafanyabiashara hawatazingatia maelekezo hayo. Hatua kali zitachukuliwa dhidi yao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ambao tumeshuhudia jitihada zao katika kusimamia tamko la bei elekezi kwa lengo la kuwalinda walaji. Aidha, niwaombe Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kote nchini kutumia Kamati za Ulinzi na Usalama kuendelea kusimamia bei za ukomo zilizotangazwa na Serikali ili wananchi waweze kupata bidhaa hii muhimu kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia EPZ imefanya tafiti tatu kutathmini tija inayopatikana kutokana na kampuni zilizowekeza chini ya EPZ. Tafiti hizo zimeonesha uwepo wa tija katika uwekezaji wa maeneo hayo. Hadi kufikia Disemba, 2019 chini ya Benjamin William Mkapu *Special Economic Zone* mauzo ya nje ya nchi yameingizia nchi bilioni 293.56. Matumizi mengine ya kuendeshea biashara yameingizia nchi bilioni 146.58. Kodi na Tozo mbalimbali zilizolipwa kupitia TRA zimeingiza shilingi bilioni 17.24 na zimepatikana ajira za moja kwa moja viwandani zipatazo 3,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na manufaa hayo Wizara kupitia EPZ imekua ikihamasisha ushiriki Serikali za Mikoa katika uendelezaji wa Maeneo ya *Special Economic Zone* ili kuiwezesha Mikoa husika kutumia Maeneo ya *Special Economic Zone* kama chanzo cha mapato na mbinu mojawapo ya kuchochea shughuli za kiuchumi katika mikoa husika. Hadi sasa Mikoa ya Arusha, Geita, Mwanza, Kigoma na Songwe imetenga maeneo yanayoendelezwa kama Maeneo Maalum ya Kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia uhamasishaji huu katika kipindi cha mwaka 2019/2020, EPZ imesajili kampuni sita na hivyo kufanya viwanda vilivyo chini ya EPZ kuongezeka kutoka viwanda 163 mpaka viwanda 169 vikichangia ongezeko la mtaji unaokadiriwa kutoka trilioni 5.41 hadi trilioni 5.47. Mauzo ya nje yanakadiriwa kuongezeka kutoka

trilioni 5.17 hadi takribani trilioni 5.21 na fursa za ajira moja kwa moja kutoka 56,442 hadi 57,342.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mradi wa Kurasini ni kuliendeleza eneo hilo kama kitu cha biashara na ugavi ya *Trade and Logistic Center*. Serikali kupitia mamlaka ya *EPZ* imedhamiria kuliendeleza eneo la Kituo cha Biashara cha Kurasini kama soko la mazao mchanganyiko kwa kuanzia na zao la chai, kahawa na mazao ya bustani. umuhimu wa kutekeleza wazo la kujenga Kituo cha Biashara na Ugavi pale Kurasini kwa ajili ya mazao ya kilimo ni kuwezesha sekta ya kilimo kuchangia vizuri zaidi katika pato la taifa na kuwezesha uongezaji wa thamani ya mazao na biashara ya mauzo ya nje kufanyika. Baada ya kilimo shughuli zinazofuata ni uchakataji kwa maana ya viwanda na hatimaye mauzo kwa maana ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia *NDC* imekamilisha upimaji wa eneo la tamko pale Kibaha ambapo jumla ya hekari 201.63 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda na miundombinu. Hadi sasa viwanda viwili vinavyofanya kazi vimeajiri watumishi 200 na ujenzi wa viwanda vipya eneo la tamko Kibaha vitaajiri watumishi 21,220.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira za kudumu; madhumuni ya Serikali ni kuwa na *Industry park* nyingi nchini ama kupitia *EPZ* ama *NDC* ama halmashauri zetu ili wafanyabiashara na wawekezaji wenye mtaji na *business plan* wakute tayari eneo lina maji, umeme na huduma nyingine muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia *SIDO* imefanikiwa kuchochea uanzishwaji wa shughuli za kiuchumi kwa kutumia mikopo inayotolewa na Skimu ya Ukopeshaji kwa Wajasiriamali yaani *SME Credit Guarantee Scheme* na Mfuko wa *NEDF*. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi Machi 2020 mtaji wa Mfuko wa *NEDF* umeongezeka kutoka shilingi bilioni 6.429 Machi 2016 hadi shilingi bilioni 8.65 Machi 2020 ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 2.2. Ongezeko hilo

limetokana na riba inayopatikana kutokana na fedha inayozungushwa yaani *revolving fund* kupitia mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, jumla ya wajasiriamali 17,693 wakiwemo wanawake 8,933 na wanaume 8,721 walipatiwa mikopo iliyowezesha kupatikana kwa jumla ya ajira 47,180. Kupitia mifuko hiyo, jumla ya viwanda vipya 437 vilianzishwa na kutoa ajira 1,481. Jitihada hizo ni kichocheo na chachu kubwa kwa huduma na taasisi za fedha ambazo nazo hutoa huduma ya mikopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Februari, 2020 yalisainiwa makubaliano kati ya *SIDO*, *VETA*, *Azania Bank*, *NSSF* na Baraza la Uwezesaji Wananchi Kiuchumi ya kuanzisha program ya kutoa mikopo kwa wajasiriamali waliohudumiwa na *SIDO* na Wahitimu wa *VETA* kupitia Benki ya Azania. Makubaliano hayo yaliyofanyika chini ya uratibu wa Baraza la Uwezesaji Wananchi Kiuchumi yanatoa fursa kwa *SIDO* na *VETA* kuwapeleka wajasiriamali na wahitimu Benki ya Azania kuomba mikopo ya viwanda kuanzia shilingi milioni 8 hadi milioni 500.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zitakazokopeshwa kiasi cha shilingi bilioni 5 zimetolewa na *NSSF* kwa mkopeshaji ambaye ni Benki ya Azania. Mwongozo wa utekelezaji wa program unaandaliwa ndipo utekelezaji wa program hiyo uanze. Wizara inakusudia kuweka msukumo mkubwa wa program hiyo ili iwafikie wajasiriamali wengi nchini na wapate kunufaika. Tunawashukuru *NSSF* na Azania Benki na natoa wito kwa mabenki yote nchini na mifuko ya jamii kuiga mfano huu ili kuinua wajasiriamali nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanikiwa kutenga maeneo maalum kwa ajili ya wajasiriamali kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi. Jitihada hizo zimewezesha ujenzi wa majengo, viwanda yaani *industrial shades* 12 katika mitaa ya viwanda ya *SIDO* iliyopo mikoa ya Dodoma, Manyara, Kagera, Mtwara na Geita. Jumla ya viwanda 29 vimeweza kusimikwa katika majengo hayo na hivyo kuzalisha ajira 648. Kutokana na umuhimu huo, Wizara inaendelea na

ujenzi wa majengo ya viwanda katika mikoa mingine kwa kuanzia Mikoa ya Kigoma, Mtwara, Ruvuma ambapo *SIDO* imekamilisha upembuzi yakinifu wa majengo matatu pamoja na michoro ya usanifu yaani *architectural drawings* katika Mikoa ya Mtwara na Kigoma na ujenzi umeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukamilishaji wa majengo ya viwanda yaani *industrial shades* unategemewa kuanzisha uanzishwaji wa viwanda vipya 7 vitakavyotengeneza ajira 77. Vilevile, Serikali imefanikisha kusogeza karibu huduma za kusaidia na kuhamasisha wananchi kushiriki katika ujenzi wa uchumi wa viwanda kwa kujenga ofisi nne za *SIDO* katika Mikoa mipya ya Simiyu, Katavi na Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutumia fursa za masoko ya Kikanda, Wizara imefanikisha kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na huduma kwenye masoko hayo yanayotoa fursa ya upendeleo maalum yaani *preferential market access*. Tanzania imekuwa na urari chanya wa mauzo ya bidhaa kwenda kwenye masoko ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika yaani *SADC*. Kwa mfano, kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki toka 2015 mpaka 2019, Tanzania imekuwa na urari chanya wa mauzo ya bidhaa kwa wastani wa dola milioni 288.04.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliandaa na kuwasilisha Waraka wa Itifaki wa Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia ili kufanya Mkataba wa Uwezeshaji Biashara yaani *Trade Facilitation Agreement* kuwa sehemu rasmi ya mikataba ya *WTO*. Tayari Waraka huo umesharidhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hati ya kuridhia Itifaki hiyo imekwishasainiwa na kuwasilishwa *WTO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Itifaki ya Marrakesh inayolenga kuwezesha Upatikanaji wa Kazi Zilizochapishwa kwa Watu Wasioona, Wenye Uoni Hafifu, Ulemavu Unaofanya Mtu Kushindwa Kusoma wa Mwaka 2013 iliridhiwa na Bunge



lako la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tayari hati ya itifaki hiyo imesainiwa na kuwasilishwa *WIPO*. Tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Rais kwa kuridhia na kufanikisha mikataba na itifaki hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwelekeo na vipaumbele vya sekta ya viwanda na biashara. Mtazamo na mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi kuhusu maendeleo ya viwanda na biashara nchini unalenga kujenga uchumi wa viwanda utakaowezesha Watanzania kunufaika na uchumi ifikapo mwaka 2025. Hatua hiyo itawezesha Watanzania kutumia fursa za kiuchumi na kijamii katika mifumo iliyoboreshwa na inayingatia haki na utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuthamini rasilimali na bidhaa za ndani ni ukombozi muhimu wa kiuchumi kwa Taifa lolote. Mifano hai ni nchi ya Japan na China ambazo wananchi wake wamejijengea utamaduni wa kuthamini bidhaa zinazozalishwa katika nchi yao. Hivyo, Wizara itaendelea kuhamasisha uimarishaji wa ubora na matumizi ya bidhaa za ndani, nguvu kazi na malighafi za ndani ili kuleta ufungamanisho wa sekta katika kujenga uchumi na kuleta maendeleo kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara kwa kushirikiana na *TanTrade* inaendelea kuhamasisha wananchi kutumia bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani kupitia kauli mbiu ya 'Nunua Bidhaa za Tanzania Jenga Tanzania (Buy Tanzania Build Tanzania). Mbinu hiyo ni muhimu sana katika kipindi cha ujenzi wa uchumi wa viwanda ili kuimarisha viwanda vya ndani na kutumia Kiswahili katika bidhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa mchango wa sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo katika uchumi na hususan ujenzi wa viwanda, Serikali itachukua hatua za makusudi kuimarisha ujasiriamali nchini. Kipaumbele kitakuwa katika kuimarisha taasisi ya *SIDO* kwa kupitia upya muundo wake na kujengea uwezo ili iweze

kubeba ipasavyo dhamana ya uendelezaji wa viwanda vidogo na biashara ndogo inayowabeba Watanzania walio wengi. Jitihada hizo zitaenda sambamba na kuendelea na ujenzi wa *shades* katika mikoa yote nchini ili manufaa yaliyoonekana ya ajira na uongezaji wa samani wa mazao na kuongeza ushindani katika soko yasambae nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia itaweka mkazo na umuhimu katika upatikanaji wa teknolojia, kuongeza miundombinu ya uzalishaji yaani *industrial shades* ili kuwawezesha wajasiriamali kupata mahali pa kufanyia uzalishaji na kuweza kuhudumiwa kirahisi na taasisi mbalimbali zikiwemo za uhibitaji ubora wa bidhaa, taasisi za fedha na mafunzo muafaka. Juhudi za kuimarisha ujasiriamali nchini zitaenda sambamba na kuimarisha *SIDO* ili imudu kutoa huduma bora na zenye kuleta tija kwa uzalishaji wa bidhaa, huduma na ufanyaji biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi himilivu unaotabirika na ushindani unatokana na jitihada za kuujenga, kuuendeleza na kuulinda. Kujilinda isitafsiriwe kuwa ndiyo kujitenga kiuchumi na nchi nyingine na wala si dhambi kwani hata nchi zilizoendelea kiuchumi duniani mbalimbali zinaendelea kutumia njia tofauti. Hivyo sera, sheria na mikakati ya kisekta itaendelea kuhakikisha kuwa kunakuwepo na ushindani wa haki ili kuulinda viwanda na biashara nchini. Tutaendelea kuulinda haki za msingi za walaji kwa kuweka utaratibu wa kisheria utakaotaka wawekezaji wenye viwanda na wafanyabiashara katika mazao, bidhaa na huduma kutotumia nguvu ya soko isivyotakiwa na kusababisha kuwakandamiza wanyongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza nguvu za utafutaji wa fursa za masoko ya nje, Wizara inafanya uchambuzi wa kina na kuona umuhimu wa kuhuisha na kurejesha Waambata wa Biashara yaani *Trade Attachee* katika ofisi za Balozzi zetu zilizo nje ya nchi ili kuweka mfumo wa kufanya tathmini na utafiti wa mahitaji ya soko la bidhaa zinazozalishwa nchini. Tathmini na tafiti hizo zitatoa picha

ya mahitaji ya soko la nje na kuwezesha wazalishaji wa bidhaa za ndani kuzalisha kwa kuzingatia mahitaji ya soko la nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji huduma bora kwa wananchi kwa kiwango kinachoridhisha ni lengo kuu la mabadiliko ya kiutendaji ambayo Serikali ya Awamu ya Tano inayapa kipaumbele. Hivyo, mweleko wetu ni kuhakikisha kuwa taasisi za kisekta zinajielekeza katika kutoa huduma kwa viwango vinavyokidhi matarajio ya wananchi. Wizara yangu na taasisi zake zitaongeza ubunifu katika utendaji kazi kwa tija na kutoa huduma kwa weledi ili kuchochea ufanisi katika sekta ya viwanda na biashara na hatimaye kuongeza pato la taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendeleza uchumi wa viwanda, Serikali inaimarisha taasisi zake ili ziweze kukidhi na kuhimili mahitaji ya maendeleo ya ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini. Wizara inajizatiti kuimarisha Taasisi za Utafiti za Maendeleo na Teknolojia yaani *TIRDO*, *TEMDO* na *CAMARTEC* kwa kufanya tathmini ya kitaalamu, kupitia upya na kwa kina majukumu na miundo ya kisheria ya taasisi hizi. Lengo ni kuzifanyia maboresho mahsusi yatakayozingatia ushauri wa kitaalamu na itakapoonekana inafaa zitafanyiwa maamuzi ya kimuundo ikiwemo kuziunganisha ili ziweze kuwa na tija na ufanisi katika kuleta mwendelezo wa mafanikio ya taasisi hizo na pia kuongeza nguvu katika kuendeleza viwanda nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe makadirio ya Wizara ya Viwanda na Biashara ya kukusanya mapato ya jumla ya Sh.15,000,000 na matumizi ya jumla Sh. 81,366,902,000 kwa mwaka 2020/2021. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Viwanda na Biashara yenye anuani ya [www.mit.go.tz](http://www.mit.go.tz).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
*(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/2021 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1. UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika;** Kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, ambayo ilichambua Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara Fungu 44 (Viwanda) na Fungu 60 (Biashara) tarehe 24 na 25 Machi, 2020 Jijini Dodoma, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu sasa likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mipango na Bajeti kwa Mwaka 2019/2020. Aidha, naliomba Bunge lako tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka 2020/2021.

2. **Mheshimiwa Spika;** Kwa kuzingatia na kutambua kuwa hii ni Hotuba yangu ya Kwanza ya Bajeti nikiwa Waziri wa Viwanda na Biashara na kwa kuwa hiki ni kikao cha mwisho cha Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa fadhili zake kwa mja wake na kwa kunijalia afya na baraka katika majukumu niliyokasimiwa. Kwa namna ya pekee niruhusu nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kunitiua kuwa Waziri na kunipa majukumu yanayobeba ajenda kuu ya Serikali ya Awamu ya Tano ya ujenzi wa uchumi wa viwanda. Nampongeza kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya SADC na namna anavyoshughulikia masuala ya biashara katika nchi za SADC na EAC ikiwa ni pamoja na kuomba kufutiwa madeni kwa nchi za Afrika katika kipindi hiki cha mlipuko wa ugonjwa wa COVID – 19. Nampongeza pia kwa namna anavyotuongoza kwa ujasiri na misingi imara, yenye kusheheni uzalendo na mapenzi kwa nchi yetu. Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa

Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; pamoja na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi; Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; kwa jinsi walivyojizatiti na kusimamia ipasavyo misingi ya utafu wetu na hususan kwa kuwahakikishia Watanzania kuwa Tanzania ni mahala salama na penye fursa za uhakika za kujiletea maendeleo kwa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

3. **Mheshimiwa Spika;** Napenda kuchukua nafasi hii, kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika kwa umakini wenu katika kuliongoza na kulisimamia Bunge letu. Pia, naipongeza na kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq, Mbunge wa Jimbo la Mvomero, Makamu wake Mheshimiwa Kanali Mstaafu Ali Khamis Masoud, Mbunge wa Jimbo la Mfenesini na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati. Ushauri na maelekezo yao yamekuwa chachu muhimu sana katika mageuzi ya kifikra na kiutendaji ya Wizara na hivyo kuchochea kasi ya maendeleo ya viwanda na biashara nchini.

4. **Mheshimiwa Spika;** Nitumie fursa hii pia kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri wapya kwa kuteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali. Kwa namna ya pekee, niwashukuru watangulizi wangu Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Jimbo la Sikonge aliyekuwa Waziri wa Viwanda na Biashara pamoja mtangulizi wake Mheshimiwa Charles John Poul Mwijage, Mbunge wa Jimbo la Muleba Kaskazini, kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipa katika kutekeleza majukumu yangu. Nikiri kuwa misingi waliyoiweka imeendelea kuwa chachu muhimu katika kuendeleza Sekta ya Viwanda na Biashara nchini.

5. **Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka 2019/2020, Bunge liliondokewa na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la

Newala Vijijini, Mheshimiwa Rashid Ajali Akbar; Mheshimiwa Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Richard Mganga Ndasa, aliyekuwa Mbunge wa Sumve; na Mheshimiwa Balozi Augustine Mahiga aliyekuwa Mbunge wa Kuteuliwa na Waziri wa Katiba na Sheria. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa familia zao na wote walloguswa na misiba hiyo. Vilevile, naomba kutoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge waliopata misiba ya kufiwa na wazazi, watoto au wanafamilia wa karibu. Pia, natoa pole kwa Watanzania waliokumbwa na kadhia ya majanga mbalimbali kama vile ajali za majini, barabarani na majanga mengine yanayofanana na hayo.

6. **Mheshimiwa Spika**; Naomba kutumia fursa hii pia kuwashukuru viongozi na watendaji wote wa sekta binafsi; hususan Baraza la Taifa la Biashara (Tanzania National Business Council – TNBC ); Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (Tanzania Private Sector Foundation – TPSF); Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (Confederation of Tanzania Industries – CTI); Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (Tanzania Chambers of Commerce, Industry and Agriculture – TCCIA); na Baraza la Kilimo Tanzania (Agriculture Council of Tanzania – ACT) kwa michango yao katika kuendeleza Sekta za Viwanda, Biashara, Masoko, Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo. Tunaendelea kuwategemea kama nguzo na mihimili muhimu ya kushirikiana katika kutekeleza kwa vitendo sera na mipango ya kisekta katika kuendeleza viwanda na biashara na kuchochea ukuaji wa uchumi wetu kwa ujumla.

7. **Mheshimiwa Spika**; Hotuba hii ya Bajeti ninayowasilisha leo ni matokeo ya uratibu na ushirikiano mzuri wa viongozi wenzangu katika Wizara, akiwemo Naibu Waziri Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Jimbo la Nyasa; Katibu Mkuu, Prof. Riziki Silas Shemdoe; Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Ludovick James Nduhiye; Wakuu wa Idara, Vitengo, Taasisi na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi. Napenda kuwashukuru na kuwapongeza kwa

kujituma na kuonesha daima utayari wa kuboresha mbinu na mikakati ya kisekta kwa vitendo.

8. **Mheshimiwa Spika;** Nawapongeza na kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Karagwe kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya kitaifa na ya Jimbo. Nawapongeza kwa namna wanavyojibidiisha katika kujiletea maendeleo. Aidha, ninawaahidi kwamba nitaendelea kutetea maslahi yenu hapa Bungeni na hata nje ya Bunge ili kuhakikisha Jimbo linaendelea kushamiri na kuleta matokeo ya mtu mmoja mmoja, Jimbo na hatimaye kuongeza mchango wake kwa Taifa kwa ujumla. Kipekee namshukuru sana mke wangu mpendwa Jennifer Bashungwa, watoto na familia yangu kwa ujumla kwa upendo wao, uvumilivu na maombi yao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu ya kitaifa.

9. **Mheshimiwa Spika;** Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuomba ushiriki wa dhati wa kila Mtanzania katika kupambana na usambaaji wa virusi vya CORONA vinavyosababisha ugonjwa wa homa ya mapafu (COVID-19) ili kulinda nguvukazi ya Taifa letu. Maendeleo ya viwanda na biashara na ufungamanishi wa uchumi kwa ujumla wake unahitaji kushirikisha rasilimali zenye ubora ikiwemo nguvukazi yenye afya. Hivyo, nawaomba sana Watanzania wote kuwa kila mmoja, kila familia na jumuiya zote nchini kutambua kuwa usalama wetu hutegemea jitihada ya kila mmoja kujilinda na kumlinda mwenzake. Kwa kufanya hivyo, tunatoa uhakika kwa Watanzania wote kuwa wanufaika wa uhakika wa matunda ya jitihada za ujenzi wa uchumi wa viwanda unaojengwa kwa nguvu zote.

10. **Mheshimiwa Spika;** Baada ya maelezo hayo ya awali, naomba sasa nijielekeze katika kuelezea Mchango wa Sekta ya Viwanda na Biashara ukifuatiwa na Mafanikio Makuu ya Sekta; Mapitio ya Bajeti na Utekelezaji wa Malengo ya Bajeti ya Wizara yangu kwa kipindi cha mwaka 2019/2020; Mwelekeo wa Sekta ya Viwanda na Biashara; na kisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa kipindi cha mwaka 2020/2021.

## **2. MCHANGO WA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA KATIKA UCHUMI**

### **2.1. Sekta ya Viwanda.**

11. *Mheshimiwa Spika*; Mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa kwa mwaka 2019 ulikuwa asilimia 8.5 ikilinganishwa na asilimia 8.05 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 0.45. Mchango huo ni matokeo ya kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji viwandani katika kipindi hicho (Kiambatisho Na.1). Vilevile, Kasi ya ukuaji wa thamani ya Uzalishaji Bidhaa Viwandani kwa mwaka 2019 ilikuwa ni Shilingi Trilioni 10.2 ikilinganishwa na Shilingi Trilioni 9.6 mwaka 2018, sawa na kasi ya ukuaji wa asilimia 5.8 (Kiambatisho Na. 2). Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo.

12. *Mheshimiwa Spika*; Mchango wa Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo katika Pato la Taifa ni asilimia 35 na Sekta hii imeajiri zaidi ya Watanzania milioni tisa ikiwa ni ya pili katika sekta za kiuchumi katika kutoa ajira ikiifuatia Sekta ya Kilimo.

### **2.2. Sekta ya Biashara**

13. *Mheshimiwa Spika*; Shughuli za Biashara ya jumla na rejareja zimechangia asilimia 8.8 kwenye Pato la Taifa kwa mwaka 2019 ikiwa ni moja kati ya sekta tatu zilizochangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Taifa.

## **3. MAFANIKIO YA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA KATIKA AWAMU YA TANO**

14. *Mheshimiwa Spika*; Ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini ni jukumu jumuisha na shirikishi linalohusisha sekta mbalimbali za uchumi ambazo zinatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia azma ya ujenzi wa uchumi wa viwanda. Hivyo, sekta hizo hutekeleza mipango jumuishi katika kujenga uchumi wa viwanda kwa kutumia rasilimali za fedha za Bajeti ya Serikali kwa kujenga miundombinu ya msingi na wezeshi ikiwemo miundombinu ya barabara, maji, umeme na



mawasiliano. Aidha, sekta za huduma huchangia katika kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na nguvukazi yenye afya, bora na ujuzi unaohitajika. Pia uwepo wa ulinzi na usalama wa mali na watu hutoa uhakika wa mazingira ya wananchi kujishughulisha katika uzalishaji wa mazao, bidhaa na huduma. Hivi, tunapoangalia mafanikio ya utekelezaji wa Bajeti ya Sekta ya Viwanda na Biashara na hususan katika ujenzi wa uchumi wa viwanda, hatuna budi kuangalia kwa ujumla na mapana yake namna Bajeti ya Serikali inavyogharamia mipango ya sekta nyingine ambazo zinajielekeza katika kuchangia utekelezaji wa azma ya ujenzi wa uchumi wa viwanda.

15. **Mheshimiwa Spika;** Kwa ujumla wake, Sekta ya Viwanda na Biashara imefanikiwa: Kuongeza uzalishaji wa bidhaa mbalimbali muhimu nchini ikiwemo sukari, mafuta ya kula, bidhaa za chuma, saruji na marumaru na hivyo kwa kiasi kikubwa kukidhi mahitaji ya ndani ya nchi; Kuvutia ujenzi wa viwanda vipya nchini na ufufuaji wa viwanda vilivyobinafsishwa; Kuongeza maeneo ya kufanyia kazi wajasiriamali na kuboreshwa kwa maeneo ya uwekezaji; Kuendelea kuimarika mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji kupitia utekelezaji wa BLUEPRINT; na Kuimarika kwa taasisi za utafiti na maendeleo ya teknolojia kwa kuboresha maabara zake na utoaji huduma. Pia, Sekta imefanikiwa Kuimarisha udhibiti wa bidhaa na huduma nchini; Kuongezeka uwezo na ujuzi wa rasilimali watu; Kuongezeka kwa uwekezaji na mapato katika viwanda; Kuendelea kujitosheleza katika baadhi ya bidhaa nchini ambazo zilikuwa zikiagizwa kwa wingi kutoka nje; Kuendelea kutoa elimu kwa wajasiriamali; Kuzalishwa kwa teknolojia mbalimbali za kuongeza thamani mazao hususan za kutumika vijijini zikiwemo za kusindika alizeti, nafaka, matunda; Kuanza kutoa leseni za biashara (Kundi A na B) kwa njia ya kielektroniki na Kutoa mikopo kwa wajasiriamali kupitia Mfuko wa NEDF na kuutunisha. Vilevile, imefanikiwa kuendelea kulinda viwanda na biashara za ndani; Kuimarisha masoko ya mipakani; Kukamilisha baadhi ya majadiliano na kuendeleza majadiliano ya kibiashara kati ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa ili kupata na kutumia fursa za masoko hayo;

Kuendelea kuunganisha wakulima na fursa za masoko; na Kuendelea kutoa taarifa za masoko ya mazao ya chakula, biashara na bidhaa mbalimbali. Aidha, taasisi za sekta zimeweza kutoa gawio lake Serikalini na pia kuchangia katika Bajeti ya Serikali.

3.1. **Mafanikio katika Sekta ya Viwanda**

16. **Mheshimiwa Spika;** Sekta ya Viwanda nchini ni miongoni mwa nguzo muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Serikali iliweka nguvu kubwa katika kufanikisha utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda sambamba na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2015/16- 2020/21 na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi 2015 – 2020. Utekelezaji huo umehamasisha na kuchochea ujenzi wa uchumi wa viwanda ili kufikia malengo ya maendeleo ya muda mrefu kama yalivyoanishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Ili kuhakikisha Sekta hiyo inachangia na kuleta tija katika uchumi wa Taifa, juhudi za makusudi zimeendelea kuchukuliwa katika uongezaji thamani wa malighafi za ndani hususan katika Sekta za Kilimo, Uvuvi, Mifugo, Maliasili na Madini. Hatua hizo zinasaidia kuchangia upatikanaji wa ajira; kuongeza uzalishaji na mauzo ya bidhaa ndani na nje ya nchi; na hivyo kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni katika uchumi.

17. **Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi hicho, msisitizo umewekwa katika ujenzi wa viwanda vipya na kuimarisha viwanda vilivyopo. Mafanikio yaliyopatikana kutokana na juhudi hizo ni pamoja na uendelezaji na uanzishwaji wa viwanda vya marumaru, saruji, chuma, vinywaji, na matunda, nyama, maziwa, nguo na mavazi, bidhaa za plastiki na ngozi. Kwa muhtasari, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitano ni kama ifuatavyo:-

i) **Uongezaji Thamani wa Mazao**

18. **Mheshimiwa Spika;** Kutokana na uhamasishaji unaofanywa na Serikali, uongezaji thamani wa mazao

ambayo malighafi zake zinazalishwa kwa wingi nchini umeendelea kuongezeka ambako kumechochewa na kuendelea kwa ujenzi wa viwanda nchini. Kwa mfano, viwanda 8 vya kusindika maziwa vyenye kusindika maziwa vimeongeza uwezo wake kutoka lita 167,620 kwa siku hadi kufikia lita 194,335 kwa siku. Vilevile, viwanda 17 vya nyama vilivyojengwa vimewezesha kuongeza usindikaji wa mazao ya mifugo ambapo zimewezesha Tanzania kuwa na jumla ya viwanda 145 vya usindikaji wa mazao ya mifugo. Viwanda hivyo vinajumuisha viwanda 33 vya nyama, viwanda 99 vya maziwa na viwanda 13 vya kusindika ngozi. Pia, Serikali imewezesha ujenzi wa viwanda vitatu vya kusindika matunda na mbogamboga. Viwanda hivyo ni Kiwanda cha Elven Agri, Sayona Fruits Limited na Dabaga. Aidha, Serikali imewezesha ujenzi wa viwanda vinne vya kusindika vyakula vya Dar Worth Company Limited kinachozalisha sembe, dona na unga wa lishe; Uniliver cha kusindika Chai; Murzah Wilmar Rice Millers cha kusindika Mpunga; na Mahashree Agroprocessing Tanzania Limited cha kufungasha mazao jamii ya kunde hususan mbaazi.

**ii) Ujenzi wa Viwanda Vipya**

19. **Mheshimiwa Spika**; Serikali inaendelea kuhamasisha uendelezaji na ujenzi wa viwanda nchini. Kutokana na jitihada hizo, jumla ya viwanda vipya 8,477 vimeanzishwa nchini kati ya mwaka 2015 hadi 2019. Viwanda hivyo vipya vinajumuisha viwanda 201 vikubwa, 460 vya kati, 3,406 vidogo; na 4,410 vidogo sana. Mfano wa viwanda katika Sekta ya Ujenzi ni Kilimanjaro Cement, Fujian Hexingwang Industry Co. Ltd na KEDA Ceramic Ltd; Sekta ya Dawa na Vifaa Tiba ni Kairuki Pharmaceutical Industry na Zesta Pharmaceutical Industry); Sekta ya Chakula na Vinywaji ni 21st Century Food processing Industry na Sayona Fruits Ltd; na Sekta ya Vifaa vya Umeme ni Inhemeter Co. Ltd na Europe Inc. Industry.

**iii) Ajira katika Sekta ya Uzalishaji**

20. **Mheshimiwa Spika**; Ajira katika Sekta za Uzalishaji zimeongezeka kutoka ajira 254,786 mwaka 2015 hadi

kufikia ajira 306,180 mwaka 2018, ikiwa ni ongezeko la asilimia 20.2. Ongezeko hilo lilitokana na ujenzi wa viwanda vipya na upanuzi wa viwanda vilivyopo ikiwemo; Kiwanda cha Goodwill Ceramic Ltd, KEDA (Twyford), Sayona Fruits Ltd (Chalinze), Sayona Drinks Ltd (Mwanza), Kiluwa Steel Ltd (Mlandizi), Fujian Hexing Wang Industry Co. Ltd (Mkuranga), Global Packaging Ltd (Kibaha), Europe Inc. Co. Ltd (Dar es Salaam), na Azam Fruits Processing Ltd (Mkuranga). Inatarajiwa kuwa, kwa mwenendo huo viwanda hivyo vitazalisha takribani ajira 370,478 ifikapo mwishoni mwa mwaka 2020.

***iv) Kujitosheleza kwa Mahitaji ya Ndani kwa Baadhi ya Bidhaa za Viwandani***

21. ***Mheshimiwa Spika;*** Nchi imejitosheleza katika baadhi ya bidhaa muhimu zinazozalishwa nchini zikiwemo: saruji, marumaru, nondo, mabati na vifaa vya umeme. Matokeo hayo yamefikwa kutokana na jitihada za Wizara za kuhamasisha wawekezaji kujenga viwanda vipya pamoja na upanuzi wa viwanda vya zamani. Kwa mfano, upanuzi wa viwanda vya saruji vya Tanga Cement Ltd na Mbeya Cement Ltd na kuanza kwa uzalishaji wa viwanda vipya kikiwemo Kiwanda cha Kilimanjaro Cement Ltd cha mjini Tanga kilichoanza kazi mwaka 2017 umewezesha kuongezeka kwa uwezo wa uzalishaji saruji (installed production capacity) hadi kufikia tani milioni 9.1 kwa mwaka 2019 ikilinganishwa na tani milioni 4.7 mwaka 2015. Uzalishaji halisi (actual production capacity) ni tani milioni 7.4 ambapo mahitaji halisi nchini ni tani milioni 4.8. Hii inamaanisha kuwa viwanda hivyo vinazalisha ziada ya tani milioni 2.6 ambazo huuzwa nje ya nchi zikiwemo Rwanda, Burundi, Malawi, Zambia, DRC Congo na Msumbiji.

22. ***Mheshimiwa Spika;*** Kutokana na jitihada za Serikali za kuhamasisha uwekezaji wa viwanda, ujenzi wa viwanda vikubwa viwili vya marumaru vya Goodwill (T) Ceramic Co. Ltd na KEDA (T) Ceramic Co. Ltd vimeanzishwa.

Kiwanda cha Goodwill (T) Ceramic Co. Ltd kina uwezo uliosimikwa wa mita za mraba milioni 18 kwa sasa uzalishaji halisi ni mita za mraba Milioni 14.4, na Kiwanda cha KEDA uwezo wa uzalishaji ni mita za mraba 28.8 na uzalishaji halisi ni mita za mraba milioni 18.

23. **Mheshimiwa Spika;** Uzalishaji wa bidhaa za chuma umeendelea kutosheleza mahitaji ya ndani na umesaidia katika upatikanaji wa malighafi za ujenzi wa miundombinu wezeshi ya viwanda nchini. Viwanda vikubwa vitatu vya chuma vya Kiluwa Steel (chenye uwezo wa kuzalisha tani 12,000 kwa mwaka), Lodhia Steel Industry chenye uwezo wa kuzalisha tani 3,700 na Lake Steel and Allied Products Ltd ambavyo vimeongeza idadi ya viwanda vya chuma nchini na kufikia 25 ni kielelezo cha mafanikio. Kati ya hivyo, viwanda 16 vinazalisha nondo na vina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani 1,082,700 kwa mwaka, wakati mahitaji ya nondo nchini kwa mwaka ni tani 295,000.

**v) Undelezaji Maeneo Maalum  
ya Uwekezaji**

24. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia Mamlaka ya EPZ, imefanya tafiti tatu zenye dhana ya kufanya tathmini ya tija inayopatikana kutokana na kampuni zilizowekeza chini ya EPZA katika uchumi wa nchi. Matokeo ya tafiti hizo yameonesha uwepo wa tija katika uwekezaji wa maeneo ya SEZ. Kwa mfano, shughuli za uzalishaji zinazotokana na uwekezaji uliofanyika ndani ya BWM-SEZ zimewezesha kupatikana Dola za Marekani 127,641,683 kutokana na mauzo ya nje ya nchi; Matumizi ya wawekezaji ya Dola za Marekani 63,730,000 kwa malipo ya wafanyakazi wa ndani, malighafi, umeme, maji na gharama nyingine za kuendesha biashara; Kodi na Tozo mbalimbali zilizolipwa kupitia TRA za Dola za Marekani 7,497,100.34; na Ajira za moja kwa moja viwandani zipatazo 3,000. Tafiti na tathmini hizo zitaendelea kufanyika kwa nia ya kuboresha ufanisi wa Mamlaka na kukuza mchango wake kwa Taifa.

### 3.2. *Mafanikio ya Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo*

#### *i) Kutoa Ajira kwa Watanzania Wengi*

25. *Mheshimiwa Spika*; Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo imetoa ajira kwa wingi kwa Watanzania ambapo kwa sasa imeajiri zaidi ya Watanzania milioni nane. Ajira hizo zimewezesha wahusika kujiongezea vipato na kutatua changamoto zao za kijamii na kiuchumi. Pia, imeweza kuongeza chachu katika azma ya ujenzi wa viwanda nchini ambapo takribani asilimia 99 ya viwanda vyote nchini vipo chini ya sekta hiyo. Hivyo, Sekta hiyo ni fungamanisho kubwa katika uchumi wa nchi kwa kuwa inahusisha sekta zote za uchumi. Vilevile, imebeba dhamana ya nchi ya kufikia uchumi wa kati unaoongozwa na viwanda ifikapo 2025, hasa ikizingatiwa kuwa inashirikisha Watanzania wengi katika shughuli za kiuchumi. Aidha, Viwanda vingi vilivyoanzishwa vimekuwa na mchango mkubwa katika kuongeza thamani ya malighafi za Tanzania hususan zitokanazo na mazao ya kilimo.

#### *ii) Mitaji kwa Wajasiriamali Wadogo*

26. *Mheshimiwa Spika*; Kupitia Sekta hiyo, Wizara imefanikiwa kuchochea uanzishwaji wa shughuli za kiuchumi kwa kutumia mikopo inayotolewa na SIDO chini ya Mfuko wa Wafanyabiashara Wananchi (NEDF). Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi Machi 2020, mtaji wa Mfuko wa NEDF umeongezeka kwa Shilingi Bilioni 2.22 kutoka Shilingi Bilioni 6.429 Machi 2016 hadi Bilioni 8.65. Ongezeko hilo limetokana na riba inayopatikana kutokana na fedha inayojizungusha (Revolving Fund) kupitia mikopo hiyo. Aidha, jumla ya wajasiriamali 17,654 wakiwemo wanawake 8,933 na wanaume 8,721 walipatiwa mikopo iliyowezesha jumla ya ajira 47,180 kupatikana.

27. *Mheshimiwa Spika*; Mwezi Februari, 2020 yalisainiwa makubaliano kati ya SIDO, VETA, Azania Bank, NSSF na NEEC ya kuanzisha program ya kutoa mikopo kwa

wajasiriamali waliohudumiwa na SIDO na wahitimu wa VETA kupitia Benki ya Azania. Makubaliano hayo yaliyofanyika chini ya uratibu wa Baraza la Uwezeshaji yanatoa nafasi kwa SIDO na VETA kuwapeleka wajasiriamali na wahitimu Benki ya Azania kuomba mikopo ya viwanda ya kuanzia Shilingi Milioni 8 hadi Milioni 500. Fedha zitakazokopeshwa kiasi cha Shilingi Bllioni 5 zimetolewa na NSSF kwa mkopeshaji ambaye ni Benki ya Azania. Program hiyo itaitwa SANVN kuwakilisha taasisi za SIDO, VETA, AZANIA BANK, NSSF na NEEC. Mwezi Aprili, 2020 vikao vya wataalam vilikamilisha Rasimu ya Mwongozo ya Utekelezaji wa Program (SANVN Viwanda Scheme – Lending Manual) na linasubiri uidhinishwe na kusambazwa ndipo utekelezaji wa program uanze.

***iii) Maeneo ya Shughuli za Uzalishaji kwa Wajasiriamali***

28. Mheshimiwa Spika; Serikali imefanikiwa kutenga maeneo maalum kwa ajili ya wajasiriamali kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi. Suala hilo limewezesha ujenzi wa majengo ya viwanda (Industrial Shades) 12 katika Mitaa ya Viwanda ya SIDO iliyopo mikoa ya Dodoma (3), Manyara (3), Kagera (1), Mtwara (1) na Geita (4). Jumla ya viwanda 29 vimeweza Kusimikwa katika majengo hayo ambapo ajira 648 zimezalishwa. Aidha, Serikali imefanikisha kusogeza karibu huduma za kusaidia na kuhamasisha wananchi kushiriki katika ujenzi wa uchumi wa viwanda kwa kujenga ofisi nne za SIDO katika mikoa mipya ya Simiyu, Katavi na Geita.

**3.3. Mafanikio katika Sekta ya Biashara**

29. ***Mheshimiwa Spika***; Sekta ya Biashara ni nguzo muhimu katika kuwezesha upatikanaji wa fursa za biashara na masoko kwa bidhaa za Tanzania za kilimo na viwandani kwenye masoko ya ndani na nje ya nchi. Biashara ni chanzo muhimu cha mapato ya Serikali na huwezesha kutawanya faida zinazopatikana kutokana na shughuli za uzalishaji. Hivyo, biashara hizo huchangia katika kuinua vipato vya wazalishaji na wafanyabiashara na kuchagiza uwekezaji

kutoka ndani na nje ya nchi. Katika kipindi cha kuanzia 2015 hadi 2019, Serikali imeendelea na utekelezaji wa Sera na Mikakati ya biashara na masoko kwa kufanya mapitio ya Sera, Sheria na Taratibu mbalimbali ili ziendane na mahitaji ya Sekta kwa kipindi kilichopo na kijacho. Juhudi hizo ni pamoja na kuendelea kuimarisha mazingira ya ufanyaji biashara nchini, kuendelea kujenga miundombinu ya masoko; na kutafuta fursa nafuu za biashara kupitia majadiliano ya biashara baina ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa.

30. **Mheshimiwa Spika;** Napenda kuchukua fursa hii kumshukuru na Kumpongeza Mhe. Rais wa Jamhuri ya Dkt. John Pombe Magufuli katika kipindi chake cha Uenyekiti wa SADC kwa kusimamia na kutetea lugha ya Kiswahili kuwa miongoni mwa lugha kuu za majadiliano. Kupitia jitihada zake, Mikutano ya SADC sasa inatumia lugha 4 za Kiingereza, Kireno, Kifaransa na Kiswahili. Kwetu sisi hiyo ni hatua kubwa na yenye manufaa kwa nchi katika Mtangamano huo wa Kikanda. Wizara itashirikiana na wadau wengi kuendelea kuuza Lugha ya Kiswahili kama bidhaa duniani kote.

**i) Mauzo ya Bidhaa na Huduma katika Masoko ya Nje**

31. **Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha miaka mitano, Sekta ya Biashara imefanikisha kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na huduma kwenye masoko ya kikanda yanayotoa fursa za upendeleo maalum (preferential market access). Tanzania imekuwa na urari chanya wa mauzo ya bidhaa kwenda kwenye masoko ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC). Mfano, kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kutoka mwaka 2015 hadi mwaka 2018, Tanzania imekuwa na urari chanya wa mauzo ya bidhaa kwa wastani wa Dola za Marekani Milioni 288.04. Thamani ya bidhaa zilizoingizwa kutoka nchi za EAC ilishuka kutoka Dola za Marekani Milioni 322.80 mwaka 2015 hadi Dola za Marekani Milioni 302.93 mwaka 2018. Kukua kwa Sekta ya viwanda nchini kumesababisha kupungua kwa uingizwaji wa bidhaa



kutoka EAC na SADC. Matokeo hayo, yametokana na Tanzania kujitosheleza na kuzalisha kwa ushindani bidhaa za saruji, marumaru, vyandarua, baadhi ya bidhaa za chuma kama vile nondo na mabati, mabomba ya plastiki, unga wa ngano na nafaka ikiwemo mahindi na mchele. Aidha, bidhaa zingine zilizouzwa zaidi katika Jumuiya hizo ni pamoja na chai, kahawa, sigara, madawa, vifaa tiba na madini ya Tanzanite.

## *ii) Biashara katika Masoko ya Nje*

32. **Mheshimiwa Spika;** Sekta ya Biashara imefanikisha kuendelea kuimarisha mahusiano ya kibiashara na nchi za Umoja wa Ulaya na zile zilizo nje ya Umoja huo. Miongoni mwa nchi hizo ambazo Tanzania imeendelea kujiimarisha kibiashara ni pamoja na nchi za Uswisi, Denmark, Uingereza, Uholanzi, Sweden na Ujerumani. Kwa mfano, mauzo ya Tanzania nchini Uswisi yaliongezeka kutoka Dola za Marekani Milioni 153,933 mwaka 2015 hadi Dola za Marekani Milioni 257,166 mwaka 2018. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni maua, mapambo, kahawa, chai, viungo, mafuta ya wanyama na mbegu, pamba na madini na vito vya thamani. Aidha, mauzo ya Tanzania yameendelea ikiwemo India, China, Japan, Uturuki na Marekani. Mfano kuongezeka kwa mauzo kwenda nchini India kutoka Dola za Marekani Milioni 20,547 mwaka 2015 hadi Dola za Marekani Milioni 42,421 mwaka 2018. Bidhaa zilizouzwa zaidi ni kahawa, pamba, chai, tumbaku, samaki na bidhaa za baharini, nguo na mavazi, bidhaa za mikono (handcrafts), na ngozi na bidhaa za ngozi.

### **3.4. Mafanikio ya Sekta ya Masoko**

#### *i) Kuboresha Mazingira ya Biashara Nchini*

33. **Mheshimiwa Spika;** Serikali imefanikiwa kuendelea na uboreshaji wa mazingira ya biashara nchini kwa kuandaa na kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhhibiti wa Biashara Nchini (Blueprint for Regulatory Reform to improve Business Environment). Mpango huo

umewezesha maboresho ya tozo 173 ambapo kati ya tozo hizo, tozo 163 zimefutwa na tozo kero 10 zimepunguzwa kiwango. Kati ya tozo zilizofutwa, 114 ni za Sekta ya Kilimo na Mifugo, 5 za OSHA, 44 za TBS, GCLA, Utalii, Maji, Uvuvi na iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa-TFDA. Aidha, tozo zilizopunguzwa ni za Mamlaka za Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA). Mpango huo umewezesha kuhamisha jukumu la usimamizi wa masuala ya chakula kutoka iliyokuwa TFDA kwenda TBS, ili kuondoa muingiliano wa majukumu. Maboresho hayo yamesaidia kuondoa urasimu na kupunguza gharama za kufanya biashara. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kutokana na kufutwa kwa tozo ni pamoja na ongezeko la usajili wa usalama mahali pa kazi (workplace) 16,457 zilizosajiliwa kwa mwaka 2019 ikilinganishwa na mahala pa kazi 11,963 zilizosajiliwa kwa mwaka 2018. Aidha, Serikali inaendelea na maandalizi ya kutunga Sheria ya Uwezeshaji Biashara ya mwaka 2020 (Business Facilitation Act, 2020), ili kuipa nguvu ya kisheria misingi ya maboresho iliyobainishwa katika Blueprint. Rasimu ya Waraka wa Sheria hiyo imekwishawasilishwa kwenye ngazi za maamuzi Serikalini.

***ii) Kudhibiti Upotevu wa Mazao baada ya Mavuno***

34. ***Mheshimiwa Spika***; Wizara kupitia Bodi ya Stakabadhi za Ghala imeendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kujenga miundombinu ya masoko ikiwa ni pamoja na ujenzi wa ghala katika maeneo mbalimbali nchini. Katika mwaka 2019/2020, ghala zifuatazo zimejengwa na zinatumika kuhifadhi mazao ya kilimo yakiwemo korosho, ufuta, dengu, kakao, mbaazi na choroko. Ghala zilizojengwa zinapatikana katika Wilaya ya Ruangwa Mkoa wa Lindi linalomilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Wilaya ya Tunduru Mkoa wa Ruvuma linalomilikiwa na Chama cha Ushirika cha Umoja Amcos Tunduru na Wilaya ya Kondoa Mkoa wa Dodoma linalomilikiwa na Chama cha Ushirika Pabu, Wilaya ya Babati Mkoa wa Manyara linalomilikiwa na Chama cha Ushirika Rivaku. Kutokana na hatua hizo, Serikali imefanikisha kupunguza upotevu wa mazao baada ya uzalishaji

(post harvest loss), kuongeza uhai wa muda wa matumizi wa bidhaa za kilimo (shelf life) na kuweka mfumo wenye uwazi na rahisi kwa wanunuzi.

35. **Mheshimiwa Spika;** Msimu wa mwaka 2019/2020, Wizara kupitia Bodi ya Stakabadhi za Ghala inayosimamia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala imesajili jumla ya ghala 51 zenye ujazo wa kati ya Mita za Ujazo 300 hadi 10,000. Jumla ya Kilo 240,218,696 zilihifadhiwa kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika Mikoa ya Ruvuma, Pwani, Lindi, Mtwara, Manyara, Mbeya, Shinyanga, Mwanza, Tabora, Songwe, Kilimanjaro na Dodoma (Kiambatisho Na. 3). Juhudi hizo zimesaidia kuongezeka mauzo ya bidhaa kutokana na kukamilika kwa Mfumo wa Mauzo ya Bidhaa kwa Njia ya Kielektroniki wa Soko la Bidhaa Tanzania (TMX). Jumla ya tani 519.89 zimeuzwa kupitia Mfumo huo. Kati ya hizo, tani 431.481 ziliuzwa Wilayani Kondo, Mkoa wa Dodoma wakati tani 88.41 ziliuzwa Wilaya ya Babati Mkoa wa Manyara. Aidha, Bodi inatarajia kuongeza mazao ya pamba, mahindi, choroko, kahawa, dengu na mbaazi katika Soko la Bidhaa Tanzania (TMX).

**iii) Kuimarisha Mifumo ya Uzalishaji na Masoko**

36. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali likiwemo Soko la Bidhaa Tanzania (TMX), Bodi ya Kahawa, Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Vyama vya Ushirika imefanikisha kuweka mifumo madhubuti ya uzalishaji na upatikanaji wa masoko ya bidhaa za kilimo. Vyama vya Ushirika vilivyoshirikishwa ni pamoja na vyama vya Ushirika vya: Kagera (KCU); Karagwe (KDCU); na Ngara (NCU). Aidha, wadau hao wamesaidia kuongeza uwazi na ushindani wa soko ambao umeendelea kuimarisha bei za mazao na kuleta manufaa kwa wakulima.

**iv) Vituo vya Mipakani**

37. **Mheshimiwa Spika;** Tanzania imeendelea kutumia fursa yake ya kijiografia (strategic geographical location) kupanua wigo wa fursa za biashara na masoko

kati ya Tanzania na nchi jirani. Katika kutekeleza jukumu hilo, Serikali imewezesha kuanzishwa kwa vituo 8. Vituo hivyo ni: Holili/Taveta (Tanzania na Kenya); Sirari/Isebania (Tanzania na Kenya); Namanga/Namanga (Tanzania na Kenya); Kabanga/Kobero (Tanzania na Burundi); Rusumo/Rusumo (Tanzania na Rwanda); Mutukula/Mtukula (Tanzania na Uganda); Horohoro/Lungalunga (Tanzania na Kenya); na Kituo cha Tunduma/Nakonde (Tanzania na Zambia). Aidha, kituo kimoja kipya cha Kasumulo/Songwe (Tanzania na Malawi) kipo katika hatua ya ujenzi ambapo kikikamilika kitahudumia mpaka kati ya Tanzania na Malawi.

**vi) Mfumo wa Usajili wa Shughuli za Biashara kwa Njia ya Mtandao**

38. **Mheshimiwa Spika;** Wizara imefanikisha kuongezeka kwa uanzishwaji na ufanyaji biashara nchini kutokana na kurahisishwa kwa taratibu za kusajili biashara nchini. Hatua ambazo Serikali imechukua ni kuboresha na kuimarisha matumizi ya Mfumo wa Usajili wa Majina ya Biashara, Makampuni, Alama za Biashara na Huduma, Hataza, Leseni za Viwanda na Leseni za Biashara kwa njia ya mtandao (Online Registration System-ORS) kupitia tovuti ya BRELA ([www.brela.go.tz](http://www.brela.go.tz)), na Dirisha la Taifa la Biashara (National Business Portal - NBP). Hadi kufikia Machi, 2020, Wakala imesajili Makampuni 7,549, Majina ya Biashara 12,627, Alama za Biashara na Huduma 1,970, Hataza 55, Leseni za Viwanda 200 na Leseni za Biashara 9,927.

**v) Kuhuisha Soko la Biashara ya Zao la Tumbaku**

39. **Mheshimiwa Spika;** Wizara imefanikiwa kuhuisha soko la zao la Sekta ya Tumbaku baada ya Serikali kufikia muafaka na wanunuzi wakuu wa zao hilo kuhusiana na madai ya ukiukwaji wa taratibu za ushindani. Hadi sasa kampuni ya JTI Leaf Services Limited katika Mpango wake wa ununuzi imethibitisha kununua tumbaku yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 12.6 kwa mwaka 2019/2020, Dola za Marekani milioni 14.1 kwa mwaka 2020/2021, Dola za Marekani milioni 15 kwa mwaka 2021/2022 na Dola za

Marekani milioni 15.5 kwa mwaka 2022/2023. Wizara kupitia Tume ya Ushindani (FCC) imeendelea kufanyia kazi jumla ya mashauri tisa (9) yanayohusu makubaliano yanayofifisha ushindani (5), miunganiko ya kampuni yaliyofanyika bila kutoa taarifa kwa Tume (2), makubaliano ya siri (1) na matumizi mabaya ya nguvu (abuse of dominance) (1). Katika mashauri yanahusu makubaliano yanayofifisha ushindani (Anti-Competitive Agreements) kutoka katika sekta ndogo ya Tumbaku, Tume imeendelea kufanya majadiliano na mmoja wa watuhumiwa aliyepomba kumalizika kwa shauri lake kwa njia ya suluhu (settlement proceeding). Aidha, Tume inaendelea kufanya uchambuzi wa utetezi wa kimaandishi wa watuhumiwa katika mashauri yaliyobaki katika mashauri yanayohusu matumizi mabaya ya nguvu za soko (Abuse of Dominance) kutoka katika Sekta Ndogo za Kufukiza (fumigation) na Sekta ya Saruji, Tume imeandaa rasimu ya maamuzi ya awali (provisional findings) kwa shauri kutoka Sekta Ndogo ya Kufukiza. Tume inaendelea kufanya uchunguzi kwa shauri kutoka Sekta Ndogo ya Saruji.

#### **4. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2019/2020**

##### **4.1. Bajeti Iliyoidhinishwa na Kupokelewa kwa Mwaka 2019/2020**

40. **Mheshimiwa Spika;** Kwa ujumla Sekta ya Viwanda ni Mtambuka ambapo utekelezaji wake hutegemea sekta nyingine za uzalishaji wa malighafi kama Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Pia, Sekta zinazosimamia upatikanaji wa miundombinu wezeshi kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda kama vile Sekta za: Ujenzi; Nishati; Maji; na Usafirishaji. Kutokana na umuhimu wa Sekta hizo katika kuendeleza na kukuza Sekta ya Viwanda Nchini, Serikali katika kipindi cha miaka mitano imewekeza rasilimali nyingi katika sekta hizo ikiwa ni jitihada za kuweka msingi bora wa kuendeleza Sekta ya Viwanda nchini.

41. **Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka 2019/2020, Wizara (Fungu 44 & 60) iliidhinishwa matumizi ya jumla ya

Shilingi 100,384,738,648. Kati ya hizo, Shilingi 51,500,000,000 ni za Matumizi ya Maendeleo na Shilingi 48,884,738,648 za Matumizi ya Kawaida. Aidha, Wizara iliidhiniwa kukusanya jumla ya Shilingi 14,300,000 (inayojumuisha Fungu 44 Shilingi 5,300,000 na Fungu 60 Shilingi 9,000,000) kutokana na uzaji wa nyaraka za zabuni na marejesho ya mishahara endapo mtumishi ataacha kazi. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2020, Wizara haikufanikiwa kukusanya kiasi chochote kutoka vyanzo hivyo. Pia, hadi kufikia mwezi Machi, 2020, Wizara ilipokea jumla ya Shilingi 33,812,276,737.40 ambazo ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Aidha, Wizara haikupata fedha kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

## **4.2. Utekelezaji wa Malengo ya Bajeti kwa Mwaka 2019/2020**

### **4.2.1. Sekta ya Viwanda**

#### ***i) Usajili wa Viwanda Vipya***

42. ***Mheshimiwa Spika***; Katika mwaka 2019/2020, jumla miradi mipya 303 imesajiliwa. Kati ya hiyo, miradi 95 ilisajiliwa chini ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), leseni za viwanda 177 (vikubwa 138 na vidogo 39) zilitolewa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) pamoja na viwanda 25 vilivyopewa leseni za muda vimepewa leseni za kudumu na miradi sita (6) ilisajiliwa chini ya Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Kuzalisha Bidhaa kwa Mauzo ya Nje (EPZA).

#### ***ii) Ulinzi wa Viwanda vya Ndani***

43. ***Mheshimiwa Spika***; Serikali imeendelea kuvilinda viwanda vya ndani kwa kuhakikisha vinapata malighafi ya kutosha kwa kutoza ushuru mkubwa, kuweka katazo kwa baadhi ya malighafi kwenda nje ya nchi na kutoa vibali maalum kwa baadhi ya bidhaa. Kwa mfano, Serikali imeweka:- Ushuru mkubwa kwenye malighafi ya ngozi, korosho, mafuta ghafi ya kula na mchuzi wa zabibu; Katazo kwa baadhi ya malighafi kwenda nje ya nchi kama vile chuma chakavu (steel scrap metal); na vibali maalum kwa

maziwa ya mtindi, sukari na clinker. Lengo la jitihada hizo ni kuhamasisha uwekezaji kwenye Sekta ya Viwanda vinavyozalisha ajira nyingi katika mnyororo mzima wa thamani. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (Tanzania Revenue Authority-TRA), na vyombo vya ulinzi na usalama vinahakikisha kuwa bidhaa zinazolingia nchini zinalipa ushuru stahiki ili kuwa na ushindani ulio wa haki sokoni. Hii ni pamoja na kuimarisha ulinzi wa mipaka yetu ili kuhakikisha kuwa hakuna bidhaa zinazopita njia za panya.

44. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia Taasisi zake, imekuwa ikichukua hatua kadhaa katika kulinda viwanda na wafanyabiashara nchini. Kwanza, kuhakikisha kuwa bidhaa zinazolingizwa nchini zinakidhi viwango vya ubora. Bidhaa ambazo hazikidhi viwango hurudishwa au kuteketezwa kulingana na taratibu za kisheria. Pili, kulinda alama na nembo za bidhaa dhidi ya wafanyabiashara wadanganyifu wanaogushi au kutumia bila ridhaa ya mmiliki. FCC, kupitia Sheria ya Ushindani 2003, wanazuia mienendo na vitendo vinavyofifisha ushindani katika soko na hivyo, kuwapa wenye viwanda na Sekta Binafsi kwa ujumla imani ya kuwekeza na kufanya biashara zao bila kuathirika na wafanyabiashara wadanganyifu. Tatu, kutoza kodi kwenye bidhaa zinazolingizwa nchini katika kiwango cha asilimia 10 kwa bidhaa ghafi na asilimia 25 kwa bidhaa zilizo tayari kutumiwa na mlaji. Aidha, viwango hivi vinaweza kutozwa kwa asilimia zaidi ya 25 kulingana na umuhimu wa bidhaa husika.

**iii) Undelezaji wa Viwanda Vilivyo binafsishwa**

45. **Mheshimiwa Spika;** Katika kufuatilia viwanda vilivyobinafsishwa, Wizara kwa kushirikiana na Msajili wa Hazina imekuwaikifuatilia utendaji kazi katika viwanda vilivyobinafsishwa ambapo kati ya viwanda 156 na Shirika moja vilivyofanyiwa tathmini, viwanda 88 vinafanya kazi na viwanda 68 havifanyi kazi. Kati ya viwanda 68 ambavyo havifanyi kazi, viwanda vitatu vimefanyiwa

maboresho ili kuendelea na uzalishaji; viwanda 30 vinakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo; ukosefu wa mitaji ya uendeshaji; uchakavu wa mitambo na mashine; uchakavu wa majengo ya viwanda; uvamizi wa maeneo ya viwanda kutoka kwa jamii inayozunguka viwanda; na matumizi ya teknolojia zilizopitwa na wakati. Serikali inaendelea kuvifuatilia viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo vilikuwa havifanyi kazi vizuri na vinahusu mazao ya kimkakati (mfano Kiwanda cha Chai Mponde) ili viweze kuzalisha kwa tija. Aidha, tararibu za kisheria za utwaaji rasmi wa viwanda ambavyo vimetelekezwa bila kuendelezwa kwa muda mrefu zinaendelelea ili viweze kutangazwa tena kwa ajili ya uwekezaji na kuendelea kuzalisha.

**iv) Uendelezaji wa Viwanda ambavyo Havikubinafsishwa**

46. **Mheshimiwa Spika;** Viwanda 7 ambavyo havikubinafsishwa kutokana na sababu mbalimbali vimeendelea kuwa mali ya umma chini ya Msajili wa Hazina. Aidha, kati ya viwanda vinne vilivyokabidhiwa kwa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, viwanda vitatu (3) katika mikoa ya Iringa, Arusha na Dodoma. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina inaendelea kutafuta wawekezaji wapya wenye nia ya kuwekeza kwa maslahi mapana ya maendeleo ya nchi yetu.

**v) Uendelezaji wa Viwanda Vinavyomilikiwa na Serikali**

**a) Kiwanda cha Viuadudu Kibaha**

47. **Mheshimiwa Spika;** Serikali inamiliki Kiwanda cha Viuadudu cha Kibaha kwa asilimia 100 kupitia Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC). Kiwanda hicho kina uwezo wa kutengeneza lita milioni 6 za dawa ya viuadudu aina ya Bactivec na Griselef kwa mwaka. Hadi sasa, Kiwanda kimetengeneza lita 677,000 za viuadudu kwa ajili ya kuua viluilui wa aina mbalimbali za mbu hususan wanaoeneza Malaria. Kiwanda hicho ni mahsusi kwa ajili ya kuunga mkono



jitihada za kupambana na ugonjwa wa Malaria nchini. Aidha, Kiwanda kimefanya mauzo ya dawa za viuadudu kwa soko la ndani na nje ambapo, Ofisi ya Rais- TAMISEMI kupitia Halmashauri mbalimbali nchini zimekuwa zikinunua dawa kutoka kiwandani kwa nyakati tofauti. Vilevile, nchi za SADC mfano, Angola zimenunua lita 106,000. Hivyo, jumla ya mauzo ya ndani na nje ni takribani lita 500,000. Hata hivyo, Kiwanda kinaendelea na uzalishaji wa dawa kadri ya mahitaji yanavyojitokeza. Hivi karibuni kiwanda kimeingia mkataba wa kuuza Lita 45,785.67 za viuadudu nchini Kenya, zenye thamani ya Dola za Marekani 231,619.44. Sambamba na hilo, NDC kwa kushirikiana na wadau mbalimbali linaendelea kukisaidia Kiwanda kukamilisha taratibu za usajili wa dawa ya kibaiolojia kwa ajili ya kuuza wadudu waharibifu kwenye zao la pamba ili kupanua wigo wa kibiashara.

**b) Mradi wa Matrekta Aina ya URSUS**

48. **Mheshimiwa Spika;** NDC imeendelea kuunganisha matrekta aina ya URSUS na zana zake na ujenzi wa kiwanda kipya cha kuunganisha matrekta katika eneo la TAMCO Kibaha. Hadi kufikia Machi, 2020 jumla ya matrekta 822 yalikuwa yamepokelewa kutoka nchini Poland na kuunganishwa. Kati ya hayo, matrekta 724, majembe ya kulimia 511 na majembe ya kusawazisha 233 yalikuwa yameuzwa katika mikoa mbalimbali nchini. Hivi sasa, ujenzi wa jengo jipya la kiwanda umekamilika na kazi inayotarajiwa kufanyika ni ufungaji wa mitambo mara baada ya kutolewa bandarini.

**vi) Uendelezaji wa Maeneo Maalum ya Uwekezaji**

49. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia Mamlaka ya EPZ imeendelea kusimamia uendelezaji wa eneo la Kurasini Trade and Logistic Centre ambapo imefanikiwa kupata Hati Miliki ya eneo la Mradi mwezi Desemba, 2019. EPZA imepokea mahitaji (specifications) kutoka Bodi ya Chai (TBT), Bodi ya Kahawa (TCB), Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) kwa ajili ya uwekezaji ambao utakidhi uendeshaji wa

shughuli za kuchakata, kufungasha na kuhifadhi mazao ya kilimo kwa ajili ya mauzo kwenda nchi za nje. Usimamizi wa uendelezaji wa Mradi utaendelea kufanyika kulingana na upatikanaji wa fedha.

50. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia Mamlaka ya EPZ imekua ikihamasisha ushiriki wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika uendelezaji wa Maeneo ya SEZ ili kuiwezesha Mikoa husika kutumia Maeneo ya SEZ kama chanzo cha mapato na mbinu mojawapo ya kuchochea shughuli za kiuchumi katika mikoa husika. Katika Mkakati huo, Mikoa imekua ikihamasishwa kushiriki katika kutenga, kumiliki na kuendeleza maeneo ya SEZ kupitia mafunzo ya uendelezaji wa Maeneo Maalum ya Kiuchumi yanayotolewa na EPZA. Hadi sasa, mafanikio yamepatikana katika mikoa ya Arusha, Geita, Mwanza, Kigoma na Songwe ambayo imekwisha pokea mafunzo na imetenga maeneo yatakayoendelezwa kama Maeneo Maalum ya Kiuchumi.

51. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia Mamlaka ya EPZ imeendelea na juhudi za kusimamia maendeleo ya SEZ. Mara baada ya eneo kuwa limeendelezwa, shughuli kubwa ya usimamizi inahusisha jukumu la kuhamasisha uwekezaji katika maeneo ya SEZ ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje. Uhamasishaji huo umechochea na kuvutia uwekezaji na usajili wa leseni za uwekezaji ambapo katika kipindi cha mwaka 2019/2020 EPZA imesajili kampuni sita. Ongezeko hilo limewezesha jumla ya uwekezaji uliopo katika viwanda vilivyo chini ya EPZA kuongezeka kutoka viwanda 163 hadi viwanda 169 vikichangia ongezeko la mtaji unaokadiriwa kutoka Dola za Marekani Bilioni 2.353 hadi Dola za Marekani Bilioni 2.379. Mauzo ya nje yanakadiriwa kuongezeka kutoka Dola za Marekani Bilioni 2.247 hadi takriban Dola za Marekani Bilioni 2.266 na fursa za ajira za moja kwa moja kutoka 56,442 hadi 57,342.

**vii) Kutoa Huduma za Kitaalam Viwandani**

52. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia TIRDO imeendelea kuwa Mshauri Elekezi katika mradi wa ujenzi wa

kiwanda kikubwa cha Karanga Leather Industries kilichopo Moshi cha kuzalisha bidhaa za ngozi kama vile; viatu, mikanda, soli za viatu, mikoba, mabegi na mipira ya ngozi pamoja na kuongeza thamani katika ngozi kwa ajili ya uuzwaji nje ya nchi. Kiwanda hicho cha ubia kati ya PSSSF na Jeshi la Magereza kitakuwa na uwezo wa kuzalisha jozi za viatu 2,800 kwa siku kwa mwaka wa kwanza hadi kufikia jozi 8,000 kwa siku baada ya miaka mitano. Katika awamu ya kwanza ujenzi wa Kiwanda umefikia asilimia 94. Pia, TIRDO imeendelea kuwa Mshauri Elekezi katika ujenzi wa kiwanda cha vifaa tiba kutokana na zao la pamba kitakachojengwa katika Mmkoa wa Simiyu kwa uwekezaji wa NHIF na WCF.

53. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia TIRDO imefanikiwa kuhakiki ubora wa sampuli za bidhaa mbalimbali za chakula na maji zipatazo 174 kutoka viwandani, wajasiriamali na kampuni mbalimbali hapa nchini. Viwanda hivyo ni pamoja na Masasi Food Industries, Kilimanjaro Natureripe, Darsh Company, Njombe Vegetable processing facility. Taasisi za kiserikali kama Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) pia wameweza kuhudumiwa na maabara hiyo. Vilevile, wazalishaji wa bidhaa za mifugo kama vile Kiliagro & Livestock Products na Rulenge Agricultural Products Co Ltd wameweza kuhakikiwa bidhaa zao za nyama ya kuku na nguruwe kwa ajili ya kupata uhakika wa ubora. Aidha, TIRDO imefanikiwa kutoa mafunzo ya uzalishaji chumvi yenye ubora unaokidhi viwango vya ubora vya nchi yetu na vya kimataifa kwa wazalishaji wa chumvi wa jumuiya ya uzalishaji na mashamba ya chumvi Wawi- Pemba.

54. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia TIRDO, imefanikiwa kutoa huduma za ukaguzi wa mazingira ili kupunguza uharibifu wa mazingira katika viwanda vinavyozalisha bidhaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na upimaji wa kiwango cha uchafuzi wa hewa, maji, udongo na kubaini kelele hatarishi. Viwanda na taasisi zilizopata huduma hizo ni pamoja na Kilimanjaro Biochem Ltd, Serengeti Breweries Ltd, Huatan Investment, na TANESCO (Mtwara Gas Power

Plant pamoja na Kinyerezi Gas Power Plant). Vilevile, Viwanja vya Ndege vya Arusha na Bukoba vilinufaika na huduma hizo.

55. **Mheshimiwa Spika;** Katika kuendelea kuvisaidia viwanda na mamlaka za maji kupunguza gharama za uendeshaji kupitia ufanisi wa matumizi ya nishati ya umeme, Wizara kupitia TIRDO imetoa ushauri kupitia tathmini za matumizi ya nishati. Kwa mfano, Mamlaka ya Maji Safi na Taka ya Tanga walipatiwa huduma hiyo. Aidha, majadiliano yanaendelea na Mamlaka ya Maji Safi na Taka ya Chalinze ili kuwapatia huduma hiyo.

**viii) Uendelezaji wa Teknolojia na Utafiti**

56. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia TIRDO imebuni na kutengeneza mashine kwa ajili ya kiwanda cha mfano cha kubangua korosho chenye uwezo wa kubangua kilo 300 kwa saa. Hadi sasa, tayari mashine imekamilika kwa asilimia 88. Lengo la Serikali ni kuhakikisha inabangua kiasi kikubwa cha korosho hapa nchini ili kutoa ajira nyingi kwa wananchi na kuhakikisha malighafi zinaongezewa thamani kabla ya kuuzwa nje ya nchi. Vilevile, TIRDO imebuni na kutengeneza mashine kwa ajili ya kiwanda cha mfano cha kuchakata mawese ambapo hadi sasa kazi zilizofanyika kama ifuatavyo: Kufanya tathmini ya malighafi iliyopo Mkoa wa Kigoma, kubaini ubora wa mawese yanayozalishwa, kubaini teknolojia inayotumika kwa sasa na teknolojia mpya inayohitajika na kununua mashine moja ya mfano kwa ajili ya kuifanyia utafiti utakaowezesha kuanza kutengeneza hapa nchini. TIRDO pia inatekeleza mradi wa ubunifu na usambazaji wa vitofali lishe vya kuzalishia uyoga wenye virutubisho (mushroom substrate blocks).

57. **Mheshimiwa Spika;** Kituo cha CAMARTEC kimeendelea kushirikiana na Intermech Engineering katika utafiti na ubunifu wa kipandio kinachovutwa na trekta la magurudumu mawili (power tiller). Katika ushirikiano huo, CAMARTEC imefanya majaribio ya kipandio hicho na kuainisha maeneo yanayohitaji kufanyiwa maboresho. Hadi sasa, CAMARTEC inaendelea kuandaa mpango wa kufanya

majaribio na maboresho ya teknolojia nyingine. Pia, CAMARTEC imefanikiwa kubuni na kuunda sampuli kifani (Prototypes) na uzalishaji wa mashine kwa ajili ya wateja. Mashine zilizotengenezwa ni Mashine ya kupura na kupepeta alizeti (3); Mashine ya kupukuchua mahindi (2); Mashine ya kupandia (11); Mashine ya kukata majani ya kulisha mifugo iendeshwayo kwa umeme (5); Mashine za kupura mazao mchanganyiko (3); Mashine ya kusaga karanga (1); na Mashine za kufyatua matofali ya udongo saruji.

58. **Mheshimiwa Spika;** Kituo cha CAMARTEC kimekamilisha Mradi wa ujenzi wa mtambo wa biogesi wenye mita za ujazo 45 katika Shule ya Genezareth iliyoko Kinyamwenda Singida. Mradi huo unakusudiwa kuzalisha nishati safi ya kupikia, mbolea hai kwa matumizi ya kuotesha mazao shambani kwa ajili ya matumizi ya shule na pia kusaidia kutibu taka zinazozalishwa chooni. Aidha, Kituo kimekamilisha zoezi la uhakiki wa mitambo ya biogesi iliyoripotiwa kujengwa wakati wa utekelezaji wa Programu ya Uenezi wa mitambo ya Biogesi kwa Ngazi ya Kaya Tanzania (TDBP). Zoezi linahusisha mitambo iliyojengwa chini ya Programu ikiwa ni mtekelezaji na pia Watekelezaji Wenza (IPs) wengine watano (5). Katika mwaka 2019/2020, jumla ya mitambo 259 ya TDBP na mitambo 817 ya watekelezaji wenza wa TDBP ilikuwa imehakikiwa.

59. **Mheshimiwa Spika;** Kituo cha CAMARTEC kimekamilisha awamu ya tatu ya mafunzo ya ujasiriamali katika Biogesi kwa wanawake vijana 100 wa jamii za kifugaji kutoka Wilayani Ngorongoro. Mafunzo hayo yamejumuisha Biashara katika Sekta ya Biogesi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mitambo ya biogesi na matumizi ya mbolea hai (bioslurry) inayotoka kwenye mtambo wa biogesi. Pia, Kituo kilitoa mafunzo kwa vitendo kwa wakulima kuhusu teknolojia za kukata na kufunga majani ya malisho ya mifugo zinavyofanya kazi katika Halmashauri ya Meru Wilaya ya Arumeru. Aidha, wakulima zaidi ya 15 wa Mbozi, Mkoani Songwe walielimishwa namna ya kutumia kipandio (Planter) kikubwa cha mazao mbalimbali kinachovutwa na trekta.

60. **Mheshimiwa Spika;** Kituo cha CAMARTEC kimefanya ukarabati wa mitambo ya biogesi iliyojengwa chini ya ufadhili wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) katika Shule ya St. Bakanja Wilayani Buhigwe, Kigoma na Shule ya Queen of Apostles Wilayani Ushirombo, Mkoani Geita umefanyika na mitambo inafanya kazi vizuri. Aidha, Kituo kimefanya tathimini ya kazi ya marekebisho ya mitambo ya biogesi na mifumo yake yanayohitajika kufanyika kwenye Mradi wa REA kwa maeneo ya Kambi ya JKT Mlale Songea- Ruvuma na Gereza la Namajani lililoko Masasi – Mtwara na kuwasilisha taarifa REA kwa hatua stahiki.

61. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia TEMDO imeweza kusanifu uundaji wa mtambo wa kuchakata na kukausha muhogo ambapo mpaka sasa asilimia 40 ya utengenezaji na uundaji wa mashine imekamilika.

**ix) Uendelezaji wa Miradi ya Kimkakati na ya Kielelezo**

62. **Mheshimiwa Spika;** Mradi wa Eneo Maalum la Kiuchumi Bagamoyo (Bagamoyo Special Economic Zone Project) ni mradi wa kielelezo wa Taifa kwa mujibu wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2nd FYDP). Kimkakati, mradi unaojumuisha uendelezaji wa eneo la Bandari (Sea Port) kwenye eneo la Hekta 800 na Uendelezaji wa Eneo Maalum la Viwanda (Portside Industrial Zone) kwenye eneo la Hekta 9000. Mradi wa Eneo Maalum la Viwanda litaendelezwa kwa kuhusisha uendelezaji wa eneo la viwanda na uendelezaji wa Kituo cha kisasa cha Technolojia (High Technology Park).

63. **Mheshimiwa Spika;** Katika eneo la Viwanda, Mamlaka ya EPZA imetoa leseni kwa jumla ya Makampuni kumi na moja ili kufanya uwekezaji. Hadi kufikia mwezi Februari 2020, makampuni mawili (Africa Dragon Enterprises Limited na Phiss Tannery Limited) yameanza uzalishaji na makampuni mengine yapo kwenye hatua mbalimbali za uendelezaji. Mchango unaotarajiwa kutokana na makampuni hayo ni kuwekeza mtaji unaokadiriwa kuwa na

thamani ya Dola za Kimarekani Milioni 67.34, ajira za moja kwa moja 1,651 na mauzo ya nje yanakadiriwa kuwa Dola za Kimarekani milioni 78.56 kwa mwaka. Aidha, Kampuni moja kati ya mawili yaliyoanza uzalishaji (African Dragon Limited), imeshachangia kodi ya Shilingi bilioni 9.86 katika kipindi cha miaka mitatu (2017 – 2019).

64. **Mheshimiwa Spika;** Katika eneo la mradi wa Kituo cha kisasa cha Technolojia (High Technology Park) kwenye eneo la Bagamoyo SEZ, Mamlaka ya EPZ imeingia mkataba wa ushirikiano na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kuendeleza mradi huu katika eneo la hekta 175. Aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya EPZ inashirikiana na Serikali ya Korea Kusini kupitia program ya 'KSP- Knowledge Sharing Program', inayoratibiwa na Korea Exim Bank yenye lengo la kufadhili uendelezaji wa miundombinu ya mradi.

65. **Mheshimiwa Spika;** Kwa msingi huo, Mradi wa Bagamoyo SEZ unaendelea kutekelezwa katika maeneo ya Eneo Maalum la Viwanda (Portside Industrial Zone) na Kituo cha kisasa cha Technolojia (High Technology Park). Aidha, kuhusu eneo la Bandari (Sea Port), Wawekezaji waliojitokeza wa Kampuni ya Merchants Port Holdings Company Limited (CMPort) ya China na Mfuko wa Hifadhi ya Hazina wa Serikali ya Oman - State General Reserve Fund-SGRF, walishaanza majadiliano na kukubaliana katika baadhi ya masuala. Hata hivyo, kuna masuala kadhaa ambayo Serikali imeweka msimamo wake na unahitaji maamuzi ya mwekezaji ili majadiliano yaweze kuendelea.

66. **Mheshimiwa Spika,** vilevile, Serikali imejielekeza katika kutekeleza Mradi wa chuma cha Liganga na makaa ya mawe ya Mchuchuma. Aidha, tafiti mbalimbali zilibainisha aina ya madini ya chuma (Magnetite Iron Ore) katika mwamba wa Liganga yanahitaji teknolojia maalum ya kuchenjua chuma na mchanganyiko wa madini mengine yakiwepo Vanadium na Titanium ambayo yana thamani kubwa. Mwaka 2010, mwekezaji Sichuan Hangda Group Ltd alipatikana na kuingia Mkataba wa Ubia na Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC). Serikali inaangalia njia bora ya

kuwezesha mradi huo kutekelezwa ikiwa ni pamoja na kurejea mikataba ya uwekezaji kwa kuzingatia Sheria Na. 5 ya Mamlaka ya Nchi ya Uangalizi wa Utajiri wa Asili ya mwaka 2017 na Sheria Na. 6 ya Mamlaka ya Nchi juu ya Majadiliano ya Mikataba yenye Masharti hasi ili uwekezaji huo uwe na maslahi mapana kwa nchi.

67. **Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka 2019/2020, Wizara kupitia TIRDO inaendelea kufanya "Techno Economic Study" katika Mradi wa Magadi Soda Engaruka. Lengo la utafiti huo ni kubainisha kiasi cha mahitaji ya magadi nchini, thamani ya uwekezaji utakaofanyika na faida za mradi huo kwa ujumla. Makadirio ya awali ya rasilimali magadi (brine) yameonesha uwepo wa kiasi cha mita za ujazo Biloni 4.68. Aidha, ilibanika kuwa rasilimali hiyo inajiongeza kwa kiasi cha mita za ujazo wa milioni 1.9 kwa mwaka. Uhakiki wa rasilimali hii unaendelea sambamba na ukamilishaji wa upembuzi yakinifu wa mradi na athari ya mradi katika mazingira na jamii. Utafiti huo unategemewa kukamilika mwisho mwa mwezi Aprili, 2020.

68. **Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka 2019/2020 Wizara kupitia NDC imekamilisha upimaji wa eneo la TAMCO. Jumla ya ekari 201.04 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda na miundombinu. Kati ya hizo, ekari 43.04 kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya kutengeneza madawa ya binadamu; Ekari 55 kwa ajili ya viwanda vya kuunganisha magari; Ekari 94 kwa ajili ya viwanda vya nguo na mavazi; na Ekari 9 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika eneo hilo.

#### ***x) Mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Viwanda***

69. **Mheshimiwa Spika;** Mapitio ya Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda (SIDP, 1996- 2020) yanaendelea na tayari Wizara imekamilisha Tathmini na mapitio ya Awali ya Sera hiyo. Kwa sasa Wizara ipo katika hatua ya kuchambua wasilisho hilo ili kuwezesha hatua za tathmini za kina na uchambuzi ili hatimaye kumwezesha Mshauri Mwelekezi kukamilisha uandishi wa Research



Background Paper na hivyo kuwezesha maandalizi ya rasimu ya Sera na Mkakati wake. Utaratibu huo unalenga kuleta ufanisi na kuwa na uratibu unaozingatia mfumo wenye mwongozo wa usimamiaji wa utungaji sera Serikalini. Sera hiyo inategemewa kukamilishwa ndani ya mwaka 2020.

***xi) Utekelezaji wa Mikakati Mbalimbali ya Uendelezaji Viwanda Nchini***

70. ***Mheshimiwa Spika;*** Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Ngozi wa mwaka 2016- 2020 umejikita katika kuendeleza mnyororo wa thamani wa zao la Ngozi. Katika kutekeleza mkakati huo, Serikali imetoa msamaha wa ushuru wa forodha kwenye malighafi na vifaa vinavyotumika kutengenezea viatu na bidhaa za ngozi vinavyoingizwa kutoka nje ya nchi. Lengo likiwa ni kupunguza gharama za uzalishaji kwa viwanda vya ngozi na kuvutia uwekezaji. Fursa hiyo imetumiwa na kiwanda cha Karanga Leather Industries ambacho hivi karibuni kimeingiza mashine na vifuasi (accessories). Vilevile, Kiwanda cha ACE leather Morogoro kimetumia fursa hiyo kuingiza mashine na vifuasi ili kusindika ngozi hadi hatua ya mwisho. Mkakati huo pia umehamashisha taasisi za umma na shule kununua bidhaa za ngozi hususan viatu kutoka viwanda vya ndani kulingana na upatikanaji. Kwa sasa maandalizi ya kuhuisha mkakati huo yanaendelea.

71. ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Mafuta ya Alizeti wa mwaka 2016-2020, Wizara kupitia TEMDO imeweza kutengeneza mtambo(prototype) wa kukamua mafuta (Oil refinery Machine). Hadi sasa mtambo huo umefanyiwa majaribio ya mwisho ili kutengenezwa na kuwapa wadau kama vile SIDO watakaoweza kutengeneza mitambo mingi kibiashara (commercialization). Pia, TEMDO imeendelea kutengeneza kwa majaribio teknolojia zilizokwisha hakikiwa na kusambaza teknolojia /mashine ya kukamua mbegu za alizeti kwa wajasiriamali (Sunflower seeds pressing machine/Oil expelling machine).

72. **Mheshimiwa Spika;** CAMARTEC imeendelea na utaratibu wa kuhaulisha mashine ya kupura na kupepeta alizeti kwa wajasiriamali wadogo. Lengo ni kuwezesha teknolojia hizo kusambazwa kwa wakulima pamoja na kuwezesha upatikanaji wake kirahisi katika maeneo ambayo zao la alizeti linalimwa kwa wingi hapa nchini. Kwa sasa, Wizara imeanza maandalizi ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa mkakati huo ambao unafikia ukomo mwaka 2020.

73. **Mheshimiwa Spika;** Mkakati wa Pamba hadi Mavazi wa mwaka 2016-2020 unalenga uongezaji thamani zao la pamba hadi mavazi unaochochea uanzishwaji wa viwanda vya nguo na mavazi na vinavyotoa huduma (auxiliary industries). Viwanda hivyo ni pamoja na viwanda vya kutengeneza vifungo, lebo na zipu. Hivi sasa, Wizara imeanza hatua za uhuishaji wa Mkakati huo ambao utekelezaji wake unaishia mwezi Juni, 2020. Katika hatua hizo, mwezi Julai, 2019 Wizara ilifanya tathmini ya sekta hiyo na kubaini kuwa inakabiliwa changamoto mbalimbali zikiwemo tija ndogo katika uzalishaji wa pamba nchini, na teknolojia hafifu katika utengenezaji wa bidhaa mwambata zinazoweza kuzalishwa kutokana na uchambuzi wa pamba mbegu. Tathmini hiyo ni msingi wa kufanya marejeo ya Mkakati huo.

**xii) Uendelezaji wa Sekta Ndogo ya Mafuta ya Mawese**

74. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na wataalam kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuendeleza Viwanda (UNIDO) na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) ilifanya uchambuzi wa mnyororo mzima wa zao la mchikichi. Lengo lilikuwa kubaini changamoto zinazokabili zao hilo, kupendekeza suluhisho na kuwezesha kuchangia katika upatikanaji wa mafuta ya kula nchini. Pamoja na uchambuzi huo, Wizara kupitia taasisi zake za utafiti wa viwanda (TIRDO, CAMARTEC, TEMDO) na SIDO zilifanya uchambuzi zaidi na kuandaa maandiko (concept papers) ya teknolojia rahisi ya kuchakata chikichi.

**xiii) Uongezaji Tija na Ufanisi wa Uzalishaji katika Viwanda**

75. **Mheshimiwa Spika;** Katika kuimarisha uratibu wa shughuli za KAIZEN, Wizara iliandaa na kukamilisha miongozo ya kufundishia na kutoa huduma za KAIZEN kwa ufanisi (KAIZEN Consultancy Services & KAIZEN Technical Guideline). Miongozo hiyo inasaidia kudhibiti ubora wa huduma za KAIZEN zinazofikishwa kwa walengwa. Vilevile, Wizara ilikamilisha maandalizi ya Mpango wa Taifa wa kueneza falsafa ya KAIZEN Nchini (Framework for Quality and Productivity Improvement (KAIZEN) in Manufacturing Sector – FKM, 2020- 2030). Mbali na kueneza KAIZEN nchini, mpango huo unahamasisha pia kuoanishwa kwa KAIZEN kwenye uendelezaji wa Kongano za Viwanda ili ziweze kuhimili ushindani.

76. **Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha mwaka 2019/2020, Wizara imeendesha mafunzo ya uongezaji endelevu wa tija na ubora kwa kutumia falsafa ya KAIZEN. Juhudi hizo ziliwezesha kuongeza idadi ya wakufunzi kutoka 91 hadi 130 watakaosaidia kueneza falsafa hiyo viwandani. Lengo ni kuwezesha viwanda vilivyoko nchini na vile vitakavyoanzishwa viwe na ukuaji endelevu. Aidha, zaidi ya viwanda 102 (asilimia 25 Viwanda vikubwa na asilimia 75 ni viwanda vidogo) katika mikoa 8 vimenufaika na mafunzo kwa vitendo.

77. **Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka 2019/2020, Wizara ilifanya tathimini ya hali ya utekelezaji wa Mradi wa KAIZEN. Tathimini hiyo ilibaini yafuatayo:- Kubadilika kwa maeneo ya kazi kuwa yenye staha; Kuongezeka kwa ubora na tija kwa bidhaa kwa viwanda vilivyopata mafunzo; Kuokoa muda wa utendaji kazi (lead time reduction); na Kubadilika kwa mtazamo wa watumishi viwandani katika utendaji kazi kuwa mzuri zaidi. Viwanda vilivyofanyiwa mafunzo viliweza kuokoa takribani Shilingi 368,609,000 kwa kutekeleza falsafa ya KAIZEN ipasavyo katika maeneo yao.

78. **Mheshimiwa Spika;** Katika kuhamasisha uenezaji wa falsafa ya KAIZEN nchini, Wizara imeendelea kuratibu Mashindano ya KAIZEN Kitaifa na kushiriki Kimataifa. Katika mashindano ya Kimataifa yaliyofanyika nchini Tunisia mwaka 2019, Tanzania ilipata ushindi wa kwanza kati ya Mataifa 16 yaliyoshiriki. Aidha, katika mashindano ya Kitaifa yaliyofanyika mwezi Februari, 2020 Kiwanda cha Shelly's Pharmaceuticals kilipata ushindi wa kwanza kwa viwanda vikubwa na kwa upande wa viwanda vidogo, Kiwanda cha Tanzania Brush Products Ltd kilipata ushindi wa kwanza. Navipongeza viwanda hivyo kwa ushindi walioupata, ambapo kupitia ushindi huo vitaiwakilisha Tanzania kwenye mashindano ya KAIZEN Barani Afrika yatakayofanyika nchini Afrika Kusini mwezi Septemba, 2020. Juhudi hizo zimeipatia Tanzania fursa ya kuwa mwenyeji wa mashindano ya KAIZEN Barani Afrika kwa mwaka 2021 yatakayohusisha zaidi ya nchi 16. Mashindano hayo yatakuwa ni fursa ya kuvutia wawekezaji, kutangaza vivutio vya utalii na hatimaye kuchangia ukuaji wa uchumi.

*xiv) Hali ya Uzalishaji Bidhaa Viwandani*

**a) Uzalishaji wa Sukari**

79. **Mheshimwa Spika;** Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuwavutia wenye viwanda vya sukari nchini kuwekeza katika kuongeza ukubwa wa mashamba kwa nia ya kuongeza uzalishaji sukari nchini. Hadi sasa, Kiwanda cha Kagera Sugar kina mpango wa kuongeza kilimo cha Miwa hekari 14,000 katika shamba la Kitengule ambapo kiwanda kitaongeza uzalishaji wa Sukari kutoka Tani 80,000 za sasa hadi kufikia Tani 180,000 katika kipindi cha miaka 5 ijayo. Vilevile, Kiwanda cha Mtibwa Sugar hivi sasa kinaendelea na ujenzi wa mabwawa ambapo utakapokamilika kiwanda kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 100,000 kutoka 30,000 zinazozalishwa sasa. Aidha, Kiwanda cha Kilombero Sugar kipo katika majadiliano na Serikali kwa lengo la kuongeza uwezo wa uzalishaji. Kupitia Mpango huo, Kiwanda kitaongeza uzalishaji wa Sukari kupitia wakulima wadogo 'Outgrower Scheme', uzalishaji

unatarajiwa kuongezeka hadi kufikia Tani 265,000 kutoka 120,000 za sasa kwa kipindi cha miaka 5.

80. **Mheshimwa Spika;** ili kuongeza uzalishaji zaidi kwa lengo la kukidhi mahitaji ya ndani na kuuza ziada nje ya nchi, Serikali imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika miradi mipya ya kilimo cha miwa na uzalishaji wa sukari kwa viwanda vikubwa na vidogo. Miradi hiyo ni pamoja: Bagamoyo ambapo kupitia mradi huo tani 35,000 ya Sukari zitazalishwa; na Mradi wa Mkulazi unatarajia kuzalisha tani 50,000. Wawekezaji wengine ambao wapo kwenye hatua ya kuhaulisha maeneo ya ardhi kama vile Nkusu Theo ya Ruvuma na Ray Sugar ya Mtwara. Wawekezaji kutoka Mauritius kwa ajili ya mradi wa shamba uliopo Rifiji hivi sasa wako kwenye mazungumzo na Serikali.

Aidha, Wizara yangu inaendelea kuhamasisha uchakataji wa miwa na kutengeneza sukari kupitia wajasiriamali wadogo na wa kati. Tayari taasisi ya TEMDO inaendelea na kubuni mtambo rahisi kulingana na mazingira yao ili kuwawezesha wajasiriamali hao kuchakata miwa na kutengeneza sukari kwa teknolojia nafuu. Suala hilo litatia chachu jitihada za kukabiliana na tatizo la sukari nchini na kutoa ajira kwa Watanzania kupitia Sekta ya Viwanda Vidogo ambayo kitakwimu ndio inatoa ajira nyingi nchini.

81. **Mheshimiwa Spika;** Makadirio ya uzalishaji wa sukari kwa msimu wa mwaka 2019/2020 yalikuwa tani 345,296 kwa viwanda vya ndani sawa na asilimia 73.46 ya kiasi cha sukari inayokadiriwa kwa matumizi ya kawaida. Aidha, hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 uzalishaji wa sukari nchini, ulikuwa jumla ya tani 298, 949, wakati mahitaji ya sukari kwa mwaka ni wastani wa tani 635,000. Kati ya mahitaji hayo, tani 470,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na tani 165,000 kwa matumizi ya viwandani. Makadirio hayo yametokana na ukweli kwamba kiasi cha mahitaji ya sukari ya matumizi ya kawaida kwa mwezi ni wastani wa tani 38,000.

**b) Uzalishaji Dawa na Vifaa Tiba**

82. **Mheshimiwa Spika;** Sekta ya Viwanda vya Dawa na Vifaa Tiba ina jumla ya viwanda 14 ambapo viwanda 12 vinatengeneza dawa za binadamu, viwanda viwili dawa za mifugo na kiwanda kimoja kinatengeneza vifaa tiba. Wizara ilichukua hatua za makusudi ili kuhakikisha Sekta hiyo inaongeza uwekezaji kwenye Viwanda vya Dawa na Vifaa Tiba ikiwa ni sambamba na kuongeza ufanisi wa viwanda vilivyopo ili kufikia asilimia 60 ya uzalishaji wa Dawa na Vifaa Tiba Nchini ifikapo Mwaka 2025. Hatua hizo ni: Kuunda Kamati ya Kitaifa inayoshughulikia Sekta ya Viwanda vya Dawa na Vifaa Tiba (NPCC); na Kuweka vivutio vya uwekezaji kwa lengo la kuhamasisha wawekezaji wa ndani na Nje ya Nchi (Kiambatisho Na. 4).

83. **Mheshimiwa Spika;** Ili kuvutia wawekezaji katika sekta hiyo, Serikali imefanya yafuatayo: kuondoa VAT kwa vifungashio vya dawa zinazozalishwa nje na ndani ya nchi; kushusha kodi ya mapato kwa asilimia 30 ambayo imesaidia kuhamasisha uwekezaji mpya na upanuzi wa viwanda, kwa muda wa miaka miwili kwa miradi mipya ya viwanda vya dawa; na Kuweka upendeleo maalum kwa ununuzi wa dawa zinazozalishwa na viwanda vya ndani kupitia MSD.

**xv) Jitihada za Wizara katika Vita Dhidi ya COVID-19**

84. **Mheshimiwa Spika;** Katika kukabiliana na janga la ugonjwa wa Covid-19 unaosababisha homa kali ya mapafu, Mwezi Machi 2020, Wizara ilikutana na wazalishaji wa malighafi ya kutengeneza vitakasa mikono (ethanol) na wazalishaji wa bidhaa hizo. Lengo likiwa ni kujadiliana na wenye viwanda pamoja na wadau wengine namna ya kufanikisha utengenezaji na upatikanaji wa vifaa kinga vya kuzuia usambaaji wa ugonjwa huo. Viwanda hivyo vimeitikia wito wa kuunga mkono Serikali katika vita dhidi ya ugonjwa huo. Kwa mfano Kiwanda cha Kilombero Sugar Ltd kinachomilikiwa kwa ubia na Serikali kilichangia jumla ya lita

30,000 za Ethanol kwa ajili ya kutengeneza vitakasa mikono ambapo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilipewa lita 20,000 na kiasi kilichobaki zilipewa Taasisi za SIDO na TIRDO. Mwitikio huo, umeweza kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya kutengeneza barakoa, vitakasa mikono, sabuni za kunawa mikono na disinfectants, ili kuongeza upatikanaji wa bidhaa hizo. Hadi sasa, kuna jumla ya viwanda na taasisi 12 ambazo zinatengeneza vifaa tiba kama Barakoa, Vitakasa mikono na mavazi maalum kwa watoa huduma za afya (Kiambatisho Na 5). Aidha, Viwanda vidogo 55 vya nguo na mavazi pia vimeunga mkono kwa kuanza kutengeneza barakoa kwa kutumia malighafi ya kitambaa. Vivyo hivyo, viwanda vya kutengeneza vitakasa mikono vilivyosajiliwa hadi sasa vimefikia 40.

85. **Mheshimiwa Spika;** Wizara inaendelea kufuatilia maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoyatoa katika kikao chake na wadau wa Sekta Ndogo ya Viwanda vya Dawa na Vifaa Tiba Nchini kilichofanyika Jijini Dar es Salaam mwaka 2018. Katika kutekeleza agizo hilo, wawekezaji 11 wanaendelea na ujenzi wa viwanda vya Dawa na Vifaa Tiba na ujenzi umefikia hatua mbalimbali kama inavyoonekana katika Kiambatisho Na. 6. Lengo la Serikali ni kuokoa fedha ambazo zinatumiwa kuagiza dawa na vifaa tiba hivyo nje ya nchi na hivyo kuendelea kutengeneza ajira hapa nchini. Aidha lengo hilo linakusudia kuhakikisha afya za Watanzania zinakuwa ni suala la kipaombebe wakati wote.

86. **Mheshimiwa Spika;** Vilevile, Wizara kupitia TIRDO imeweza kutengeneza mtambo unaotumika kuzalisha bioethanol inayotokana na zao la muhogo ambayo inafaa kutumika kwa matumizi mbalimbali ya hospitali, viwanda vya pombe na majiko. Kutokana na bioethanol hiyo, TIRDO imeweza kutengeneza kitakasa mikono (sanitizer) ambacho tayari kinatumika kwa wanajamii kwa matumizi ya kujikinga na kuzuia kuenea kwa maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19). Mpaka sasa, TIRDO imeweza kutengeneza lita

202 za vitakasa mikono na kuwafikia watu mbalimbali kwa ajili ya matumizi.

87. **Mheshimiwa Spika;** Wizara inaendelea na kazi ya ufanyaji tathmini ya mahitaji ya vitakasa mikono nchini kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Mkemia Mkuu wa Serikali, Wazalishaji wa Ethanol, TMDA na TPMA. Aidha, kupatikana kwa takwimu halisi kutasaidia Serikali kufanya maamuzi ya haraka hususan ya kuagiza Ethanol ambayo ni malighafi muhimu katika kutengenezea vitakasa mikono.

88. **Mheshimiwa Spika;** Napenda kuchukua nafasi hii kutoa onyo kwa wafanyabiashara wanaotumia mazingira ya ugonjwa huo kama fursa ya kujinufaisha badala ya kuunga mkono juhudi za Serikali katika kupambana na Janga hili kuacha mara moja vitendo hivyo. Nawasihaji wajielekeze katika kulinda afya za wananchi wetu kwani Serikali haitasita kuchukua hatua kali za kisheria kwa wote watakaobainika kujihusisha na vitendo vya aina hiyo.

**i) Jitihada za kuwalinda Wakulima Dhidi ya Mifumo ya Kinyonyaji katika Soko**

89. **Mheshimiwa Spika;** Kipekee naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali anayoingoa kwa namna alivyosimama imara na kuweka msimamo thabiti dhidi ya mifumo ya kumnyonya mkulima katika mazao mbalimbali na hususan korosho na pamba. Wizara itahakikisha kupitia taasisi zake ikiwemo FCC inasimamia maeneo mengine kuharibu mifumo ya aina hiyo iliyowekwa na wafanyabishara wasio waaminifu kwa lengo la kumnyonya mkulima. Mheshimiwa Rais ni mfano wa kuigwa katika utendaji wetu hasa katika kuhakikisha haki za wakulima na wananchi wanyonge zinalindwa. Na hii inadhihirisha utayari wake katika kuhamasisha wananchi kufanya kazi kwa kujituma na hivyo kuakisi kauli yake ya "HAPA KAZI TU".

**ii) Kuendeleza Teknolojia za Uongezaji Thamani Mazao ya Kimkakati**



90. **Mheshimiwa Spika;** Katika kuhakikisha Mazao ya kimkakati yanaongezwa thamani, Wizara kupitia taasisi zake za utafiti imeendelea kubuni teknolojia mbalimbali rafiki ambazo zitatumika katika kuongeza thamani ya Mazao ya Kimkakati yaani, Korosho, Chikichi, Mkonge, Zabibu, Miwa kwa ajili ya kutengeneza sukari, mbegu za mafuta hususan alizeti na karanga na Mazao ya Ngozi. Jitihada hizo zinaenda sambamba na utekelezaji wa Mradi wa ASDP II kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Sekta nyingine za uzalishaji katika kuhakikisha kuwa tunaongeza thamani ya mazao hayo kabla ya kuuzwa ili kuhakikisha mkulima anapata soko la uhakika na bei shindani.

**iii) Teknolojia ya Kupura na Kupepeta Alizeti**

91. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia Kituo cha CAMARTEC inaendelea na utaratibu wa kuhawilisha teknolojia za mashine ya kupura na kupepeta alizeti kwa Makau Engineering ambaye ni mjasiriamali mdogo. Lengo ni kuwezesha teknolojia hiyo iliyobuniwa na CAMARTEC kuweza kusambazwa kwa wakulima na kuwezesha upatikanaji wa teknolojia hiyo kirahisi kutokana na mahitaji yake katika maeneo ambayo zao la alizeti linalimwa kwa wingi hapa nchini. Hivi sasa wakulima wa zao hilo wanatumia mbinu za kizamani ambazo zinabakisha alizeti nyingi kwenye upuraji. Vilevile, mbinu hizo zinapunguza ubora wa alizeti inayovunwa na kumsababishia mkulima hasara.

**iv) Uendelezaji wa Sekta Ndogo ya Mafuta ya Mawese**

92. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na wataalam kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuendeleza Viwanda (UNIDO) na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) ilifanya uchambuzi wa mnyororo mzima wa zao la mchikichi. Lengo lilikuwa kubaini changamoto zinazokabili zao hilo, kupendekeza suluhisho na kuwezesha kuchangia katika upatikanaji wa mafuta ya kula nchini. Pamoja na uchambuzi huo, Wizara kupitia taasisi zake za utafiti wa viwanda (TIRDO, CAMARTEC, TEMDO) na

SIDO zilifanya uchambuzi zaidi na kuandaa maandiko (concept papers) ya teknolojia rahisi ya kuchakata chikichi.

**v) Upatikanaji wa Teknolojia Rahisi za Kuchakata na Kuongeza Thamani Mazao ya Kimkakati kwa Wajasiriamali Wadogo**

93. **Mheshimiwa Spika;** katika kuhakikisha upatikanaji wa Sukari unakuwa wa uhakika na wakutabirika, Wizara kupitia taasisi ya TEMDO inaendelea kubuni mtambo wa kukamua miwa na kutengeneza Sukari kwa ajili ya wajasiriamali wa kati na wadogo. Tayari baadhi ya wajasiriamali wameonesha nia ya kupata teknolojia hiyo pindi itakapokamilika. Suala hilo litasaidia kwa kiasi kikubwa kukabiliana na upungufu wa Sukari nchini na kuongeza ajira kwa kuwa itahamasisha wananchi wengi kujihusisha na kilimo cha miwa.

**Upatikanaji wa Teknolojia Rahisi za Kuchakata Mkonge**

94. **Mheshimiwa Spika;** Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu inaendelea na jitihada za dhati kufufua zao la Mkonge ambalo lilikuwa moja ya mazao ya biashara yaliyokuwa yanaliingizia Taifa fedha nyingi za kigeni na kuchangamsha uchumi wa Mikoa ya Tanga na Morogoro. Wizara inaenda na kasi hiyo ili kuhakikisha jitihada hizo zinakuwa na faida kubwa kwa mkulima na Taifa kwa ujumla. Hivyo, Wizara kupitia TEMDO iko katika hatua ya kukamilisha mashine ndogo (Korona) kwa ajili ya kuchakata mkonge. Lengo ni kuwarahisishia wajasiriamali wadogo kuchakata Mkonge ili kupata nyuzi. Kukamilika kwa mashine hiyo na kusambazwa kwa wajasiriamali itasaidia wakulima kuuza nyuzi badala ya Mkonge ghafi. Utamaduni tuliozoea wa kuuza malighafi ambayo huuzwa kwa bei ya chini ulisababisha kwa kipindi kirefu kuwakatisha tamaa wakulima na kupunguza uzalishaji na wengine kuacha kabisa kilimo cha Mkonge.

## **Upatikanaji wa Teknolojia Rahisi za Kuchakata Zabibu**

95. **Mheshimiwa Spika;** Wizara inaendelea kuhakikisha zao la zabibu zinapata soko la uhakika ili kuhamamisha ulimaji wa zao hilo. Katika jitihada hizo Bunge kupitia Sheria ya fedha ya mwaka 2019 ilipunguza baadhi ya tozo katika Mvinyo ili kuleta chachu kwa Kampuni kubwa kununua mchuzi wa Zabibu kwa wazalishaji wadogo na wa kati wa mchuzi. Sambamba na hilo, Wizara kupitia TEMDO imebuni teknolojia ya kukamua mchuzi wa zabibu (Grapes Distemer) ambayo ikikamilika itaongeza kasi ya uongezaji thamani zao hilo na hivyo wakulima wadogo kupata soko la uhakika la zao hilo.

## **Uendelezaji na Uongezaji Thamani katika Zao la Ngozi**

96. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia TIRDO imefanikiwa kutoa mafunzo kwa wafugaji zaidi ya mia mbili (200) katika Halmashauri za Wilaya za Arumeru, Arusha, Longido na Monduli juu ya namna ya kuongeza thamani katika ngozi (Skin and hide value addition) kwa kutumia teknolojia zilizopo hapa nchini ambazo zilikuwa hazijulikani kwa wafugaji. Mafunzo hayo yamesaidia kuongeza thamani kwenye bidhaa za ngozi pamoja na kuwaongezea kipato wafugaji kupitia bei bora za ngozi.

### **4.2.2. Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo**

#### ***j) Mapitio ya Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo***

97. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaendelea kufanya marejeo ya Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ya mwaka 2003. Kwa sasa, Wizara inakamilisha kufanya tafiti katika maeneo mawili ambayo ni Rural Industrialization na Technology and Innovation. Baada ya kukamilika kwa tafiti hizo uandishi wa Sera hiyo pamoja na Mkakati wa Utekelezaji wake utaanza.

Wizara inatarajia kukamilisha Sera ifikapo mwishoni mwa mwaka 2020.

## **ii) Upatikanaji wa Huduma za Fedha kwa Wajasiriamali**

98. **Mheshimiwa Spika;** Upatikanaji wa mitaji kwa wajasiriamali wadogo ni nyenzo muhimu katika kuanzisha na kuendeleza miradi mbalimbali ya kiuchumi. Wizara, kupitia SIDO imekuwa ikitoa mikopo kwa wajasiriamali kupitia Mfuko wa Wafanyabishara Wananchi (National Entrepreneurship Development Fund - NEDF). Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020 jumla ya mikopo 2,020 yenye thamani ya Shilingi Biloni 3.885 ilitolewa kwa wajasiriamali mbalimbali kote nchini. Kati ya mikopo hiyo, asilimia 51.3 ilitolewa kwa wanawake na asilimia 48.7 ilitolewa kwa wanaume. Aidha, asilimia 39.2 ya mikopo hiyo ilitolewa maeneo ya vijijini na asilimia 60.2, ilitolewa mijini. Mikopo hiyo imekuwa chachu ya uendelezaji viwanda ambapo jumla ya shilingi Biloni 1.374 zilizokopeshwa ziliwezesha kuanzishwa kwa viwanda 551 na kuwezesha ajira 6,193 kupatikana.

## **iii) Uzalishaji na Usambazaji wa Teknolojia**

99. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo nchini, imewasaidia na kuwaendeleza wajasiriamali 42 wenye ubunifu wa teknolojia na mawazo ya bidhaa mpya kupitia programu ya kiatamizi (Incubation Programme). Wajasiriamali hao hupatiwa huduma mbalimbali kama vile maeneo ya kufanyia kazi, mafunzo, ushauri wa kiufundi pamoja na mitaji ili waweze kukua na kufikia viwango vya kujitegemea sambamba na kuzalisha bidhaa bora zenye kukubalika sokoni.

100. **Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka 2019/2020, jumla ya teknolojia na mawazo ya bidhaa mpya 25 yalihudumiwa katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mbeya, Mara, Manyara na Tanga. Teknolojia hizo zilihusu utengenezaji wa sabuni, mafuta ya losheni, utengenezaji wa kemikali za viwandani, usindikaji vyakula,

uchakataji na utengenezaji wa bidhaa za ngozi, utengenezaji wa mkaa mbadala (briquettes) na utengenezaji wa zana za kilimo. Bidhaa na zana hizo zimeweza kuingia sokoni na kutumiwa na wananchi kadri ya mahitaji yao. Jitihada za uendelezaji teknolojia imejitokeza pia kwa taasisi zetu kuingia katika uzalishaji wa sanitizer kama njia ya kupambana na kujilinda na corona. Kupitia wajasiriamali wake, SIDO imetengeneza mtambo wa kutakasa mwili mzima ambao utafaa sana kuwekwa kwenye maeneo ya maofisi, vivuko, stendi za mabasi, vituo vya mipakani, nk. UNDP kwa kuona jitihada na nguvu hizo imeonesha interest ya kununua kati ya mitambo 50 na 100 ili iweze kutumika kwenye maeneo mbali mbali ya umma.

101. ***Mheshimiwa Spika;*** Karakana zilizoko katika Ofisi za SIDO mikoani ziliweza kutambua au kuzalisha jumla ya teknolojia mpya 272 na kusambaza kwa wajasiriamali. Teknolojia hizo zilihusu ubanguaji wa korosho, usindikaji wa mihogo, ukamuaji wa mafuta ya mawese, usindikaji na ufungashaji wa vyakula mbalimbali, utengenezaji wa sabuni na vitakasa mikono, usindikaji wa ngozi na utengenezaji wa chaki, usindikaji wa asali, mitambo ya kuvunia mpunga, mahindi na mtama, mashine za kuchakata tangawizi, kutengeneza misumari na mashine za kutengeneza vyakula vya mifugo kwa kutaja maeneo machache ya teknolojia hizo. Teknolojia hizo zimeweza kurahisisha kazi kwa wakulima na zile za matumizi ya moja kwa moja zimeingia sokoni na kutumiwa na wananchi.

***iv) Uendelezaji Maeneo na Majengo ya Uwekezaji wa Wajasiriamali kuendeleza Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo***

102. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia SIDO imeendelea kupanua huduma za upatikanaji wa maeneo ya uzalishaji bidhaa kwa wajasiriamali ambapo mwezi Juni mwaka 2019 Wizara ilipokea Shilingi Bilioni moja toka Bajeti ya mwaka 2018/2019 kwa ajili ya ujenzi wa majengo viwanda (industrial sheds) katika mikoa ya Kigoma, Mtwara na

Ruvuma. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 SIDO imekamilisha upembuzi yakinifu wa majengo matatu pamoja na michoro ya usanifu (architectural drawings) katika mikoa ya Mtwara (2) na Kigoma(1) na kuanza ujenzi. Kwa upande wa Mkoa wa Ruvuma, SIDO wamepata kiwanja cha ekari 19.9 katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa kwa ajili ya ujenzi wa Mtaa wa Viwanda na Ofisi itakayokuwa na kituo cha mafunzo. Ukamilishaji wa majengo viwanda (industrial sheds) unategemewa kuwezesha uanzishwaji wa viwanda vipya saba vitakavyotengeneza ajira 76.

#### v) Uendelezaji wa Vituo vya Teknolojia

103. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia SIDO, inamiliki na kusimamia vituo saba vya uendelezaji teknolojia katika mikoa ya Arusha, Iringa, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Mbeya na Shinyanga. Vituo hivyo vimekuwa vikibuni, kutengeneza na kuendeleza teknolojia mbalimbali kulingana na mahitaji ya wajasiriamali katika maeneo hayo kwa kuzingatia mkakati wa Wilaya Moja Bidhaa Moja (One District One Product – ODOP) na fursa nyingine zinazojitokeza. Vituo hivyo viliweza kutengeneza jumla ya mashine 268 na kuziua kwa wajasiriamali.

104. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia SIDO imeendelea kuboresha vituo hivyo vya teknolojia kwa kufanya ukarabati wa mitambo iliyopo na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi kwa kutumia dhana ya KAIZEN katika uzalishaji ili kuongeza tija. Wizara ilipokea jumla ya Shilingi Billioni moja mwezi Juni 2019 kutoka katika bajeti ya mwaka 2018/2019 kwa ajili ya kufanya maboresho katika vituo vya Lindi, Shinyanga na Kigoma kwa kuvinunulia baadhi ya mitambo ya kisasa. Hadi kufika mwezi Machi 2020, tayari vipimo vya mitambo hiyo (specifications) pamoja na gharama zake zimeainishwa. Kwa sasa shirika limeagiza mashine hizo za kisasa (computerized) kutoka kampuni ya Jiangsu Longshen Machine Manufacturing Co.Ltd ya China ambapo tayari malipo ya awali yamefanyika.

**vi) Utoaji wa Mafunzo na Huduma za Ushauri wa Kiufundi kwa Wajasiriamali**

105. **Mheshimiwa Spika;** Wizara imeendelea kutoa huduma za ushauri wa kiufundi kupitia SIDO hasa katika maeneo ya uthibiti wa ubora wa bidhaa, michoro ya majengo ya viwanda, ufungaji wa mashine, ukarabati wa mashine, upangaji wa mashine viwandani (equipment layout) pamoja na uchaguzi wa teknolojia sahihi kulingana na aina ya bidhaa inayozalishwa na mjasiriamali. Katika mwaka 2019/2020 jumla ya wajasiriamali 5,145 walipata ushauri wa kiufundi katika mkoa yote ya Tanzania Bara. Vilevile, SIDO imeendelea kutoa huduma ya mafunzo mbalimbali kwa wajasiriamali ili kuwawezesha kupata ujuzi wa kubuni, kuanzisha na kuendesha shughuli mbalimbali za kiuchumi. Kupitia ofisi zake zilizoko mikoani shirika lilitoa mafunzo kwa wajasiriamali 12,589 ambapo mafunzo hayo yalijikita katika stadi mbalimbali.

106. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia SIDO imeendelea kuboresha Vituo vya Mafunzo kwa wajasiriamali (Training Cum Production Centres-TPCs) kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo. Katika mwaka 2019/2020, Wizara kwa kushirikiana na Mradi wa "Local Investment Climate" (LIC) imefanya ukarabati wa jengo la mafunzo na ofisi katika TPC ya Dodoma ambayo inajihusisha na utoaji wa mafunzo ya uzalishaji bidhaa za ngozi. Aidha, Kupitia Mradi huo kituo hicho cha mafunzo ya bidhaa za ngozi kimenunuliwa mashine na vifaa vya kisasa vya uzalishaji pamoja na vifaa vya kufundishia. Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa vituo vingine vya mafunzo na uzalishaji (TPCs) vilivyopo katika ofisi za SIDO mikoani.

**vii) Kuhamasisha Ujenzi wa Viwanda Vidogo Nchini**

107. **Mheshimiwa Spika;** Wizara imeendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda nchini hususan viwanda vidogo na vya kati ambavyo ni rahisi kuanzishwa kutokana na uwepo wa malighafi za kutosha kwa aina hiyo ya

viwanda pamoja na kutohitaji mitaji mikubwa katika uanzishwaji wake. Uhamasishaji huo umekuwa ukifanyika kupitia uongezaji wa mitaji kwa wajasiriamali kwa kuwapa mikopo kupitia Skimu ya Ukopeshaji kwa Wajasiriamali (SME Credit Guarantee Scheme-CGS) inayosimamiwa kwa pamoja kati ya SIDO na CRDB. Aidha, kupitia Mfuko wa NEDF unaosimamiwa na SIDO, wajasiriamali wamekuwa wakipatiwa mikopo kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza viwanda vidogo katika maeneo ya mijini na vijijini. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Machi 2020 kupitia mifuko hii, jumla ya viwanda vipya 437 vilianzishwa na kutoa ajira 1,481. Viwanda hivyo ni pamoja na vya kusindika nafaka, korosho, mafuta ya alizeti, asali, kutengeneza bidhaa za ngozi, sabuni, chaki, vyakula vya mifugo, ushonaji na useremala.

108. **Mheshimiwa Spika;** Sambamba na utoaji mikopo kwa wajasiriamali, Wizara kupitia SIDO imekuwa ikitoa mafunzo na huduma za kiufundi kwa wenye viwanda pamoja na kuwapatia sehemu za kufanyia kazi baadhi ya wajasiriamali wenye mawazo/ubunifu wa teknolojia mbalimbali za uzalishaji mali kupitia programu ya kiatamizi (incubation programme). Huduma hizi zimehamasisha uanzishaji na uendelezaji wa viwanda pamoja na kuongeza tija katika uzalishaji wa bidhaa zenye ubora.

**viii) Kuimarisha Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO)**

109. **Mheshimiwa Spika;** Wizara imeendelea kuimarisha SIDO kwa kutoa fursa za mafunzo kwa wataalamu wake kwa kubadilishana ujuzi katika nyanja mbalimbali zikiwemo za teknolojia. Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020 wafanyakazi wa SIDO waliweza kwenda China, India na kushirikiana na taasisi za ndani vikiwemo vyuo vikuu vya Mbeya, SUA na Dar es Salaam kwa ajili ya kuongeza ujuzi. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha SIDO hususan katika maeneo ya Vituo vyake vya maendeleo ya Teknolojia (TDCs), Ujenzi na uboreshaji miundombinu katika mitaa ya viwanda ya SIDO na utumiaji wa TEHAMA.



### 4.2.3. Sekta ya Biashara

#### i) Hali ya majadiliano ya Fursa Mbalimbali za Masoko

110. **Mheshimiwa Spika;** Wizara imeendelea kufanya juhudi mbalimbali ili kuimarisha matumizi ya fursa nafuu za biashara zilizopatikana na kutafuta fursa nyingine kupitia majadiliano ya kibiashara. Lengo ni kuhakikisha bidhaa zinazochakatwa viwandani kwa kutumia malighafi nchini, pamoja na huduma kutoka Tanzania zinapata fursa za uhakika za biashara hususan katika masoko ya nje ya nchi. Sambamba na hilo, Wizara imeendelea kuweka utaratibu madhubuti na shirikishi katika kusimamia na kufuatilia uondoaji wa Vikwazo vya Kibiashara Visivyokuwa vya Kiushuru (NTBs). Hatua hiyo imesaidia kupunguza NTBs kadhaa zilizokuwa zikififisha biashara ya bidhaa na huduma za Tanzania; kuimarisha ushirikiano wa wadau wa Sekta ya Umma na Binafsi Tanzania Bara na Zanzibar wanaohusika na masuala ya kibiashara kwa kuweka utaratibu wa kufanya kazi kwa pamoja kwa lengo la kufungamanisha shughuli za wadau hao; Kuwajengea uwezo na uelewa wa wadau/ wafanyabiashara kuhusu fursa na namna ya kutumia fursa hizo kupitia ziara, makongamano na shughuli nyingine za kibiashara ndani na nje ya nchi; na kuibua vyanzo mbadala vya fedha na kiufundi kupitia miradi mbalimbali vinavyosaidia juhudi za Serikali za uendelezaji na uwezeshaji biashara. Baadhi ya matokeo ya juhudi hizo yaliyopatikana kabla ya kujitokeza kwa janga la ugonjwa wa COVID-19, ni kuongeza wigo wa fursa za biashara ya bidhaa na huduma baina ya nchi na nchi (bilateral), Kikanda na Kimataifa. Hali hiyo, imewezesha kuimarika kwa urari wa biashara ya Tanzania katika masoko ya nje, hususan EAC na SADC.

111. **Mheshimiwa Spika;** Wizara ilishiriki katika Mkutano wa 36 wa Dharura wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Viwanda, Biashara, Fedha na Uwekezaji la Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika tarehe 09 – 13 Septemba 2019 Jijini Arusha Tanzania. Lengo la Mkutano huo lilikuwa ni kupitia na kujadili masuala mbalimbali yanayoihusu Jumuiya hiyo

ambayo ni pamoja na:- Uandaaji wa Mkakati wa Utekelezaji na Ukuzaji wa Sekta ya Pamba, Nguo na Mavazi; na Mkakati wa Utekelezaji na Ukuzaji wa Sekta ya Ngozi, Bidhaa za Ngozi na Viatu. Masuala mengine yaliyojadiliwa ni kuhusu taarifa ya Mkakati na Mwongozo wa Sera ya uanzishwaji wa viwanda vya uchenjuaji na uongezaji wa thamani wa madini; na Zoezi la Mapitio ya Wigo wa Pamoja wa Forodha wa EAC(Comprehensive Review of the EAC CET).

112. **Mheshimiwa Spika;** Kupitia mkutano huo, Mawaziri walipitia taarifa ya maendeleo ya zoezi la Mapitio ya Wigo wa Pamoja wa Forodha wa EAC na kuridhia viwango vipya vya wigo wa pamoja wa ushuru wa forodha (tariff bands) kuwa nne ambazo ni 0%, 10%, 25% na zaidi ya 25%. Hata hivyo, pendekezo la ukomo wa juu wa zaidi ya 25% ambao uliwasilishwa na nchi wanachama wa kutoza kati ya 30% na 35% haukuweza kuridhiwa hadi tarifa muhimu za uchambuzi zitakapowasilishwa. Hivyo, mkutano huo uliagiza ufanyike uchambuzi zaidi ikiwemo kubainisha bidhaa zinazopendekezwa kutozwa ukomo wa juu wa asilimia 30 na asilimia 35 (product mapping) ili hatimaye uchambuzi huo uwasilishwe kwenye kikao kijacho cha Mawaziri kwa ajili ya kufanya maamuzi ya ukomo wa juu.

113. **Mheshimiwa Spika;** Pia, Wizara ilishiriki katika Mkutano wa ngazi ya juu (EAC High-Level Conference) uliofanyika kuanzia tarehe 25 hadi 27, Septemba 2019 jijini Nairobi, Kenya. Lengo kuu la Mkutano huo, lilikuwa ni kujadili masuala mbalimbali katika Jumuiya Masuala hayo ni pamoja na:- Utekelezaji wa Umoja wa Forodha ndani ya Jumuiya (EAC Customs Union); Majadiliano ya uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara Barani Afrika (African Continental Free Trade Area - AfCFTA); na Masuala ya Vikwazo vya Kiiashara Visivyokuwa vya Kiushuru (NTBs). Aidha, Mkutano huo ulitoa fursa kwa Nchi Wanachama kujadili changamoto mbalimbali zinazokwamisha utekelezaji wa masuala muhimu ya biashara ndani ya Jumuiya pamoja na kuweka mikakati endelevu ya kuimarisha biashara miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

*ii) Majadiliano ya Kuanzishwa kwa Eneo Huru la Biashara kwa Nchi za Afrika (Africa Continental Free Trade Area – AfCFTA)*

114. **Mheshimiwa Spika;** Wizara ilishiriki katika Mkutano wa wataalam kutoka nchi wanachama wa EAC tarehe 26 – 27 Agosti, 2019 jijini Arusha. Miongoni mwa malengo ya Mkutano huo yalikuwa ni:- kupitia na kujadili rasimu ya kwanza ya tariff offer ya EAC iliyoandaliwa na nchi wanachama; kujadili msimamo wa pamoja wa EAC kwenye masuala ya Uasili wa Bidhaa na kuandaa rasimu ya jedwali la makubaliano ya Biashara ya Huduma kwenye Sekta tano za kipaumbele ambazo ni: Sekta za Biashara; Utalii; Mawasiliano; Fedha; na Uchukuzi, zilizokubalika kwenye majadiliano ya AfCFTA. Masuala mengine yaliyojadiliwa ni pamoja na: Jedwali la pamoja la ufunguaji wa Biashara ya Bidhaa (EAC Schedules of Tariff Concessions); Msimamo wa Jumuiya katika masuala ambayo majadiliano yake hayajakamilika hususan vigezo vya Uasili wa Bidhaa (Rules of Origin-RoO); Hali ya majadiliano ya Biashara ya Huduma; Kiwango cha kuanzia kufunguliana biashara ya huduma; Uandaaji wa Jedwali la Pamoja la Biashara ya Huduma la EAC; na Ushirikishwaji wa wadau katika kila hatua za majadiliano.

115. **Mheshimiwa Spika;** Majadiliano ya kuelekea katika Eneo Huru la Biashara la Afrika bado yanaendelea na tunaamini kuwa yatakuwa na faida kubwa kwa nchi wanachama, hususan kwa nchi zilizojiandaa vyema katika uzalishaji na hivyo kuhitaji kupata masoko mapya ya kuuzia bidhaa zao pamoja na huduma. Wizara kwa kushirikiana na taasisi nyingine za umma na binafsi bado inaendelea kufanya utafiti kuhusu faida na hasara pamoja na kuandaa mikakati madhubuti itakayoifanya nchi kuweza kunufaika na Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Afrika. Baadhi ya Mikakati ambayo Wizara inaifanyia kazi hivi sasa ni pamoja na kufanyia Mapitio Sera ya Taifa ya Biashara, Sera ya Maendeleo ya Viwanda, Sera ya SMEs pamoja Sera nyingine mbali mbali ambazo kwa namna moja au nyingine, zitaweza kuifanya nchi kunufaika na mkataba huo. Kukamilika kwa

Sera hizo kutasaidia kuvutia Uanzishaji wa Viwanda vipya, kuongeza ajira nchini pamoja na kulinda viwanda vinavyokua dhidi ya ushindani mkubwa kutoka Nje.

116. **Mheshimiwa Spika**; Aidha, Mkutano huo ulikubaliana kutumia vigezo vifuatavyo katika kuboresha rasimu ya mapendekezo ya ufunguaji (tariff offer) :-Tariff offer iliyopo kwenye Eneo Huru la Biashara la Utatu (COMESA, EAC-SADC Tripartite FTA); Tariff offer zinazotumiwa na nchi wanachama ndani SADC na COMESA; Madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na uingizaji wa bidhaa ndani ya Afrika (threats of AfCFTA imports); Kulinda viwanda vinavyokua; Mapendekezo yaliyopo kwenye maboresho ya CET; na Mwenendo wa biashara ndani ya Jumuiya.

117. **Mheshimiwa Spika**; Katika kutekeleza maazimio ya Mkutano huo, Wizara ya Fedha na Mipango, ambayo ina jukumu la kusimamia masuala ya fedha/kodi, imeratibu zoezi la kupitia na kuandaa (tariff offer) kwa kushirikiana na wadau nchini. Taarifa hiyo inaendelea kufanyiwa kazi kabla ya kuwasilisha msimamo wa Tanzania katika EAC kuhusu suala hilo.

***iii) Kukamilisha Majadiliano ya Biashara ya Huduma kwa Sekta Sita za Kipaumbele katika Nchi Wanachama wa SADC***

118. **Mheshimiwa Spika**; Nchi Wanachama wa SADC zinaendelea na majadiliano yanayolenga kufunguliana fursa zaidi za biashara hususan kwenye biashara ya huduma. Majadiliano hayo yanafanyika kwa kuzingatia Itifaki ya Biashara ya Huduma ambayo inahimiza nchi hizo kufunguliana biashara ya huduma. Wizara imeratibu vema majadiliano hayo na kupitia Mkutano wa Kamati ya Baraza la Mawaziri wa Biashara wa SADC uliofanyika Windhoek Namibia tarehe 14 Juni, 2019 Nchi Wanachama zilizoridhia Itifaki hiyo ni saba (7) ambazo ni Afrika Kusini, Botswana, Lesotho, Eswatini, Msumbiji, Mauritius na Shelisheli. Nchi nyingine ikiwemo Tanzania, zimesaini na ziko katika hatua mbalimbali za kuridhia Itifaki hiyo. Itifaki hiyo itaanza utekelezaji wake

mara baada ya Akidi ya nchi kumi (10) kutimia. Ufunguaji huo unatarajiwa kuchochea biashara na kukuza biashara ya huduma ili kusaidia katika juhudi za uendelezaji wa viwanda kwa kuongeza uwekezaji wa utoaji huduma na hivyo kuongeza fursa za ajira, ufanishi na uhaulishaji wa teknolojia ili kukuza Pato la Taifa.

119. **Mheshimiwa Spika;** Nchi za SADC zimeendelea kuhakikisha biashara inaendelea kufanyika katika kipindi hiki ambacho Nchi hizo na Dunia kwa ujumla zinaendelea na mapambano dhidi janga la COVID-19. Katika kutekeleza hilo, SADC imeandaa muongozo ambao uliidhinishwa na Baraza la Mawaziri wa SADC ambao utawezesha biashara hususan usafirishaji wa mizigo bila kuwa na masharti magumu ili kuwezesha nchi wanachama kuendelea kupata huduma muhimu wakati huu ambao nchi nyingi zimeweka zuio la watu kuingia au kutoka.

*iv) Kukamilisha Majadiliano ya Kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Utatu linalojumuisha Kanda za COMESA, EAC na SADC*

120. **Mheshimiwa Spika;** Wizara imeshiriki na kutetea maslahi ya nchi katika majadiliano yanayoendelea ya ufunguaji wa Soko la Biashara kwa nchi za Utatu linalojumuisha Kanda za COMESA, EAC na SADC. Kupitia majadiliano hayo, Mkutano wa Wataalam uliofanyika tarehe 16 - 27 Septemba 2020 Nairobi, Kenya pamoja na mambo mengine, ulipitia na kuidhinisha baadhi ya Vigezo vya Uasili wa Bidhaa kwenye Mafuta ya kula, Saruji, Nguo pamoja na Magari. Vilevile, Mkutano ulipitia rasimu ya Mwongozo (Simplified Trade Regime) unaolenga kusaidia wajasiriamali wadogo kufanya biashara ndani ya nchi za utatu. Utaratibu huo, unalenga kuanza kutumika mara moja kabla ya kukamilisha majadiliano kwenye vigezo vya Uasili wa Bidhaa. Mwongozo unapendekeza bidhaa zenye thamani chini ya Dola za Marekani 2,000 ndizo ziruhusiwe kuuzwa kwenye soko la Utatu. Hata hivyo, Mkutano uliamua kuwa Mwongozo huo unahitaji maboresho zaidi na hivyo kukielekeza Kikosi Kazi cha Utatu kufanya marekebisho na

kukamilisha uchambuzi ili kujiridhisha na ukomo wa thamani ya bidhaa unaopendekezwa.

**v) Kuendeleza Majadiliano ya Biashara kati ya Tanzania na Nchi nyingine**

121. **Mheshimiwa Spika;** Katika kuendelea kutafuta fursa za biashara katika masoko ya nchi rafiki, Wizara ilishiriki katika Kongamano la Kibiashara kati ya Tanzania na Misri lililofanyika tarehe 10-14 Septemba, 2019 Jijini Dar es Salaam. Lengo la Kongamano hilo lilikuwa ni kutangaza fursa za Biashara kati ya Tanzania na Misri zitakazopelekea kukuza biashara na uwekezaji baina ya nchi hizo mbili na kuendeleza juhudi za kutafuta fursa za masoko kwa bidhaa za ndani zinazozalishwa nchini. Kupitia Kongamano hilo, nchi zote mbili ziliweza kujadili na kuweka mikakati ya kuendeleza fursa za biashara na uwekezaji katika sekta mbalimbali zikiwemo Ujenzi, Madawa, Umeme na Usafirishaji.

**vi) Mikataba na Itifaki za Biashara**

122. **Mheshimiwa Spika;** Wizara iliandaa na kuwasilisha Waraka wa kuomba ridhaa ya Serikali kuridhia Itifaki ya Marekebicho ya Mkataba wa Marrakesh ulionzisha Shirika la Biashara la Dunia ili kufanya Mkataba wa Uwezeshaji Biashara (Trade Facilitation Agreement) kuwa sehemu rasmi ya mikataba ya WTO. Waraka huo ulipata ridhaa ya Serikali na kuridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo tarehe 13 Novemba 2019. Tayari Hati ya Kuridhia (Instrument of Ratification) ya Mkataba huo imeshasainiwa na Mamlaka husika na kuwasilishwa Sekretarieti ya WTO kupitia Ubalozzi wetu Geneva. Baada ya taratibu za uridhiwaji kukamilika, kinachofuata kwa sasa ni utekelezaji wa Mkataba huo wa Uwezeshaji Biashara.

123. **Mheshimiwa Spika;** Vilevile, maandalizi muhimu ya awali ya utekelezaji wa Mkataba huo yalifanyika kupitia Kikao cha Kamati ya Kitaifa ya Uwezeshaji Biashara tarehe 19-22 Novemba 2019, Dar es Salaam. Kupitia Kikao hicho, Kamati iliweza kuandaa rasimu ya taarifa mbambali

(notifications) ambazo zinapaswa kuwasilishwa katika Sekretarieti ya WTO kulingana na matakwa ya Mkataba wa Uwezeshaji Biashara wa WTO. Taarifa zilizoandaliwa ni pamoja na Maeneo ya Kundi B (Category B Measures) pamoja na muda wake wa utekelezaji; Maeneo ya Kundi C ambayo nchi itahitaji msaada wa kiufundi na kifedha katika utekelezaji, na Maeneo ya uwazi (transparency notification). Taarifa hizo ziliwasilishwa kwenye Kikao cha Kamati ya Uongozi kilichofanyika tarehe 13 Februari 2020 jijini Dodoma. Hatua inayofuata kwa sasa, ni ukamilishaji wa taratibu za uwasilishaji wa taarifa hizo Sekretarieti ya WTO kwa ajili ya hatua zaidi.

**vii) *Mapitio ya Sera ya Taifa ya Biashara***

124. ***Mheshimiwa Spika***; Wizara inaendelea na marejeo ya Sera ya Taifa ya Biashara (2003) ambapo rasimu ya Sera, Mkakati wa Utekelezaji na Mkakati wa Mawasiliano pendekezwa vipo tayari. Wizara inaipitia rasimu hiyo ili kuhakikisha kuwa inakidhi na kuakisi mahitaji na hali halisi ya sasa ikiwa ni pamoja na kuendana na mabadiliko mbalimbali yanayoendelea kujitokeza katika ngazi ya kitaifa (national level), kikanda (regional) na kimataifa (multilateral) ili hatimaye ipate ridhaa ya Serikali. Katika ngazi ya kitaifa, msisitizo kwa sasa ni ujenzi wa uchumi wa viwanda na uhamasishaji biashara. Katika ngazi ya kikanda mabadiliko yaliyotokea ni pamoja na uimarishaji wa mtangamano wa kibiashara kupitia utekelezaji wa Itifaki mbalimbali kama vile Itifaki ya Jumuiya ya nchi za Kusini mwa Afrika (SADC); Itifaki ya Umoja wa Forodha na Itifaki ya Soko la Pamoja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sera hiyo itazingatia kupanuka kwa wigo wa biashara kikanda na katika bara la Afrika, kuanzishwa kwa Eneo Huru la Biashara la Utatu litakalojumuisha kanda za EAC, SADC na COMESA na Eneo Huru la Biashara Afrika.

**viii) *Utungaji wa Sheria ya Kujilinda Dhidi ya Athari za Biashara (Trade Remedies Act, 2020)***

125. ***Mheshimiwa Spika***; Wizara inaendelea na taratibu za kutunga Sheria ya Kujilinda Dhidi ya Athari za

Kibiashara ya mwaka, 2020 (Trade Remedies Act, 2020) ambayo inalenga kulinda biashara na viwanda vya ndani. Ulinzi huo unalenga kuzuia uingizwaji wa bidhaa kwa wingi (import surge); bidhaa kuuzwa kwa bei ya chini ikilinganishwa na bei ya bidhaa kama hizo kwenye nchi zinakotoka (dumping); na bidhaa nyingine kupewa ruzuku (subsidies) na nchi zao au taasisi nyingine na hivyo kuathiri bidhaa ambazo zinazalishwa ndani ya nchi bila kupata ruzuku. Mapendekezo ya kutunga Sheria hiyo yameshawasilishwa Serikalini kwa ajili ya maamuzi.

**ix) Nafasi ya Tanzania katika Biashara ya Nchi na Nchi, Kikanda na Kimataifa**

**a) CHINA**

126. **Mheshimiwa Spika;** Mauzo ya bidhaa kwenye masoko ya upendeleo yalikuwa kama ifuatavyo: soko la China yaliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 144.28 mwaka 2018 hadi Dola za Marekani milioni 233.60 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 61.9. Ongezeko hilo linatokana na uzalishaji na uuzaji kwa wingi mbegu za ufuta. Bidhaa zingine zilizouzwa kwa wingi ni pamoja na tumbaku, pamba, jute, manila (coconut, abaca) na nguo na mavazi. Manunuzi ya Tanzania kutoka China yalikuwa Dola za Marekani milioni 1,762.78 mwaka 2018 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 1,987.60 mwaka 2019 sawa na asilimia 12.8. Ongezeko hilo limetokana na uagizaji kwa wingi bidhaa zenye thamani kubwa ambazo zinatumiwa katika uzalishaji na ujenzi wa miundombinu, bidhaa hizo ni matrekta, matairi ya magari, gas oil na vifaa vinavyotumiwa katika ujenzi wa reli (tramway track construction material of iron and steel). Urari wa biashara unaonyesha nakisi ya Dola za Marekani 1,754.00 milioni. (Kiambatisho Na. 7 )

**b) INDIA**

127. **Mheshimiwa Spika;** Mauzo katika Soko la India yaliongezeka kutoka Dola za Marekani Milioni 734.27 mwaka 2018 hadi Dola za Marekani Milioni 867.70 mwaka 2019 sawa



na ongezeko la asilimia 18.2. Ongezeko hilo lilitokana na uuzaji kwa wingi bidhaa za maua, kahawa, alizeti, madini. Aidha, Manunuzi ya Tanzania kutoka India yaliongezeka kutoka Dola za Marekani Milioni 1,218.07 mwaka 2018 hadi Dola za Marekani Milioni 1,258.40 mwaka 2019 sawa na asilimia 3.3. Hali hiyo ilisababishwa na uagizaji kwa wingi bidhaa za madawa gesi na mafuta. Kutokana na hali hiyo urari wa biashara unaonyesha nakisi ya kiasi cha Dola za Marekani Milioni 90.70. (Kiambatisho Na. 7).

**c) JAPAN**

128. **Mheshimiwa Spika;** Mauzo katika soko la Japan yalipungua kutoka Dola za Marekani Milioni 66.72 mwaka 2018 hadi Dola za Marekani Milioni 64.10 mwaka 2019 sawa na upungufu wa asilimia 3.9. Mwaka 2018, manunuzi ya bidhaa kutoka Japan yalikuwa na thamani ya Dola za Marekani Milioni 398.13 ikilinganiswa na Dola za Marekani Milioni 485.10 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 21.8. Ongezeko hilolinatokana na uagizaji kwa wingi bidhaa zinazotumika kwenye uzalishaji viwandani kama vile mitambo na kemikali. Urari wa biashara umeonyesha nakisi ya Dola za Marekani Milioni 421. (Kiambatisho Na. 7)

**d) JUMUIYA YA UMOJA WA ULAYA- EU**

129. **Mheshimiwa Spika;** Bidhaa zilizonunuliwa na Tanzania kutoka Jumuiya ya Ulaya zilikuwa na thamani ya Dola za Marekani milioni 1,015.76 mwaka 2018 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 909.01 kwa mwaka 2019, ikiwa ni upungufu wa asilimia 10.5. Bidhaa zilizoagizwa kwa wingi ni pamoja na; vifaa vya mitambo, vipuri vya magari, magari,nguo, vyombo vya majini (marine vessels), gesi na mafuta, vifaa vya madawa (medical apparatus), paper board, fittings, gas tubes, mineral/chemical fertilizers, data processing machines, vifaa vya mawasiliano na vifaa vya uchunguzi wa kimaabara. Pia, mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda Jumuiya ya Ulaya yalipungua kutoka Dola za Marekani Milioni 497.82 kwa mwaka 2018 hadi kufikia Dola za Marekani Milioni 399.30 mwaka 2019, ambayo ni sawa na

upungufu wa asilimia 19.8. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni bidhaa za tumbaku, madini, kahawa, maharage ya soya, alizeti, pamba na maua. Kutokana na hali hiyo urari wa biashara umeonesha nakisi ya Dola za Marekani Milioni 509.71 ikimaanisha thamani ya bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ni kubwa ikilinganishwa na thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania katika soko hilo. Hii inatokana na Tanzania kuuza zaidi malighafi katika soko la Jumuiya ya Ulaya wakati Tanzania inaagiza bidhaa za viwandani (finished products). Kutokana na hali hiyo urari wa biashara umeonyesha nakisi ya Dola za Marekani Milioni 509.71. Kupungua kwa biashara baina ya Tanzania na Jumuiya ya Ulaya kumechagiwa na kudorora kwa uchumi kwa baadhi ya nchi za Jumuiya ya Ulaya pamoja na kuimarika kwa uzalishaji wa viwanda vya ndani na kuimarisha bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi. (Kiambatisho Na. 8)

**e) AGOA**

130. **Mheshimiwa Spika;** Mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda Marekani kupitia Mpango wa AGOA kwa mwaka 2019 yaliongezeka na kufikia Dola za Marekani Milioni 21,116 ikilinganishwa na Dola za Marekani Milioni 42,432 kwa mwaka 2018 (Kiambatisho Na. 8) Mauzo hayo kwa kiasi kikubwa yalichangiwa na Sekta ya Nguo na Mavazi. Aidha, ili kuongeza mauzo zaidi katika soko hilo, Wizara imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Kukuza Mauzo ya Tanzania katika soko la Marekani kupitia Mpango wa AGOA.

**f) JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC)**

131. **Mheshimiwa Spika;** Katika kutumia fursa za masoko ya kikanda, mauzo ya Tanzania katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 2019 yalikuwa Dola za Marekani Milioni 674.40 ikilinganishwa na Dola za Marekani Milioni 447.50 mwaka 2018 sawa na ongezeko la asilimia 50.70. Ongezeko hilo limetokana na mauzo ya bidhaa za chai, mahindi, ngano, alizeti, mchele, bidhaa za karatasi, mabati, vigae, vyandarua, kemikali (methyl bromide), saruji na mafuta ya kupaka. Aidha, bidhaa za Tanzania zilizouzwa kwa

wingi katika soko hilo ni pamoja na mbogamboga, chai, matunda, magunia, mifuko ya plastiki, wanyama hai, viazi, samaki, udongo asilia, kahawa, mahindi, mchele, unga wa nafaka, karanga, mawese, ufuta, pamba na makaa ya mawe. Mauzo hayo kwa kiasi kikubwa yanaenda katika nchi ya Kenya ikifuatiwa na Rwanda. Kwa upande mwingine, ununuzi wa Tanzania kutoka nchi za Jumuiya hiyo uliongezeka kutoka Dola za Marekani Milioni 302.93 mwaka 2018 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 329.10 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 8.6. (Kiambatisho Na. 8)

**g) JUMUIYA YA MAENDELEO YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA (SADC)**

132. **Mheshimiwa Spika;** Mauzo ya Tanzania kwenda katika soko la nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), mwaka 2019 yalikuwa Dola za Marekani Milioni 1,330.90 ikilinganishwa na Dola za Marekani Milioni 999.34 mwaka 2018 sawa na ongezeko la asilimia 33.20. Ongezeko hilo linatokana uuzaji kwa wingi bidhaa za madini, pamba, chai, kahawa, vigae, vyandarua, kemikali (methyl bromide), petroleum coke, saruji, sabuni na mafuta ya kupaka. Aidha, bidhaa hizo ziliuzwa katika nchi za Afrika Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia na Malawi. Ununuzi wa Tanzania kutoka katika soko hilo ulipungua kutoka Dola za Marekani milioni 604.32 mwaka 2018 hadi Dola za Marekani Milioni 155.10 mwaka 2019 sawa na upungufu wa asilimia 74.3. Upungufu huo unatokana na kuimarika kwa uzalishaji viwandani hususan bidhaa zinzotumiwa kwa wingi nchini (consumable goods). (Kiambatisho Na. 8)

**4.2.4. Sekta ya Masoko**

**i) Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara Nchini**

133. **Mheshimiwa Spika;** Katika kuhakikisha kwamba mazingira ya biashara nchini yanaendelea kuboreshwa, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Sekta

imeendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhhibiti wa Biashara Nchini (Blueprint for Regulatory Authority Reforms to Improve the Business Environment) ambao ulipata ridhaa ya Serikali na kuanza kutekelezwa rasmi Julai 2019. Aidha, Blueprint imeandaliwa Mpango Kazi (Blueprint Action Plan-BAP) ili kuongoza utekelezwaji wake na utungaji wa Sheria ya Uwezeshaji Biashara (Business Facilitation Act) uko hatua ya juu. Waraka wa Mapendekezo ya kutunga Sheria hiyo umekamilika kwa ajili ya maamuzi ya Serikali. Sheria hiyo itaweka misingi ya kusimamia maboresho kwenye Sekta ya Biashara na kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali zinazoathiri mazingira ya biashara.

134. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Wizara ya Fedha na Mipango na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imeendelea na jitihada za kuhakikisha Leseni za Biashara Kundi A na B zinatolewa kwa njia ya mtandao kupitia Dirisha la Taifa la Biashara (National Business Portal - NBP). Leseni za Biashara za Kundi “A” ambazo hutolewa na BRELA sasa zinatolewa kwa njia ya mtandao kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2019. Aidha, utoaji wa leseni za Biashara Kundi B ambazo ziko chini ya TAMISEMI zimeendelea kutolewa kwa njia ya mtandao kwa kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2019 katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza na Halmashauri ya Manispaa ya Ilala. Hata hivyo, Halmashauri za Manispaa ya Bukoba, Chalinze, Mafinga na Karagwe zilifanyiwa mafunzo ya majaribio na taratibu za utekelezaji wake ziko mbioni. Majaribio ya Mfumo huo yamewezesha kubaini uwezo wa Halmashauri katika utoaji leseni kwa njia ya mtandao. Majaribio hayo yaliambatana na utoaji wa mafunzo ya nadharia na vitendo kwa Maafisa Biashara 45, Maafisa TEHAMA 42 na Wafanyabiashara 250.

135. **Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha majaribio, jumla ya Leseni 12,621 zimetolewa zinazojumuisha Leseni za Kundi ‘A’ 4,332, na Leseni Kundi ‘B’ 1,957 katika Jiji la Mwanza na Leseni 6332 katika Manispaa ya Ilala. Wizara imefanikisha kuunganishwa kwa Mfumo wa NBP na Mifumo ya GePG, Benki Kuu ya Tanzania na Mfumo wa Taarifa za Makusanyo ya Mapato wa Mamlaka za Serikali za Mitaa

(Local Government Revenue Collection Information System - LGRCIS). Mafanikio hayo yanatokana na jitihada za BRELA za kuboresha mazingira ya Biashara nchini ili kumwezesha mfanyabiashara kupata huduma popote alipo na kumpunguzia mteja gharama na muda unaohitajika kutumika.

136. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kwa kushirikiana na BRELA imekamilisha Mfumo wa Utoaji wa Taarifa za Biashara za Kimataifa (Trade Information Portal). Mfumo huo unawezesha wafanyabiashara kupata taarifa muhimu za hatua za kupata leseni na vibali vinavyohitajika kutoka Taasisi mbalimbali kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi, kuingiza au kupitisha nchini mazao na bidhaa mbalimbali. Mfumo huo una taarifa zinazohusiana na taratibu za uuzaji wa mazao kama vile maua, Mwani, Parachichi, Maziwa na mazao yake, Asali, Nyama na mazao yake, Kahawa, Karafuu, Korosho, Chai na mengine. Kwa upande wa uingizaji bidhaa nchini, kuna taarifa zinazohusu bidhaa za Madawa, urembo, vyakula, vipodozi, vifaa tiba na magari. Aidha, katika kipindi cha mwezi Julai 2019 hadi Aprili 2020, jumla ya wadau 42,390 walitumia taarifa hizo, ambapo asilimia 85 ni Watanzania, ikilinganishwa na wadau 5,958 waliotumia taarifa hizo katika kipindi cha Julai 2018 hadi Juni, 2019.

137. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania imeanzisha Mfumo wa Kupata Huduma ya Usajili wa Majengo, Maeneo ya Uzalishaji, Uuzaji, Usambazaji wa Bidhaa za chakula, vipodozi na ukaguzi wa shehena zinazotoka nje ya nchi kwa njia ya mtandao, TBS Online Applicaton System-OAS. Mfumo huo, umewezesha wateja kuomba huduma za TBS popote alipo kwa njia ya mtandao, kupunguza gharama mbalimbali (usafiri, mawasiliano, utoaji wa vivuli kwa nyaraka), kuokoa muda ambao ungetumika kufuata huduma katika ofisi za Shirika na kuepusha mazingira ya rushwa kwa kutokuonana ana kwa ana na mtoa huduma. Vilevile, Shirika lina mfumo wa Quality Management System (QUALIMIS) ambao hutumika kumfikishia mteja taarifa za sampuli alizopeleka katika maabara kwa njia ya barua pepe.

138. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imeendelea kutoa huduma za usajili wa Makampuni; Majina ya Biashara; Alama za Biashara na Huduma; Kutoa Hataza; Kutoa Leseni za Viwanda na Leseni za Biashara ikiwa ni pamoja na huduma baada ya usajili (Post Registration Services) kwa kutumia Mfumo wa Usajili kwa Njia ya Mtandao (ORS). Katika kipindi cha Julai 2019 hadi kufikia Machi 2020 BRELA imesajili Makampuni 7,549 ikilinganishwa na 6,918 Aprili, 2014; Majina ya Biashara 12,627 ikilinganishwa na 11,382 Aprili, 2019; Alama za Biashara na Huduma 1,970, Hataza 55 ikilinganishwa na 28 Aprili, 2019 na imetoa Leseni za Viwanda 200 ikilinganishwa na 166 Aprili, 2019 na Leseni za Biashara 9,927.

**ii) Mwenendo wa Bei za Baadhi ya Mazao**

139. **Mheshimiwa Spika;** Wizara imeendelea kukusanya na kuchambua taarifa za mwenendo wa bei za mazao (mahindi, mchele, mtama, uwele, ulezi, maharage, ngano, viazi mviringo na pamba) pamoja na taarifa za bei za baadhi ya bidhaa za viwandani (saruji, nondo na bati) upande wa Tanzania Bara kupitia Mifumo ya FAMS na One2two. Taarifa hizo hukusanywa , huchambuliwa na kusambazwa kila siku ya Jumatatu, Jumatano na Ijumaa kwa wadau mbalimbali wakimemo Ofisi ya Rais, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Kilimo (Usalama wa Chakula), Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Shirika la Chakula Duniani (WFP), Benki ya NMB, Taasisi za Utafiti na Wakala wa Ununuzi Serikalini (GPSA).

140. **Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha mwezi Machi, 2020, wastani wa bei kwa gunia la kilo 100 nchini ni shilingi kwa 65,217 mahindi, shilingi 179,410 kwa maharagwe, Shilingi 183,859 kwa mchele, shilingi 114,062 kwa mtama, Shilingi 121,117 kwa ngano, Shilingi 128,463 kwa ulezi, Shilingi 117,461 kwa uwele na Shilingi 71,000 kwa viazi mviringo.(Kiambatisho Na.9(a),(c),(d))

141. **Mheshimiwa Spika;** Wastani wa bei ya mazao hayo ya chakula umepanda ikilinganishwa na robo ya tatu ya mwaka 2018/2019 na robo ya tatu ya mwaka 2019/2020. Kwa mfano, bei ya gunia la kilo 100 la mahindi imepanda kwa asilimia 57; maharage yamepanda kwa asilimia 24; mchele umepanda kwa asilimia 14; wakati viazi mviringo na ulezi bei imeshuka kwa asilimia 4 na 6 mtawalia. Aidha, ongezeko la bei limetokana na kupungua kwa ugavi wa mazao hao katika soko.(Kiambatisho Na.9(a),(c),(d))

142. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia tarehe 16 Februari, 2020 Kilo 348,909,841 za pamba zenye thamani ya Dola za Marekani 3.5 zimenunuliwa katika Mikoa ya Shinyanga, Simiyu, Geita, Mwanza, Mara, Tabora, Singida, Kigoma, Kagera, Katavi, Dodoma, Manyara, Morogoro, Iringa, Pwani na Tanga Aidha, Kilo 348,501,838 inayojumuisha kilo 348,133,421 katika Kanda ya Magharibi zimesafirishwa na kilo 776,420 katika Kanda ya Mashariki. Aidha, hadi kufikia tarehe 3 Aprili, 2020 tani 58,547 za kahawa zenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 111.3 ziliuzwa. Kati ya hizo, tani 24,282 ziliuzwa kupitia minada ya ndani na tani 34,265 ziliuzwa moja kwa moja kwenye soko la nje.

143. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia tarehe 4 Aprili, 2020 wastani wa bei ya jumla ya Sukari kwa wafanyabiashara ni kati ya Shilingi 2,400 na Shilingi 2,610 kwa kilo na bei za rejareja ni kati ya Shilingi 2,700 na Shilingi 2,900 kwa kilo na baadhi ya maeneo bei imefikia Shilingi 3,500. Aidha, bei ya juu katika baadhi ya maeneo imetokana na gharama za biashara kutoka sukari inakozalishwa au kusambazwa. Katika kipindi hicho, jumla ya tani 5,588.28 za Sukari zilikuwepo ghalani, ambapo tani 3,437.05 zikiwa kwenye ghala ya wazalishaji Sukari nchini na tani 2,151.23 zilikuwepo katika ghala ya Wafanyabiashara. Aidha, katika kuhakikisha kwamba nchi inaendelea kujitoshleza kwa Sukari, Serikali kupitia Bodi ya Sukari, ilitoa idhini kwa wazalishaji kuagiza tani 40,000 za sukari ya kuziba pengo la mahitaji kwa mwaka 2019/2020. Kiasi halisi kilichoagizwa ni tani 37,866 ambapo shehena ya kwanza ya tani 9,990 ilifika Bandari ya Dar es Salaam na kuanza taratibu za kiforodha kuitoa shehena hiyo

tarehe 15 Aprili,2020 na shehena ya awamu ya pili ya tani 9,990 imewasili tarehe 27 na 28 Aprili 2020 tayari kwa kuingia sokoni.

**iii) *Kuhamasisha na Kuwezesha Wananchi Kutangaza Bidhaa na Huduma za Tanzania***

144. **Mheshimiwa Spika;** Wizara pamoja na Taasisi zake 15 zilishiriki katika Maonesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yaliyofanyika katika Viwanja vya Mwl. J. Nyerere, kuanzia tarehe 28 Juni hadi tarehe 13 Julai, 2019. Sambamba na wazalishaji na wafanyabiashara kuonesha bidhaa na huduma mbalimbali wanazozalisha, Wizara iliratibu mikutano ya kibiashara kati ya wafanyabiashara/wazalishaji na wanunuzi na kutenga siku maalum ya kutangaza fursa za masoko na usindikaji kwa mazao ya kimkakati na huduma za biashara. Tukio la siku hiyo liliambatana na utoaji wa mada kutoka Taasisi mbalimbali, wazalishaji/wafanyabiashara pamoja na wananchi walioshiriki kwa kuchangia na kutoa maoni yao.

145. **Mheshimiwa Spika;** Kupitia Maonesho hayo 43, wadau wa biashara pamoja na wazalishaji, wasindikaji na wafanyabiashara waliunganishwa kupitia Mikutano ya Biashara (B2B) iliyofanyika kuanzia tarehe 4 hadi 6 Julai, 2019 ikiwa ni mbinu ya kutafuta masoko. Katika mikutano hiyo, Wazalishaji walipata fursa ya kujitangaza na kuainisha bidhaa wanazozalisha ili kuzitambulisha kwa makampuni mbalimbali ya ndani na nje yenye uhitaji wa bidhaa hizo. Wafanyabiashara wapatao 520 walishiriki na kusaini mikataba ya awali yenye thamani ya Shilingi 6,089,750,000.00 ikihusisha Sekta Ndogo za Mboga Mboga na Matunda pamoja na Shilingi 4,240,000,000.00 katika Sekta Ndogo ya Asali.

146. **Mheshimiwa Spika;** Vilevile, Maonesho hayo yalitenga siku maalum kwa baadhi ya mazao kama korosho, viungo na mwani. Katika siku maalum ya viungo na mwani iliyofanyika tarehe 05 Julai, 2019 alipatikana mnunuzi wa Iliki kutoka Pakistani aliyehitaji tani 1,000. Aidha, Kampuni 437



ziligata oda ya kufanya biashara (Business deals) zenye thamani ya Shilingi Bilioni 7.93 pamoja na Mauzo ya papo kwa papo yenye thamani ya wastani wa Shilingi 209,450,000.

147. **Mheshimiwa Spika;** Maonesho ya Kilimo (Nanenane) ya mwaka 2019 yalifanyika Kitaifa katika viwanja vya Nyakabindi Wilayani Bariadi mkoani Simiyu kuanzia tarehe 31 Julai hadi tarehe 8 Agosti, 2019. Katika Maonesho hayo, jumla ya wajasiriamali 49 wanaojihusisha na uchakataji wa mazao ya kilimo na mifugo walishiriki kupitia banda la Wizara. Lengo likiwa ni kuwahamasisha wadau kurasimisha shughuli za kibiashara, kuwaunganisha na masoko, na pia kujifunza mbinu bora za uchakataji wa mazao ya Kilimo kutoka kwa washiriki wengine. Pia, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zilizo chini yake ilitoa huduma mbalimbali zikiwemo usajili wa majina ya biashara, usajili wa Makampuni na elimu kuhusu ujasiriamali. Aidha, Wizara kwa uratibu wa TanTrade iliendesha Kliniki ya Biashara ambapo ushauri kuhusu utatuzi wa changamoto za kibiashara, maelezo na ufafanuzi kuhusu Sheria, Kanuni na taratibu zinazosimamia kibiashara nchini yalitolewa pamoja na huduma mbalimbali za Kibiashara. Jumla ya wajasiriamali na wakulima wapatao 155 walipata mafunzo mbalimbali kupitia darasa hilo ambapo pia walipata taarifa za masoko.

148. **Mheshimiwa Spika;** Maonesho hayo pia yalitumika kuonesha na kutambulisha teknolojia na mashine mbalimbali ambazo zimebuniwa kulingana na mazingira halisi ya nchi yetu. Baadhi ya teknolojia hizo ni: Mashine ya kupura mpunga, alizeti na maharage; Mashine ya kuchakata Ngozi; Mashine ya kukausha mbogamboga na matunda; Mashine ya kukausha Korosho na Karanga; Trekta na Planta yake; Planta ya Pamba ya kukokotwa na wanyamakazi na Jiko la kutumia mwanga wa jua.

149. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia BRELA imekusanya taarifa za bidhaa mbalimbali kutoka Taasisi za Serikali zaidi ya ishirini (20) za kutoka Tanzania Bara na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Vilevile imeweza kukusanya taarifa kutoka taasisi tatu (3) zisizo za kiserikali zinazosimamia ufanyaji

wa biashara nchini. Tayari taarifa za bidhaa zaidi ya 18 zinazosafirishwa nje ya nchi (Export) na zaidi ya bidhaa 8 zinazoingizwa nchini (Import) zimeshakusanywa na kuingizwa kwenye Mfumo. Bidhaa ambazo taarifa zake zimeshaingizwa kwenye mfumo ni Korosho, Kahawa, Chai, Nafaka, mikunde, Mbolea, Madawa, Vifaa tiba, Vipodozi, vyakula vilivyosindikwa, Mbao, Maziwa na bidhaa zake, Nyama na bidhaa zake, Asali na bidhaa zitokanazo na asali, Matunda na mboga za majani, Parachichi, Viungo, kakao, Maua, Karafuu na Mwani. Aidha, kwa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje ya nchi, taarifa na taratibu za kupata leseni na vibali zilizowekwa katika mfumo ni; Madawa, Vipodozi, Vifaa tiba, Magari, Nafaka na jamii ya Mikunde, Mbao, Maziwa na bidhaa zake, Nyama na bidhaa zake pamoja na Mbolea.

***iv) Kuwaunganisha Wazalishaji, Wasindikaji na Wafanyabiashara na Masoko ya Ndani na Nje;***

150. Mheshimiwa Spika; Wizara imefanya uchambuzi wa kampuni za ndani zinazofanya biashara ya uuzaji na uingizaji wa mazao na bidhaa zake kwa lengo la kuwaunganisha wazalishaji, wasindikaji na wafanyabiashara. Jumla ya kampuni 19 zinajishughulisha na zao la mahindi, kampuni 9 kwa zao la vitunguu, Kampuni 23 kwa zao la Pamba, na wasindikaji wapatao 33 wametambuliwa kwa ajili ya kuwahamasisha kutumia rasilimali za ndani. Aidha, mwaka 2019 minada mitatu ya Kahawa imeanzishwa katika mikoa ya Kagera, Ruvuma na Songwe lengo likiwa ni kuwasogezea na kuwaunganisha na soko wazalishaji katika mikoa husika. Hadi kufikia tarehe 3 Aprili, 2020 tani 58,547 za Kahawa zenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 111.3 ziliuzwa. Kati ya hizo, tani 24,282 ziliuzwa kupitia minada ya ndani na tani 34,265 ziliuzwa moja kwa moja kwenye soko la nje.

151. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kupitia Ubalizi wa Tanzania nchini China iliratibu ushiriki wa kampuni 10 za Kitanzania katika Maonesho ya Pili ya Kimataifa ya Bidhaa za Nje (China International Importation

Expo) yaliyofanyika jijini Shanghai kuanzia tarehe 5 hadi 10 Novemba 2019. Maonesho hayo yalivutia zaidi ya kampuni 3,000 kutoka sehemu mbalimbali ulimwenguni na kutoa fursa kwa kampuni za Kitanzania kubadilishana taarifa, uzoefu na mbinu za kibiashara. Aidha, jumla ya wageni 500,000 walitembelea maonesho hayo kwa lengo la kujionea bidhaa mbalimbali.

152. **Mheshimiwa Spika;** Katika maonesho hayo, Tanzania kupitia Banda la Kitaifa ilionesha bidhaa za korosho, kahawa, viungo, karafuu, chai, vito vilivyotengenezwa kwa madini ya Tanzanite na bidhaa zilizotengenezwa kwa Ngozi kama vile pochi na mikanda. Jumla ya wageni 6,000 walitembelea Banda la Tanzania na jumla ya kampuni 120 zilionesha nia ya kununua bidhaa mbalimbali za Tanzania hususan bidhaa za kilimo hasa korosho, ufuta, wanga wa muhogo, karafuu, bidhaa za ngozi, bidhaa za mbao, bidhaa za madini ya Tanzanite, sapphire, ruby, spinal, tsavorite, gold, na tourmarine. Kati ya kampuni 120, kampuni 38 zilionesha nia ya kununua korosho ambazo zilizielekezwa taratibu za kufanikisha azma hiyo.

153. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia TanTrade iliwezesha Wajasiriamali 38 kushiriki katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Nairobi yaliyofanyika tarehe 30 Septemba hadi 6 Oktoba, 2019 kwa ajili ya kukuza soko la Bidhaa na Huduma za Tanzania nchini Kenya ikiwa ni sehemu ya jitihada ya kutumia vyema fursa za soko katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vile vile, kampuni 7 kutoka Sekta ndogo za nguo, Sanaa za Mikono na ngozi ziliwezesha kushiriki katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Eswatin yaliyofanyika tarehe 30 Agosti hadi 9 Septemba, 2019. Maonesho hayo yalitoa fursa ya kutangaza bidhaa za Tanzania katika soko la Ukanda wa Kusini wa Afrika.

v) ***Taarifa za Ununuzi katika Baadhi ya Mazao ya Biashara***

154. **Mheshimiwa Spika;** Wizara imeendelea kufuatilia mwenendo wa bei ya uuzaji na ununuzi wa mazao

ya kahawa, tumbaku, pamba na korosho. Katika msimu wa mwaka 2019, ununuzi na uuzaji wa Kahawa ulifanyika katika minada mitatu katika mikoa ya Songwe, Ruvuma na Kilimanjaro. Kwa minada iliyofanyika katika Wilaya za Songwe, Mbinga na Moshi kati ya tarehe 9 Agosti, 2019 na tarehe 19 Desemba, 2019, Kilo 22,409,218 zenye thamani ya Dola za Marekani 48,851,583 kiliuzwa. Vile vile katika kipindi hicho mauzo ya nje yalikuwa Kilo 25,948,538 zenye thamani ya Dola za Marekani 40,851,931. Hivyo, jumla kuu ya mauzo ya Kahawa katika kipindi hicho yalikuwa Kilo 48,357,756 yenye thamani ya Dola za Marekani 89,714,514.

155. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia tarehe 31 Agosti, 2019 kiasi cha Tumbaku ya mkataba kilichonunuliwa ni Kilo 60,691,972.21 yenye thamani ya Dola za Marekani 92,927,331.79. Tumbaku iliyonunuliwa ni asilimia 105.9 ya matarajio ya uzalishaji ya kilo 57,305,127 yaliyobainishwa kwenye Mikataba ya Kilimo. Aidha, jumla ya Kilo 9,395,078.12 zilinunuliwa nje ya utaratibu wa mkataba ikiwa na thamani ya Dola za Marekani 7,232,521.78. Hivyo, hadi kufikia mwezi Desemba 2019, jumla ya Kilo 70,087,048.43 zenye thamani ya Dola za Marekani 100,159,853.51 zimeuzwa na wakulima.

156. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia tarehe 22 Desemba, 2019 Kilo 348,331,518 za pamba zenye thamani ya Dola za Marekani 182,060,796.6 zilinunuliwa kutoka katika Mikoa ya Simiyu, Shinyanga, Mwanza, Geita, Singida, Kagera, Kigoma, Dodoma, Katavi, Tabora na Mwanza. Kiasi hicho kimenunuliwa na kampuni 21 na Kilo 348,501,838 tu zilisafirishwa ambapo katika Kanda ya Magharibi kiasi kilichosafirishwa ni Kilo 348,030,378 na Kanda ya Mashariki ni Kilo 471,460.

157. **Mheshimiwa Spika;** Katika msimu wa Korosho wa mwaka 2019/2020, kampuni 61 zilisajiliwa baada ya kutimiza vigezo vyote ikiwa ni pamoja na kuweka kinga ya zabuni (Security Bond) na kupatiwa leseni. Aidha, katika msimu huo minada ya Korosho ilianza rasmi tarehe 31 Oktoba, 2019 na kuisha 2 Februari, 2020 ambapo minada 72 imefanyika kupitia vyama Vikuu vya CORECU, TAMCU, MAMCU, TANECU,

RUNALI, LINDI MWAMBAO pamoja na TACACU. Hadi kufikia tarehe 2 Februari, 2020, Tani 224.426.283 za Korosho ghafi zenye thamani ya Shilingi 575,416,173,694.90 ziliuzwa.

158. **Mheshimiwa Spika;** Kupitia Mradi wa ASDP II, Wizara inafanya maandalizi ya kufanya tafiti za mazao ya Kahawa, Korosho, Pamba, Chai, Mkonge, Tumbaku na Pareto. Lengo la tafiti hizo ni kubaini maeneo ya uzalishaji, kiwango cha uzalishaji, bei ya mkulima, mauzo ndani na nje ya nchi na changamoto za biashara na usindikaji wa mazao ya kilimo katika kuyaongeza thamani.

### ***Taarifa za Bei ya Vifaa vya Ujenzi***

159. **Mheshimiwa Spika;** Bei ya nondo mm 16 imeshuka kutoka wastani wa Shilingi 36,571 kipindi cha mwezi Machi, 2019 na kufikia wastani wa Shilingi 35,454 mwezi Machi, 2020 na bei ya juu kuwa Shilingi 42,500 mkoani wa Mtwara. Vilevile, nondo mm 12 imepanda kutoka wastani wa Shilingi 20,404 na kufikia wastani wa Shilingi 20,639, nondo mm10 zimeshuka na kufikia Shilingi 15,346 kutoka wastani wa bei ya Shilingi 15,364 na nondo mm 8 zimeshuka kutoka wastani wa Shilingi 12,143 na kufikia wastani wa Shilingi 12,089 kwa kipindi cha mwezi Machi, 2020.

160. **Mheshimiwa Spika;** Kufikia mwezi Machi 2020 wastani wa bei ya bati geji 32 imepanda na kufikia Shilingi 15,404 ikilinganishwa na wastani wa bei ya Shilingi 15,377 ya mwezi Machi, 2019, bati ya geji 30 imeshuka kutoka wastani wa Shilingi 18,705 na kufikia wastani wa Shilingi 18,473 na geji 28 imepanda kutoka wastani wa Shilingi 25,594 na kufikia wastani wa Shilingi 26,643 kwa bati. Aidha, Wastani wa bei ya rejareja ya saruji kwa mfuko wa kilo 50 imepanda na kufikia Shilingi 16,037 ikilinganishwa na wastani wa bei ya mwezi Machi, 2019 ya Shilingi 15,633. (Kiambatisho Na. 9(b))

161. **Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha kuanzia Julai-Desemba 2019, wastani wa bei ya jumla ya Sukari kwa wafanyabiashara ni kati ya Shilingi 2,120 na Shilingi 2,583 kwa kilo na bei za rejareja ni kati ya Shilingi 2,400 na Shilingi 2,900

kwa kilo. Hata hivyo, bei ya sukari ilipanda ghafla katika kipindi cha mwezi Aprili 2020 na kufikia wastani wa Shilingi 3,500 katika mkoa mingi nchini na baadhi ya maeneo kufikia kiwango cha Shilingi 4,000. Hali hiyo, imedhibitiwa kwa Serikali kuhakikisha kiasi cha sukari kilichoidhinisha tani 40,000 kuziba kiasi cha upungufu wa mahitaji ya sukari nchini (Gap sugar) kuanza kuingia nchini na kusambazwa kwa ajili kurekebisha mwenendo wa soko hususan katika kipindi hiki ambacho mvua zinaendelea kunyesha na kuathiri ufanisi wa usafirishaji wa bidhaa na uzalishaji wa sukari viwandani.

**vi) Kufanya Utafiti wa Masoko ya Nje ambapo Bidhaa za Tanzania zina Fursa**

162. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia TanTrade imeratibu tafiti za kutambua fursa za masoko ili kuongeza mauzo ya bidhaa za Tanzania katika masoko ya nje. Kipaumbele ni katika masoko ya: China (Madini, Vito, Nyama, Tumbaku, Korosho na Muhogo); India (Mikunde, Korosho, Ngozi na Nafaka); Ulaya (Matunda, Mbogamboga, Asali, Kahawa na Korosho); na Nchi za EAC (nafaka, bidhaa za ujenzi, bidhaa za ngozi, bidhaa za viwandani na vyakula vya mifugo); Nchi za SADC (Madini, nafaka, bidhaa za viwandani, bidhaa za ujenzi). Aidha, mikutano na misafara ya kibiashara iliyoratibiwa ilizingatia na kutumia matokeo ya tafiti hizo na hivyo na kufanikisha kutumia fursa hizo za biashara. Kwa mfano, ushiriki wa TanTrade katikamakongamano mawili ya kibiashara nchini Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo; na ujio wa misafara ya kibiashara kutoka Misri, Uganda, India, China pamoja na mikutano ya kisekta ilitumia taarifa za fursa hizo za biashara.

163. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia TanTrade ilitoa taarifa za biashara kwa Kampuni 3,200 za uzalishaji bidhaa na huduma mbalimbali zinazozalishwa nchini kama sehemu ya mkakati wa kuimarisha uwezo wa upatikanaji wa taarifa za biashara kwa ajili ya kuwezesha kufanyika kwa maamuzi yenye tija ya kukidhi ushindani. Katika kipindi hicho, TanTrade ilipokea na kusambaza majibu ya mauulizi 205 kuhusu upatikanaji wa masoko, bidhaa na mazao

mbalimbali kama vile nafaka, mbogamboga, mazao jamii ya kunde, muhogo, mashudu, viungo, asali, soya, pamba, mbegu za chia, ufuta, alizeti, soyambuzi, samaki, mbaao, na vifaa vya ujenzi, katika soko la Kenya, Uganda, India, China, Rwanda, Congo, Morocco, Jumuiya ya Nchi za Falme za Kiarabu (UAE) na Jumuiya ya Ulaya (EU). Aidha, jumla ya wafanyabiashara 284 waliunganishwa na wanunuzi wa bidhaa za kilimo, uvuvi, misitu na mifugo katika masoko hayo.

**vii) Uendelezaji wa Masoko ya Kimkakati na Biashara Mipakani**

164. **Mheshimiwa Spika;** Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na masoko ya kimkakati kwa ajili ya kukuza biashara na mauzo nje ya nchi kwa maendeleo ya wananchi wake na Taifa kwa ujumla. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imekuwa ikichukua hatua za kuanzisha, kuboresha na kuendeleza masoko ya kimkakati ya mipakani kutokana na umuhimu wa eneo husika ili kurasimisha ufanyaji biashara. Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) inaratibu Mradi wa Ujenzi na Uboreshaji wa Masoko ya Mipakani ya Rusumo (Tanzania/Rwanda) na Tarakea (Tanzania/ Kenya) kuhakikisha wananchi waishio mipakani wananufaika ipasavyo. Jitihada hizo zimekwenda sambamba na mpango wa Wizara wa ujenzi wa masoko ya Kimkakati katika mipaka ya Tunduma (Tanzania/Zambia), Mutukula (Tanzania/Uganda) na Holili (Tanzania/Kenya) kwa kushirikiana na TMEA. Ujenzi wa masoko hayo pamoja na uwepo wa Vituo vya OSBP utasaidia kurahisisha ufanyaji biashara mipakani, kuimarisha usalama wa biashara mipakani na hivyo kuiwezesha Serikali kurasimisha biashara kwa urahisi na kupata taarifa na takwimu muhimu na za uhakika katika biashara za mipakani.

165. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zinazosimamia ufanyaji biashara mipakani imeendelea kuhamasisha na kusimamia utekelezaji wa Sheria, Kanuni na

taratibu za biashara mipakani na kuhakikisha Taasisi za Umma zinawezesha biashara badala ya kukwamisha biashara kati ya nchi na nchi. Timu ya Wizara ikiongozwa na Naibu Waziri Mhe. Injinia Stella Manyanya (Mb) ilifanya ziara ya kutathmini hali ya biashara katika mipaka ya Namanga tarehe 15 Novemba 2019 na ziara katika mkoa wa Mara kuanzia Desemba 2 hadi 5, 2019 katika mpaka wa Sirari, mpaka wa Kilongwe na eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa soko la mpakani la Lemagwe wilayani Tarime. Aidha, Wizara imeendelea kuhamasisha Wafanyabiashara wa mipakani kutoa taarifa juu ya vikwazo, changamoto au kero za kibiashara hasa zile zisizokuwa za kikodi.

166. ***Mheshimiwa Spika;*** Vituo vya Pamoja Mipakani (OSBP) vimeongeza ufanisi wa ufanyaji biashara kwa kuwezesha watu, magari na bidhaa mipakani kukaguliwa kwa urahisi na kwa haraka zaidi hivyo kupunguza muda unaotumiwa na kuwaondolea wafanyabiashara gharama za ziada watumiazo mipakani wakisubiri kupatiwa huduma. Katika kujenga uendeleu wa huduma bora, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka zinazosimamia taasisi za Umma zinazoshughulika na biashara mipakani imeanzisha mfumo wa mawasiliano kwa njia ya mtandao (WhatsApp Group) unaojumuisha Viongozi na watendaji wote mipakani kwa ajili ya kubadilishana taarifa kwa urahisi na haraka lengo likiwa ni kutolea ufumbuzi changamoto zinazojitokeza katika mipaka husika. Aidha, mfumo huo pia unatumiwa na wadau katika sekta ya biashara kutoa taarifa ya vikwazo, changamoto na kero za kibiashara hasa zile zisizokuwa za kikodi (NTBs).

***viii) Kutangaza Bidhaa na Huduma Zinazozalishwa Nchini na Kuwaunganisha Wazalishaji Watanzania katika Masoko Nje na kuongeza ushiriki wa Tanzania katika biashara ya nje***

167. ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia TanTrade imeratibu na kusimamia zoezi la kuwaunganisha wanunuzi wa bidhaa na wazalishaji kwa kufanikisha yafuatayo: - Mkataba kati ya Nchi ya Zimbabwe na Wakala wa Hifadhi



ya Chakula ya Taifa (NFRA) kununua tani 83,000 za mahindi; Mkataba kati ya Kampuni ya Rafael Group ya Mbeya na Kampuni ya Dar Lion ya Ufaransa kuuza tani 360 za mchele; Mkataba kati ya Bakhresa Food Products na Umoja wa Wafanyabiashara wa Matunda Buguruni wa kununua ukwaju tani 30 wenye thamani ya Shilingi milioni 18; Mkataba kati ya Kampuni ya Eleven Agri na World Farmers Tanzania Ltd, kununua unga wa Ubuyu tani 50; Mkataba kati ya Kampuni ya Bakhresa Food Products na Asasi ya Sustainable Agriculture Tanzania Ltd, kununua unga wa ubuyu tani 20, machungwa tani 5 na nazi tani 5; na Kiwanda cha ALAF kilipata oda ya kuuza tani 1,200 za chuma nchini Rwanda.

168. **Mheshimiwa Spika**; Makubaliano kwa Kampuni 3 kufanya biashara ya mbogamboga na matunda zenye thamani ya jumla Shilingi 8,376,235,793.36 kwa mwaka yalifanyika. Kampuni husika ni TanzaNice ambayo ilipata oda ya kuuza tani 700 za parachichi zenye thamani ya Euro 3,250,000 kwenye nchi za Ufaransa, Ujerumani, Uingereza na Uholanzi; Frank Horticultural & Timber Company Ltd ilipata oda ya kuuza parachichi, maharage machanga (green beans), njegere changa (snow peas) na njegere mbichi (Garden peas) zenye thamani ya Dola za Marekani 1,980,000 kwenda Denmark, Dubai, Kuwait na Ubelgiji; na Kampuni ya Hortanzia ilipata oda ya kuuza kitunguu jani (chives) yenye thamani ya Euro 2,000 kwenda Ujerumani. Aidha, TanTrade kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) kusimamia mauzo ya tani 215,484.90 za korosho kwa njia ya minada kwa msimu wa Mwaka 2019/2020; Kuunganisha wadau wa muhogo na kampuni yenye uwezo wa kununua wastani wa tani 100 za muhogo mbichi kwa wiki kutoka kwa wakulima wadogo; na kushiriki katika mnada wa mauzo ya miti katika mashamba ya miti ya Serikali yaliyopo Mtibwa katika Mkoa wa Morogoro, na Longuza, Muheza katika Mkoa wa Tanga ambapo mauzo ya jumla ya Shilingi Bilioni 4.77 yalifanyika.

169. **Mheshimiwa Spika**, Baada ya mikutano ya B2B iliyofanyika katika maonesho ya 43 ya Kimataifa ya Biashara kampuni kadhaa zilifanikiwa kuendelea kufanya biashara. Kampuni hizo ni pamoja na Dow elef Agri yenye bidhaa za

Pilipili zenye thamani ya Shilingi Milioni 400, Dar Carton yenye bidhaa ya Mihogo zenye thamani ya Shilingi Milioni 90, Follow Honey yenye bidhaa ya Nta yenye thamani ya Shilingi Milioni 900 na Shilingi Milioni 390 za bidhaa ya asali. Kampuni hizo zina fursa ya kuuza kwa miezi 10 toka kumalizika kwa Maonesho ya 43 ya DITF.

170. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia TanTrade ilifanikiwa kushiriki maonesho ya nje na kutangaza bidhaa za Tanzania nchini China na Ujerumani. Katika Maonesho ya China yaliyofanyika Beijing, TanTrade ilifanikiwa kupata Kampuni ya Jingsu Overseas Group Company Limited ambayo inajihusisha na uuzaji wa nyama ili kuitembelea Tanzania na kuwakutanisha na wauzaji wakuu wa nyama. Aidha, kikao cha maandalizi ya kutambua mahitaji ya mnunuzi kwa ajili ya kukidhi fursa ya soko hilo kilifanyika na wauzaji kubainishwa. Katika maonesho ya Ujerumani ya Fruit Logistica, TanTrade iliambatana na msafara wa kampuni 18 na katika ushiriki kampuni 20 za Ujerumani zilionyesha uhitaji wa bidhaa za matunda, hivyo kuunganishwa na kampuni za kitanzania. Aidha, kulipatikana kampuni 20 nyingine za teknolojia ambazo zilitoka mataifa mbalimbali ya Ulaya na Amerika ambapo kampuni hizo ziliingia makubaliano ya kibiashara na kampuni tano (5) za Kitanzania.

**ix) Uimarishaji Ushindani katika Soko na Biashara ya Ndani**

171. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) Mwaka 2019, limetoa leseni za ubora 358 ikilinganishwa na leseni 259 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 38.2. Ongezeko hilo limetokana na mafunzo yaliyotolewa kwa wazalishaji mbalimbali kuhusu umuhimu wa kuzingatia ubora wa bidhaa. Aidha, mafunzo 108 ya udhibiti ubora yalitolewa kwa washiriki 7,464 ikilinganishwa na mafunzo 59 yaliyotolewa kwa washiriki 4,208 mwaka 2018.

172. **Mheshimiwa Spika;** Vilevile Wizara kupitia Wakala wa Vipimo imeendelea kutoa huduma za kuhakiki usahihi wa vipimo na mifumo ya upimaji katika Sekta ya

Biashara, Afya, Usalama na Mazingira kwa lengo la kumlinda mlaji. Katika kipindi cha mwaka 2019, Wakala imekagua vipimo 841,518 ikilinganishwa na vipimo 732,912 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 14.8. Hii imetokana na kuongezeka kwa vitendea kazi vikiwemo magari na vifaa vya kisasa vya kupima dira za maji na mizani ya kuhakiki usahihi wa vipimo vya madini. Vilevile, Wakala imetoa leseni za ufundi na uundaji wa vipimo kwa wadau 300 mwaka 2019 ikilinganishwa na wadau 200 mwaka 2018.

173. **Mheshimiwa Spika;** Vilevile, Mwaka 2019, Wakala imeongeza uwezo wa kuhakiki magari yanayobeba mafuta kutoka wastani wa magari nane na kufikia magari 70 kwa siku. Hii imetokana na kukamilika kwa ujenzi wa Kituo cha Kisasa cha Uhakiki wa Magari kilichopo Misugusugu-Kibaha. Aidha, Wakala umeongeza Kituo cha Tarakea mkoani Kilimanjaro kwa lengo la kuboresha udhibiti wa bidhaa zinazofungashwa mipakani na hivyo kuwa na jumla ya vituo nane.

174. **Mheshimiwa Spika;** Katika kuhakikisha udhibiti wa bidhaa bandia nchini, Mwaka 2019 Serikali kupitia Tume ya Ushindani ilikagua makasha 3,260 ya kusafirishia mizigo ambapo makasha 114 yalibainika kuwa na bidhaa bandia. Bidhaa bandia zilizokamatwa zilikuwa na alama zilizogushiwa pamoja na kukosa alama za utambulisho wa bidhaa, anuani ya mzalishaji na nchi ya uasili ilipotengenezwa. Aidha, Tume ilifanya kaguzi 32 za kushtukiza katika ghala na maduka mbalimbali kwa lengo la kubaini bidhaa bandia. Tume ilifanikiwa kukamata bidhaa bandia ikiwa ni pamoja na vifaa vya ujenzi (pisi 12,571); mafuta na vipodozi (pisi 850); vifaa vya ofisi (pisi 6,652); vipuri na vilainishi (dazeni 129); nguo na viatu (jozi 6,906) pamoja na vifaa vya elektroniki (pisi 3,750) na kuchukua hatua kwa mujibu wa Sheria.

x) **Uendelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala**

175. **Mheshimiwa Spika;** Wizara imeendelea kuhamasisha na kusimamia matumizi ya Mfumo wa

Stakabadhi za Ghala kwenye mazao ya kilimo. Hadi sasa, jumla ya mazao 10 yameingizwa katika Mfumo huo ambayo ni Mbaazi, Dengu, Soya, Mpunga, Ufuta, Kakao, Kahawa, Alizeti, Korosho, na Mahindi. Katika msimu wa 2019, jumla ya Tani 5,926.726 za ufuta zimeuzwa kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala, Mbaazi Tani 775.543, Dengu Tani 80.804, Soya Tani 2,892.004, Kahawa Tani 1,406.205 na Kakao Tani 6,603.240. Aidha, hadi kufikia Desemba 22, 2019 jumla ya Tani 187,273. 252 za kahawa zimeuzwa kupitia minada 43 na ghala 21 zimesajiliwa na kupewa leseni ya kushiriki katika Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa zao la korosho katika msimu wa mwaka 2019.

176. **Mheshimiwa Spika;** Katika msimu wa Mwaka 2019/2020, jumla ya leseni 55 zilitolewa kwa waendeshaji wa ghala katika mazao mbalimbali nchini. Kati ya hiyo, sekta ndogo ya Zao la Korosho leseni 34; Zao la Kahawa leseni tano; Zao la Ufuta leseni sita; Zao la Kakao leseni mbili; Zao la Soya leseni nne; Zao la Mbaazi leseni mbili ; Zao la Dengu leseni moja; Zao la Mpunga leseni moja. Pia, Bodi imepewa mamlaka ya kutoa leseni kwa Mameneja Dhamana pamoja na Wakaguzi wa Ghala. Hivyo, kwa mwaka 2019/2020, Bodi imetoa jumla ya leseni tatu kwa Meneja Dhamana katika Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

177. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala na kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeandaa miongozo minne mipya ifuatayo:

Mwongozo Namba 10 wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika zao la Soya Toleo Namba 1; Mwongozo Namba 11 wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala zao la Dengu Toleo Namba 1; Mwongozo Namba 15 wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala zao la Mbaazi Toleo Namba 1; na Mwongozo Namba 16 wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala zao la Pamba Toleo Namba 1. Aidha, miongozo miwili ilifanyiwa marejeo kabla ya kuendelea kutumika katika mazao husika ambayo ni: Mwongozo Namba 1 wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala Sekta Ndogo ya Korosho Toleo Namba 10; na Mwongozo

Namba 9 wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala Sekta Ndogo ya Ufuta Toleo Namba 4. Kuandaliwa kwa miongozo hiyo kutasaidia kikamilifu utekelezaji wa Mfumo huo katika mazao hayo mapya yaliyoingizwa.

178. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) kwa kushirikiana na Mfuko wa Kuimarisha Sekta ya Fedha (FSDT), Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), Soko la Bidhaa Tanzania (TMX),Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), taasisi za fedha za CRDB na NMB, Shirika la Bima la Taifa (NIC) na Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) ziliunda Jukwaa Jumuishi kwa lengo la kuhamasisha na kutoa elimu kuhusu mifumo rasmi ya kifedha kwa mkulima na huduma za kifedha ili kuwawezesha kuendeleza shughuli zao. Uhamasishaji huo ulifanyika katika Mkoa wa Kagera Wilaya za Karagwe, Bukoba (M), Bukoba (V), Misenyi, Kyerwa, Muleba, Ngara na Biharamulo kwa kuhamasisha na kutoa elimu katika AMCOS na wakulima waliopo katika Wilaya hizo. Zoezi hilo liliambatana na ufunguzi wa akaunti ambapo zaidi ya wakulima 3,200 walipata elimu ya huduma za kifedha na baadhi yao kuweza kufungua akaunti na kuunganishwa na huduma nyingine za kifedha kupitia simu kama vile Simu Account na NMB mobile.

179. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kwa kushirikiana na Bodi ilihamasisha na kutoa mafunzo ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika Mkoa wa Manyara Wilaya ya Babati na Mkoa wa Dodoma Wilaya ya Kondoa. Vilevile, Elimu ilitolewa kwa viongozi wa Serikali Mkoa wa Dodoma, wakulima 60 katika Wilaya ya Babati na wakulima 70 katika Wilaya ya Kondoa. Aidha, Elimu ya Mfumo ilitolewa kwa wakulima wa mpunga wa Pawaga Iringa chini ya Kampuni ya Tuungane Company Limited wanaoendesha ghala la IGODI KAVU ambapo jumla ya wakulima 34 walipata mafunzo ya kina ya namna ya kuendesha Mfumo.

180. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala na kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa ilikamilisha ujenzi wa

ghala na kuweza kulitumia katika Mfumo wa Stakabadhi kuhifadhi zao la korosho. Aidha, ghala la kuhifadhi mazao lililojengwa kupitia Mradi wa MIVARF Wilayani Kondo, limeweza kutumika kwa mara ya kwanza katika msimu wa 2019/2020 katika Mfumo kwa kufanya biashara.

**xi) Udhhibitiwa Ubora na Viwango vya Bidhaa zinazozalishwa Nchini**

181. **Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Wizara kupitia TBS imekamilisha viwango muhimu 228 ambavyo ni sawa na asilimia 50.7 ya lengo la kutayarisha viwango 450 kwa mwaka. Viwango hivyo ni katika kilimo, chakula, uhandisi na viwango vya vifungashio mbalimbali. Kati ya viwango 228 vilivyokamilika, viwango 31 ni katika nyanja za uhandisi mitambo (mechanical), 16 katika nyanja ya kemikali (chemical), 19 katika nyanja ya uhandisi umeme (electro technical), 27 katika nyanja za nguo na ngozi (textile and leather), viwango 17 katika nyanja ya mazingira (environmental), 17 katika nyanja ya madini (Mining and minerals) na 101 katika sekta ya kilimo na chakula (food and agriculture). Pia, Shirika liliendelea kusimamia viwango vya kitaifa kwa kutumia mifumo iliyopo ya kuhakiki ubora (Certification Schemes).

182. **Mheshimiwa Spika;** Kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, jumla ya leseni 366 za nembo ya ubora ya TBS zilitolewa ambayo ni sawa na asilimia 101.7 ya lengo la kutoa leseni 360 kwa mwaka 2019/2020. Miongoni mwa leseni hizo, leseni 126 zilitolewa kwa wajasiriamali wadogo wanaozalisha kashata, mafuta ya kula, pombe, unga wa ngano, unga wa muhogo na lishe, maji ya kunywa, tindikali ya betri, kachumbari, mvinyo, pombe isiyotokana na nafaka, siagi ya karanga, pilipili, kripsi za maembe na kripsi za ndizi. Shirika limeendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali (SMEs) na wadau mbalimbali katika dhana nzima za kuzingatia mifumo ya ubora ili kuzalisha bidhaa zenye ubora.

*xii) Udhibitiwa Ubora na Viwango vya Bidhaa Zinazozalishwa Nje ya Nchi*

183. **Mheshimiwa Spika;** Kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Wizara kupitia TBS imetoa jumla ya vyeti vya ubora (Certificate of Conformity - CoCs) 25,821 kwa shehena za bidhaa zitokazo nje ya nchi; hii ni sawa na asilimia 68.0 ya matarajio ya kutoa jumla ya vyeti vya ubora wa bidhaa 38,000 kwa mwaka mzima. Aidha, jumla ya vyeti vya ukaguzi wa magari 28,820 vilitolewa sawa na asilimia 70.3 ya malengo ya kufikisha jumla ya vyeti 41,000. Jumla ya sampuli 20,854 zilipimwa katika maabara mbalimbali za Shirika kwa lengo la kuhakiki ubora wake, hii ni sawa na asilimia 90.7 ya lengo la kupima sampuli 23,000 kwa mwaka. Jumla ya mitambo 7,157 ilifanyiwa Ugezi, hii ni sawa na asilimia 95.4 ya lengo la kufanyia ugezi mitambo 7,500 kwa mwaka.

184. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia WMA imeendelea kufanya kazi ya udhibiti wa bidhaa zilizofungashwa mipakani. Wizara imeongeza kituo cha Tarakea Mkoani Kilimanjaro hivyo kufanya Wizara kuwa na jumla ya vituo nane vya ukaguzi ambavyo ni Sirari (Mara), Mutukula(Kagera), Namanga (Arusha), Holili (Kilimanjaro), Tunduma (Songwe), Tarakea (Kilimanjaro), Horohoro (Tanga) na Kasumuru (Mbeya). Vilevile, Wizara iliendelea na usimamizi wa mafuta yanayoingia nchini jamii ya petrol na mafuta ya kula (edible oil) ambapo kwa sasa Wizara inahudumia bandari za Mtwara, Tanga na Dar es Salaam.

185. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia TBS, imeendelea kutoa mafunzo kwa Wajasiriamali (SMEs) na wadau mbalimbali katika dhana nzima za kuzingatia mifumo bora ili kuzalisha bidhaa zenye ubora. Kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, jumla ya mafunzo na semina 87 zilitolewa; idadi hii ni sawa na asilimia 96.7 ya lengo la kutoa mafunzo na semina 90 kwa mwaka. Mafunzo na semina hizo zilitolewa kwa wajasiriamali wadogo pamoja na wadau mbalimbali wapatao 6,328 katika mikoa ya, Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Katavi, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi,

Manyara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, na Pwani, Ruvuma, Tanga.

186. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia Wakala wa Vipimo imekagua na kuhakiki idadi ya vipimo 626,552 ikiwa ni sawa na asilimia 91 ya lengo la kukagua vipimo 686,765 vilivyokadiriwa katika kipindi cha Julai, 2019 hadi mwezi Februari, 2020. Aidha, WMA imeendelea kutoa elimu kwa wakulima wa zao la korosho katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Ruvuma. Pia, Wakala imeendesha zoezi la ukaguzi (wa kawaida na wa kushitukiza) wa mizani itumikayo kupimia zao la korosho. Katika kaguzi hizo jumla ya mizani 1,924 ilikaguliwa ambapo kati ya mizani hiyo, mizani 326 ilikutwa na makosa na kuamriwa kurekebisha kabla ya kuendelea kutumika tena. Aidha, Wakala imeendelea kukagua bidhaa zilizofungashwa ili kuhakiki usahihi wa kiasi kilichotamkwa. Baadhi ya bidhaa zilizokaguliwani ni vyakula (unga, Mchele, mafuta ya kula, Maji, maziwa na vinywaji), vilainishi, saruji, rangi, mitumba, mabati na nondo. Hivyo, kufanya malengo kufikiwa kwa zaidi ya asilimia 90.

187. **Mheshimiwa Spika;** Jumla ya taarifa/ maandiko 44 yalitolewa kwenye magazeti mbalimbali katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020. Pia, Vipindi Saba (7) vya Redio, vipindi tisa (9) vya TV, na mikutano mitatu (3) (press conference) ilifanyika. Aidha, Wakala imeshiriki katika maonesho ya Sabasaba, Nanenane na maonesho ya Viwanda. Pia, Wakala ilitoa elimu kwa wakulima wa korosho sambamba na zoezi la ukaguzi lililofanyika wakati wa msimu wa ununuzi wa korosho katika Mikoa ya Mtwara, Ruvuma, Pwani na Lindi ambapo Elimu ilitolewa kwa Wakulima ma vyama vya Msingi (AMCOS) 725. Elimu ilihusu Matumizi sahihi ya Vipimo ili waweze kutambua mizani sahihi na iliyohakikiwa na Wakala wa Vipimo. Pia Wakulima walipatiwa namba ya bure ya WMA ambayo ni 0800110097 ili waweze kutoa taarifa kwa Wakala wa Vipimo Makao Makuu pale wanapokutana na changamoto au wanapobaini matumizi yasiyo sahihi ya Mizani katika vyama vya Msingi. Ukaguzi uliofanyika ni Ukaguzi wa Mizani ya Korosho.



**xiii) Udhhibiti wa Ushindani Usio Haki katika Soko**

188. **Mheshimiwa Spika;** Wizara kupitia Tume ya Ushindani (FCC) imeendelea kufanyia kazi jumla ya mashauri tisa (9). Mashauri hayo yanahusu makubaliano yanayofifisha ushindani (5), miunganiko ya kampuni yaliyofanyika bila kuiarifu Tume (2), makubaliano ya siri (1) na matumizi mabaya ya nguvu (1). Katika mashauri yanahusu makubaliano yanayofifisha ushindani (Anti-Competitive Agreements) kutoka katika sekta ndogo ya Tumbaku, Tume imeendelea kufanya majadiliano na mmoja wa watuhumiwa aliyeomba kumalizika kwa shauri lake kwa njia ya suluhu (settlement proceeding). Aidha, Tume inaendelea kufanya uchambuzi wa utetezi wa kimaandishi wa watuhumiwa katika mashauri yaliyobaki. Katika mashauri yanayohusu matumizi mabaya ya nguvu za soko (Abuse of Dominance) kutoka katika Sekta Ndogo za Kufukiza na Sekta ya Saruji, Tume imeandaa rasimu ya maamuzi ya awali (provisional findings) kwa shauri kutoka Sekta Ndogo ya Kufukiza. Tume inaendelea kufanya uchunguzi kwa shauri kutoka Sekta Ndogo ya Saruji.

189. **Mheshimiwa Spika;** Tume inaendelea kufanya uchunguzi dhidi ya shauri linalohusu makubaliano ya siri (cartel) kutoka katika Sekta Ndogo ya Chuma. Aidha, katika mashauri yanayohusu muungano wa kampuni bila kuiarifu Tume (Un-notified Merger) kutoka katika Sekta Ndogo ya Nishati Mbadala na Sekta ya Usafirishaji, Tume ilitoa hati ya shauri (statement of case) pamoja na maamuzi ya awali (provisional finding) kwa shauri kutoka Sekta Ndogo ya Nishati Mbadala. Aidha, katika shauri kutoka katika Sekta ya Usafirishaji, mtuhumiwa ameahidi kutekeleza maamuzi ya makubaliano (settlement agreement).

190. **Mheshimiwa Spika;** Pia, Tume imefanya kaguzi katika Bandari ya Dar es Salaam na ICDs ambapo jumla ya makasha elfu moja mia nne thelathini na moja (1,431) yalikaguliwa. Kati ya hayo, makasha arobaini na nane (48) yalikatwa kwa kukiuka Sheria ya Alama za Bidhaa ya Mwaka 1963 (kama ilivyorekebishwa). Bidhaa zilizokatwa katika kaguzi hizo ni pamoja na vifaa vya umeme kama

(fridge, fridge guard na viyoyozi), vifaa vya ujenzi, miswaki yenye nembo ya Goldegate, vipuri vya magari na pikipiki, vikombe, viatu (vya wanaume na wanawake), vitenge, box tupu zenye nembo ya Vim na Harpic.

191. **Mheshimiwa Spika;** Tume imefanya kaguzi za kustukiza (raids) mara kumi na tisa (19) katika Mkoa wa Dar Es Salaam kwenye bidhaa za wino wa kudurufu karatasi (toner) zenye alama ya HP na CANON, nguo na viatu 127 vyenye alama ya HUGO, BOSS na NGK, dawa za nywele zenye nembo ya SUPER BLACK, bidhaa za tochi zanye alama ya TOURCH, nyembe zenye alama ya RUNGU MAX na SUPER MAX pamoja na fulana (T-shirts) zenye alama ya AFRICAN BOY. Kupitia kaguzi hizo za kushtukiza, bidhaa bandia zenye thamani ya Shilingi 1,031,163,532 zilikamatwa kwa kukiuka Sheria ya Alama za Bidhaa ya Mwaka 1963 kama ilivyorekebishwa.

**xiv) Kukamilisha Sera ya Ubora**

192. **Mheshimiwa Spika;** Wizara inaendelea na maandalizi ya Kutunga Sera ya Taifa ya Ubora ambayo itasaidia wazalishaji wakubwa kwa wadogo kuweza kukidhi viwango vya Kitaifa na Kimataifa na hatimaye kufikia masoko ya nje ya nchi. Rasimu ya Sera pamoja na Mkakati wake wa utekelezaji umekamilika. Hatua inayofuata ni kupata maoni ya wadau mbalimbali kuhusiana na Rasimu hizo zilizokwishaandaliwa ili hatimaye Serikali ifanye maamuzi ya mwisho.

**xv) Mikataba/Itifaki na Marekebisho ya Sheria za Taasisi**

193. **Mheshimiwa Spika,** Itifaki ya Marrakesh iliridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa 16 uliofanyika Jijini Dodoma kuanzia tarehe 3 hadi 13 Septemba 2019. Itifaki ya Marrakesh inalenga kuwezesha upatikanaji wa kazi zilizochapishwa kwa watu wasioona, wenye uoni hafifu, ulemavu unaofanya mtu kushindwa kusoma wa mwaka 2013 (The Marrakesh Treaty to

Facilitate Access to Published Works for Persons who are Blind, Visually Impaired or Otherwise Print Disabled 2013) ili kuwawezesha wanufaika wa mkataba huo kuweza kupata wasaa wa machapisho na vifaa vya kuwawezesha kupata elimu kwa njia rahisi. Wizara kwa kushirikiana na COSOTA na COSOZA iliandaa Mpango kazi wa utekelezaji na azimio la kuridhia Itifaki ya Marrakesh na kuwasilisha Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt John Pombe Joseph Magufuli alitia saina azimio la Itifaki hiyo mnamo Januari, 2020 na Hati hiyo kuwasilishwa WIPO mwezi Machi, 2020. Hatua za utekelezaji wa mkataba wa Itifaki hiyo unatarajia kuanza kwa kufuata mpango kazi ulioandaliwa.

#### **xvi) Athari za Mlipuko wa Virusi vya Corona katika Sekta ya Biashara**

194. **Mheshimiwa Spika;** Kwa kuzingatia kuwa Sekta ya Biashara ni mtambuka, mlipuko wa homa ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona (Covid-19) umesababisha sekta mbalimbali za uchumi kuathirika na kiasi kikubwa kuathiri sekta hii. Kutokana na mlipuko ugonjwa huo, Mamlaka za nchi zimejazimika kuchukuwa hatua mbalimbali kwa ajili ya kujikinga na kupambana na janga hili. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni kusitishwa kwa usafiri wa anga kuingia katika nchi mbalimbali na hatua zingine ambazo kwa kwa kiasi kikubwa zimeathiri shughuli za kibiashara. Kimsingi Sekta zote za kiuchumi zimeathirika na miongoni mwao ni Sekta ya Viwanda na Biashara. Fursa za masoko zinatokana na Tanzania kuwa mwanachama wa Shirika la Biashara Duniani (WTO), Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Tanzania pia inategemea Jumuiya ya Ulaya (EU) kama soko la mazao na bidhaa za mazao, Asia kupitia (Quota Free Duty Free - QDFD) China, India na Japan na katika soko la AGOA bidhaa inaouza huko kwa wingi almasi, dhahabu, chai, kahawa, maua na viungo (spices).

195. **Mheshimiwa Spika;** Baadhi ya mazao ya kimkakati ikiwemo pamba, korosho na kokoa bei zake

zimeshuka. Katika kipindi cha mwezi Februari na Machi 2020, bei ya pamba duniani imeshuka kwa kiasi cha asilimia 12; bei ya kakao imeshuka kwa asilimia 22; na kahawa imeshuka kwa asilimia 5 (Arabika) na asilimia 3.5 (Robusta). Kushuka kwa ununuzi wa kahawa kumesababishwa kwa kiasi kikubwa na kufungwa kwa maduka nchini China, Ulaya na Marekani kutokana na zuio la kutotoka nje. Mfano, Kampuni ya Starbucks imefunga maduka 2,150 kati ya 4,300 nchini China. Aidha, mauzo (volumes) ya mazao na bidhaa za kilimo yameshuka. Kiwango cha ununuzi wa kakao kilishuka kutoka tani 116,440 mwezi Februari 2020 hadi kufikia tani 38,354 mwezi Machi 2020 ikiwa ni sawa na asilimia 67.1.

196. **Mheshimiwa Spika;** Wazalishaji wa mazao Mbogamboga, Matunda, Maua na Viungo (horticulture) wamekuwa kwa miaka mingi wakitegemea soko la nje hasa Ulaya, Marekani na Asia. Kutokana na mlipuko wa ugojwa huo na kufungwa kwa mipaka, kumeathiri biashara hiyo ambayo mazao yake yanaharibika kwa wepesi. Sekta hiyo imeathirika kama ifuatavyo: Mauzo ya mazao ya mbogamboga na matunda nchini umeshuka kwa asilimia hamsini (50). Hali hiyo imesababishwa na kushuka kwa mahitaji ya bidhaa hizo hususan katika soko la nje, na kupungua kwa safari za ndege. Mfano, Shirika la KLM limepunguza safari zake kutoka safari 7 kwa wiki hadi 3. Hata hivyo, uhitaji wa mazao hayo katika masoko ya ndani ni mdogo na kukosa masoko mbadala ya kupeleka bidhaa zao zaidi ya kuendelea kuzihifadhi kwa muda mfupi na baadaye kuziteketeza kabisa

#### **4.2.5. Maendeleo ya Rasilimali Watu na Utoaji Huduma**

197. **Mheshimiwa Spika;** Wizara ilipokea IKAMA ya watumishi kwa mwaka 2019/2020 kutoka Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora ambayo inatoa mwongozo wa kuajiri baada ya kibali cha kuajiri kutolewa. Aidha, Wizara imepokea muundo mpya ambao utasaidia katika kujaza nafasi za uteuzi zilizoko wazi.

198. **Mheshimiwa Spika;** Katika kuwajengea uwezo watumishi wake, Wizara imepeleka watumishi saba katika vyo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi katika mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Kati ya hao, mtumishi mmoja anashiriki Shahada ya Uzamivu (Phd), watumishi watano wanashiriki mafunzo ya Shahada ya Uzamili (Masters Degree), na mmoja anashiriki mafunzo ya Diploma ya Utunzaji Kumbukumbu. Aidha, watumishi 17 wameweza kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi katika kozi mbalimbali zilizochangia katika kujenga uwezo na kuongeza ufanisi katika maeneo yao ya kazi.

199. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka 2019/2020, Wizara imewapeleka watumishi wawili katika mafunzo ya muda mfupi ya ujasiriamali ambao wamestaafu katika Utumishi wa Umma, ikiwa ni kuwaandaa na maisha baada ya kustaafu. Aidha, watumishi hao tayari wamekwisha andaliwa nyaraka zao muhimu na kuwasilishwa katika mamlaka husika kwa ajili ya uandaaji wa mafao yao kwa wakati.

200. **Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha mwaka 2019/2020, Wizara imefanikiwa kufanya kikao kimoja cha Kamati Maalum ya Maadili ya Wizara kikilenga kupanga mikakati ya kudumisha uadilifu kwa watumishi wa Wizara. Pia kupitia vikao vya idara vinavyofanyika kila mwezi, elimu imetolewa kwa watumishi athari za vitendo visivyo na uadilifu kazini vikiwemo vya rushwa lakini pia kusisitiza uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya kiutumishi wakati wa kutoa huduma.

201. **Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka 2019/2020, Wizara imeendelea kutoa huduma ya lishe bora na posho ya usafiri kila mwezi kwa watumishi saba (7) wanaoishi na Virusi vya UKIMWI ambao wamejiweka wazi kwa mujibu wa Mwongozo wa Serikali. Wizara pia iliweza kushiriki katika semina zilizofanyika kuanzia tarehe 27 Novemba 2019 na kufikia kilele siku ya maadhimisho ya siku ya kimataifa ya UKIMWI tarehe 1 Desemba, 2019 iliyofanyika jijini Mwanza.

202. **Mheshimiwa Spika;** Katika kuendelea na jitihada za kupambana na kujikinga maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI (VVU) na Magonjwa Sugu yasiyoambukiza (MSY) kazini. Wizara imeweza kufanya kikao kimoja cha Kamati Maalum ya Masuala ya UKIMWI na Magonjwa Sugu yasiyoambukiza (MSY) kilichofanyika tarehe 21 Januari, 2020. Aidha, Wizara inatoa vifaa tiba na vifaa kinga kwa watumishi wake bure pamoja na elimu kwa watumishi kujikinga yanaendelea kutolewa.

#### **4.2.6. Ukaguzi wa Ndani**

203. **Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka wa fedha wa 2019/2020, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kulingana na Sheria, miongozo na kanuni zilizowekwa. Katika kuhakikisha kuwa kunakuwepo kwa matumizi sahihi ya rasilimali za serikali, Wizara imefanya ukaguzi wa fedha, rasilimali watu na ununuzi na kuhakikisha kwamba sheria, kanuni na taratibu zinafuatwa na hatimaye Wizara imepata hati safi ya Ukaguzi. Aidha, Kamati ya ukaguzi ya Wizara ilifanya vikao vinne ili kupitia taarifa za hesabu pamoja na ukaguzi na kutoa ushauri unaostahili kwa Afisa Masuuli.

#### **4.2.7. Ununuzi na Udhhibiti wa Matumizi ya Fedha**

204. **Mheshimiwa Spika;** Katika Mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara kupitia Kitengo cha Ununuzi kiliweza kutekeleza yafuatayo:- Kusimamia shughuli za ununuzi wa bidhaa na huduma kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi Na.7 ya mwaka 2011 na kanuni zake GN Na, 446 ya mwaka 2013, kama zilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2016 pamoja na miongozo inayotolewa na Mamlaka ya Udhhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA); Kuandaa Mpango wa Ununuzi kwa mwaka fedha 2019/2020; Kuwezesha Watumishi watatu (3) kupata mafunzo ya mfumo wa ununuzi kwa njia ya kielektroniki Tanzania Electronic Procurement system(TANePS); Kuratibu vikao vitatu (3) vya Bodi ya Zabuni ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020; Kuandaa taarifa za ununuzi za kila mwezi, robo pamoja na taarifa ya mwaka na kuziwasilishwa

Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA); na Kufanya uhakiki mali za Wizara na kuhisha taarifa za Daftari la Mali la Wizara kwa mujibu wa muongozo wa mali za Serikali wa mwaka 2019 pamoja na Sheria ya Fedha Na. 6 ya mwaka 2001 na Kanuni zake, GN.132 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2004.

#### 4.2.8. Mawasiliano Serikalini

205. *Mheshimiwa Spika*; Katika mwaka wa fedha 2019/2020 kitengo kimeendelea kutoa elimu na kuhabarisha Umma kupitia vyombo vya Habari ikiwemo Radio, Televisheni, Magazeti, Majarida, Mitandao ya Kijamii na kupitia maonesho ya Biashara yanayofanyika nchini. Aidha, Kitengo kimekamaliza Makala (Documentary) inayohusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano katika sekta ya Viwanda na Biashara ambayo inarushwa kupitia Televisheni mbalimbali za hapa nchini.

#### 4.2.9. Huduma za Sheria

206. *Mheshimiwa Spika*; Katika mwaka 2019/2020, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanya Marekebisho ya Sheria tatu. Sheria hizo ni:- Sheria ya Viwango Sura 130 ili kuhamishia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) majukumu ya chakula na vipodozi kutoka iliyokuwa TFDA (TMDA ya sasa) ikiwa ni utekelezaji wa Andiko la BLUEPRINT; Sheria ya Makampuni Sura 212 ili BRELA ibaki na majukumu ya makampuni yanayohusika na biashara tu kama ilivyo dhamana ya Wizara; na Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Sura, 218 kwa kuiwezesha COSOTA kufifilisha makosa mbalimbali, kuboresha adhabu chini ya sheria hiyo kuendana na muda wa sasa na kuitambua re-sale right.

207. *Mheshimiwa Spika*; Pia, Wizara imefanya upekuzi na kutangaza kwenye Gazeti la Serikali Alama mbalimbali za Viwango chini ya Sheria ya Viwango, Sura 130 ili kumlinda mlaji na mtumiaji wa bidhaa na huduma mbalimbali Tanzania.

#### 4.2.10. TEHAMA na Takwimu

208. *Mheshimiwa Spika*; Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara ilitekeleza yafuatayo:- Kusimamia na kuratibu matumizi bora, salama na sahihi ya miundombinu na Rasilimali za TEHAMA; na Kuimarisha ulinzi wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA kwa kufanya tathmini ya ulinzi wa mifumo ya TEHAMA. Tathmini hiyo ilifanywa na Wakala ya Serikali Mtandao (eGA) mwezi Oktoba, 2019 na kubaini kuwa mifumo ya TEHAMA wizarani ina ulinzi na usalama wa kutosha na kuipa wizara alama ya utoshelevu ambao ni zaidi ya asilimia 40.

### 5. MWELEKEO NAVIPAUMBELE VYA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA

#### 5.1. Mwelekeo wa Sekta ya Viwanda na Biashara

209. *Mheshimiwa Spika*; Mtazamo na mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi kuhusu maendeleo ya viwanda na biashara nchini, unalenga kujenga uchumi wa viwanda utakaowawezesha Watanzania kufikia na kunufaika na uchumi wa kati ifikapo 2025. Hatua hiyo itawezesha Watanzania kutumia fursa za kiuchumi na kijamii katika mifumo iliyoboreshwa na inayozingatia haki na utawala bora. Ni dhamira ya nchi yetu kumfanya kila Mtanzania kuwa na maisha bora na kunufaika na rasilimali na fursa zilizopo na zinazojitokeza. Hivyo, ni jukumu letu sote kuwaandaa na kuwawezesha Watanzania kuchangamkia fursa zilizopo ipasavyo.

#### i) *Kuimarisha Taasisi za Utafiti na Maendeleo ya Teknolojia na Uwekezaji*

210. *Mheshimiwa Spika*; Katika kuendeleza uchumi wa viwanda, Serikali inaimarisha taasisi zake ili ziweze kukidhi na kuhimili mahitaji ya maendeleo na ujenzi wa viwanda nchini. Wizara inajizatiti kuimarisha Taasisi za Utafiti na Maendeleo ya Teknolojia yaani TIRDO, TEMDO na CAMARTEC, kwa kupitia upya na kwa kina majukumu na



miundo ya kisheria ya taasisi hizo. Lengo ni kuzifanyia maboresho mahsusi na itakapoonekana inafaa, zitafanyiwa maamuzi ya kimuundo ikiwemo kuziunganisha ili ziweze kuwa na tija na ufanisi katika kuleta mwendelezo wa mafanikio ya taasisi hizo na pia kuongeza nguvu katika kuendeleza viwanda nchini.

211. **Mheshimiwa Spika;** Serikali itajielekeza katika kuimarisha taasisi za uwekezaji nchini hususan EPZA na NDC ili ziwe mihimili na nguzo za uwekezaji katika viwanda ambavyo ni muhimu katika kujenga uchumi wa Taifa lakini wakati mwingine sekta binafsi haiko tayari kuwekeza. Msukumo ukiwa ni kujenga viwanda mama, viwanda vya kimkakati na viwanda ambavyo kutokana na unyeti wake haviwezi kuachiwa sekta binafsi.

**ii) Kuimarisha SIDO**

212. Mheshimiwa Spika; Kwa kutambua umuhimu na mchango wa Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo katika uchumi na hususan ujenzi wa viwanda, Serikali itachukua hatua za makusudi kuimarisha ujasiriamali nchini. Kipaumbele kitakuwa katika kuimarisha taasisi ya SIDO kwa kupitia upya muundo wake na kujengea uwezo ili iweze kubeba ipasavyo dhamana ya uendelezaji wa viwanda vidogo na biashara ndogo inayowabeba Watanzania walio wengi.

**iii) Utoaji Huduma kwa Kulenga Wateja**

213. **Mheshimiwa Spika;** Utoaji huduma bora kwa wananchi kwa kiwango kinachoridhisha ni lengo kuu la mabadiliko ya kiutendaji ambayo Serikali ya Awamu ya Tano inayapa kipaumbele. Hivyo, mwelekeo wetu ni kuhakikisha kuwa taasisi za kisekta tukianzia na TBS na BRELA zinajielekeza katika kutoa huduma kwa kiwango kinachokidhi matarajio ya wananchi. Wizara yangu na taasisi zake zitaongeza ubunifu katika utendaji kazi kwa tija na kutoa huduma kwa weledi ili kuchochea ufanisi katika Sekta ya Viwanda na Biashara na hatimaye kuongeza Pato la Taifa.

xvii) **Kuimarisha Huduma ya Usajili Biashara kwa Njia ya Mtandao**

214. **Mheshimiwa Spika;** Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) inatoa huduma za usajili wa Makampuni, Majina ya Biashara, Hataza na Alama za Biashara kwa kutumia Mfumo wa Online Registration System (ORS) na utoaji wa Leseni za Biashara kupitia Mfumo wa National Business Portal (NBP). Utekelezaji wa mifumo hiyo katika kutoa huduma umesaidia kuongeza tija na ufanisi wa utendaji kazi wa Taasisi na Jumuiya ya Wafanyabiashara ambapo cheti cha usajili kilichokuwa kikipatikana katika kipindi cha siku saba sasa kinapatikana ndani ya siku moja kwa mteja aliyekamilisha taratibu zote kama inavyotakiwa. Aidha, mifumo hiyo imewezesha wafanyabiashara na wawekezaji kupata huduma za usajili wa kampuni, majina ya biashara na leseni za biashara wakiwa mahali popote ndani na nje ya nchi. Pia, mifumo hiyo imesaidia kupunguza urasimu na vitendo vya rushwa kwa baadhi ya watumishi wasiokuwa waaminifu.

215. **Mheshimiwa Spika;** Kutokana na mifumo hiyo, wasimamizi wa mifumo (System Administrators) wanafuatilia hatua kwa hatua maombi (Application) ya wateja na kutambua kila mtumishi na muda uliotumika kushughulikia suala husika. Aidha, mifumo inaweza kutoa taarifa za jumla ya maombi yaliyofanyiwa kazi na Afisa husika kwa kipindi husika. Hatua hiyo imeongeza umakini na uwajibikaji kwa watumishi na hivyo kuongeza ufanisi katika utoaji huduma kwa wateja. Aidha, mifumo imewezesha taarifa za wateja kupatikana kirahisi tofauti na ilivyokuwa hapo awali ambapo kulikuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wafanyabiashara ya kupotea kwa baadhi ya taarifa katika mafaili ya usajili wa makampuni.

216. **Mheshimiwa Spika;** Wakala pia kupitia mifumo hiyo imefanikiwa kupunguza gharama za uendeshaji ambazo ilikua ikizipata kabla ya kuanza kutumia mifumo. Baadhi ya gharama zilizopunguzwa ni pamoja na matumizi ya karatasi za kuchapisha vyeti vya usajili na leseni za biashara

ambapo kwa sasa mfanyabiashara anachapisha cheti cha usajili na leseni za biashara akiwa ofisini kwake.

*xviii) Kuimarisha Huduma za Wasanii Nchini*

217. **Mheshimiwa Spika;** Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA) imeendelea kutekeleza majukumu yake ambayo ni pamoja na kubainisha, kutetea na kulinda maslahi ya watunzi wa kazi mbalimbali za sanaa. Hadi kufikia Machi, 2020 COSOTA imekusanya Shilingi 257,987,500 ambapo Shilingi 152,557,500 ni fedha zinazotokana na makusanyo ya mirabaha kutoka kwenye biashara za vileo, hoteli, klabu, casino na kumbi za shughuli; Shilingi 17,010,000 ni makusanyo kwenye kazi za maandishi; usajili wa kazi za Sanaa Shilingi 33,420,000; na Vyombo vya utangazaji (TV na radio) Shilingi 55,000,000. Aidha, COSOTA imeendelea kufanya ukaguzi wa watumiaji haramu wa kazi za Hakimiliki kwenye mikoa mbalimbali ikiwa ni pamoja na Mwanza, Kilimanjaro, Manyara, Dodoma, Arusha, Pwani na Dar es Salaam. Aidha, COSOTA imeingia Mkataba wa Makubaliano (MOU) na WIPO kwa ajili ya kutatua migogoro ya kisanaa (Alternative Dispute Resolutions (ADR) activities).

218. **Mheshimiwa Spika;** utakumbuka Bunge lako tukufu lilifanya Marekebicho ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na 7/1999 yaliyopitishwa na Bunge mwezi Juni, 2019 kupitia Misc. Written Laws Act No. 3 of 2019 (Gazeti la Serikali Na 27 la tarehe 30 Juni, 2019). Kifungu cha 16 cha Sheria hiyo kimerekebisha Sheria kwa kuongeza Kifungu 42A kinachohusu Compounding of Offences. Kupitia kifungu hicho, COSOTA imepewa mamlaka ya kutoza faini za papo kwa papo katika makosa ya ukiukwaji wa Hakimiliki mara baada ya mtuhumiwa kukiri kosa lake bila ulazima wa kwenda Mahakamani. Aidha, marekebicho hayo yameleta pia kifungu cha resale right kwa ajili ya kufuatilia na kusimamia faida ya wabunifu kila kazi zao zinapouzwa kwa zaidi ya mara moja kutoka mtumiaji mmoja kwenda mtumiaji mwingine. Hatua hiyo ni ya msingi sana kwa COSOTA na Sekta Ndogo ya Sanaa na Ubunifu.

**xix) Kuimarisha Sekta Binafsi na Wajasiriamali**

219. **Mheshimiwa Spika;** Mtazamo wa sera za Taifa zinatambua nafasi ya sekta binafsi kama injini ya maendeleo ya kiuchumi. Kujenga sekta binafsi hasa wajasiriamali wadogo kwa kuwawekea mazingira wezeshi na rafiki kupitia upatikanaji wa mitaji, teknolojia rahisi na rafiki, masoko ya uhakika na huduma muhimu zinazolenga kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji ni suala lisilohitaji mjadala. Hivyo, katika kuendeleza Sekta ya Viwanda na Biashara, mtazamo wa kisera utalenga kukuza na kutengeneza uwekezaji kuanzia ngazi ya ujasiriamali mdogo hadi kuwa matajiri wazalendo wa baadaye. Aidha, sera na mikakati itazingatia mahitaji ya uwekaji mazingira wezeshi, yanayotabirika na yanayojenga kuaminika kwa mwekezaji na hivyo kumfanya mwekezaji aamini na kuamua kuwekeza mtaji wake nchini.

**xx) Kuboresha Mazingira ya Biashara Nchini**

220. **Mheshimiwa Spika;** Ujenzi wa mazingira bora na endelevu ya biashara ni kichocheo kikubwa na muhimu katika kuvutia wawekezaji wa ndani na nje. Hivyo, Serikali kupitia Wizara yangu imejizatiti kwa kuhakikisha kuwa inaendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini. Maboresho hayo yatakutia wawekezaji wa ndani na nje katika viwanda na biashara na hivyo kuwezesha kutumia fursa mbalimbali za ndani na nje ya nchi kadri zinavyojitokeza. Misingi ya maboresho ya mazingira ya kibiashara yanategemewa kuwekewa nguvu ya kisheria na utaratibu wenye ushirikishaji mpana zaidi wa wadau. Aidha, katika kuhakikisha uendelevu na uhakika wa kuvutia wawekezaji na upatikanaji wa soko kwa bidhaa zetu nje ya nchi, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imeendelea kutumia Ofisi za Balozi zetu nje ya nchi kutangaza bidhaa zetu ikiwa ni pamoja na kuzishirikisha katika maonesho ya Kimataifa ambayo nchi inashiriki.

**xxi) Kulinda Soko na Biashara ya Ndani**

221. **Mheshimiwa Spika;** Uchumi himilivu, unaotabirika na shindani unatokana na jitihada za makusudi za kuujenga, kuuendeleza na kuulinda. Kujilinda isitafsiriwe

kuwa ndiyo kujitenga kiuchumi na nchi nyingine na wala siyo dhambi, kwani hata nchi zilizoendelea kiuchumi duniani mbinu mbalimbali zinaendelea kutumika kwa njia tofauti. Hivyo, sera, sheria na mikakati ya kisekta itaendelea kuhakikisha kuwa kunakuwepo ushindani wa haki ili kulinda viwanda na biashara nchini. Aidha, tutaendelea kulinda haki za msingi za walaji kwa kuweka utaratibu wa kisheria utakaotaka wawekezaji, wenye viwanda na wafanyabiashara katika mazao, bidhaa na huduma kutotumia nguvu ya soko isivyotakiwa na kusababisha kuwakandamiza wanyonge walio wengi.

***xxii) Kuhamasisha Uuzaji wa Bidhaa na Mazao Yanayozalishwa Nchini***

222. **Mheshimiwa Spika;** Ni dhahiri kuwa nchi yetu inazalisha mazao na bidhaa nyingi ambazo zinapaswa kupewa kipaumbele katika kuzilinda na kuzitangaza ipasavyo. Kupitia maonesho mbalimbali yakiwemo Maonesho ya Bidhaa za Viwanda vya Ndani yanayofanyika mwezi Desemba kila mwaka katika Viwanja vya Sabasaba, nimejiridhisha kuwa bidhaa hizo zina ubora wa hali ya juu. Ni wakati muafaka sasa kupitia Bunge lako tukufu kuangalia namna ya kipekee kama nchi kushiriki kujitangaza na kuhamasisha matumizi ya bidhaa zetu za ndani kupitia kampeni ya NUNUA BIDHAA ZA TANZANIA JENGA TANZANIA - NUBITAJETA. Moja ya njia ya kuzitangaza bidhaa zetu ni kuhamasisha jitihada za branding na Made in Tanzania kwa Watanzania waliopo ndani na nje ya nchi. Jitihada hizo zinaweza kuanzishwa hapa Bungeni kwa kutenga siku maalum ya kuvaa vazi la kitaifa lililobuniwa na wabunifu wetu wa ndani. Vilevile, ofisi za Serikali zinaweza kuangalia namna ya kujiwekea utaratibu kama huo wa kuvaa vazi hilo angalau kwa siku moja katika wiki. Hatua mahsusi kama hizo zitachochea uzalendo na kuhamasisha jamii zinazotuzunguka kupenda, kuthamini na hatimaye kutumia bidhaa za ndani kwa wingi zaidi na kwa uendelevu.

***xxiii) Kuhuisha Kada ya Waambata wa Biashara***

223. **Mheshimiwa Spika;** Ili kuongeza nguvu za utafutaji na utumiaji wa fursa za masoko ya nje, Wizara

inafanya uchambuzi wa kina kuhusu nafasi ya Waambata wa Kibiashara na mchango wa kada hiyo katika utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi. Lengo ni kutathmini tija itakayokuwepo katika kuhuisha na kurejesha Waambata wa Biashara (Trade Attachee) katika ofisi za Balozi zetu zilizo nje ya nchi. Sambamba na hilo, Wizara itatathmini nafasi ya Mawakala/ madalali ikiwa ni pamoja na wanafunzi wa Kitanzania nje ya nchi wanaotumiwa na Jumuiya ya Wafanyabiashara katika kufanikisha upatikanaji na uzaji wa bidhaa ndani na nje ya nchi. Lengo ni kuweka mfumo wa kufanya tathmini na utafiti wa mahitaji ya soko la bidhaa zinazozalishwa nchini kwa kutumia Waambata hao. Tathmini na tafiti hizo zitatoa picha ya mahitaji ya soko la nje na kuwezesha wazalishaji wa bidhaa za ndani kuzalisha kwa kuzingatia mahitaji ya soko la nje.

***xxiv) Kuimarisha Mfumo wa Utendaji na Usimamiaji Kazi za Kisekta katika Ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa Nchini***

224. ***Mheshimiwa Spika***; kwa kuzingatia umuhimu wa utendaji kazi wenye tija katika ngazi za Makatibu Tawala Mkoa (RAS) na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs), Kada za Maafisa Biashara zitapewa msukumo wa kipekee ili kuhakikisha inahuishwa na kufanya kazi zake kitaalam. Aidha, Wizara imeanza mazungumzo na Ofisi ya Rais TAMISEMI ili kuandaa Mkataba wa Makubaliano (Memorandum of Understanding) wa kuweka mifumo na mazingira bora ya kufanya kazi pamoja na kwa kushirikiana. (Kubadilika kimawazo (change of mindset) ni moja ya tiba muhimu katika kuleta mabadiliko yenye matokeo na yenye tija na endelevu katika uchumi wetu).

***xxv) Upatikanaji wa Teknolojia Rahisi na Nafuu kwa Wajasiriamali***

225. ***Mweshimiwa Spika***; Wizara pia itaweka mkazo na umuhimu katika upatikanaji wa teknolojia za kuongeza tija katika uzalishaji kwa kuimarisha taasisi za teknolojia zilizo chini ya Wizara. Jitihada hizo zitakwenda

sambamba kwa Wizara kujikita zaidi katika ujenzi wa maeneo yenye miundombinu ya uzalishaji (Industrial shades) inayosimamiwa na SIDO. Hiyo itawawezesha wajasiriamali kupata mahali muafaka pa kufanyia kazi za uzalishaji na kuweza kuhudumiwa kirahisi na taasisi mbalimbali zikiwemo za uhibitaji wa ubora wa bidhaa, taasisi za fedha na mafunzo. Aidha, juhudi za kuimarisha jasiriamali nchini zitaenda sambamba na kuimarisha SIDO ili imudu kutoa huduma bora na zenye kuleta tija katika uzalishaji wa bidhaa, huduma na ufanyaji biashara.

***xxvi) Uendelezaji wa Ujuzi na Nguvukazi Nchini***

226. ***Mheshimiwa Spika***; Suala la kuwa na Rasilimali watu ya kutosha yenye sifa, uwezo na inayotumika vizuri ni muhimu katika kujenga uchumi endelevu wa viwanda. Wizara imejipanga kuendeleza kimkakati rasilimali watu iliyonayo kwa kuwa na mpango mpana wa kuwaendeleza na kuwajengea uwezo watumishi wa wizara ili kuongeza ujuzi na weledi katika kutekeleza majukumu yao. Hii itawezesha kuboresha huduma zitolewazo na kukidhi matarajio ya wadau na umma wa ujumla. Pia tutajielekeza zaidi katika maeneo ya kuboresha huduma (service delivery) kwa njia mbalimbali, kuimarisha usimamizi na uratibu wa shughuli za kisekta (Regulatory role) na kuishirikisha sekta binafsi na wadau wengine kuchangia kikamilifu katika kukuza uchumi. Ili kuwa na rasilimali watu wenye afya, Wizara itahakikisha kuwa watumishi wanapata elimu ya afya na huduma za kinga dhidi ya magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza. Jitihada pia zitafanywa za kushawishi taasisi za elimu kuandaa mitaala inayozingatia mahitaji ya soko ili kukidhi mfungamanisho wa kitaaluma unaohitajika katika ujenzi wa uchumi wa viwanda.

***xxvii) Ujenzi wa Miundombinu ya Msingi na Wezeshi kwa Ajili ya Uwekezaji wa Viwanda***

227. ***Mheshimiwa Spika***; Kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu ya msingi na wezeshi kwa ajili ya ujenzi wa viwanda na ufanyaji biashara ni suala la msingi. Uendelezaji

wa miundombinu hiyo kwa kushirikiana na sekta binafsi utapewa msukumo zaidi ili kuleta tija na mvuto kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Jitihada za kushirikisha Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika kumiliki, kuendeleza na kusimamia maeneo maalum ya uwekezaji nazo zitapewa kipaumbele kabla ya kukimbilika kutafuta wawekezaji wa nje. Wizara pia itashirikiana na Balozi za Tanzania pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu, Bunge na Uwekezaji kuja na mkakati wa kuvutia wawekezaji kutumia sehemu ambazo zimefidiwa chini ya EPZA. Mradi wa ujenzi wa Kongano la Viwanda Kizota (Kizota Industrial Cluster) kwa Mkoa wa Dodoma ambao umezindua miradi ya ujenzi wa miundombinu hiyo katika mikoa yote nchini ni moja ya jitihada zinazolenga kuendelezwa katika maeneo mengine ya mikoa nchini. Maeneo hayo yatakuwa Center of Excellency ambazo pamoja na mambo mengine itafungamanisha miradi mikubwa na ya kimkakati katika mnyororo wa thamani.

228. **Mheshimiwa Spika**; katika kujengea uwezo na kuendeleza uwekezaji wa wajasiriamali wadogo na wa kati nchini, mwelekeo wa Wizara ni kuhakikisha kuwa ujenzi wa Industrial Shades unafanywa katika mikoa yote nchini na msukumo ukiwa katika kukamilisha miradi iliyoanza na ikifuatiwa na maeneo mengine ya pembezoni mwa nchi hususan Kyela, Nyasa, Kigoma, Karagwe ikiwa ni msukumo wa kufungamanisha maboresho ya vituo vya biashara za mipakani na viwanda katika maeneo hayo.

***xxviii) Kuthamini Bidhaa na Huduma zinazozalishwa Nchini Tanzania***

229. **Mheshimiwa Spika**; Kuthamini rasilimali na bidhaa za ndani ni ukombozi muhimu wa kiuchumi kwa Taifa lolote kwani nchi huwa soko la kwanza kabla ya kutafuta soko jingine. Suala la msingi ni wananchi kujenga imani na kupata thamani na ubora wanaohitaji katika bidhaa na huduma za ndani ya nchi. Mifano hai ni nchi za Japan na China ambazo wananchi wake wamejijengea utamaduni wa kuthamini bidhaa zinazozalishwa katika uchumi wao.



Kwa kutambua msingi huo, Wizara itaendelea kuhamasisha uimarishaji wa ubora na matumizi ya bidhaa za ndani, nguvukazi na malighafi za ndani ili kuleta ufungamanisho wa sekta katika kujenga uchumi na kuleta maendeleo kwa wananchi wake. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na TanTrade inaendelea kuhamasisha wananchi kutumia bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani kupitia kauli mbiu ya Nunua Bidhaa za Tanzania, Jenga Tanzania (Buy Tanzania, Build Tanzania). Mbinu hii ni muhimu sana katika kipindi hiki cha ujenzi wa uchumi wa viwanda ili kuimarisha viwanda vya ndani kwa kutegemea soko la uhakika la ndani ya nchi. Hii itajumuisha kusimamia matumizi ya bidhaa, mazao na nguvukazi ya ndani katika miradi na shughuli kubwa za nchi ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Local Content.

## 5.2. Vipaumbele kwa Bajeti ya Mwaka 2020/2021

230. *Mheshimiwa Spika*; Katika mwaka 2020/2021, Wizara ina vipaumbele vifuatavyo:

(a) Kuendeleza na kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kimkakati na vya kielelezo;

(b) Kufufua Viwanda Vilivyobinafsishwa, upanuzi na ukarabati wa viwanda vilivyopo na kuchochea/kuhamasisha uwekezaji/uanzishwaji wa viwanda vipya;

(c) Kuendeleza miundombinu ya msingi na saidizi ya maeneo ya uwekezaji na huduma ya viwanda kwa wawekezaji na wajasiriamali;

(d) Uendelezaji na uwekezaji katika maeneo maalum ya uwekezaji na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje;

(e) Uendelezaji wa taasisi za utafiti na maendeleo ya teknolojia ya viwanda na kuvutia na kuchochea matumizi ya teknolojia ya kisasa;

(f) Kulinda viwanda na biashara za ndani dhidi ya ushindani usio haki;

(g) Kudhibiti ubora na viwango vya bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini na zile zinazoagizwa kutoka nje;

(h) Kujenga mifumo imara ya soko la ndani na kuhamashisha utafutaji na utumiaji wa fursa nafuu za masoko;

(i) Kujenga uwezo wa watumishi wa Wizara na taasisi kwa kuwapa fursa za kupata elimu na ujuzi, vitendea kazi na huduma nyinginezo; na

(j) Kujenga uwezo wa Taasisi kuchangia Bajeti ya Serikali na kutoa gawio stahiki.

## **6. MALENGO YA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA KWA MWAKA 2020/2021**

### **6.1. Malengo ya Makuu ya Wizara**

231. ***Mheshimiwa Spika***; Kwa muhtasari malengo na mikakati ya Wizara itakayotekelezwa kwa mwaka 2020/2021 ni kama ifuatavyo:

(a) Kuendeleza miundombinu ya maeneo ya Uwekezaji nchini;

(b) Kuendeleza utafiti na maendeleo ya teknolojia;

(c) Kuboresha mazingira ya biashara nchini;

(d) Kulinda viwanda na biashara za ndani na kuimarisha ushindani;

(e) Kushughulikia masuala ya ubora na viwango nchini;

(f) Kutafuta fursa za masoko na kuwaunganisha na wazalishaji wa ndani;

(g) Kuwawezesha wajasiriamali kwa kuwapa elimu na mitaji;

(h) Kuendeleza biashara; na

- (i) Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi.

### **6.1.1. Sekta ya Viwanda**

232. **Mheshimiwa Spika;** Katika Mwaka 2020/2021 Sekta ya Viwanda itatekeleza malengo yafuatayo:-

- (a) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera (SIDP) na Mikakati ya Mafuta ya Kula, Ngozi, Nguo na Mavazi;
- (b) Kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Viwanda Nchini;
- (c) Kusimamia na Kufuatilia Miradi ya Kimkakati;
- (d) Kutekeleza Mkakati wa Kuvilinda Viwanda vya Ndani;
- (e) Kuhamasisha Uwekezaji wa Sekta Binafsi katika Maeneo Maalum ya EPZ/SEZ;
- (f) Kuhamasisha Uendelezaji wa Sekta ya Mafuta ya Kula;
- (g) Kueneza falsafa ya KAIZEN nchini; na
- (h) Kuhamasisha ukuaji wa Sekta ya Viwanda nchini.

### **6.1.2. Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo**

233. **Mheshimiwa Spika;** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

- (a) Kuendelea kufuatilia utekelezaji wa utengaji na uendelezaji wa maeneo kwa ajili ya uanzishaji wa viwanda vidogo na biashara ndogo kupitia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI);
- (b) Kuratibu uanzishwaji na uendelezaji wa Kongano za Viwanda kwa ajili ya wajasiriamali;
- (c) Kukamilisha marejeo ya Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo na kuandaa mkakati wake;
- (d) Kuimarisha/kuboresha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wajasiriamali;

- (e) Kuendelea kutafuta fursa za masoko ya ndani na nje kwa ajili ya bidhaa za Wajasiriamali;
- (f) Kufanya utafiti juu ya mahitaji ya teknolojia (Technology Needs Assessment) kwa ajili ya uanzishwaji na uendelezwaji wa viwanda vidogo na vya Kati;
- (g) Kuratibu na kutathmini utendaji wa shughuli za Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO); na
- (h) Kuhamasisha urasimishaji wa wajasiriamali wasio rasmi.

### 6.1.3. Sekta ya Biashara

234. **Mheshimiwa Spika;** Katika Mwaka 2020/2021 Wizara kupitia Sekta ya Biashara itatekeleza malengo yafuatayo:-

- (a) Kuendeleza majadiliano ya kibiashara kati ya Nchi na Nchi (Bilateral), Kikanda (Regional) na Kimataifa (Multilateral) kwa ajili ya kupanua fursa za masoko na uwekezaji ili kuvutia uwekezaji nchini;
- (b) Kuendeleza majadiliano ya biashara kwenye nchi za China, Urusi, Mauritius, Uturuki, Misri, Israel, DRC Congo, Sudani ya Kusini, Vietnam na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na kuingia nazo makubaliano ya biashara kwa kushirikiana na Sekta Binafsi;
- (c) Kuendelea na majadiliano ya kuanzishwa kwa Eneo Huru la Biashara kwa Nchi za Afrika (Continental Free Trade Area – CFTA);
- (d) Kukamilisha majadiliano ya kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Utatu linalojumuisha Kanda za COMESA, EAC na SADC;
- (e) Kukamilisha majadiliano ya biashara ya huduma kwa sekta sita (6) za kipaumbele katika nchi wanachama wa SADC;
- (f) Kutekeleza Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye masuala ya biashara ya bidhaa na huduma;
- (g) Kuratibu na kushiriki kwenye majadiliano ya biashara ya kimataifa katika mashirika yaliyo chini ya Umoja

wa Mataifa na mengineyo ikiwemo WTO, UNCTAD, CFC na ITC;

(h) Kuhamasisha Jumuiya ya Wafanyabiashara kuhusu fursa za masoko ya upendeleo yatokonayo na majadiliano ya Nchi na Nchi, Kikanda na Kimataifa;

(i) Kukamilisha utungaji wa Sheria ya Kujilinda Kibiashara (Trade Remedies Act);

(j) Kutekeleza Mkataba wa Shirika la Biashara Duniani (WTO) unaohusu uwezeshaji wa Biashara;

(k) Kukamilisha mapitio na kuanza utekelezaji wa Sera mpya ya Taifa ya Biashara;

(l) Kuimarisha kamati za kitaifa za kusimamia urahisishaji wa biashara nchini; na

(m) Kuandaa miradi na program mbalimbali kwa ajili ya kujenga uwezo kwa wataalam na Sekta Binafsi;

#### 6.1.4. Sekta ya Masoko

235. **Mheshimiwa Spika;** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Sekta ya Masoko itatekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini;

(b) Kuwaunganisha wazalishaji, wasindikaji na wafanyabiashara na masoko ya ndani na nje ya nchi;

(c) Kupanua wigo wa Matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala;

(d) Kuhamasisha na kurahisisha biashara mipakani;

(e) Kuhamasisha na kuwezesha wananchi kutangaza bidhaa na huduma za Tanzania;

(f) Kuimarisha Mfumo wa Ukusanyaji wa Taarifa za Masoko; na

(g) Kuandaa na kupitia Sera, Sheria na Kanuni mbalimbali.

#### 6.1.5. Maendeleo ya Rasilimali Watu

236. **Mheshimiwa Spika;** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Idara ya Utawala na Rasilimali Watu itatekeleza masuala yafuatayo:-

### Maendeleo ya Rasilimali Watu:

(a) Kuajiri watumishi wapya 58 wa kada mbalimbali kwa lengo la kuwezesha Idara na Vitengo kuwa na watumishi wa kutosha;

(b) Kupandisha vyeo watumishi 124 wa kada mbalimbali;

(c) Kupeleka watumishi kumi na mmoja (11) katika mafunzo ya muda mrefu, ishirini na watano (25) mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi na ya uongozi na usimimamizi wa mabadiliko (Leadership and Change Management) kwa viongozi zikulingana na majukumu yao;

(d) Kuandaa mpango mpana wa kuendeleza rasilimaliwatu, kuandaa watumishi wanaotarajia kustaafu karibuni na warithi wanaonyesha kuwa na sifa uwezo utayari (Talent pool) kujaza nafasi zinazoachwa wazi ili kukidhi mahitaji ya kimuundo na malengo ya muda mrefu ya Wizara;

(e) Kutekeleza Mfumo wa Wazi wa Mapitio ya Tathmini ya Utendaji Kazi – MWAMTUKA (OPRAS) kwa kutoa mafuzo ya ujazaji wa fomu, watumishi 204 wanasaini na kufanya mapitio na tathmini ya utendaji ya mikataba yao kwa wakati;

(f) Kuratibu na kusimamia masuala yote ya uendeshaji na utendaji kazi wa watumishi katika shughuli za Wizara;

(g) Kutoa huduma stahiki kwa viongozi na watumishi wa Wizara kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali katika Utumishi wa Umma;

(h) Kuandaa programu mbalimbali za michezo kama vile mabonanza na kushiriki katika mashindano ya SHIMIWI kwa lengo la kujenga afya za watumishi, kuongeza ushirikiano na kufahamiana; na

(i) Kuhakikisha watumishi watakaohitimisha ajira zao wanalipwa mafao kwa wakati.

### Masuala Mtambuka:

(a) **Rushwa:** Kuendeleza jitihada za kupambana na kudhibiti rushwa kwa watumishi kwa kuweka mikakati

mbalimbali na kutoa mafunzo juu ya Sheria Kanuni na Taratibu kuhusu uzingatiji wa maadili, uwajibikaji na utoaji huduma bora katika utumishi wa umma na kuhakikisha zinafuatwa na watumishi wote. Vilevile, Wizara kupitia Dawati la Malalamiko itaendelea kukusanya na kupokea malalamiko na kero kutoka kwa wateja wa ndani na nje ya ofisi kwa lengo la kuzitatua ikiwa ni njia mojawapo ya kudhibiti na kupambana na rushwa mahali pa kazi.

**(b) UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza:**

Wizara itaendelea na jitihada za kupambana na maambukizi ya VVU mahala pa kazi kwa kuzingatia Waraka wa Utumishi Na. 2 wa mwaka 2014 kuhusu Kudhibiti Virusi vya UKIMWI, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa Mahali pa Kazi katika Utumishi wa Umma na kuwahudumia watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWI na waliojiweka wazi. Aidha, Wizara itaendesha Semina kwa watumishi ikiwa ni njia ya uhamasishaji na uelimishaji wa masuala ya UKIMWI pamoja na upimaji afya wa hiari ili kudhibiti UKIMWI na Magonjwa sugu yasiyoambukizwa mahala pa kazi.

**(c) Masuala ya Jinsia:**

Wizara kupitia Dawati la Jinsia itaendelea kuratibu masuala ya kijinsia na kuyahuisha kwenye sera, mipango, mikakati na program za Wizara pamoja na Taasisi zake katika Mwaka 2020/2021.

**6.1.6. TEHAMA na TAKWIMU**

**237. Mheshimiwa Spika;** Katika Mwaka 2020/ 2021, Wizara kupitia Kitengo cha TEHAMA na Takwimu kitatekeleza masuala yafuatayo:-

(a) Kusimamia matumizi bora na sahihi ya miundombinu ya TEHAMA katika kutoa huduma ndani na kwa wateja wa nje;

(b) Kuboresha miundombinu ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi kwa wafanyakazi katika utoaji wa huduma kwa umma;

(c) Kutoa mafunzo kwa watumishi kuhusu matumizi bora na sahihi ya Miundombinu na Rasilimali za TEHAMA; na

(d) Kuimarisha mifumo ya ukusanyaji Takwimu/taarifa za Viwanda, Biashara na Masoko.

#### 6.1.7. Ununuzi na Udhhibiti wa Matumizi ya Fedha

238. **Mheshimiwa Spika;** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Kitengo cha Ununuzi kitaendelea kusimamia shughuli za ununuzi wa bidhaa na huduma kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi Na.7 ya Mwaka 2011 na kanuni zake GN Na, 446 ya Mwaka 2013, kama zilivyo fanyiwa marekebisho mwaka 2016 pamoja na miongozo inayotolewa na Mamlaka ya Udhhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA). Masuala yafuatayo yatatekelezwa:-

a) Kuandaa Mpango wa Ununuzi kwa mwaka 2020/2021;

b) Kufanya ununuzi wa bidhaa na huduma kupitia Mfumo wa Kielektroniki (Tanzania Electronic Procurement system - TANEPS);

c) Kuratibu vikaovinne (4) vya Bodi y a Zabuni ya Wizara kwa mwaka 2020/2021;

d) Kuandaa taarifa za ununuzi za kila mwezi, robo pamoja na taarifa ya mwaka na kuziwasilisha Mamlaka ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA); na

e) Kuhakiki mali za Wizara, kuhuisha taarifa za Daftari la Mali la Wizara kwa mujibu wa Muongozo wa Mali za Serikali wa mwaka 2019 pamoja na Sheria ya Fedha Na. 6 ya mwaka 2001 na Kanuni zake, GN.132 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2004.

### 6.2. MALENGO YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA 2020/2021

#### 6.2.1. Taasisi za Kuendeleza Uwekezaji

##### *i) Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)*

239. **Mheshimiwa Spika;** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-



- (a) Kuanzisha Kilimo shirikishi cha Ufuta na Mawese (Block farming) katika mikoa ya Pwani na Kigoma;
- (b) Kuzalisha zana ndogo ndogo za kilimo na Vipuri kwa kushirikiana na Taasisi za Utafiti na KMTC;
- (c) Kuanzisha Kiwanda cha Mbolea na Upimaji wa afya ya Udongo;
- (d) Kuanza utekelezaji wa mradi wa Mchuchuma na Liganga;
- (e) Kukamilisha tafiti za mradi wa Magadi soda na kujenga kiwanda Engaruka;
- (f) Kuendelea na Utekelezaji wa Mradi wa Matrika ya URSUS;
- (g) Kufanya ukarabati wa kiwanda cha KMTC kwa kujenga foundry na kubadilisha baadhi ya mashine;
- (h) Kufufua na kuendesha Kiwanda cha Matairi cha Arusha bila kutegemea wawekezaji binafsi; na
- (i) Kuchimba makaa ya mawe Katewaka.-

**ii) Mamlaka ya Maeneo Huru ya Uzalishaji wa Bidhaa kwa ajili ya Mauzo Nje ya Nchi (EPZA)**

240. **Mheshimiwa Spika;** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Mamlaka ya Maeneo Huru ya Uzalishaji wa Bidhaa kwa Mauzo Nje ya Nchi (EPZA) itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Uendelezaji wa miundombinu ya msingi katika maeneo yaliyokwisha lipiwa fidia, maeneo yanayosimamiwa na Serikali za Mikoa na Halmashauri pamoja na maeneo yanayoendelezwa na Sekta binafsi;
- (b) Kuweka alama na kuimarisha ulinzi katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi yaliyokwisha lipiwa fidia ili yasivamiwe;
- (c) Kuhamasisha uwekezaji katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi SEZ;
- (d) Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi iliyo chini ya SEZ - (Monitoring and Evaluation);
- (e) Kupitia Sheria zinazosimamia Mamlaka ya EPZ ili kuendana na wakati;
- (f) Kuboresha mifumo ya utoaji huduma kwa kutumia TEHAMA; na

(g) Kuimarisha Rasilimali Watu katika Mamlaka ya EPZ.

**6.2.2. Taasisi za Utafiti, Maendeleo ya Teknolojia na Mafunzo**

**i) Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO)**

241. **Mheshimiwa Spika;** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) itatekeleza malengo yafuatayo:

(a) Kuendeleza Mitaa ya Viwanda ya SIDO na kutengeneza Mfumo Unganishi wa shughuli za TEHAMA za Shirika;

(b) Kuhawilisha teknolojia kwa Kuimarisha vituo vya uendelezaji teknolojia (TDCs) na Vituo vya mafunzo na uzalishaji (TPC) vya SIDO; Kutunisha Mtaji wa Mfuko wa Wafanyabiashara Wananchi (NEDF); na

(c) Kuanzisha kituo kimoja cha kutengeneza vifungashio na kununua kwa wingi na kuimarisha usambazaji wa vifungashio kwa wajasiriamali mikoa yote.

**ii) Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO)**

242. **Mheshimiwa Spika;** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO) itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea kutoa huduma za kitaalam viwandani zenye lengo la kuongeza uzalishaji wa bidhaa bora bila kuchafua mazingira pia zinazolenga matumizi bora ya nishati;

(b) Kuendelea na mchakato wa kufanya utafiti na kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali wa Sekta ya Ngozi jinsi ya kupunguza uharibifu wa mazingira kwa kuhifadhi na kurejesha taka za ngozi ili kutengeneza bidhaa kama 'Leather boards';

(c) Kuendelea na kukamilisha mchakato wa kuhakiki (Accreditation) na kuboresha maabara ya chakula

na mazingira ili ziweze kufikia viwango vya kimataifa na kuweza kutoa huduma bora kwa wazalishaji viwandani;

(d) Kuendelea kutekeleza miradi mbalimbali yenye lengo la kuleta teknolojia mpya za uzalishaji;

(e) Kuendelea kukamilisha marejeo ya Sheria ya Bunge Na.5 ya mwaka 1979 iliyoanzisha TIRDO kwa kufuatilia ripoti ya mapitio ya Sheria iliyokwishawasilishwa Wizara mama na hatimaye kupelekwa Bungeni, na

(f) Kukamilisha Jengo la Utawala (Complete and furnish TIRDO administration block for Industrial Clinic, ICT and Information Centre).

**iii) Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC)**

243. **Mheshimiwa Spika;** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC) itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kufanya uchunguzi wa namna bora ya kudhibiti kinyesi cha kuku wanaofugwa kwenye v i o t a (cage) katika eneo finyu kwenye miji na maeneo yanayozunguka miji ili kutunza na kuboresha usafi wa mazingira;

(b) Kubuni na kuunda teknolojia ya kutenganisha maganda na kiini cha mbegu ya chikichi ambayo inahamishika;

(c) Kuunda teknolojia ya Kipandio kinachofaa kupanda mbegu za ufuta, alizeti, pamba na karanga ili kuchangia kuongeza uzalishaji wa mazao yenye kutoa mafuta ya kula nchini;

(d) Kufanya usanifu wa teknolojia ili kufikia hatua bora kabisa (design optimization) na kuziingiza kwenye soko la wadau;

(e) Kufanya tathmini ya mahitaji ya teknolojia katika hali ya uchimbaji madini kwa wachimbaji wadogo;

(f) Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Wajasiriamami wadogo 5 wanaojishughulisha na ubunifu na utengenezaji wa zana za kilimo na teknolojia za vijijini;

(g) Kuanzisha Vituo vya Ukaguzi na Majaribio katika maeneo matatu (3) muhimu ya Bandari na mipakani ambayo ni Bandari ya Dar es Salaam, Horohoro mkoani Tanga, naTunduma mkoani Songwe;

(h) Kununua vifaa, mitambo, machine na magari ya kusaidia kufanikisha kazi za ukaguzi na majaribio ya Zana za Kilimo na teknolojia za vijijini;

(i) Kujenga ufahamu na kusimamia utekelezaji wa Kanuni za Majaribio na Ukaguzi wa zana za Kilimo na teknolojia za vijijini; na

(j) Kujenga uwezo wa rasilimali watu kwenye Kada ya utafiti na wafanyakazi wengine wasio watafiti kwa kuwapa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu.

#### ***iv) Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (TEMDO)***

244. Mheshimiwa Spika; Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Shirika la Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (TEMDO) litatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea na uboreshaji wa karakana na ofisi ya usanifu pamoja na miundombinu ya Taasisi kwa ujumla;

(b) Kujenga uwezo wa wafanyakazi wa Taasisi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu ili kuboresha utendaji kazi;

(c) Kuendeleza ubunifu na kutengeneza chasili cha mtambo wa kuchakata na kukausha mazao ya kilimo (Muhogo) na kukausha korosho pamoja na kubangua (drying and scooping) ili kuongeza thamani;

(d) Kubuni na kuendeleza chasili cha mtambo mdogo wa kuchakata miwa na kutengeneza sukari (Mini/small scale sugar processing technology);

(e) Kuendeleza ubunifu na maboresho katika utengenezaji wa mtambo wa kukamua na kusindika mafuta ya mbegu za alizeti;

(f) Kusanifu na kuendeleza chasili cha mtambo wa kuchakata michikichi ili kupata mafuta ya kula pamoja na mazao yake mbalimbali;

(g) Kuendeleza ubunifu na maboresho ya kutengeneza mtambo wa kuteketeza taka ngumu za hospitali (Existing biomedical solid waste incinerator) ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi pamoja na kuweza kutumika katika kuteketeza/kuchoma damu zisizo salama na madawa ya hospitali yaliyokwisha muda wake kwa kiwango cha nyuzi joto 1500 – 2000 (Ni maombi ya MSD kusanifu "incinerator" hiyo);

(h) Kubuni na kuendeleza chasili cha jokofu la ngazi tatu la kuhifadhi maiti katika hospitali;

(i) Kubuni na kuendeleza chasili cha mtambo wa kuchakata zao la mkonge;

(j) Kuhawilisha teknolojia na kuhamasisha utengenezaji kibiashara wa mitambo iliyobuniwa na Taasisi ukiwemo mtambo wa kusindika mafuta ya kula yatokanayo na mbegu za mchikichi; na

(k) Kujitangaza ili kujenga uelewa kwa umma kuhusu shughuli zinazofanywa na Taasisi ya TEMDO kwa kushiriki kwenye maonesho angalau manne ya teknolojia/biashara (kama vile DITF, Nane nane, Maonesho ya kanda ya SIDO, n.k).

#### v) **Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE)**

245. **Mheshimiwa Spika;** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Chuo Cha Elimu ya Biashara (CBE) itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuimarisha na kuendeleza rasirimali watu hasa katika hatua ya shahada za Uzamivu;

(b) Kufanya upembuzi yakinifu katika kuboresha makazi ya watumishi katika eneo la Oysterbay Dar es Salaam;

(c) Kuimarisha na kuboresha mifumo ya TEHAMA;

(d) Kufanya ukarabati mkubwa wa minudombinu ya kufundishia na kujifunzia, Kampasi ya Dar es salaam na Dodoma; na

(e) Ujenzi wa Kampasi ya Mbeya.

### 6.2.3. Taasisi za Ushindani na Udhhibiti wa Ubora wa Bidhaa na Huduma

#### *i) Shirika la Viwango Tanzania (TBS)*

246. Mheshimiwa Spika; Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kutayarisha viwango 500 vya kitaifa katika sekta ndogo, ambavyo kati ya hivyo 260 ni vya uhandisi (Engineering) na 240 ni vya usindikaji (Process Technology);
- (b) Kutoa leseni ya ubora kwa bidhaa 500 kutoka katika sekta mbalimbali zikiwemo bidhaa za wajasiriamali wadogo (SMEs);
- (c) Kusajili na Kutoa vibali 5,900 vya chakula na maeneo ya uzalishaji;
- (d) Kusajili na Kutoa vibali 5,400 vya vipodozi na maeneo ya uzalishaji;
- (e) Kukagua ubora wa bidhaa 39,000 zitokazo nchi za nje kabla ya kuingia nchini (Pre- Shipment Verification of Conformity to Standards- PVoC (CoCs));
- (f) Kufanya ukaguzi wa ubora na kutoa leseni za ukaguzi 43,000 za magari yaliyotumika (used motor vehicles) yanayoingizwa nchini;
- (g) Kutoa mafunzo na semina 120 kuhusu viwango na udhibiti wa ubora (Quality Assurance Training) kwa wadau mbalimbali;
- (h) Kupima sampuli 25,000 za bidhaa mbalimbali;
- (i) Kufanya ugezi kwa vifaa/mashine mbalimbali vipatavyo 8,000;
- (j) Kuanzisha ofisi mbili za mipakani; na
- (k) Kuanza ujenzi wa Viwango House Dodoma.

#### *ii) Wakala wa Vipimo (WMA)*

247. *Mheshimiwa Spika*; Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Wakala wa Vipimo (WMA) itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kusimamia, kuhakiki na kukagua vipimo vyote vitumikavyo na viingavyo nchini kwa lengo la kumlinda mlaji;
- (b) Kuendelea na ukaguzi wa bidhaa zilizofungashwa kwenye maeneo ya mipakani, bandarini na viwandani kwa lengo la kuhakiki usahihi wa kiasi/ idadi iliyotamkwa (decreased quantity);
- (c) Kununua vitendea kazi yakiwemo magari Mawili na vitendea kazi vya kitaalam;
- (d) Kuongeza idadi ya watumishi 300 (Maafisa Vipimo 200, Maafisa Vipimo wasaidizi 50 na Madereva 50);
- (e) Kuendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu matumizi sahihi ya vipimo; na
- (f) Kuwajengea uwezo (Capacity building) watumishi wa Wakala wa Vipimo kwa kuwapeleka mafunzo ndani na nje ya nchi ili kuongeza elimu na ujuzi.

**iii) Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA)**

248. Mheshimiwa Spika; Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kufanya maboresho makubwa ya Mifumo a ya mitandao ya ORS na NBP ili kuwa rafiki zaidi kwa watumiaji na kutoa huduma bora na kuleta tija;
- (b) Kuendelea kutoa mafunzo kwa Maafisa Biashara nchini na kuweka taratibu za ushirikiano katika utoaji huduma na Wakurugenzi wa Halmashauri na Maafisa Biashara ili kuweza kuwahudumia wananchi katika maeneo yao kwa urahisi;
- (c) Kukamilisha mapitio ya sheria zote zinazosimamiwa na Wakala ikiwa ni pamoja na kuanzisha Daftari la kuwatambua Wanufaika wa mwisho wa Makampuni (Beneficial Ownership Register);
- (d) Kuendelea kueleleisha umma juu ya umuhimu wa kufanya sajili mbalimbali za kibiashara zinazofanywa na Wakala na urasimishaji wa Biashara kwa ujumla katika ngazi za Mikoa na Wilaya kwa kushirikiana na Maafisa Biashara kote nchini; na

(e) Kuendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi pamoja na mafunzo kwa watumishi kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi kwa wateja.

**iv) Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB)**

249. Mheshimiwa Spika; Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kujenga uwezo wa Bodi kuwezesha usimamizi wa majukumu yake kikamilifu kwa kuomba muundo mpya, ajira zaidi za watumishi, vitendea kazi na kubuni vyanzo vya mapato;

(b) Kushirikiana na wadau mbalimbali kuwezesha mazao yanayohifadhiwa kupitia mfumo wa stakabadhi kuuzwa kupitia soko la mazao na bidhaa (commodity exchange market) ili kuongeza ushindani, kupunguza gharama za uendeshaji na urasimu katika kuwalipa wakulima;

(c) Kuimarisha matumizi ya mfumo wa stakabadhi kwa mazao ya nafaka hususan mahindi na mpunga ili kufanikisha biashara ya mazao haya kwenda nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki/SADC;

(d) Kutoa elimu ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika maeneo yanayozalisha mazao ya chai, pamba, ufuta, dengu, mbaazi, soya, mahindi na mpunga katika mikoa ya Mbeya, Dodoma, Pwani, Lindi, Ruvuma, Iringa, Njombe, Rukwa, Sumbawanga, Songwe, Shinyanga, Mwanza, Kagera, Tabora na Mara;

(e) Kuendelea kuimarisha matumizi ya mfumo wa stakabadhi za ghala kwa mazao ya korosho, ufuta na kahawa kwa kukamilisha viwango vya mazao hayo, na kuboresha mfumo wa mauzo;

(f) Kuanzisha matumizi ya mfumo wa stakabadhi kwa kuwezesha mazao ya chai, pamba, dengu na mbaazi kutumika katika mfumo huu; na

(g) Kuhamasisha wahisani wa maendeleo, sekta binafsi na Mamlaka za Serikali za Mitaa kujenga ghala zinazofaa kwa matumizi ya mfumo wa stakabadhi za ghala.



v) Chama cha Hakimiliki Tanzania  
(COSOTA)

250. **Mheshimiwa Spika**; Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA) itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kukamilisha na kutumia kwa mfumo wa kieletroniki ili kurahisisha zoezi la usajili wa wabunifu wa hakimiliki na hakishiriki na kazi zao;

(b) Kushiriki katika marekebisho ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7/1999 kupitia Sheria ya Mazingira ya Ufanyaji Biashara (Ease of doing business) na utekelezaji wa marekebisho ya Sheria hiyo;

(c) Kutoa elimu kwa umma kuhusiana na mfumo wa usajili na masuala ya Hakimiliki na Hakishiriki;

(d) Kukamilisha Kanuni za ukaguzi na kufanya ukaguzi wa kazi zinazolindwa na Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki (anti piracy raids) katika utekelezaji wa marekebisho ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki;

(e) Kukamilisha na kuanza kutumika kwa Kanuni za Resale rights kwa kazi za sanaa za ufundi; na

(f) Kushughulikia migogoro na kesi za Hakimiliki na Hakishiriki ndani na nje ya Tanzania na kukuza ushirikiano na usimamizi wa migogoro hii kwa ushirikiano na Shirika la Miliki Ubunifu Duniani (World Intellectual Property Organization – WIPO).

vi) Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania  
(TANTRADE)

251. **Mheshimiwa Spika**; Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuimarisha upatikanaji wa Masoko na kuongeza mauzo ya bidhaa za Tanzania katika masoko ya nje kwa kuimarisha intelijensia ya biashara, kuanzisha madawati ya biashara ubalozini katika nchi za kimkakati na kutangaza bidhaa kupitia Maonesho, misafara na mikutano ya biashara;

(b) Kuimarisha sekta ndogo ya biashara (SMEs) ili iweze kujiendesha kiushindani kwa kutoa mafunzo, kuimarisha na kuanzisha vikundi vya kibiashara na kuendeleza bidhaa zenye fursa katika masoko ya nje;

(c) Kuimarisha biashara Zanzibar kwa kutafuta masoko yenye tija ya bidhaa za kimakakati (viungo, chumvi, dagaa na mwani) na kujenga uwezo wa wazalishaji kuwa na ushindani;

(d) Kuimarisha biashara za mipakani kwa kuimarisha mfumo shirikishi wa upokeaji malalamiko ya kero za biashara mipakani, kutoa mafunzo kwa wafanyabiashara, na kuimarisha Kamati za Pamoja na Vyama vya wafanyabiashara za Mpakani;

(e) Kusimamia uendeshaji wa Maonesho nchini kwa kukamilisha uandaaji wa kanuni za kusimamia Maonesho nchini; kudhiti uratibu wa maonesho kwa kutoa vibali vya kuandaa maonesho, kusimamia ratiba ya maonesho na kusimamia ubora wake;

(f) Kushiriki katika utekelezaji wa BLUEPRINT kwa kuandaa mfumo wa kubaini vikwazo na kero za ufanyaji biashara nchi na kuratibu uendeshaji wa Klinik ya Biashara ya Biashara; na

(g) Kuimarisha Uwezo wa Taasisi kujiendesha kiushindani kwa kuimarisha vyanzo vya mapato.

**vii) Tume ya Ushindani (FCC)**

252. **Mheshimiwa Spika;** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Tume ya Ushindani (FCC) itatekeleza yafuatayo:

(a) Kuboresha hali ya ushindani katika soko (Competition Protection and Promotion improved) kupitia;

(b) Kumlinda mlaji dhidi ya mienendo hadaifu (Consumer Protection Enhanced) kupitia; na

(c) Kuongeza ufanisi katika kutoa huduma (Service delivery capacity improved) kupitia.

**viii) Baraza la Ushindani (FCT)**

253. **Mheshimiwa Spika;** Katika Mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Baraza la Ushindani (FCT) itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kupokea, kusikiliza na kutoa maamuzi ya mashauri ya rufaa yanayowasilishwa katika Baraza ambapo lengo letu ni kutoa maamuzi ya mashauri 65 kwa mwaka 2020/2021;

(b) Kuimarisha uwezo wakutekeleza majukumu ya Baraza. Hii ikiwa pamoja na uboreshaji wa mifumo ya Baraza (ikiwemo: case management system; na information management system); na Mafunzo ilikuongeza kasi ya usikilizwaji wa mashauri yanayowasilishwa katika Baraza;

(c) Kuendelea kufanya utafiti wa kisheria na kiuchumi katika ushindani na udhibiti kwa ajili ya kusaidia katika uendeshaji wa mashauri ya Baraza;

(d) Kuongeza uelewa kwa Wadau wengi zaidi na Jamii kwa ujumla juu ya shughuli za Baraza na haki katika ushindani wa soko;

(e) Kuboresha vitendea kazi vya Baraza; na

(f) Kushughulikia masuala Mtambuka.

## **7. MAKADIRIO YA MAKUSANYO NA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/2021**

### **7.1. Makusanyo ya Serikali**

254. *Mheshimiwa Spika*; Katika mwaka 2020/2021, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya Shilingi 15,000,000 kutokana na uuzaji wa nyaraka za zabuni na makusanyo mengine. Kati ya fedha hizo, Shilingi 9,000,000 zitakusanywa katika Fungu 44 na Shilingi 6,000,000 zitakusanywa katika Fungu 60.

### **7.2. Maombi ya Fedha**

255. *Mheshimiwa Spika*; Kwa mwaka 2020/2021, Wizara ya Viwanda na Biashara inaomba kutengewa jumla ya Shilingi 81,366,902,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 51,679,016,000 ni za Matumizi ya Kawaida na Shilingi 29,687,886,000 ni za Matumizi ya Maendeleo. Aidha, katika Bajeti hiyo, Shilingi 57,414,395,000 ni za Fungu 44 na Shilingi 23,952,507,000 ni za Fungu 60.

## 8. SHUKRANI

256. **Mheshimiwa Spika;** Ujenzi wa uchumi wa viwanda ni shirikishi na jumuishi, hivyo huhitaji ushiriki wa wadau mbalimbali. Kwa kutambua umuhimu huo, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Denmark, Finland, India, Ireland, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Norway, Sweden, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi. Aidha, tunayashukuru Mashirika ya Kimataifa ikiwa ni pamoja na: ARIPO, Benki ya Dunia, CFC, DANIDA, DFID, EU, FAO, IFAD, JICA, Jumuiya ya Madola, KOICA, SIDA, Taasisi za Umoja wa Mataifa (UNCTAD, UNDP, UNIDO, UNWOMEN), USAID, WIPO, FSDT, TMEA, SADC na WTO. Vilevile, nashukuru taasisi zote, Sekta Binafsi, taasisi zisizo za kiserikali (CBOs & FBOs) kwa kuwa sehemu muhimu ya ujenzi wa uchumi wetu. Kama nchi, tunaendelea kutegemea ushirikiano wenye tija katika kufikia malengo endelevu ya jamii nzima ya Watanzania.

257. **Mheshimiwa Spika;** Naomba nihitamishe kwa kuwashukuru tena Watanzania na hasa Wazalendo wa nchi yetu ya Tanzania kwa kuendelea kuunga mkono jitihada za Serikali katika ujenzi wa uchumi wa viwanda na hivyo kuwa kichocheo cha kukua kwa sekta nyingine za uchumi. Ni dhahiri kuwa Taifa kwa kipindi hiki kinahitaji kuendeleza ari hiyo katika kupambana na majanga mbalimbali ikiwemo ugonjwa wa mafua makali wa CORONA. Kwa pamoja tuungane kujikinga na kulindana ili Taifa libaki salama na likiwa na nguvukazi ya kutegemewa.

## 9. HITIMISHO

258. **Mheshimiwa Spika;** Wizara ninayoisimamia imeazimia kuendeleza maamuzi makini na yenye mashiko ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujenga uchumi wa viwanda wenye mafanikio ambayo yanajitafsiri katika ubora wa maisha ya kila mwananchi na Taifa kwa ujumla. Hivyo, Sera, Sheria na Mikakati iliyopo itaendelea kuboreshwa ili kuendeleza mafanikio yaliyopatikana na kuchochea mbinu za utekelezaji ili kufikiwa kwa malengo ya Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi. Ni dhahiri

kuwa jitihada hizo pamoja na utekelezaji wa Blueprint utatutoa hapa tulipo na kutupaisha katika maendeleo na kufikia lengo la uchumi wa kati kama ilivyoazimiwa na Dira ya Taifa ya 2025. Ni dhahiri kuwa tunahitaji ushiriki usio na shaka wa kila Mtanzania, wadau wa sekta na washirika wa maendeleo. Inawezekana, endapo kila mmoja wetu atachukua nafasi yake na kujituma ipasavyo.

## 10. MAOMBI RASMI YA FEDHA

259. **Mheshimiwa Spika;** Naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe makadirio ya Wizara ya Viwanda na Biashara ya kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi 15,000,000 na matumizi ya jumla ya Shilingi 81,366,902,000 kwa mwaka 2020/2021.

## 11. MWISHO

260. **Mheshimiwa Spika;** Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara yenye anuani ifuatayo: [www.mit.go.tz](http://www.mit.go.tz).

261. **Mheshimiwa Spika;** Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana.

Tutaendelea na utaratibu wetu, nimwite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

**MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara; Fungu 44 - Viwanda na Fungu 60 – Biashara, kwa mwaka wa

fedha 2019/2020 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 40 na 60 kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya, uzima na nafasi nyingine ya kukutana hapa Dodoma katika Mkutano huu wa Kumi na Tisa wa Bunge la Kumi na Moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) na 117(1)(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara, Fungu 44 - Viwanda na Fungu 60 - Biashara kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Fungu 44 na 60 kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilizingatia matakwa ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ambapo ilifanya ziara katika baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2019/2020 ili kuona hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo. Vilevile, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara; Fungu 44 na 60 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na kuchambua mpango wa bajeti wa Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 98(2).

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii inatoa maelezo ya uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo, utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020, makadirio na mapato na matumizi ya ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu taarifa hizo.

Nheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ya Viwanda na Biashara iliidhinishiwa jumla

ya Sh.51,500,000,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Katika miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha mwaka 2019/2020, Kamati ilifanikiwa kutembelea baadhi ya maeneo nchini. Maeneo yaliyotembelewa na Kamati ni pamoja na *Kurasini Trade and Logistic Centre; TAMCO Industrial Kibaha*; Shirika la Utafiti wa Maendeleo na Viwanda (*TIRDO*); na Wakala wa Vipimo (WMA) - Misugusugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Kurasini Trade and Logistic Centre* ni mradi unaolenga kujenga Kituo cha Biashara na Ugavi. Mpango wa Serikali kupitia mamlaka ya *EPZ* ni kuliendeleza eneo hili kama soko la mazao mchanganyiko. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, mradi huu ulitengewa jumla shilingi bilioni 3 kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali. Maelezo juu ya mpango wa uwekezaji katika eneo la mradi na shughuli zilizopangwa kutetelezwa pamoja na hali ya mradi huu ni kama inavyoonekana katika taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ziara katika mradi wa *EPZ Development* Kurasini, Kamati ilikuwa na ushauri ufuatao:-

(i) Serikali ihakikishe mradi huu unaanza utekelezaji wake mara moja kwa kuwa eneo lile lilikuwa limeshalipiwa fidia. Fedha zilizotumika kulipa fidia ni kubwa shilingi bilioni 101 ambapo kwa sasa fedha hizo zimekuwa kama zimetupwa tu. Hadi sasa ni takribani miaka 7 tangu eneo limefidwa lakini utekelezaji wa mradi haujaanza. (*Makofi*)

(ii) Serikali kwa kushirikiana na mamlaka ya *EPZ* isimamishe mara moja biashara ya kuegesha magari na makasha katika eneo la mradi kwa kuwa shughuli hiyo siyo lengo kuu la eneo hilo la mradi.

(iii) Kabla ya mwaka wa fedha 2019/2020 kuisha, Serikali iipatie *EPZA* fedha iliyoidhiinishiwa na Bunge kwa mwaka huu ili iweze kuzungushia uzio eneo la mradi kwa lengo la kuzuia wavamizi.

(iv) Serikali ifuatilie kwa ukaribu mapato yatokanayo na shughuli za uwekezaji magari na makontena katika eneo la EPZA Kurasini na kubaini fedha zilizokuwa zikikusanywa kama zilikuwa zinafika katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa kuwa taarifa zilizopo ni kwa gari moja linaegeshwa kwa Sh.5,000 na kwa siku magari yanayoegeshwa ni zaidi ya 200. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo juu ya hali ya mradi mingine iliyotembelewa na Kamati ni kama inavyoonekana kwenye taarifa hii na kutokana na changamoto ya muda naomba nisisome.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipokea na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Uchambuzi wa Kamati ulilenga kufanya ulinganisho na kubaini kuhusu utekelezaji wa malengo ya Wizara, ukusanyaji wa mapato na upatikanaji wa fedha kwa Wizara ikilinganishwa na kiasi kilichoidhinishwa na Bunge hadi kufikia mwezi Machi, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ya Viwanda na Biashara chini ya Fungu 44 na 60 ilipanga kukusanya jumla ya shilingi milioni 14.3 kutokana na uuzaji wa nyaraka za zabuni na marejesho ya mishahara endapo mtumishi ataacha kazi. Hadi kufikia Machi 2020, Wizara ilikuwa haijafanikiwa kukusanya kiasi chochote cha malengo ya mapato walichokuwa wamejiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kuishauri Wizara ya Viwanda na Biashara kutafuta vyanzo vipya vya mapato ambapo vitaweza kuwaletea mapato ya uhakika. Vilevile ipange malengo ya makusanyo yanayoendana na uwezo wake halisi wa kukusanya na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ya Viwanda na Biashara iliidhinishwa jumla ya shilingi bilioni 100.38 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake kwa Fungu 44 na Fungu 60. Mgawanyo wa fedha hizo shilingi



bilioni 51.5 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 48.88 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2020, Wizara ilikuwa imepokea jumla shilingi bilioni 26.02 kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Wizara na taasisi zilizopo chini yake. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 25.92 tu ya fedha zote zilizotengwa katika bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi bilioni 26.02 zilizopelekwa zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo hadi kufikia mwezi Machi, 2020 hakuna kiasi chochote cha fedha kilichopokelewa na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina siyo wa kuridhisha kwa kuwa hadi kufikia Machi 20 fedha zilizotolewa ni za matumizi ya kawaida pekee na zilitolewa kwa asilimia 53.2. Upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka Hazina siyo wa kuridhisha. Hadi kufikia Machi 2020 hakuna kiasi cha fedha kilichotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa maana ya kwamba kwa mwaka wa fedha 2019/2020 miradi ya maendeleo ilitekelezwa kwa asilimia 0.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtazamo wa Kamati ni kwamba mwenendo huo wa upatikanaji wa fedha kwa Wizara ya Viwanda na Biashara unaashiria kukwama kwa utekelezaji wa baadhi ya majukumu yaliyopangwa na Wizara hususan utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha fedha zinazoidhinishwa na Bunge zinapelekwa tena kwa wakati ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yote yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifuatilia utekelezaji wa malengo ya Wizara ya Viwanda na Biashara yaliyopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kwa lengo la kujiridhisha na utekelezaji wake. Wizara

ilibainisha hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa malengo hayo. Kamati ilipongeza hatua hizo, hata hivyo, inaendelea kusisitiza Serikali kuongeza kasi katika maeneo mbalimbali kama ilivyoonekana kwenye taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kupitia na kuchambua taarifa za utekelezaji wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo mbalimbali. Naomba kulliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati. Hata hivyo, kuna maeneo ambayo Kamati inaendelea kuyasisitiza. Maeneo hayo ni kama yanavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ya Viwanda na Biashara imejipangia malengo na vipaumbele mbalimbali kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri. Kamati ilipitia malengo na vipaumbele vya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati juu ya malengo ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 umebaini kuwa malengo haya yalikuwa yanaendana na hati idhini Serikali iliyoainisha majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Aidha, Kamati ilibaini kuwa malengo hayo yamejitosheleza na kuwa utekelezaji wake unatarajiwa kuboresha hali ya biashara nchini na kukuza uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ushauri wa Kamati kuwa ili malengo haya yatekelezwe kikamilifu Serikali inapaswa kuhakikisha fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara zinatolewa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara ya Viwanda na Biashara, Fungu 44 na 60, imepanga kukusanya shilingi 15,000,000.00 kutokana na uuzaji wa nyaraka za zabuni na makusanyo mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kiasi kilichopangwa kukusanywa na Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kimeongezeka kwa asilimia 4.89 ukilinganisha na mpango wa makusanyo ya Mwaka wa Fedha 2019/2020. Kamati inapata wasiwasi na jinsi Wizara inavyojiwekea makadirio ya makusanyo. Wasiwasi wa Kamati unatokana kutofikiwa kwa lengo la makusanyo ya Wizara hii katika mwaka angalau kwa asilimia 75.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Wizara kufanya makadirio yenye uhalisia kulingana na vyanzo vya mapato ilivyonyavyo. Aidha, Kamati inaendelea kuisisitiza Wizara kuweka mikakati mahususi ya kutafuta vyanzo vipya vya mapato ili waweze kuongeza makusanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ya Viwanda na Biashara imetengewa jumla ya shilingi bilioni 81.36 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake chini ya mafungu yote mawili Fungu 44 na 60. Kati ya fedha zinazoombwa ni shilingi bilioni 51.67 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 29.68 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa magawanyo wa fedha hizo kwa mafungu yote mawili ni kama unavyoonekana katika taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati kuhusiana na mpango wa bajeti umebaini mambo yafuatayo:-

(i) Kiasi cha bajeti kilichotengwa kwa ajili ya mafungu yote mawili ni pungufu kwa asilimia 18.9 ukilinganisha na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ya Mwaka wa Fedha unaoishia yaani 2019/2020;

(ii) Upungufu wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara una athari kubwa kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo ambayo imepungua kwa asilimia 42.4 ukilinganisha na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/2020;

(iii) Kwa miaka miwili mfululizo fedha za bajeti zinazotengwa kwa Wizara hii zimeendelea kupungua kwa

Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/2020 ilipungua kwa asilimia 29.9 na kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 imepungua kwa asilimia 18.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, kushuka kwa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kunaashiria kukwama kwa utekelezaji wa baadhi ya majukumu ya Wizara hususani miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Kamati inaishauri Serikali kuongeza Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara na kuhaikisha fedha hizi zinatolewa, tena kwa wakati, ili kuleta ufanisi katika miradi husika kwa lengo la kupata matokeo yenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati; kutokana na uchambuzi huo na yale yaliyobainika, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na mwenendo usioridhisha wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina hususani fedha za miradi ya maendeleo. Mfano katika Mwaka 2019/2020 mpaka kufikia sasa hakuna fedha za maendeleo zilizopokelewa, jambo linalokwamisha utekelezaji wa miradi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa Serikali inaendelea kutekeleza miradi mingine ambayo inatazamiwa kuwa kichocheo kwa Sekta ya Viwanda, Kamati inaona bado kuna umuhimu kwa Wizara hii mama ya Viwanda inayojihusisha na utekelezaji wa Azma ya Ujenzi wa Viwanda ikapewa kipaumbele katika kutengewa fedha za kutosha na fedha hizo zitolewe kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya Mchuchuma na Liganga, Magadi Soda Engaruka, Bagamoyo *SEZ, Kurasini Logistic Centre* na Mtwara *Free Port* ni miradi iliyotambuliwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa kama miradi ya kimkakati na kipaumbele. Utekelezaji wa miradi hii umekusudiwa kuwa kichocheo cha Sekta ya Viwanda nchini

kwani inatarajiwa kuzalisha malighafi ambazo zingetumiwa na viwanda vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa tunapoelekea kufikia ukomo wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021 utekelezaji wa miradi hii umeonekana kusuasua. Kamati inaishauri Serikali kuongeza juhudi katika kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo kwa lengo la kuikamilisha, kukuza na kuanza kupata tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya majukumu ya Mamlaka ya *EPZ* ni kutwaa maeneo ambayo hutambulika kama maeneo maalumu ya uwekezaji. Baada ya kutwaa maeneo hayo Mamlaka ya *EPZ* hupaswa kuyaendeleza kwa kuyawekea miundombinu wezeshi na kuyaweka tayari kwa uwekezaji. Mpango huu umekumbana na changamoto ya uhaba wa fedha za kuendeleza maeneo hayo hivyo yameishia kuachwa tu wazi, jambo linalotoa mianya kwa watu wengine kuvamia maeneo hayo na kufanya shughuli zao bila kibali cha *EPZ* (mfano *EPZA* Kurasini).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha fedha zinazotengwa kwa ajili ya kuendeleza maeneo ya *EPZA* zinatolewa kwa wakati ili kuwezesha kutekeleza majukumu husika. Hatua hii itavutia uwekezaji kwa kuwa muwekezaji atakuta eneo tayari likiwa na miundombinu wezeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali katika kurudisha Serikalini viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo havifanyi kazi, Kamati inatambua changamoto wanayokumbana nayo katika kutekeleza zoezi hilo ambayo ni baadhi ya mikataba ya mauziano kukosa kipengele cha kurejesha Serikalini. Kamati inatoa rai kwa Serikali kuongeza umakini katika mikataba inayoendelea kuiingia juu ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ubia au wanayopatiwa wawekezaji moja kwa moja kwa kuhakikisha inazingatia Sheria ya Makinikia ili kuepuka mikwamo kama hii iliyojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhamasisha Ujenzi wa Tanzania ya Viwanda ni lazima Serikali iweke mazingira ya kusaidia wawekezaji wadogo wa ndani kushiriki kikamilifu. Kama tunavyofahamu, wazalishaji wadogo wa ndani wanakabiliana na changamoto ya rasilimali fedha. Katika kutatua changamoto hii, Kamati inatoa rai kwa Serikali kuutumia vyema Mfuko wa Maendeleo wa Wajasiriamali, *NEDF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfuko huu upo lakini hauna mtaji wa kutosha kuhudumia wahitaji walio wengi. Aidha, mfuko huu umekuwa ukitengewa fedha kila bajeti za wizara za kila mwaka lakini fedha hizo hazipelekwi. Kamati inashauri Serikali kuendeleza mfuko huu kwa kuupatia fedha zinazopitishwa na Bunge ili uendelee kuwasaidia na kuwanufaisha Watanzania wengi. Aidha, Kamati inatoa rai kwa taasisi za fedha kuunga mkono juhudi za Serikali kwa kuamua kuanzisha mikopo yenye masharti nafuu yanayoendana na masharti ya Mfuko huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; naomba kutumia fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Spika na kumpongeza sana kwa kulongoza Bunge letu kwa weledi mkubwa katika kipindi chote cha uhai wa Bunge la Kumi na Moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza wewe pia kwa weledi wako na umahiri mkubwa wa kumsaidia Mheshimiwa Spika kuongoza Bunge. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kumshauri Mheshimiwa Spika na kusaidia katika kuendelea kuendesha vikao vya Bunge la Kumi na Moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati yangu naomba nitumie fursa hii kutoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hatua mbalimbali anazoendelea kuzichukua zikilenga kuboresha utekelezaji wa azma ya kujenga Tanzania ya Viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa kushiriki kikamilifu wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni kuhusu Bajeti ya Wizara hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Majina yao ni kama yanavyoonekana hapo chini, na kwa ruhusa yako naomba majina yao yote yaingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Innocent Lugha Bashungwa (Mb), Naibu Waziri wake Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya (Mb), Makatibu Wakuu, pamoja na wataalam wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa jinsi walivyoshirikiana na Kamati katika kujibu hoja za Wajumbe wa Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na kufafanua kwa kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, naomba kumshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati, Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati, Zainab Mkamba na Mwajuma Ramadhan, pamoja na Msaidizi wa Kamati, Paulina Mavunde, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba niliombe Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Fungu 44 na 60 kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, kiasi cha shilingi 81,366,902,000 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA, FUNGU 44-VIWANDA NA FUNGU 60-BIASHARA KWA MWAKA 2019/2020 NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI FUNGU 44 NA 60 YA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) na 117 (11) ya Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara, Fungu 44-Viwanda na Fungu 60-Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Fungu 44 na Fungu 60 kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika**, jukumu la Uchambuzi wa Bajeti linaendana sambamba na jukumu la ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Katika kutekeleza jukumu hili, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilifanya ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa lengo la kujionea hali halisi ya utekelezaji wa miradi hiyo na kuishauri Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ilifanya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii



pamoja na Taasisi zilizopo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, pamoja na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inatoa maelezo ya Uchambuzi wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa Fedha unaoisha; Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Taarifa hizo. UCHAMBUZI WA TAARIFA YA MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 PAMOJA NA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA MPANGO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020.

## **2.1 Mapitio ya Taarifa za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016, Kamati ilifanya ziara ya kutembelea baadhi ya miradi iliyotengewa fedha na inatekelezwa na Wizara hii, kwa lengo kujionea hali halisi na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara ya Viwanda na Biashara iliidhinishiwa Shilingi 51,500,000,000/= kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya Maendeleo. Katika miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2019/2020, Kamati ilifanikiwa kutembelea baadhi ya maeneo chini ya Mradi Na 6260 ambao ulitengewa Shilingi 29,940,000,000.00. Maeneo yalitotembelewa na Kamati ni pamoja na:-

- i) TAMCO Industrial Parks Kibaha;
  - ii) Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO);
  - iii) Kurasini Trade and Logistic Centre - EPZ Development; na
  - iv) Wakala wa Vipimo (WMA) - Misugusugu – Pwani, Kituo cha kupima magari ya mafuta na Kipima Dira za Maji (Water Meter Test Bench).
- a) **TAMCO Industrial Parks Kibaha (Mradi Na. 6260, Fungu 44);**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara ya Viwanda na Biashara, Fungu 44 iliidhinishiwa shilingi 7,500,000,000/= kwa ajili ya kutekeleza mradi Na. 6260 – NDC- Industrial Park (TAMCO-Kibaha) unaohusisha kuendeleza maeneo maalumu ya Viwanda. Shughuli zilizopangwa kutelezwa katika mradi huu kwa mwaka wa fedha 2019/2020 zilikuwa ni ujenzi wa mtandao wa barabara za ndani ya eneo la Mradi, ujenzi wa matanki ya kuhifadhia maji safi, ujenzi wa mabwawa ya kuhifadhi maji taka pamoja na mradi wa kuunga matrika wa URSUS.

Hadi Kamati inafika eneo la Mradi fedha za Maendeleo zilikuwa hazijapokelewa hivyo shughuli zilizokuwa zimepangwa kutekelezwa kwa fedha hizo zilikuwa hazijatekelezwa. Pamoja na kuwa shughuli za maendeleo zilizokusudiwa kutekelezwa katika kipindi cha mwaka huu wa fedha zilikuwa hazijaanza kutekelezwa, lakini eneo la TAMCO – Kibaha ni eneo la Viwanda hivyo Kamati ilifanikiwa kutembelea Viwanda vinne (4) vilivyopo katika eneo hilo, viwanda vilivyotembelewa ni pamoja na;-

i) **Kiwanda cha GF TRACKS AND EQUIPMENT CO. LTD,**

Kiwanda hiki kinajihusisha na uunganishaji wa magari makubwa (trucks) hususani ya aina ya FAW TRUCKS hapa Nchini. Kiwanda kipo katika hatua za kukamilisha ufungaji wa mitambo na kinatarajia kuanza kufanya kazi mwezi Mei, 2020.

Mheshimiwa Spika, kiwanda kinatarajiwa kutoa ajira na kuchangia katika pato la Taifa (Kodi) pamoja na faida hizi, kiwanda pia kitasaidia kupunguza gharama/bei za magari aina ya FAW TRUCKS lakini pia kutapunguza uingizaji wa magari chakavu ya aina hiyo na hivyo kupelekea kupungua kwa madhara yatokanayo na matumizi ya magari chakavu katika mazingira.

ii) **Kiwanda cha HEISTER BIO SCIENCE AFRIKA LTD,**

kiwanda hiki kinamilikiwa kwa asilimia mia na kampuni ya kigeni kutoka India na kinajihusisha na uzalishaji wa chanjo za Mifugo za aina 37. Kwa sasa kiwanda kipo katika hatua za mwisho za ujenzi na kinatarajia kufanya uzalishaji wa majaribio mnamo mwezi Agosti, 2020 ambapo zitazalishwa chanjo mbili za majaribio. Kukamilika kwa kiwanda hiki kutaleta chachu katika Sekta ya Mifugo kwani kitarahisisha upatikanaji wa aina mbalimbali za chanjo za mifugo hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kiwanda hicho kinakabiliana na changamoto ya muingiliano wa maamuzi kwa mamlaka za

Serikali ambapo muwekezaji huyo amewekeza chini ya Masharti ya EPZA, lakini mamlaka nyingine za Serikali ikiwepo TRA imekuwa ikikwamisha kwa kukataa/ kupingana na vivutio alivyopatiwa muwekezaji chini ya masharti ya Mamlaka ya EPZ.

**Mheshimwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuzisimamia mamlaka husika kuhakikisha zinazungumza na kukubaliana, ili kuwahudumia wawekezaji kwa kauli moja na kuacha tabia ya kutofautiana mbele ya muwekezaji jambo ambalo halileti picha nzuri.

- iii) Kiwanda cha GLOBAL PACKAGING, kiwanda hiki kinamilikiwa kwa ubia kati ya Kampuni ya Wande Printing and Packaging LTD (94%) na Shirika la Taifa la Maendeleo NDC (6%) na kilianza uzalishaji Januari, 2017. Kiwanda kinajihusisha na uzalishaji wa vifungashio (mifuko ya safleti) vinavyotumiwa katika kilimo, viwandani hasa viwanda vya mbolea.

**Mheshimiwa Spika**, kiwanda hiki kinatazamia kuongeza uzalishaji na kupanua eneo la kiwanda, kutokana na lengo hilo, kamati ilijulishwa changamoto wanayokabiliana nayo ambayo ni mkwamo/ uchelewaji wa NDC kufanya maamuzi ya kutoa eneo kwa kiwanda. Jambo hili ni lakushangaza kwa kuwa eneo lipo na lipo wazi tu ambapo lingetolewa kwa kiwanda hiki ili kuwawezesha kujipanua na kuongeza uzalishaji, ambapo kodi na ajira kwa watanzania pia vingengezeka.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Wizara ya Viwanda na Biashara kufuatilia jambo hilo kwa ukaribu ili kutatua changamoto hii na kuhakikisha muwekezaji huyu anapatiwa eneo analohitaji ili kuongeza ufanisi wa kiwanda.

**iv) Kiwanda cha TANZANIA BIOTECH PRODUCTS LTD,**

kiwanda hiki kinamilikiwa kwa ubia kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Cuba, Kiwanda kinajihusisha na uzalishaji wa viuadudu (vimelea vya kibiolojia). Kiwanda kilianzishwa kwa lengo la kuzalisha viuadudu ambavyo vinalengwa kutumika kupambana na ugonjwa wa Malaria kwa kumtokomeza kiluilui wa mbu wa malaria akiwa katika hatua ya lava hatua ambayo bado hajawa sugu kwa madawa.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi ulianza Machi, 2015 na ulipaswa kutekelezwa kwa muda wa miaka mitano kwa maana kuwa ulipaswa kuishia Machi, 2020, na mteja mkubwa aliyelengwa kuchukua bidhaa hii alikuwa ni Wizara ya Afya. Uwezo wa kiwanda ni kuzalisha lita Milioni Sita (6) kwa mwaka na kiwanda kiliingia makubaliano na Wizara ya Afya kuwa Wizara itachukua lita Milioni Tano (5) kwa mwaka.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa changamoto ya kiwanda ni kuwa kwa kipindi cha miaka 4 tangu kuanzauzalishaji Kiwanda kimezalisha lita 676,000 tu na hii ni kutokana na kuwa mteja mlengwa wa bidhaa hiyo (Wizara ya Afya) hakutekeleza makubaliano. Wizara ya Afya kwa kipindi

hicho cha miaka minne (4) imechukua lita elfu 96 tu.

Aidha, Kamati iliarifiwa kuwa mwitikio wa kuchukua hizo lita elfu 96 ulikuja baada ya Mheshimiwa Rais Dr. John Pombe Magufuli, kupita katika kiwanda hicho na kutoa maelekezo kwa Wizara ya Afya kuhakikisha Halmashauri zote nchini zikachukue dawa hiyo ndipo kiasi hicho kilichukuliwa lakini mpaka sasa fedha za kiasi kilichochukuliwa hazijalipwa kiwandani.

**Mheshimiwa Spika**, kiwanda hiki kilianzishwa kwa lengo mahsusi la kutaka kutokomeza ugonjwa wa Malaria Nchini, lakini utekelezaji umekuwa na changamoto ambapo mteja mlengwa (Wizara ya Afya) amevunja makubaliano ya awali jambo ambalo linaleta sintofahamu na kukwamisha uendeshaji wa kiwanda.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haijafurahishwa na kinachoendelea katika kiwanda hiki na ikitazamiwa kuwa kwa sasa Nchi yetu imejielekeza katika Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda, wakati huohuo Kiwanda kama hiki kutopata ushirikiano tena na Mamlaka kubwa ya Serikali jambo hili halileti picha nzuri.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Wizara ya Viwanda kukaa chini na Wizara ya afya nakufanya marejeo ya makubaliano ya awali, sambamba Kamati inatoa rai kwa Serikali kutafakari upya nia ya kuanzishwa kiwanda kile kwa kuzingatia nafasi ya Tanzania katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa Malaria.

- b) Shughuli za Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO) (Mradi Namba 6260, Fungu 44);

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO) chini ya Mradi Na. 6260–Institutional Support liliidhinishiwa jumla ya Shilingi 4,000,000,000/= kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake.

Majukumu yaliyopangwa kutekelezwa kutokana na fedha hizi ni pamoja na kuanzisha na kukidhi vigezo vya kupata ithibati kwa maabara ya mafuta na gesi asili, maabara ya makaa ya mawe, maabara ya vipimo vya chuma ngumu, upatikanaji wa ithibati na kuboresha maabara ya chakula; kukamilisha vigezo vya upatikanaji wa ithibati kwa maabara ya kemia na maabara ya mazingira; kuhuisha teknolojia ya kutumia sensor kufuatilia uzalishaji viwandani kwa wajasiliamali; kutengeneza na kuhuisha teknolojia kwa ajili ya usalama viwandani; kukamilisha Ujenzi wa jengo la Utawala kwa ajili ya kliniki ya viwanda na kituo cha taarifa za kiteknolojia.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 13 Machi, 2020, siku ambayo Kamati ilitembelea Shirika, fedha zilizotengwa kwa ajili ya Shirika zilikuwa hazijapokelewa hivyo shughuli zote zilizokuwa zimepangwa kufanyika zilikuwa hazijafanyika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata wasaa wa kuzunguka katika eneo la Shirika na kujionea shughuli nyingine mbalimbali zinazoendelea. Maeneo yaliyotembelewa ni pamoja na Maabara ya Chakula na Maabara ya Mazingira ambapo kwa pamoja maabara hizi hufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu wa namna

ya kuzalisha bidhaa kwa kutumia teknolojia rafiki kwa mazingira lakini pia bidhaa zenye ubora bila kutumia kemikali hatarishi kwa Binadamu na Mazingira pia.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilishuhudia umahiri wa Maabara hizi mbili kwani zilikuwa zimewezeshwa kwa kupatiwa mashine na mitambo inayoendana na teknolojia ya kisasa. Aidha, Kamati ilibaini kuwa kuna mfanano wa majukumu ya Maabara hizi na yale yanatekelezwa na Taasisi nyingine za Serikali ambapo jukumu la Mazingira linatekelezwa na Baraza la Tiafa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira – NEMC huku jukumu la Chakula likitekelezwa na Shirika la Viwango Tanzania – TBS. Kwa kuzingatia mfanano huo Kamati inatoa rai kwa Serikali kuangalia namna ya kuzisimamia taasisi hizi, ili ikiwezekana vitengo husika vikaunganishwa na kufanya kazi pamoja.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilitembelea maabara ya Elektroniki na Teknolojia ya Habari ambayo inajihusisha na utafiti wa mifumo ya kielektroniki na TEHAMA yenye kurahisisha ufanyaji kazi viwandani.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kazi kubwa zinazoendelea kutekelezwa na Shirika, Kamati ilielezwa changamoto mbalimbali ambazo zinalikumba Shirika. Changamoto hizo ni pamoja na:-

- i) Upungufu wa Watumishi hususani katika maeneo ya kihandisi kama vile metalajia, nishati, ngozi na mitambo;
- ii) Kutopokea fedha za maendeleo;
- iii) Ukosefu wa ithibati katika maabara tano zilizopo chini ya taasisi hii jambo



linalopelekea Shirika kukosa sifa ya kuhudumia baadhi ya wadau hususani kampuni za kigeni; na

- iv) Kushindwa kulipa madeni ya wazabuni na ardhi kutokana na Shirika kutotengewa Fedha za matumizi mengineyo (O/C)

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tano imelenga kujenga Uchumi wa Viwanda, na kwa kuwa Shirika hili lilianzishwa kwa lengo la kupata chombo kitakachofanya utafiti na kutoa huduma za kitaalamu ili kusaidia maendeleo ya viwanda, Kamati inaishauri Serikali kuliwezesha kikamilifu Shirika hili ili liweze kutekeleza majukumu yake ambayo yatasaidia katika ukuaji wa Sekta ya Viwanda nchini.

- c) Mradi wa EPZ Development Kurasini Trade and Logistic Centre (Mradi Na. 6260 Fungu 44);

**Mheshimiwa Spika**, Kurasini Trade and Logistic Centre ni Mradi unaolenga kuliendeleza eneo hilo kwa kujenga Kituo cha Biashara na Ugavi. Mpango wa Serikali kupitia Mamlaka ya EPZ ni kuliendeleza eneo hilo kama Soko la Mazao mchanganyiko. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Mradi huu ulitengewa jumla ya Shilingi 3,000,000,000/= kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali.

Shughuli zilizopangwa kutekelezwa kutokana na fedha hizo ni pamoja na kukamilisha hatua za utwaaji wa ardhi iliyobaki ili kupata hati; kufanya upembuzi yakinifu na kuandaa Masterplan; kufanya usanifu wa kina na ujenzi wa miundombinu ya ndani; na kuweka uzio wa eneo la Mradi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa ya Mpango wa uwekezaji katika eneo la EPZA – Kurasini iliyojumuisha eneo la maghala kwa ajili ya kuhifadhi mazao ya Chai, kahawa, mazao ya mbogamboga na matunda, Maghala ya Bodi ya Mazao Mchanganyiko (CPB) na ujenzi wa Kituo cha Huduma zote kwa pamoja (One Stop Service Centre).

Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 14 Machi, 2020, Kamati ilipotembelea eneo la Mradi, Fedha za Maendeleo zilikuwa hazijapokelewa hivyo shughuli zote zilizopangwa kutekelezwa hazikuwa zimeanza. Aidha, katika kutembelea eneo la mradi Kamati ilishuhudia shughuli za Uegeshaji wa Magari na makasha (makontena) jambo ambalo sio lengo kuu (Co business) la eneo hilo la Mradi. Kamati ilihoji jambo hilo na kupewa taarifa kuwa shughuli hizo zinazoendelea katika eneo hilo zinatekelezwa/kusimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Temeke.

Mheshimiwa Spika, Kamati haikuridhishwa na jibu hasa hilo, kitendo cha Mamlaka ya EPZ kuruhusu shughuli hizo zifanyike ikifahamu fika kuwa sio shughuli rasmi ya eneo lile, pia kutokufuatilia juu ya mapato yanayopatikana kutokana na shughuli hizo ili kujua yanapokwenda kwani hayaingii kwenye Mamlaka ya EPZ.

Mheshimiwa Spika, baada ya ziara katika Mradi wa EPZ Deveelopment Kurasini Kamati ilikuwa na inaushuri ufuatao;-

- i) Serikali kuhakikisha Mradi huu unaanza utekelezaji wake mara moja kwa kuwa eneo lile lilikuwa limeshalipiwa fidia na fedha iliyotumika kulipa fidia ni kubwa (Bilioni 101) ambapo kwa sasa fedha hizo zimekuwa kama zimefukiwa tu, hadi sasa ni takribani miaka saba (7) tangu eneo

limefidiwa lakini utekelezaji wa mradi haujaanza na kama nchi hakuna tunachonufaika kutokana na fedha iliyofidiwa;

- ii) Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka ya EPZ isimamishe mara moja biashara ya kuegeshaji wa Magari na makasha katika eneo la mradi kwa kuwa shughuli hiyo sio lengo kuu katika eneo hilo la Mradi;
  - iii) Kabla ya Mwaka wa fedha 2019/2020 kuisha Serikali iipatie EPZA fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka huu ili iweze kuzungushia uzio eneo la mradi kwa lengo la kuzuia wavamizi; na
  - iv) Serikali ifuatilie kwa ukaribu mapato yatoanayo na shughuli ya uegeshaji wa magari na makontena katika eneo la EPZA Kurasini na kubaini fedha zilizokuwa zinakusanywa kama zilikuwa zinafika katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa kuwa taarifa zilizopo ni kuwa Gari moja linaegeshwa kwa shilingi elfu tano (5,000) na kwa siku magari yanayoegeshwa ni zaidi ya mia mbili 200.
- d) **Wakala wa Vipimo (WMA), Kituo cha kupima magari yabebayo mafuta na Kupima Dira za Maji (Water Meter Test Bench) Misugusugu – Pwani.**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara ya Viwanda na Biashara iliidhinishwa Shilingi **1,000,000,000/=** kwa ajili ya kutekeleza Mradi **Na. 6260 Istitutional Support** katika Taasisi ya Wakala Vipimo (WMA). Fedha iliyoidhinishwa ililenga kununua Mashine (Leser Scanner) ya uhakiki wa matanki ya kupokelea mafuta katika bandari ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Hadi kufikia

siku ya ziara ya Kamati, WMA ilikuwa haijapokea fedha hizo jambo lililokwamisha utekelezaji wa jukumu hilo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifuatilia pia utekelezaji wa majukumu ya Wakala Vipimo (WMA), ambapo ilitembelea Mradi wa Kituo cha Uhakiki cha WMA kilichopo Misugusugu – Pwani, kwa lengo la kukagua ufanisi wa kituo hicho. Mradi huu unahusu Ujenzi wa kituo cha Upimaji wa matanki ya mafuta pamoja na mita za maji katika eneo la Misugusugu – Pwani, ulianza Juni, 2015 na uligharimu Biloni 7.3. Kituo kimekamilika na kina uwezo wa kukagua matanki 60 – 70 kwa siku na pia kina uwezo wa kupima mita za maji 1000 kwa siku.

Mradi ulitekelezwa kwa lengo kuongeza ufanisi wa Wakala wa Vipimo (WMA) katika upimaji, hivyo kwa kuwa kituo cha awali kilikuwa na uwezo wa kukagua matanki 8 tu kwa siku lakini pia Wakala haikuwa inafanya ukaguzi wa mita za maji hapo awali.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kazi nzuri inayoendelea kufanywa na kituo hiki, Kamati iliarifiwa changamoto ya uwepo wa baadhi ya Wamiliki na Madereva wa magari ya mafuta kukosa uaminifu na kufanya vitendo vinavyopelekea kuchakachua taarifa vipimo vilivyoripotiwa na cheti cha ukaguzi cha Wakala wa vipimo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri WMA kuongeza kasi ya utoaji elimu juu ya umuhimu wa kuzingatia vipimo na kuwataka wamiliki na madereva wa magari ya mafuta kuacha tabia ya kuchakachua vipimo halali vinavyotolewa na WMA kama ilivyo kwenye Sheria lakini pia kujiwekea uaminifu kwa wateja wao.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa ukaguzi wa Mita za Maji, Kamati inaishauri WMA kuendelea kuzikumbusha Mamlaka za Maji kuwaelimisha Wazabuni wanaopata tenda za kuleta mita za maji juu ya uwepo wa WMA na kazi wanayoifanya ya ukaguzi, pamoja na gharama watakatolingia kutokana na ukaguzi huo. Jambo hili litaondoa changamoto iliyopo sasa ambapo baadhi ya wazabuni bado hawajui kama kuna ukaguzi wa WMA na gharama ya ukaguzi inapaswa kulipwa na wao wazabuni.

## 2.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 13 Mei 2019, Bunge lako tukufu liliidhinisha Bajeti kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali ya Wizara ya Viwanda na Biashara, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Kamati ilipokea na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii na uchambuzi huu ulilenga kufanya ulinganisho na kubaini kuhusu Utekelezaji wa malengo ya Wizara, Ukusanyaji wa mapato na Upatikanaji wa fedha kwa Wizara ikilinganishwa na kiasi kilichoidhinishwa na Bunge hadi kufikia mwezi Machi, 2020.

### 2.2.1 Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara ya Viwanda na Biashara chini ya **Fungu 44 – Viwanda** na **Fungu 60 – Biashara** ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi **14,300,000.00** (Shilingi **5,300,000.00** chini ya **Fungu 44** na Shilingi **9,000,000.00** chini ya **Fungu 60**) kutokana na uuzaji wa nyaraka za zabuni na marejesho ya mishahara endapo mtumishi ataacha kazi.

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Machi, 2020 Wizara ilikuwa haijafanikiwa kukusanya kiasi

chochote cha malengo ya mapato walichokuwa wamejiwekea. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba utekelezaji wa lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ni asilimia sifuri (0). Aidha, kutokana na muda mchache uliobaki ambao ni robo moja tu ya mwaka wa fedha, matumaini ya kukusanya kiasi chote cha shilingi 14,300,000.00 ni hafifu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuishauri Wizara ya Viwanda na Biashara kutafuta vyanzo vipya vya mapato ambavyo vitaweza kuwaletea mapato ya uhakika, Vilevile ipange malengo ya makusanyo yanayoendana na uwezo wake halisi wa kukusanya, na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.

## 2.2.2 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha **2019/2020**, Wizara ya Viwanda na Biashara iliidhinishiwa jumla ya shilingi **100,384,738,848.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake kwa mafungu yote mawili (**Fungu 44 – Viwanda & Fungu 60 – Biashara**). Mgawanyo wa fedha hizo ulikuwa kama ifuatavyo:-

### i) **FUNGU 44**

Fungu 44 – Viwanda, lilitengewa kiasi cha shilingi 79,149,452,000.00, kati ya fedha hizo shilingi 51,500,000,000.00 zilitengwa kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, kiasi hiki ni sawa na asilimia 51 ya fedha zilizotengwa kwa Wizara hii. Kiasi kilichosalia ambacho ni shilingi 27,649,452,000 zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kiasi hiki ni sawa na asilimia 28 ya Fedha zote za Wizara.

ii) **FUNGU 60**

Fungu 60 – Biashara, lilitengewa Shilingi 21,235,286,648.00 kwa ajili ya Matumizi ya kawaida, kiasi hiki ni sawa na asilimia 21 ya fedha zilizotengwa katika Wizarahii. Aidha, katika fungu hili hakuna kiasi chochote cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina**

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2020 ambayo ni robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya Shilingi 26,020,185,845.00 kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Wizara na taasisi zote zilizopo chini yake kwa Mafungu yote mawili (Fungu 44 na 60). Kiasi hiki ni sawa na asilimia 25.92 tu ya fedha zote zilizotengwa katika Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika,** Shilingi **26,020,185,845.00** zilizopokelewa zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, aidha, kiasi hicho ni sawa na asilimia **53.2** ya Shilingi **48,884,739,000.00** ambazo ni fedha zilizokuwa zimeidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mafungu yote mawili (**Fungu 44 & 60**).

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi, 2020, hakuna kiasi chochote cha fedha kilichopokelewa na Wizara kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa kina wa Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka fedha 2019/2020, Kamati ilibaini kwamba:-

- i) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina si wa kuridhisha kwa kuwa hadi kufikia Februari, 2020 fedha zilizotolewa ni fedha za Matumizi ya kawaida pekee na zimetolewa kwa asilimia 53.2 tu;
- ii) Upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

kutoka Hazina sio wa kuridhisha, hadi kufikia Februari, 2020 hakuna kiasi cha fedha kilichotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya maendeleo kwa maana ya kwamba kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Miradi ya Maendeleo ilitekelezwa kwa asilimia sifuri (0);

**Mheshimiwa Spika**, mtazamo wa Kamati ni kwamba mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha kwa Wizara ya Viwanda na Biashara unaashiria kukwama kwa utekelezaji wa baadhi ya majukumu yaliyopangwa na Wizara hii hususani utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha fedha zinazoidhinishwa na Bunge zinapelekwa tena kwa wakati ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yote yaliyokusudiwa.

### **2.2.3 Utekelezaji wa Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifuatilia utekelezaji wa malengo ya Wizara ya Viwanda na Biashara yaliyopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kwa lengo la kujiridhisha na utekelezaji wake. Wizara ilibainisha hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa malengo hayo.



Kamati ilipongeza hatua hizo, hata hivyo iliendelea kuisisitiza Serikali kuongeza kasi katika maeneo yafuatayo: -

- i) Kukamilisha maandalizi ya kuandaa waraka ambao utasaidia katika kutunga Sheria ya kusimamia biashara ya Chuma Chakavu. Biashara hii ya chuma chakavu inachangamoto nyingi na ikisimamiwa vizuri inauwezo wa kuleta mchango mkubwa kwenye mapato ya nchi.
- ii) Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini na mahusiano ya kibiashara ya kikanda na kimataifa, hivyo kuwezesha kupanua fursa za biashara na masoko kwa bidhaa zinazozalishwa nchini.
- iii) Kuendelea kuziboresha na kuzipatia fedha taasisi za utafiti ambazo zipo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa lengo la kuziwezesha kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa.

### **3.1 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI KUHUSU BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo mbalimbali. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati, hata hivyo kuna maeneo ambayo Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wake na inaendelea kuisisitiza Serikali kuongeza juhudi ya utekelezaji wa maagizo hayo. Maeneo hayo ni pamoja na:-

- i) Kukamilisha mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Viwanda (SIDP 1996-2020) ili iweze kuendana na mazingira ya sasa ya sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Aidha, Sera inayoandaliwa itoe nguvu kwa Wizara ya Viwanda na Biashara kusimamia masuala ya viwanda na yale masuala mtambuka yanayohusika moja kwa moja katika kuhudumia ujenzi wa viwanda. Vilevile, Sera iwe na kauli mbiu zote zinazohusika katika ujenzi wa viwanda. Mfano upatikanaji wa vibali vya uwekezaji, upatikanaji wa ardhi ya uwekezaji, upatikanaji wa vibali vya kufanya kazi nchini, upatikanaji wa huduma za maji, umeme na usafiri.
- ii) Changamoto ya ushindani usio wa haki unaotokana na uingizwaji holela wa bidhaa kutoka nje na kuuzwa kwa bei nafuu. Kamati imejulishwa mpango wa Serikali kutunga Sheria ya Kujilinda Dhidi ya Athari za Kibiashara (Trade Remedies Act), Kamati inasisitiza kuharakisha kupatikana kwa sheria hiyo ili tuweze kuvilinda viwanda vyetu hatua ambayo itachochea sekta ya viwanda nchini kwani soko litapatikana na uzalishaji utaongezeka.
- iii) Kutatua changamoto ya ushindani katika bidhaa ya vyandarua vinavyozalishwa hapa nchini na vile vinavyoingia kutoka nje ya nchi, hii ifanyike kwa kuondoa VAT katika malighafi zinazotumiwa na viwanda vya ndani vinavyozalisha vyandarua. Kamati inatoa rai kwa Serikali kufanyiakazi mapendekezo yaliyowasilishwa na Wizara ya Viwanda na Biashara juu ya changamoto hii, ili kuweza kulinda viwanda vyetu vya ndani vinavyozalisha chandarua na kuvipa uwezo wa kushindana katika soko.

#### 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

##### 4.1.1 Uchambuzi wa malengo/mpango

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ya Viwanda na Biashara imejipangia malengo na vipaumbele mbalimbali kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri. Kamati ilipitia malengo na vipaumbele vya Wizara hii kwa lengo la kubaini tija inayoweza kupatikana kutokana na malengo yaliyopangwa kutekelezwa kwa fedha zinazoombwa katika Fungu 44 na 60.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati juu ya malengo ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umebaini kuwa Malengo haya yalikuwa yanaendana na hati idhini Serikali iliyoainisha majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara; Aidha, Kamati ilibaini kuwa malengo hayo yamejitosheleza na kuwa utekelezaji wake unatarajiwa kuboresha hali ya biashara nchini na kukuza Uchumi wa Nchi. Ni ushauri wa Kamati kuwa ili malengo haya yatekelezwe kikamilifu Serikali inapaswa kuhakikisha fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara zinatolewa kwa wakati.

##### 4.1.2 Makisio ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia mafungu yake yote mawili yaani Fungu 44 – Viwanda na Fungu 60 – Biashara imepanga kukusanya shilingi 15,000,000.00 kutokana na uuzaji wa nyaraka za zabuni na makusanyo mengineyo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kiasi kilichopangwa kukusanywa na Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kimeongezeka kwa asilimia 4.89 ukilinganisha na mpango wa makusanyo ya Mwaka wa fedha 2019/2020. Kamati inapata wasiwasi na jinsi Wizara inavyoweka makadirio yake ya makusanyo, wasiwasi wa Kamati unatokana kutofikiwa kwa lengo la makusanyo ya Wizara hii katika kila mwaka angalau kwa asilimia 75.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Wizara kufanya makadirio yenye uhalisia kulingana na vyanzo vya mapato ilivyonyavyo. Aidha, Kamati naendelea kuinasisitiza Wizara kuweka mikakati mahususi ya kutafuta vyanzo vipya vya mapato ili waweze kuongeza makusanya.

#### **4.1.3 Mpango wa Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ya Viwanda na Biashara imetengewa jumla ya Shilingi 81,366,902,000.00 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake chini ya mafungu yote mawili Fungu 44 na 60. Kati ya fedha zinazoombwa ni shilingi 51,679,016,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Mawaida na shilingi 29,687,886,000.00 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

##### **i) FUNGU 44- VIWANDA**

Fungu 44 – Viwanda limetengewa jumla ya shilingi 57,414,395,000 kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Wizara chini ya fungu hili, kiasi hiki ni sawa na asilimia 70.6 ya fedha zote zinazoombwa na Wizara ya Viwanda na Biashara.

Bajeti inayoombwa chini ya Fungu 44 imejumuisha shilingi 27,726,509,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya kawaida ambayo inajumuisha shilingi 22,606,136,000.00 ya mishahara ya watumishi na shilingi 5,119,373,000.00 ya matumizi mengineyo (OC). Kiasi kilichosalia ambacho shilingi 29,687,886,000 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo, ambapo shilingi 29,187,886,000.00 fedha za ndani na shilingi 500,000,000.00 fedha za nje.

**ii) FUNGU 60- BIASHARA**

Fungu 60 – Biashara inaombewa Shilingi 23,952,507,000 ambazo ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kiasi kinachoombwa chini ya fungu hili kimejumuisha Shilingi 1,470,091,000 ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo na Shilingi 22,482,416,000 kwa ajili ya mishahara.

**Mheshimiwa Spika**, chini ya Fungu hili haijatengwa fedha yoyote kwa ajili ya miradi ya maendeleo na hii ni kutokana na ufinyu wa ukomo wa bajeti kwa fungu hili. Aidha, hali ya FUNGU 60 kukosa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo imeendelea kujitokeza kwa miaka miwili mfululizo ambayo ni Mwaka wa Fedha 2019/2020 na 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati kuhusiana na Mpango wa bajeti umebaini mambo yafuatayo:-

- i) Kiasi cha bajeti kilichotengwa kwa ajili ya mafungu yote mawili ni pungufu kwa asilimia 18.9 ukilinganisha na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ya Mwaka wa Fedha unaoishia yaani 2019/2020;
- ii) Upungufu wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara unaathari kubwa kwa upande wa fedha za Miradi ya

Maendeleo ambayo imepungua kwa asilimia 42.4 ukilinganisha na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/2020;

- iii) Kwa miaka miwili mfululizo fedha za bajeti zinazotengwa kwa Wizara hii zimeendelea kupungua kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 ilipungua kwa asilimia 29.9 na kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imepungua kwa asilimia 18.9.

Mheshimiwa Spika, kushuka kwa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kunaashiria kukwama kwa utekelezaji wa baadhi ya majukumu ya Wizara hususani Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Aidha, hali hii inaleta mashaka katika utekelezaji wa kipaumbele cha taifa cha kuwa na Uchumi wa Kati kwa kupitia Viwanda ifikapo 2025 kwa kuwa miradi hii ni miradi ya kichocheo kwa Sekta hii ya Viwanda. Kamati inaishauri serikali kuongeza bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara na kuhaikisha fedha hizo zinatolewa tena kwa wakati, ili kuleta ufanisi katika miradi husika kwa lengo la kupata matokeo yenye tija.

## **5.1 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo na kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2018/2019, pamoja na kuchambua mapendekezo ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa fedha 2019/2020 ya Wizara hii, Kamati ina Maoni na Ushauri kadhaa kwa Serikali.

**i) Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina**

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mwenendo usioridhisha wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina hususani fedha za miradi ya maendeleo. Mfano katika mwaka 2019/2020 mpaka kufikia sasa hakuna fedha za maendeleo zilizopokelewa jambo linalokwamisha utekelezaji wa miradi husika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Serikali inaendelea kutekeleza miradi mingine ambayo inatazamiwa kuwa kichocheo kwa Sekta ya Viwanda, Kamati inaona bado kuna umuhimu kwa Wizara mama ya Viwanda inayohusika na utekelezaji wa Azma ya Ujenzi wa Viwanda ikapewa kipaumbele katika kutengewa fedha za kutosha na fedha hizo zitolewe kwa wakati.

**ii) Utekelezaji wa Mradi ya Kimakati**

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Mchuchuma na Liganga, Magadi Soda Engaruka, Bagamoyo SEZ, Kurasini Logistic Centre na Mtwara Free Port ni Miradi iliyotambuliwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa kama miradi ya kimkakati na kipaumbele. Utekelezaji wa miradi hii umekusudiwa kuwa kichocheo cha Sekta ya Viwanda Nchini kwani inatarajiwa kuzalisha malighafi ambazo zingetumiwa na viwanda vingine.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa tunapoelekea kufikia ukomo wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka mitano 2016/2017 – 2020/2021 utekelezaji wa miradi hii umeonekana kusuasua. Kamati inaishauri

Serikali kuongeza juhudi katika kufuatilia na kusimamia Utekelezaji Miradi hiyo kwa lengo la kuikamilisha na kuanza kupata tija iliyokusudiwa.

**iii) Uendelezaji wa maeneo maalumu ya Uwekezaji chini ya Mamlaka ya EPZ**

**Mheshimiwa Spika**, moja ya jukumu la Mamlaka ya EPZ ni kutwaa maeneo ambayo hutambulika kama maeneo maalumu ya uwekezaji, baada ya kutwaa maeneo hayo Mamlaka ya EPZ hupaswa kuyaendeleza kwa kuyawekea miundombinu wezeshi na kuyaweka tayari kwa uwekezaji. Mpango huu umekumbana changamoto ya Uhaba wa Fedha za kuendeleza maeneo hayo hivyo yameishia kuachwa tu wazi jambo linalotoa mianya kwa watu wengine kuvamia maeneo hayo na kufanya shughuli zao bila kibali cha EPZA (Mfano EPZA Kurasini). Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha fedha zinazotengwa kwa ajili ya kuendeleza maeneo ya EPZA zinatolewa kwa wakati ili kuwezesha kutekeleza majukumu husika. Hatua hii itachochea/itavutia uwekezaji kwa kuwa muwekezaji atakuta eneo tayari likiwa na miundombinu wezeshi yote.

**iv) Utekelezaji wa Mradi wa Kufufua Viwanda vilivyobinafsishwa**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na juhudi mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali katika kurudisha Serikalini Viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo havifanyi kazi, Kamati inatambua changamoto wanayokumbana nayo katika kutekeleza zoezi hilo ambayo ni baadhi ya mikataba ya mauziano kukosa kipengele cha kurejesha Serikalini. Kamati inatoa rai kwa Serikali kuongeza umakini katika mikataba



inayoendelea kuiingia juu ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Ubia au wanayopatiwa wawekezaji moja kwa moja kwa kuhakikisha inazingatia Sheria ya Makinikia ili kuepuka mikwamo kama hii iliyojitokeza.

v) **Uendeshaji wa Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Wajasiriamali NEDF**

**Mheshimiwa Spika**, katika kuhamasisha Ujenzi wa Tanzania ya Viwanda ni lazima Serikali iweke mazingira ya kusaidia wawekezaji wadogo wa ndani kushiriki kikamilifu. Kama tunavyofahamu wazalishaji wadogo wa ndani wanakabiliana na changamoto ya rasilimali fedha. Katika kutatua changamoto hii, Kamati inatoa rai kwa Serikali kuutumia vyema Mfuko wa Maendeleo wa Wajasiriamali NEDF.

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko huu upo lakini hauna mtaji wa kutosha kuhudumia wahitaji walio wengi. Aidha, Mfuko huu umekuwa ukitengewa fedha katika Bajeti za Wizara za kila mwaka lakini fedha hizo hazipelekwi. Kamati inashauri Serikali kuendeleza mfuko huu kwa kuupatia fedha zinazopitishwa na Bunge ili uendelee kuwasaidia na kuwanufaisha watazania wengi.

Aidha, Kamati inatoa rai kwa Taasisi za Fedha kuunga mkono juhudi za Serikali kwa kuamua kuanzisha mikopo yenye masharti nafuu yanayoendana na masharti ya Mfuko wa NEDF.

vi) **Taasisi za Udhhibiti kutowasiliana**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na uwepo wa jitihada mbalimbali za Serikali katika kuhakikisha mamlaka za udhibiti zinatekeleza majukumu yake bila kuonekana kero kwa wawekezaji na

wafanyabishara, bado yapo malalamiko kutoka kwa baadhi ya wawekezaji kuwa baadhi ya mamlaka hupinga misamaha (exemption) au vivutio vinayotolewa na mamlaka nyingine, (mfano kivutio kilichotolea chini ya Mamlaka ya EPZ kupingana na Sheria mama ya TRA). Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuongeza nguvu katika kuzisimamia mamlaka hizo kwa kuhakikisha zinawasiliana na kufanya kazi kwa pamoja.

vii)

**Sekta ya Sukari na Sekta ya Mafuta ya Kula Mheshimiwa Spika**, Kamati iliarifiwa juu ya tathmini inayofanywa na Wizara ya Viwanda na Biashara juu ya hali halisi ya mahitaji ya bidhaa ndani ya nchi, uwezo wa uzalishaji wa viwandani pamoja na gepu lililopo ili kukidhi mahitaji ya nchi. Kamati inaishauri Serikali kutilia msisitizo Sekta ambazo mara kwa mara zimekuwa zikikumbana na changamoto kama Sekta ya Sukari na Sekta ya Mafuta.

**Mheshimiwa Spika**, katika kutatua changamoto ya Sekta ya mafuta ya kula na sukari, Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Wizara ya Kilimo zifanye kazi kwa pamoja ya kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya kilimo cha miwa na mbegu za mafuta ili kuzalisha malighafi za kutosha kwa ajili ya kulisha viwanda vyetu. Jambo hilo litaongeza uzalishaji katika viwanda vilivyopo ndani ya Nchi.

viii) **Malimbikizo ya Kodi ya Ongezeko la thamani (VAT refund) pamoja na Ushuru wa Forodha 15% (refundable import duty 15%) katika Sukari ya Viwandani**

**Mheshimiwa Spika**, bado kuna malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara na wamiliki wa viwanda juu ya ucheleweshaji unaofanywa na TRA katika kurejesha Kodi ya Ongezeko la

thamani (VAT refund) pamoja na Ushuru wa Forodha 15% (refundable import duty 15%) katika Sukari ya Viwandani. Jambo hili linapelekea kupungua kwa mitaji yao kutokana na malimbikizo makubwa ya madai yao kwa Serikali na hivyo kuwapunguzia uwezo wao wa kujiendesha. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kufanya marejesho ya kodi hizo kwa wakati.

ix) **Changamoto ya upatikanaji wa vibali vya kufanya kazi Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Uhamasishaji wa Ujenzi wa Tanzania ya Viwanda umevutia pia uwekezaji wa teknolojia mpya kutoka sehemu mbalimbali nje ya Tanzania. Jambo hili linaambatana na uhitaji wa taaluma na wataalamu kutoka nje ya nchi ambao kwa sasa hawapatikani hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, utaratibu wa kupata vibali vya ajira unatekelezwa chini ya Sheria ya Kazi pamoja na Sheria ya Uwekezaji ya TIC ambapo zimeonekana kuleta msigano. Sheria ya TIC inaruhusu muwekezaji kuja na watu watano lakini Sheria ya Kazi inataka watu hao watano wawe ni wale ambao taaluma zao hazipatikani kabisa nchini lakini imeacha kipengele cha uzoefu (experience). Kamati inaishauri Serikali kufanya mapitio na maboresho katika Sheria hizi mbili ikiwezekana kuipa nguvu Sheria ya Uwekezaji ya TIC ikizingatiwa kuwa wawekezaji wengi kabla ya kuja kuwekeza nchini huangalia Sheria ya Uwekezaji inasema nini.

6.0 **HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru na kukupongeza sana kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu kwa weledi mkubwa katika

kipindi chote hiki cha uhai wa Bunge la Kumi na Moja.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Spika, kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge. Niwapongeze pia Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukushauri na kukusaidia katika kuendelea kuendesha vikao vya Bunge la Kumi na Moja.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati yangu naomba nitumie fursa hii kutoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa John Pombe Mgufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hatua mbalimbali anazoendelea kuzichukua zikilenga kuboresha utekelezaji wa azma ya kujenga Tanzania ya Viwanda.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa kushiriki kikamilifu wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni kuhusu Bajeti ya Wizara hii mbele ya Bunge lako tukufu. Majina yao ni kama inavyosomeka hapa chini na kwa ruhusa yako naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge (Hansard).

ii)	Mhe. Suleiman Ahmed Sadiq, Mb	<b>Mwenyekiti</b>
ii)	Mhe. Kanal (Mst.) Masoud Ali Khamis, Mb	<b>M/Mwenyekiti</b>
iii)	Mhe. Salim Hassan Turkey, Mb	Mjumbe
iv)	Mhe. Gimbi Dotto Masaba, Mb	Mjumbe
v)	Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma, Mb	Mjumbe
vi)	Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb	Mjumbe
vii)	Mhe. Munira Mustafa Khatibu, Mb	Mjumbe
viii)	Mhe. Musa Rashid Ntimizi, Mb	Mjumbe
ix)	Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb	Mjumbe
x)	Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb	Mjumbe
xi)	Mhe. Khamis Ali Vuai, Mb	Mjumbe

xii) Mhe. Zainabu Mndolwa Amiri, Mb	Mjumbe
xiii) Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb	Mjumbe
xiv) Mhe. Sylvestry F. Koka, Mb	Mjumbe
xv) Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb	Mjumbe
xvi) Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb	Mjumbe
xvii) Mhe. Jafar Sanya Jussa, Mb	Mjumbe
xviii) Mhe. Machano Othman Said, Mb	Mjumbe
xix) Mhe. Kalanga Julius Laizer, Mb	Mjumbe
xx) Mhe. Saed Kubenea, Mb	Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Innocent Lugha Bashungwa (Mb), Naibu Waziri wake Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya (Mb), Makatibu Wakuu, pamoja na wataalamu wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa jinsi walivyoshirikiana na Kamati katika kujibu hoja za Wajumbe wa Kamati, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, na kufafanua kwa kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, naomba kumshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bw. Michael Chikokoto, makatibu wa Kamati Bi. Zainab Mkamba na Bi Mwajuma Ramadhan pamoja na Msaidizi wa Kamati Bi. Paulina Mavunde kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 44 – Viwanda na Fungu 60 – Biashara, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kiasi cha shilingi 81,366,902,000 ambapo shilingi 51,679,016,000 ni kwa

ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 29,687,886,000 ni kwa ajili matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

.....  
**Mhe. Kanal (Mst) Masoud Ali Khamis, Mb**  
**MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA,**  
**BIASHARA NA MAZINGIRA**

6 Mei, 2020

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kanali Masoud, Makamu Mwenyekiti wa Kamati, kwa taarifa hiyo. Waheshimiwa Wabunge, Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya Viwanda na Biashara haikuwekwa Mezani kwa hiyo, sitamwita sasa kwa ajili ya kuwasilisha. Ninayo majina hapa kwa ajili ya uchangiaji kwenye hii Wizara ya Viwanda na Biashara, kwa hiyo, tutaanza kama utaratibu wetu ulivyo.

Tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni, anaweza kuwa yuko Msekwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Mheshimiwa Raphael Michael Japhary ajiandae. Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni.

Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Raphael Michael Japhary, Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu ajiandae.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, na awali kabisa nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na kwa kazi nzuri ambayo ameendelea kuifanya

kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu. Nitumie fursa hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na watendaji wote katika Wizara ya Viwanda na Biashara kwa utekelezaji mzuri wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Bagamoyo kuna maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya *EPZ*. Maeneo haya ni mengi na makubwa na baadhi ya maeneo haya bado hayajalipiwa fidia takribani sasa hivi miaka kumi na moja tangu ambapo yametwaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuja Bagamoyo kufungua kiwanda cha Elven mwaka 2017 alitoa maelekezo kwamba maeneo yote yale ambayo hayajalipiwa fidia wananchi warudi katika maeneo hayo waendeleze maeneo yao na waweze kujipatia faida na maeneo hayo. Ila sasa kuna kikwazo; wananchi hawa wanaporejea katika maeneo hayo na kutaka kupima maeneo na kuyamiliki maeneo hayo, halmashauri ya wilaya inawagomea kupima maeneo, *EPZ* nayo pia haikubali maeneo hayo yapimwe na wananchi wayamiliki kama ambavyo wangependa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hoja ni kwamba bado *GN* ya Serikali inaelekeza kwamba maeneo hayo ni maeneo ya *EPZ*. Kwa hiyo, mradi tu *GN* inaonesha hivyo kwa hiyo maeneo hayo bado wananchi hawawezi wakayatumia kama vile maelekezo ya Mheshimiwa Rais ambayo ameyatoa. Sasa Mheshimiwa Rais ameyatoa maelekezo haya miaka mitatu sasa au zaidi, tuseme mwaka wa nne huu umeenda na maelekezo ya Mheshimiwa Rais ndiyo maelekezo ya mwisho katika miongozo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri makini Bashungwa, kijana mchapakazi, asimamie kwa umakini sana kazi hii ya kuandaa *GN* ili kuyaondosha maeneo yale yote ambayo hayajalipiwa fidia kama alivyoelekeza Mheshimiwa Rais basi maeneo haya yarudi kwa wananchi wayaendeleze. Na kwa wale ambao wangependa kuyauza

maeneo hayo kwa watu wengine basi yawafaidie kwa kuyauza maeneo hayo kwa watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba GN hii ambayo Mheshimiwa Waziri aiandae pia iondoshe maeneo yale ya Mradi wa EPZ Awamu ya Pili ambao una jumla ya hekta 3,338. Maeneo yote ambayo yanaangukia EPZ Awamu ya Pili, moja, hayajatahminiwa; namba mbili hayajapimwa; namba tatu, hayajalipiwa fidia. Kwa hiyo, nayo pia yanaangukia katika maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwamba maeneo haya hayajalipiwa fidia kwa hiyo basi yarudi tu katika mikono ya wananchi waendeleo kuyatumia na wafanye kazi nyingine katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo namwomba sana Mheshimiwa Waziri ajitahidi kwa juhudi zake zote, yeye ndio mwenye dhamana katika jambo hili na utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais basi ayatekeleze ili wananchi wasipate unyonge. Kwasababu sasa hivi jimboni wananchi wanalalamika sana kwamba nani kwani mkubwa katika nchi hii ikiwa Mheshimiwa Rais wetu ametupa maelekezo haya. Lakini ukienda halmashauri wanakataa, EPZ wanakataa; nani mwingine aje kusema neno ambalo wanaweza kukubali likatekelezwa zaidi ya yale ambayo tumeelezwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la fidia ya wananchi wa Pande na Mingotini wanaopisha mradi wa Bandari ya Bagamoyo. Kuna wananchi takribani 687, wamehakikiwa mapunjo yao ya fidia na Mthamini Mkuu wa Serikali baada ya TPA kuilipa fedha Ofisi ya Mthamini Mkuu. Lakini wananchi hawa mpaka leo baada ya kuhakikiwa bado hawajalipwa fidia zao stahiki. Naiomba Serikali yetu Tukufu ifanye juhudi kuhakikisha kwamba wananchi hawa wanalipwa mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la makazi mbadala kwa wananchi ambao wanapisha Mradi wa Bandari na wananchi hawa waliahidiwa na Serikali kupitia barua ya Mkurugenzi Mkuu wa EPZA tarehe 20, Januari, 2014



kwamba watahamishiwa katika Shamba la Kidagoni Bagamoyo ili waondoke kwenye mradi huo; takribani kaya 460 zenye wakazi 1,670 itabidi waondoke.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Kijiji kizima cha Pande lazima kiondoke na sehemu ya Kijiji cha Mingotini kiondoke. Wananchi hawa hawatakuwa na mahali pengine pa kwenda kwa kuzingatia kwamba Bagamoyo ni ndogo na haina ardhi ya kuwawezesha wananchi hawa kuhamia katika maeneo yoyote yale watakapopenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kengele imelia, muda wangu umeisha; nakushukuru sana kunipa fursa. Namtakia kila la heri Mheshimiwa Waziri, naitakila kila la heri Serikali ya Awamu ya Tano katika utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kawambwa. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Raphael Michael Japhary, nadhani atakuwa yuko Msekwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mheshimiwa Deogratias Ngalawa ajiandae.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Kwanza, niendeleo kutoa pole kwa wenzetu ambao wameshatangulia mbele ya haki, Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Waziri wa Viwanda na Biashara inaonekana kwamba Sekta ya Viwanda ina mchango mkubwa sana katika Pato la Taifa katika miaka hii ya karibuni kuliko ilivyokuwa huko nyuma. Mchango wa viwanda kwenye Pato la Taifa ni asilimia 8.5, mchango wa viwanda vidogo na biashara ndogo ni asilimia 35, mchango wa Sekta ya Uzalishaji ni asilimia 8.8 katika Pato la Taifa. Lakini kuna Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogondogo imeajiri zaidi ya watu milioni tisa na Sekta ya Uzalishaji imeajiri zaidi ya watu 306,180.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika haya mafanikio yanayotajwa na Waziri kwenye hotuba yake ni lazima tuone namna gani sasa kutokana na hali hii tuliyonayo ya Janga hili la *corona* ambalo kwa kiwango kikubwa litakuwa limeathiri sana wafanyabiashara wa viwanda, wafanyabiashara wadogowadogo, wafanyabiashara wa jumla na rejareja, namna gani kama Serikali, kama Taifa, tunawasaidia wafanyabiashara baada ya janga hili kuisha katika nchi yetu ama kupungua katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tuwe na mpango na najua inawezekana, Serikali ina timu inayofanya hiyo tathmini, kwa hiyo ni vizuri kwenye Bajeti Kuu tuone kwamba ni unafuu gani umetolewa kwa wafanyabiashara, ni unafuu gani umetolewa kwa wenye viwanda, ni unafuu gani umetolewa kwa wazalishaji mbalimbali ili hao watu wasaidiwe. Na siku zote nasema ni lazima tuone hawa watu kama ng'ombe wetu wa maziwa ambaye tunatakiwa tumlishe ili tuweze kumkamua maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vizuri tuone namna gani tunawasaidia watu hawa ili pia haya mafanikio yaliyozungumzwa yasiptotee, na wao waweze kuendelea ku-*sustain* kwenye hiyo Sekta yao ya Viwanda na Biashara. Ni jambo la muhimu sana ambalo kama Serikali tunatakiwa tuliangalie kwa sababu kwa vyovyote vile athari zake ni kubwa mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu la pili ni suala la sukari. Huu ni Mwezi wa Ramadhani na bahati nzuri Waziri wa Viwanda alishajibu kwamba inawezekana upungufu wa sukari unasababishwa na kufichwa kwa sukari na baadhi ya wafanyabiashara waliopeva dhamana ya kusambaza hiyo sukari, lakini inawezekana Mheshimiwa Waziri alikuwa sahihi ama kwa kiwango fulani bado kuna maeneo hayajafanyiwa kazi vizuri kwa sababu mpaka tunavyoongea sasa hivi hapa bado sukari ni tatizo. Eneo mojawapo ninalolizungumzia ni eneo la Moshi Mjini ambalo mimi ndiye Mbunge wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyoongea sasa hivi hapa maduka hayana sukari, lakini ni kwa nini hayana sukari? Ni kwa sababu, bei elekezi ya Serikali haiendani na uhalisia wa soko. Bei elekezi ya Serikali kwa mfano kwa Moshi kwa rejareja ni kwa bei ya shilingi 2,700/= ambayo kwa kilo 50 ni shilingi 135,000/=, lakini bei inayotakiwa iuzwe na wafanyabiashara wa jumla ni shilingi 128,000/=. Dar es Salaam sukari tunanunua shilingi 126,000/=:, bahati nzuri mimi nina kibiashara changu kidogo cha *wholesale*, kwa Dar es Salaam tunanunua sukari shilingi 126,000/=; mpaka uifikishe Moshi ni shilingi 130,000/= pamoja na *overhead estimates*. Sasa unaiuzaje kwa shilingi 128,000/=?

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake ili wafanyabiashara wasigombane na Serikali, wameamua kuacha kuagiza sukari. Kwa hiyo, sukari hakuna Moshi. Inawezekana hakuna Arusha na maeneo mengine ambayo kwa kweli siwezi kuyajua kwa sababu, sijapita huko. Kwa hiyo, ninachoomba Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ni vizuri waone namna gani wanatoa bei elekezi inayoendana na uhalisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyozungumza leo, inawezekana *TPC* wakaingiza sukari yao tarehe 18. Watu wanaendelea kuumia bila sukari na hatujui watauza shilingi ngapi, lakini mpaka sasa hivi hapa ni *supplier* mmoja tu Dar es Salaam ambaye ana-*supply* hiyo sukari ambaye bei yake ni shilingi 126,000/= kwa Dar es Salaam. Sasa tutafanyaje watu wetu wapate sukari kwa bei elekezi ambayo kidogo ni *affordable*?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani suala la sukari bado liangaliwe kwa mapana ili mwezi huu wa Ramadhani watu waweze kuumaliza wakiwa nao pia wako katika hali ambayo ni nzuri kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la viwanda vilivyokuwa vimebinafsishwa. Mojawapo ya ahadi ya Mheshimiwa Rais ilikuwa ni kuhakikisha kwamba viwanda vilivyobinafsishwa vinarejeshwa kadiri

inavyowezekana. Mheshimiwa Waziri aliyetangulia nyuma kabla ya Mheshimiwa Kakunda alijaribu kuonesha kwamba kuna hiyo jitihada; aliyemfuata Mheshimiwa Kakunda akaonesha kwamba kuna hiyo jitihada; sasa hivi hapa inawezekana kuna hizo jitihada, lakini eneo la Moshi Mjini viwanda vilivyobinafsishwa bado havijafufuliwa, havifanyi kazi katika malengo yaliyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vile ndio vilikuwa vinatoa ajira kwa watu wetu wa Moshi. Kwa hiyo, Moshi *mostly* watu sasa wamekuwa wanategemea biashara ndogo ndogo, biashara za jumla za rejareja, lakini viwanda vile vilivyokuwa vimebinafsishwa ni kama vimekufa na hakuonekani jitihada zozote za kuvifua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba ile ahadi ambayo ilitolewa na Serikali ya kufufua viwanda ambavyo vilikuwa vimebinafsishwa na havikufanya kazi iliyokusudiwa, basi viweze kufanyiwa kazi ili angalau maeneo mbalimbali yaliyokuwa yanafanya vizuri kwenye masuala ya viwanda, basi yaendelee kupata hiyo nafuu na watu waendeleo kupata ajira na haya yaliyozungumzwa kwenye hotuba, basi yawe na maana; kwa maana kwamba yaguse watu wengi kwa kadiri inavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, bila viwanda hivyo kufufuliwa maana yake ni kwamba, bado hatutakuwa tumesaidia na eneo la Mkoa wa Kilimanjaro liliathirika sana na sera ya ubinafsishaji wa viwanda. Kwa misingi hiyo, ni vizuri sasa tukaona namna gani tunawasaidia watu wa Kilimanjaro na nchi nzima kwa ujumla kuhakikisha kwamba viwanda vilivyokuwa vimebinafsishwa vinafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu la mwisho ni kuomba bado kwamba, tuone namna gani tunazidi kuwapa elimu watu kuhusu suala la ugonjwa huu wa *corona* kwa sababu ugonjwa huu utaathiri sana hiyo kada ya uzalishaji. Kwa hiyo, ni vizuri watu waelimishwe kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba imeonesha kwamba kuna hizo jitihada, lakini ni vizuri jitihada ziongezeke watu wasifanye hili jambo ni la kawaida kwa sababu hili tatizo ni kubwa kweli kweli, ni lazima lifanyiwe kazi na bidii ya kutosha ili kukabiliana nalo kwa umoja wetu kama Taifa na tuweze kuliondoa katika nchi yetu na nchi yetu iendelee kubaki salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Dkt. Dalali Peter Kafumu, atafuatiwa na Mheshimiwa Deogratius Francis Ngalawa na Mheshimiwa Riziki Saidi Lulida, ajiandae.

Mheshimiwa Kafumu, Msekwa. Mheshimiwa Deogratius Francis Ngalawa.

**MHE. DEOGRATIUS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuchangia katika Wizara hii ya Viwanda na Biashara. Kwanza nampongeza Waziri kwa hotuba nzuri na kazi anayoifanya, lakini leo niende moja kwa moja kuongelea miradi ua kimkakati ya Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, imekuwa ni muda mrefu sasa tokea ilipoanza kuzungumziwa Mchuchuma na Liganga. Ni kipindi kirefu na bado hatuoni kama kuna hatua stahiki ambazo zinachukuliwa kuhakikisha kwamba miradi hii inatekelezwa. Kwa sababu naona kwenye ripoti ya Waziri amekuwa akizungumzia kwamba kuna tatizo la mwekezaji kwenye masuala ya mkataba, lakini masuala haya ya mkataba yamechukua muda mrefu. Sasa nadhani Serikali ije na tamko sasa ili suala la kimkataba kati ya mwekezaji, mbia na *NDC* lijulikane litaisha lini? Kwa sababu imeshakuwa ni muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika hii Miradi ya Liganga na Mchuchuma kuna watu ambao wamepisha yale

maeneo ili hii miradi ifanyike. Imeshakuwa ni muda mrefu sana hawa watu hawajalipwa fidia na bado wamekuwa wakiendelea kuilalamikia Serikali yao. Nakumbuka tuliishauri Serikali kwamba ikiwezekana hii hela ya fidia ilipe Serikali, halafu Serikali itashauriana na mwekezaji namna bora, lakini wakati huo wananchi wetu watakuwa wameshalipwa ile fidia yao na wanaendelea na shughuli nyingine. Kwa hiyo, imeshafika mahali wananchi wamepisha maeneo, lakini mpaka leo wanashindwa kuyatumia yale maeneo kwa sababu hawajui hatima ya miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizingumzie suala la biashara. Mpaka leo hii nashindwa kujua kama tunazo *data base* sahihi za wafanyabiashara wetu hapa nchini kwa sababu biashara inayofanyika ni kubwa na asilimia 95 ni wafanyabiashara wadogo. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu hili tulishawahi kulishauri huko nyuma, kwamba ifike mahali lazima wafahamike wafanyabiashara wote kwa majina na ndio sababu ya kuwepo kule Maafisa Biashara kwenye Halmashauri, kwenye manispaa na kwenye Majiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani imeshafika wakati sasa tuwe na *data* na hapo tutaweza kuwa tumetengeneza *tax base* nzuri ya kuendeleza uchumi wetu kwa sababu wafanyabiashara wadogo ndio wengi zaidi kuliko wafanyabiashara wengine wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kwenye hili eneo la Mchuchuma na Liganga, *NDC* imechukua eneo kubwa sana la wananchi. Ifike mahali sasa *NDC* itoe yale maeneo kwa wananchi kwa ajili ya uwekezaji kwa ajili ya uchimbaji. Mfano kule kwenye makaa ya mawe, Mchuchuma, tuna eneo kubwa, lakini kimsingi halifanyiwi kazi kama ambavyo linafanyiwa kazi lile eneo la Ngaka kule Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ifike mahali sasa wananchi wafikiriwe na wana uwezo wa kufanya hiyo kazi na ninaamini kupitia mabenki na kupitia taasisi zinazotoa fedha wanaweza kujishughulisha wakafanya biashara

wakapata faida na wakalipa kodi kwenye nchi. Kwa hiyo, ifike mahali tuwafikirie hawa watu kwa sababu lile eneo limekaa na *NDC* ni kama imeshindwa na ndiyo maana sasa inafika mahali kwamba tumezalisha mapori mengi ya bila sababu yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishie hapo. Nashukuru na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Riziki Saidi Lulida, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke na Mheshimiwa Sixtus Raphael Mapunda ajiandae.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru na nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia na kutujalia wote tukiwa hapa tukiwa salama. Naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na nina sababu za msingi za kuiunga mkono hoja hii iliyokuwepo mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ninapozungumza mradi wa *LNG* ambao tumeupigania kwa muda mrefu zimeshatolewa pesa shilingi bilioni 5,200 kulipa fidia ya wananchi wa Manispaa ya Lindi ili kupisha Mradi wa *LNG* ambao utasaidia maendeleo na ukuaji wa viwanda Tanzania na Mkoa wa Lindi utaweza kunufaika kiuchumi. Leo Lindi tulikuwa tunapigania kwa muda mrefu tuwe na viwanda kwa vile Lindi ni Mkoa mmojawapo ambao haukuwa na viwanda. Sasa mpaka leo tunavyosikia tayari pesa zimeshakwenda kule wananchi wa Lindi watajaa matumaini na nchi yao na Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Waziri na wengine wote wanaohusika na kuhakikisha mradi huu wanalipwa watu fidia. Namshukuru Mheshimiwa Rais mwenyewe kwa vile aliona ni wakati muafaka watu wa Lindi nao wale matunda ya maendeleo ya viwanda na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiunga tena mkono hoja, kwanza Mheshimiwa Waziri Bashungwa nilimpigia simu

nikamwambia tuna kiwanda Mchinga kinasumbuliwa na watu wa *TANESCO* na watu wa *TRA* na baadhi ya watu wa Wizara yake; alifuatilia kwa makini, sikutegemea kama kijana huyu yuko ana busara kubwa sana. Hivyo, Mheshimiwa Rais hakufanya makosa kumchagua Mheshimiwa Bashungwa kuwa Waziri wa Biashara na Viwanda. Mimi niko Bungeni kwa muda mrefu; watu wanaochapa kazi kama akina Mheshimiwa Bashungwa hawa na wasikivu ni lazima tuwapongeze ili tuwatie moyo na tuwatie nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Watanzania wote na tuwarehemu na kuwaombea maombi mengi wale ambao wamepata misiba kipindi hiki kwa ajili ya corona na inawezekana kuna wengine, lakini wengine katika vifo vya kawaida. Tumwombe kwa Mwenyezi Mungu Rais, anatumia Watanzania tunaondokana na hofu, tuwe na Mwenyezi Mungu akitusimamia. Tukisema sisi tunapata hofu kwa kutegemea propaganda za nchi za ki-*western* haitatusaidia kabisa, wao hawana machungu na sisi, wao wanahangaika na kuhakikisha watugawanye ili waweze ku-*penetrate* wapate faida na nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, janga la *Corona* ni biashara, *Corona* ni siasa. Sasa wao katika biashara zao wanataka kuuza dawa, ni lazima watugawe. Wao katika biashara zao wanatafuta wanasiasa wenye kutumia siasa za majitaka watugawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema kwanza Bunge lako limetulia, Bunge lako limekuwa zuri, Bunge lako limekuwa Bunge la watu wanaotoa hoja wakiwa wametulia, hakuna papara wala vuruguvurugu wala kukemeana. Nilitegemea kama kutakuwa na kanuni, wale walioondoka wasirudi tena mpaka Bunge tumemaliza. Wanatufanya sisi tufanye kazi kwa hofu, kutaka kugombana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge siyo eneo la kutukanana na kufanya vitu vya ajabu ajabu. Bunge lina heshima, Bunge linataka ulete hoja na upinge kwa hoja siyo



kwa kukaa leo tokeni nje; wananchi wanategemea uje uwasimamie bajeti zao; umekaa nje. Una faida gani katika Bunge hili? Wasirudi tena, wakae huko huko maana wanaweza wakaja humu ndani wakatingizia matatizo zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, muda mrefu nilizungumzia suala la viwanda, lakini viwanda tulivyokuwanavyo ambavyo sasa hivi mwelekeo wake ni kurudishwa Serikalini na kufanya kazi. Tuliletewa utapeli wa kusema tubinafsishe, wakabinafsisha na wale waliochukua vile viwanda wakakaa navyo. Sasa hivi ni wakati muafaka. *Corona* imekuja kutuonesha kama kweli azma ya Mheshimiwa Rais ya kusimamia viwanda ni azma ya kimakini sana. Leo tunahitaji viwanda vyetu vya sukari vifanye kazi, lakini kama leo viwanda vile viko kwa wawekezaji ambao hawakutaka kutufanyia kazi yetu vizuri, kuna faida gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumuunge mkono Mheshimiwa Rais kwani viwanda vyote vilivyofungwa, nitataja kwa majina; viwanda vya korosho vyote Mheshimiwa Rais visimamie korosho zibanguliwe ndani, sisi wenyewe ndani tule. Viwanda vya nguo vifanye kazi maana leo unashindwa kwenda China kuchukua nguo, lakini tulikuwa na nguo zetu Tanzania; kulikuwa na viwanda vya *Gossage*, viwanda vya Urafiki, viwanda vya *Mwatex* ambavyo vilikuwa vinafanya kazi kuhakikisha Watanzania tunajitegemea sisi wenyewe. Wakatuletea machafuzi ya kibiashara tukavifunga tukasema tuna wawekezaji, kumbe tumewekeza watusimamishe tusiende mbele katika maendeleo ya viwanda, wao watuletee makanga mabovu, manguo mabovu, kumbe wenyewe Tanzania tunajiweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema tena kuwaambia Watanzania, Tanzania yenye viwanda na maendeleo ya viwanda inawezekana na twende tupige kazi, twende mbele na tusingine wanaotaka kutia hofu watajihofu wao wenyewe. Wisi Watanzania tumefunguka, tunahitaji maendeleo ya kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe ushauri. Tunakwenda katika uchaguzi, hizi pesa nyingi ambazo zilitaka kwenda katika uchaguzi zipunguzwe nusu ya pesa ziende katika maendeleo ya kutibu janga kubwa la *Corona*, lakini vilevile zisaidie maendeleo ya wananchi. Hizi chaguzi ziende katika pesa ndogo sana ambayo itatufanya sisi Watanzania na watu wetu ambao wametutuma kuja hapa tuwatumikie na tuwafanyie kazi iliyokuwa nyepesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi nina imani uchumi utayumba, lakini Mwenyezi Mungu anajua nini anachokifanya na ndiyo maana mpaka leo Afrika ni nchi ya kimasikini, watu wetu masikini, lakini ametuona kama tuko kwake, tunapiga magoti kwake kumwomba Mwenyezi Mungu alete nusura juu ya hii *Corona*. Mwenyezi Mungu ametuonesha kama hakuna bosi katika *Corona*. Leo utasema aah, Watanzania hatujifungii ndani, Uingereza, Waziri Mkuu wa Uingereza amepata *Corona* anatomia ma-*hygiene* ya kila aina, mbona amekaa ndani? Kwa nini amekaa ndani? *Corona* haichagui mtu. Leo wendawazimu wanakaa katika vichaka humo hawana usafi wowote, lakini Mwenyezi Mungu anawalinda. Nasi tuombe Mwenyezi Mungu kila mtu alipokaa afunge macho amwombe Mwenyezi Mungu atuepushe na *Corona*.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna viwanda vya korosho vimefungwa; vifunguliwe. Kuna viwanda vya nguo, vifunguliwe. Leo hatutaki tena kuagizia mafuta nje, tuna viwanda vyetu ambavyo tulikuwa tunatumia mafuta ya ndani; mafuta ya *Super Ghee* ambayo yalikuwa mazuri, mafuta ya *Pride* ambayo yalikuwa mazuri, tulikuwa tunatumia *Tanbond* ya Tanzania, tunaomba Mwenyezi Mungu avijalie viwanda hivi vyote vifunguliwe Watanzania wapate ajira na tupeleke kwa wenzetu na tusitegemee tena kuwa na utegemezi kupata vitu kutoka nje, havina maana yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ya Tanzania watanyweshwa Watanzania, vyakula vya Tanzania vitawalisha Watanzania ili tufanikiwe tumuunge mkono Rais

Mheshimiwa Dkt. John Joseph Magufuli aweze kufanya kazi kwa bidii. Nilikuwa naye humu ndani Bungeni, bajeti yake ilikuwa haisumbuliwi kwa vile Mheshimiwa Rais ana uwezo mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tusidanganyane kusema kutatokea hivi. Hawa waliokaa nje na wasikanyage humu ndani, wakae huko huko nje tufanye kazi. Bunge letu lifanye kazi kwa heshima na taadhima.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja na ninasema ahsanteni sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, nadhani atakuwa yuko Msekwa. Atafuatiwa na Mheshimiwa Sixtus Raphael Mapunda na Mheshimiwa Wilfred Muganyizi Lwakatare, ajiandae.

Mheshimiwa Sixtus Raphael Mapunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Lwakatare na Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve ajiandae.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nichangie kwenye hii bajeti ya viwanda na biashara. Awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Waziri wa Viwanda na Biashara, kaka yangu Mheshimiwa Innocent Bashungwa na Naibu Waziri dada yangu Mheshimiwa *Eng.* Stella Manyanya na wasaidizi wenu wote katika Wizara. Kwa kweli, katika kipindi hiki cha muda mfupi tunaona kabisa kuna maendeleo makubwa yenye mwelekeo chanya wa kukuza viwanda ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye bajeti hii naomba nichangie mambo makubwa mawili; viwanda ndiyo moyo wa uchumi wa nchi, viwanda ndiyo kitu pekee kinachoweza kutuhakikishia kuna ajira zinazoeleweka. Kwa muda mrefu sana tumeongelea kuhusu kukuza Sekta ya Viwanda, lakini tulikuwa tunashindwa kupata *road map* na kufungamanisha Sekta ya Elimu, Sekta ya Ufundi na Sekta ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nakuta kwenye mpango wenu mmefanya kitu kikubwa sana. Mmekuja na mpango jumuiifu kati ya *SIDO*, *VETA*, *Azania Bank* na *NSSF* ili kwenda kuwasaidia wale waliotoka *VETA* wapate vitendea kazi kutoka *SIDO* na wakitoka pale wasiishie hapo tu, wapewe na mtaji kwa ajili ya kufanyia hiyo kazi. Hili ni jambo kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi ukaongea mambo ya viwanda, hujagusa elimu. Huwezi ukaongelea suala la elimu ya viwanda bila kugusa mtaji, huyu mtu atapata mashine wapi? sasa kuiweka *SIDO* pale, kumweka *funder* pale ukaweka *NSSF*, na *Azania Bank* na kuweka pale eneo la *VETA* kama sehemu ya elimu, unatengeneza mfumo jumuiifu ambao una uhakika kabisa natoa elimu ya aina fulani kwa mtu fulani ili nipate matokeo ya aina fulani. Hili mimi nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe jambo moja, *VETA* haijagusa kila wilaya, ili twende kwa *speed* zaidi, tuhakikishe *VETA* ifike kila wilaya na hiyo *chain* watakapoitengeneza, tupate ile *vibe* yake kutoka kila wilaya, tupande mpaka *level* ya Mikoa na Kitaifa tuone viwanda vinakua ndani ya muda mfupi. Tutakuwa na uhakika wa ajira na kila kitu ndani ya nchi yetu kitaenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili naomba niseme kuhusu makaa ya mawe ya Mchuchuma na Liganga. Kwa muda wa miaka hiyo miwili mfululizo, 2018/2019 nilikuwa sambamba sana na kaka yangu Deo Ngalawa, tulikuwa tunasikitika sana kwa nini Mchuchuma na Liganga haiendi kwa *speed*? Leo nimefurahi kupata ripoti ambayo naona sasa Serikali kuchelewa sijui waliongozwa na Mungu, lakini wamefanya jambo zuri sana. Imekuja kugundulika, mkataba ule ambao ilibidi tuchimbe kina, ndani yake kuna madini zaidi ya moja, kuna *magnet iron wire*, *vanadium* na *titanium*. Sasa hivi vitu vyote ukiingia kwenye mkataba mmoja tu wa chuma, sisi kama nchi tunaumizwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, mwaka juzi tumepitisha hapa sheria. Sheria Na. 5 ya Mamlaka ya Nchi ya Uangalizi wa Utajiri wa Asili na Sheria Na. 6 ya Mamlaka ya Nchi Juu ya Majadiliano ya Mikataba Yenye Masharti Hasi ya Mwaka 2017. Sisi tutakuwa watu wa ajabu sana, tumeumia sana kwenye migodi kwa sheria zilizopita, tuna mkataba ambao haujaanza na una changamoto nyingi. Tumepitisha sheria nzuri ya kutusaidia, lakini hatujaifungamanisha yale mambo mazuri kwenye mkataba. Nadhani kwa mara ya kwanza nitatofautiana kidogo na Ngalawa, tuipe Serikali muda ipitie ule mkataba, ifungamanishe zile sheria mbili na hicho tunachokihitaji ili nchi isiendeleo kuibiwa tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki kwa sababu kuna vitu vingine lazima vifanyike, niombe Serikali kwenye suala la miundombinu ya barabara, reli na umeme wa uhakika kufika kule pamoja na fidia, hivi vyote vifanyike kwa haraka ili teknolojia hiyo mpya ya uchenjuaji itakapokuja kugundulika, tuwe tayari tumeshapiga hatua hizi nyingine za miundombinu na mradi usichelewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ngoja niseme kidogo kwenye *Covid -19*. *Great leaders* wanapatikana kipindi kile ambacho watu wamekata tamaa na dunia nzima hawajui kwa kwenda. Sasa kiongozi unaisoma nchi yako, unawasoma watu wako halafu unakuja na njia ambayo haijaandikwa popote ila wewe kwa maono na uwezo wako unakuja na kitu ambacho kinakuwa *modal* dunia nzima. Rais wetu alipokuja na *agenda* ya kusema hata-*lockdown*, dunia nzima ilimshangaa. Ildhani Tanzania imepotea na kiongozi wao amepotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii Marekani wanafikiria kuondoka na *lockdown*, miezi mitatu baadaye. Rais wa Tanzania kaona miezi mitatu iliyopita. Nchi tajiri kama Marekani, wanakuja kuona leo. *South Africa*, wamepiga *lockdown* watu wametoka njiani wanatembea barabarani kwa ajili ya kutafuta chakula, nao wanafikiria kuondokana na *lockdown*. Sweden hawajafanya *lockdown* kama sisi. Ukiangalia kwa hesabu, aliyefanya *lockdown* ana wagonjwa

22,000, wewe ambaye haujafanya *lockdown* mpaka leo una 480. Kenya aliyeweka *lockdown* mpaka leo ana 490, namba hazidanganyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhalisia wa mkakati ambao Rais wetu ametuongoza kwenye kukabiliana na *Covid – 19* la kutoku-*lockdown* limeleta manufaa makubwa kwa nchi yetu kuliko kama tungefanya vile. Sasa tunafanya nini kutoka hapa? Kama Watanzania inabidi sasa tutumie hii fursa ya sisi kwenda mbele kwa sababu wenzetu wali-*lockdown*, sisi tuendeleo kuvuna mahindi, kuvuna viazi. Baada ya miezi mitatu, hawa watu watahitaji chakula kutoka kwetu, hapo ndipo Taifa la Tanzania litakuwa lipo mbali kiuchumi, litakuwa na soko la kueleweka, litakuwa na mahitaji, ndiyo hatutapata anguko la uchumi kama nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maneno haya machache, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Wilfred Muganyizi Lwakatare, atafuatiwa na Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve na Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu ajiandae.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikuchukuru kwa kunipa nafasi na kwa bahati nzuri nachangia mara ya pili tangu tumeanza *session* hii. Nilipopata nafasi wakati wa TAMISEMI kwa dakika tano, miongoni mwa mambo niliyozungumzia ni kuwashukuru wananchi wa Bukoba na viongozi wa *phases* mbalimbali ambazo zimepita nikiwa Mbunge kuanzia mwaka 2,000 na nikatangaza kwamba sitarajii, nimeshafanya maamuzi ya kutogombea tena katika Awamu hii inayokuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nipende kuwashukuru wafanyabiashara wa Jimbo la Bukoba Mjini kwa kipindi cha uongozi wangu wamekuwa nguzo kubwa sana ya kuweza kunishauri na kupanga nao mipango mbalimbali na pia kuwakilisha hoja zao mbalimbali ambazo kimsingi zilikuwa zinalenga katika kuboresha biashara zao.

Nitakuwa siwatendei haki kama katika kikao changu cha mwisho, sitazungumzia hoja ambazo kimsingi walinituma niziwakilishe ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza hivyo kwa sababu Jimbo la Bukoba Mjini ni jimbo ambalo asilimia 70 ni watu wanaotafuta riziki zao kwa kufanya biashara, iwe biashara ndogo ndogo, ya kati au biashara kubwa. Ndiyo watu ambao wanajumuisha idadi kubwa ya watu wanaoishi ndani ya bukoba Mjini. Kuna Wabunge wenzangu huwa nawaeleza wakati yanapozungumziwa mambo ya stakabadhi ghalani ndani ya mjengo, huwa wakati mwingine natoka nje kidogo kufanya *consultation* ya mambo mengine. Nazungumza hivyo kwa sababu *interest* ya watu wangu wa ndani ya Bukoba Mjini, idadi kubwa ni pale wanapotetewa kutokana na mwenendo wa shughuli zinazowaingizia pato kwa ajili ya kuangalia familia zao lakini pia kukidhi mahitaji yao mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Jimbo langu la Bukoba Mjini wao wamekuwa wanategemea mambo mbalimbali ambayo yanaamuliwa kwa misingi aidha ya kuboresha biashara au namna ya uendeshaji biashara au namna ya muunganiko au *networking* zao za kibiashara. Tunafahamu kabisa Mkoa wa Kagera kijiografia ni mkoa ambao umepakana na nchi zaidi ya nne lakini pia kuna nchi nyingine ambazo hatupakani lakini tunaungana nao kwa sababu ya ukaribu na kwa namna nyingine jiografia ya kuzihudumia nchi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninapooonea wakati hata Waziri wa Biashara, mdogo wangu Mheshimiwa Bashungwa anatoka katika mkoa huu, anafahamu fika adha za wafanyabiashara wa mkoa wetu. Sisi kwa kupakana na Uganda, ukivuka katika eneo la Mutukula kwenda upande wa Uganda ni kwamba biashara unakuta mizania hailingani. Unakuta *policy* ambazo wenzetu wa Uganda wanakwenda nazo na zinazotawala, zinazosimamia biashara zao, zinakuwa *favorable* kwa upande wa wafanyabiashara wa Uganda kuliko upande wa kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo pale Wizara hii na Serikali kwa ujumla na vyombo vyake, inapokuwa inapanga masuala ya kibiashara ambayo yanaweza kuweka hali ya ushindani ikawa sawa kati ya upande na upande, wazingatie mambo hayo kwamba tunapakana na nchi ambazo sisi pia tunapaswa kushindana nazo kibiashara. Ndiyo maana unaweza ukakuta ndani ya Mji wa Bukoba, wafanyabiashara wanaona bora pamoja na kodi zote kuagiza maji ya kunywa kutoka Uganda yaje yashindane na maji ya Kilimanjaro. Ndiyo maana leo hii ninapozungumza ni kwamba wavuvi wote ambao kimsingi walikuwa ni sehemu muhimu ya watu wanaozungusha fedha nyingi ndani ya mkoa wetu, sasa hivi wavuvi wamehamia upande wa Uganda kwa sababu sheria na kanuni zinazosimamia uvuvi upande wa Uganda ziko *favorable*. Matokeo yake sasa ni kwamba mzunguko wa hela ndani ya Mji wa Bukoba umekuwa *null*, lakini pia hii Sekta ya Uvuvi ilikuwainatoa idadi kubwa ya ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukishawahamisha wafanyabiashara wakubwa wa Bukoba wakaenda Uganda na tunatambua kabisa samaki wenyewe hawajui mipaka ya maji, Ziwa la Victoria ndiyo hilo hilo. Kwa hiyo mvuvi anapokwenda kuvua upande wa pili wa Uganda na akakuta mazingira ni mazuri kwa upande wa Uganda anaendelea kufanya shughuli kule. Hiyo ni kwa upande wa uvuvi nimetoa mfano huo, lakini hii ni pamoja na biashara mbalimbali ambazo zinafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizungumzie suala la njia za usafirishaji. Niipongeze Serikali kwa taarifa ambazo nimepewa na Naibu Waziri ndani ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwamba meli yetu ya Victoria ambayo ni meli ilianza tangu wakati wa mkoloni na mtu yeyote wa Kagera, Mhaya yeyote hata babu wa babu ukianza kumuuliza atakwambia suala la historia ya meli ya Victoria. Nashukuru kwamba hii meli kwa picha tulizoziona mtandaoni inakaribia kumalizika. Naibu Waziri aliniambia hii shughuli ya kuzindua ingekuwa tayari kama isingekuwa suala la *corona*.



Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali iweke utaratibu wa namna gani pamoja na janga la *corona* basi hii meli izinduliwe ili iweze kuwasaidia wananchi wetu wa Mkoa wa Kagera. Meli hii ni maisha kwa wananchi wa Kagera, kuanzia ajira lakini pia biashara, kwa sababu kusafirisha mizigo kwa njia ya meli, bidhaa zinakuwa bei nafuu kuliko kusafirisha kwa njia ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni kwamba tayari sio suala tena la kujadili, uwanja wa Chato umeshajengwa na upo. Naomba sasa kupitia Wizara hii hebu tujipange ki-*strategy* kwamba huu uwanja unaweza ukatumikaje kwa manufaa ya Mkoa wa Kagera na mikoa iliyo karibu ili angalau uanze kutumika kwa *cargo planes* za kuweza kutoa bidhaa katika Mkoa wetu wa Kagera. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ulitaka kumpa Taarifa, labda sasa litakuwa ni jambo la ufafanuzi, sio taarifa tena kwa sababu ameshamaliza kuchangia. Mheshimiwa Waziri Kamwelwe.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nilitaka tu kuongeza maneno kwamba meli ya *MV Victoria* imekamilika. Tulikuwa na changamoto ya wataalam wale sita kuja kuifanyia *ramming* lakini leo namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu ameruhusiwa tunabadilisha *notum* kwenye usafiri wa ndege ambao sasa tutaanza kupokea ndege maalum, kwa hiyo inawezekana na hawa watu sita tukafanya utaratibu wakaja ili kuja kui-*test* ile meli na ianze kufanya kazi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa ufafanuzi huo. Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt, Dalaly Peter Kafumu na Mheshimiwa Zainab Mndolwa ajiandae.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa

mchango wangu kwenye Wizara muhimu sana hii Wizara ya Viwanda na Biashara. Awali ya yote naomba nitoe pongezi zangu za dhati kwa Serikali yetu hasa kwa Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutupa moyo pale ambapo tumeonekana tunakata tamaa, amekuwa akitupa moyo na kuendelea kuliongoza Taifa hili ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili nichukue fursa hii nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara pamoja na watendaji wake wa Wizara. Tumemwona akipambana kuhakikisha anaweka mahitaji hasa yale mahitaji ya muhimu kwa kipindi hiki kigumu kuhakikisha Watanzania wanapata mahitaji haya kwa urahisi na kwa bei nafuu. Kwa hili nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, kama nilivyosema kama Taifa sasa hivi tunapitia kipindi kigumu sana, mimi nimpe moyo. Historia inaonesha hata baadhi ya Mataifa makubwa sasa hivi, wengi walipitia vipindi vigumu kama hivi. Wakatumia vipindi hivi kuhakikisha wanajipanga vizuri, wakaweka mikakati yao mizuri na wakaweza kupiga hatua kubwa. Nasi basi tujue tatizo hili lipo hapa nchini, *how long* itatuchukua kujikwamua hapa tulipo, bado hatujajua, lakini ni imani yangu Mungu atatusaidia tutaweza kuvuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu sasa kwa Serikali kupitia kwa Wizara hii muhimu, Wizara ya Viwanda na Biashara, nadhani ni wakati muafaka wa kuhakikisha tunajipanga vizuri tukatengeneza mkakati, tuseme kama *blue print* ambayo itatusaidia kwa kipindi hiki cha mpito ambacho kiwe kimejaa mapendekezo na mabadiliko ya kisheria ambayo yataendana na nyakati hizi ambazo tunazipitia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulijipanga kama Taifa kuhakikisha tunafikia uchumi wa kati ambao utaongozwa na viwanda na biashara. Kama nilivyosema, huu mwongozo utatusaidia kuhakikisha viwanda vyetu na biashara za hapa nchini zinaendelea ku-*survive regardless* ya changamoto ambazo tunapitia na pia tuweke mikakati ambayo zile

biashara na viwanda ambavyo vitashindwa ku-*survive* kwa kipindi hiki tutafanyaje kuhakikisha tunazikwamua ili tuendelee kusonga mbele kama Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri nimeona mkakati mzuri ambao ameweka kuhakikisha tutatumia hizi Balozi zetu. Najua wakati changamoto ya ugonjwa huu ikitokea Ubalozu wetu wa China ulifanya kazi nzuri sana kupitia Serikali yetu kujulisha hali ya maambukizi na hali inavyokwenda, kwa hiyo kwa dhana hiyo hiyo, nadhani utaratibu wa kuhakikisha tunatumia Balozi zetu wao wahakikishe wanapata taarifa ikiwemo hizi Balozi zetu za China, Congo, Uganda na Rwanda ambao wanatumia sana bidhaa zetu kutoka hapa Tanzania tujue tunajipange wakati milango inafunguka, basi tuweze ku-*take advantage* ya soko wannachi wetu wapate kipato basi na sisi tuweze kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la zaidi niendeleo kusisitiza kuhakikisha tunaweka mazingira rafiki kwenye viwanda vyetu. Tunajua mataifa mengine sasa hivi wako kwenye *lockdown*, uzalishaji umepungua na sisi tumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea na msimamo wake kuhakikisha sisi kama Taifa tunaendelea kuzalisha bidhaa mbalimbali hapa nchini. Sasa naomba vile viwanda ambavyo vinazalisha hizi *consumable goods*, tuzipe *incentive*, huu ni wakati wa kuzalisha ili mipaka itakavyofunguka kwa mfano badala ya kusafirisha mahindi tutasafirisha sasa unga ambao tayari umeshakwishaandaliwa. Badala ya kusafirisha mchele hasa Rwanda wanachukua mpunga kutoka Tanzania, tuisafirishe mpunga, tuhakikishe sasa tunasafirisha mchele ambao tayari umeshatayarishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe maoni yangu kidogo juu ya hili janga la *corona*. Naomba niseme kuwa hakuna Serikali duniani, hakuna rais yeyote katika dunia hii ambaye ana majibu sahihi juu ya janga hili. Hakuna Waziri yeyote wa Afya mwenye *manual* ambayo inamwongoza ni jinsi gani tutamaliza janga hili kwa haraka na bila madhara

yoyote. Maamuzi ambayo yanachukuliwa na Serikali na Rais wetu, *they are just doing the best they can* kwa *information* walizonazo na *resources* ambazo tunazo kama Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi wamekuwa wanalalamika kwamba Serikali yetu imefanya maamuzi mabaya au hawajachukua njia stahiki kuhakikisha tunapambana na janga hili. Naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla kwamba wakati janga hili limetokea kule China kuna video nyingi zilirushwa zikionesha vijana wetu wanalia, wanaomba kurudishwa nchini. Serikali ikafanya maamuzi yake kuhakikisha inawalinda wale vijana wetu na kupitia Ubalozi wetu, Mheshimiwa Kairuki alifanya kazi kubwa kutupa *update* njia gani zinatumika na shughuli mbalimbali ambazo zimewasaidia vijana wetu wakawa salama mpaka sasa hivi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi huku nyumbani tukawa na *opinion on both sides including me*, wengine walitaka wale vijana warudishwe hapa nyumbani, wengine wakafanya dhihaki mpaka kusema *what's a point* ya kuwa na ndege kama tunashindwa kwenda kuchukua vijana wale lakini Serikali ikawa na msimamo wake, wale vijana wetu mpaka leo wapo salama. Sasa kwa dhana hiyohiyo Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kama nilivyosema maamuzi ambayo yanachukuliwa na Serikali sasa hivi ni kutokana na *information* na *resources* ambazo tunazo kuhakikisha tunawalinda Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni *pause a question* hapa, sisi ni Wabunge tunalipwa mishahara mizuri na posho, hivi ni Mbunge gani ambaye sasa hivi anaweza akasaidia familia au ukoo wake uwekwe ndani asiende kazini na tuweze ku-*supply* hivyo vitu vyote ambavyo wanahitaji ili waweze ku-*survive*, *none of them*. Sasa ni nani anafikiri sasa hivi Mheshimiwa Rais ataweza kusaidia watu zaidi ya milioni 60, *it's impossible*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Watanzania tuendeleo kumpa moyo Mheshimiwa Rais, tuendeleo kufanya kazi kwa bidii. Kama nilivyosema janga lipo, tuendeleo kujidhatiti kwa msaada wa Mungu na hili litapita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dakika moja, kwa sababu ni Bunge langu la mwisho, naomba nitumie fursa hii niwashukuru sana wananchi wote wa Mkoa wa Iringa hususan wanawake ambao walinipa dhamana ya mimi kuja kuwatumikia hapa Bungeni. Najua tunapitia kipindi kigumu, najua pamoja tutafika; niliapa kuwatumikia wakati wa raha na shida, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve.

Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu atafuatiwa na Mheshimiwa Zainab Mndolwa, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu ajjandae.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja hii. Kwanza nianze kwa kusema naiunga hoja hii asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze mdogo wangu, niseme mjomba wangu kwa kazi nzuri ambayo anaifanya. Mheshimiwa Waziri hongera sana, umefanya kazi nzuri sana. Kwa niaba ya wananchi wa Igunga nikupongeze sana kwa kazi ambayo umeifanya ya kutafuta soko la choroko kwa wakulima wa Igunga. Wewe na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo mmejithahidi sana wananchi wanafurahi kwa sababu mmeanzisha mnada ambao wananchi sasa wanapata soko kwa ajili ya choroko yao. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mdogo wangu uendeleo kutafuta tena soko la mpunga. Sisi tunalima sana mpunga kule Igunga, tunahitaji kupata soko la mchele, zamani tulikuwa na soko kule Uganda Mheshimiwa Kingu

alikuwa DC wetu alitutafutia soko kule Uganda sasa hivi hatuna uwezo huo. Tunaomba basi Mheshimiwa Waziri kama umeweza choroko tunaomba basi na mpunga tuweze kupata soko tuuze nchi za jirani ili wananchi wetu waweze kujikimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili nataka niseme kidogo kuhusu miradi mikubwa ambayo imechelewa sana na ipo chini ya NDC, mradi wa Mchuchuma na Liganga. Naona Wabunge wengi wamesema pamoja na kutofautiana lakini suala la mradi huu limechelewa sana. Vilevile kuna mradi wa *General Tyre* wa Arusha pia naona kama haumo tena kwenye maelezo ya Serikali. Pia kuna mradi wa Magadi Soda kule Engaruka. Hii miradi yote ilikuwa chini ya NDC ikisimamiwa na Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii ni ya kielelezo na inaweza kuchochea wanda vya ndani (viwanda mama). Ukiwa na chuma ni rahisi sana kutengeneza viwanda vyako vingine, ukiwa na magadi soda viwanda vingi vya kemikali na madawa vitaenda kuendelea. Pia *General Tyre*, tuna magari mengi kweli Tanzania, tunaweza kuwa ni soko kubwa lakini miradi hii imechelewa na imeshindikana. Tangu mimi nikiwa Mwenyekiti wa Kamati hii ya Viwanda na Biashara mwaka 2015 miradi hii ilikuwa mikubwa kweli na tulitegemea baada ya miaka mitano iwe imeshakuwa tayari lakini mpaka tumefika imeshindikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niishauri Serikali hatua zinazochukuliwa sasa hebu ziharakishwe kidogo. Kwa kweli miradi hii inaweza ikatutoa, ikatufikisha kwenye uchumi wa kati. Hatujachelewa, miaka mitano imepita lakini bado tuna miaka mitano tena mingine ya Mheshimiwa Rais wetu hebu tuchangamke. Bwana mdogo najua unaweza ukaendelea safari ijayo, ukiendelea basi naomba hii miradi uichukulie kwa ukubwa wake kabisakabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba tumekuwa na matatizo makubwa sana ya kuhamasisha uwekezaji katika nchi yetu na mpaka tulifika

mahali tukaandika *blueprint*, kile kitabu maalum kinachoeleza jinsi gani tunaweza tukahamasisha uwekezaji na kuwasaidia wafanyabisahara katika nchi yetu na uchumi wetu ukakua. Bahati mbaya sana *blueprint* inatekelezwa taratibu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Kilimo hebu itekelezeni hii *blueprint* itatusaidia sana kwa sababu imeeleza mambo yote vizuri. Bado sasa hivi wafanyabiashara wetu wengi wanaonekana kama wezi na wanyang'anyi. Napenda kutumia neno hili kwa sababu wanaonekana kwamba hawapokelewi vizuri, hata wafanyabiashara wadogo ukienda kule Igunga TRA inawasumbua sana, inawafungia maduka yao. Sasa mazingira ya kufanya biashara yakiwa mabaya, watu wengi watafunga biashara na kweli wengi wamefunga na wamekimbia katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri hebu kafungue hicho kitabu cha *blueprint*, mimi huwa nakisoma sana. Mheshimiwa Mzee Mwijage mnyonge mnyongeni haki yake mpeni, alitengeneza jambo kubwa sana hili, ukitumia hiyo kama *guideline* yako Mheshimiwa Waziri utafanikiwa sana. Nakuombea sana urudi kuwa Mbunge na uendelee na Wizara hiyo ili uweze kutufikisha mahali ambapo tunatakiwa kufika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, niwaombe basi Watanzania na hasa wana Igunga kule tuendeleo kujikinga na janga la *Corona*. Tunawe mikono kwa maji na sabuni, tutumie *sanitizer* lakini tuwe na *social distance*. Tujipake *sanitizer* sana, kila ukitoka na ukirudi unajipaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana nimalizie kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake hasa juu ya jambo hili la *Corona*. Tumuunge mkono kwa sababu ni jambo ambalo kila mtu hajui tunaelekea wapi, kwa hiyo, anatupa uongozi. Kama alivyosema dada/mtoto wangu Rose hapa kila mtu ana maongozi yake kulingana na

Mwenyezi Mungu alivyompa, Rais wetu anajitahidi sana tumuunge mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishukuru sana na naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Dkt. Kafumu.

Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Zainab Mndolwa atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Mheshimiwa Kanali Mst. Masoud Ali Khamis ajiandae.

**MHE. ZAINAB M. AMIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Viwanda na Biashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema siku ya leo na kuweza kusimama katika Bunge hili Tukufu ili kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapa pole ndugu zetu wote waliopoteza ndugu zao (wamefiwa) kutokana na *Corona* na maradhi mengine. Nawaombea kwa Mwenyezi wawe na moyo wa subira na kifo kinapangwa na Mungu na kila kifo kina sababu. Kwa hiyo, naomba wawe wastahamilivu katika kipindi hiki, isipokuwa tuwaombe kwa Mungu azipumzishe roho zao mahali pema peponi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana hapa nilichangia katika bajeti hii kuhusu wafanyabiashara kulipa kodi kabla ya kuanza biashara zao; kwamba walikuwa wanalipa kodi kabla ya kuanza biashara. Katika mchango wangu ule, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa ufafanuzi baadaye na kutoa maelekezo kwamba watu wapewe *grace period at least* ya miezi sita ili wafanye biashara kisha waweze kukadiriwa, nashukuru kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dar es Salaam ni kitovu cha biashara katika nchi yetu hii na ndiyo maana Mheshimiwa



Rais wetu ameona kuwa kuna umuhimu wa kuendelea na shughuli zetu za kawaida. Katika pato la Taifa Dar es Salaam ina mchango mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Dar es Salaam sasa hivi biashara zimedorora, hakuna mzunguko wa fedha, soko au wateja wakubwa ni kutoka nchi za nje na mikoa ya jirani. Walkuwa wanapata wateja kutoka Congo, Zambia, Malawi na pia Visiwa vya Comoro na ndugu zetu wa Zanzibar na mikoa ya Tanzania Bara. Ieleweke kuwa wafanyabiashara hao walipewa makadirio ya kulipa kodi, mwezi wa tatu wanatakiwa walipe kodi, wa sita, wa tisa na pia wa kumi na mbili lakini kutokana na janga hili la *Corona* naomba Wizara ya Fedha na Wizara ya Viwanda ikae kwa pamoja ione haja sasa ya kuwasaidia wafanyabiashara wetu hawa kwa sababu itakapofika mwisho wa mwaka endapo hawatalipa kodi hizo ambazo walishakadiriwa, watapewa *fine* na masuala ya *Corona* itakuwa baadaye mpaka uandike barua. Kwa hiyo, naomba kwa hili Serikali ilichukue na ione haja ya kuwasaidia wafanyabiashara wetu hawa. Ni kwa Dar es Salaam na pia kwa Tanzania nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu sukari ya viwandani. Wenzangu wamezungumzia sukari hii ambayo tunaitumia majumbani lakini mimi nazungumzia sukari ya viwandani ambayo inatumiwa na wenye viwanda wanaozalisha *soft drinks*, pipi na *biscuits*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitembelea viwanda vingi ambavyo vinatumia sukari hiyo lakini changamoto kubwa iliyopo ni kwamba kuna *fifteen percent withholding tax* ambayo inachukuliwa na Serikali ili kuhakikisha kwamba sukari ile inaenda kutumika kwa matumizi yaliyokusudiwa, mwisho wa siku huwa wanarudishiwa. Sasa hivi ni takribani miaka minne mfululizo malipo hayo ni ya kusuasua. Wakati tunatembelea viwanda hivyo Mheshimiwa Waziri yeye alikuwa ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara, changamoto hizi anazijua na kwenye Kamati tunazizungumzia. Mwisho wa siku tuliomba basi tujue *status*

ya kila kiwanda na malipo yalipofikia lakini mpaka tunawasilisha bajeti hakuna chochote wala maelezo yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri atakapofika hapa ku-*wind-up* atueleze ni kizungumkuti gani kinaikumba Serikali kuwalipa fedha zao wale wanaotumia hizi sukari za viwandani? Kwa sababu ni haki yao, baada ya matumizi wanatakiwa waandike ripoti na pia ipigwe hesabu warudishiwe fedha zao kama zilivyo, lakini wamekwamisha biashara, mitaji imeshikiliwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natambua kwamba nia na madhumuni ya Serikali ni kuwawezesha na kuwasaidia wenye viwanda na wafanyabiashara kwa ujumla lakini isiwe Serikali ni kikwazo ambacho wafanyabiashara hawa wanalalamika mitaji yao imeshikiliwa, pato la Taifa linapungua, pia inafikia wakati mpaka kupunguza wafanyakazi na mitambo mingine imesimamishwa, tumekagua tumeona. Kwa hiyo, naomba suala hili lifanyiwe kazi kwa umakini, walipwe fedha zao ili waweze kuzalisha kwa wingi na kuleta pato la Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ipo haja ya kufungamanisha kilimo na biashara. Watu/wananchi wetu wanalima kilimo kwa mazoea, naomba Waziri wa Viwanda na Waziri wa Kilimo wakae na waone sasa viwanda vile vinavyohitaji *raw materials* au mazao, ni mazao gani yanahitajika kwa kiwanda gani ili kuweza kuwahamasisha wale wakulima walime ili wajue kabisa soko litapatikana eneo gani ili sasa Tanzania iweze kupata tija pia pato la Taifa lipatikane kwa kila Mtanzania na viwanda viendeleo kuzalisha kuliko kutegemea *raw materials* kutoka nje ambazo wakati zinaingizwa na kufanyiwa kazi ile *product* inakuwa bei kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa napenda kumshukuru pia Waziri kwa juhudi zake. Nimeona janga hili la *Corona* jinsi anavyojitahidi kwenda kwenye viwanda mbalimbali vya *sanitizer* kuweza kuona ni jinsi gani wanatengeneza kwa wingi na pia barakoa. Kuna

changamoto, kutokana na hotuba ya Rais wetu wapo wenye hofu kununua zile barakoa za madukani na ni kweli kabisa kwa sababu ile barakoa ukinunua kwenye *box* inaonesha *country of the origin*, lakini yenyewe ukiiona haina nembo yaani mlaji/mtumiaji wa mwisho hajui hii inatoka wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nashauri Mheshimiwa Waziri viwanda vyetu vinavyozalisha hizi barakoa ziweke nembo angalau hata kikaratasi kilichoandikwa *made in Tanzania* mtu hata akinunua anajua inatoka nchi gani kwa sababu sio wote wana uwezo wa kununua *box* zima lile. Hii itasaidia mtu atakapovaa kuwa *comfortable* kwa sababu sasa hivi kila mtu ana hofu kununua za dukani, hajui zinatoka wapi na sasa hivi mtu ananunua moja, uwezo wa kununua *box* kwa Sh.150,000 au Sh.200,000 hana uwezo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri wakati unatembelea vile viwanda tunashauri *country of origin* iwe *labeled* pembeni ya hiyo barakoa ili watu waondokane na hofu kwa sababu wengine wanaona kabisa hizi za madukani ndiyo zinazidisha, labda ndiyo zina vimelea. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri utakapotembelea viwanda, najua sisi Wanakamati hatuna muda tena wa kutembelea, ni wewe ambaye utaenda ulifanyie kazi suala hili kwa umakini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu viwanda vilivyobinafsishwa. Ni takribani viwanda 156 vimebinafsishwa na tunajua nia na madhumuni ya Serikali kuvibinafsisha viwanda vile ni kuweza kuzalisha na kuleta tija, ajira na pia kuleta pato la Taifa lakini viwanda vingi waliovichukua wamevitelekeza, wengine wameviacha kama vilivyo, hawaviendelezi. Kwenye Kamati wamekuja wameelezea kwamba Serikali inajitahidi kuvirejesha ili kutafuta wawekezaji wengine. Tatizo linakuja kuna kipengele ambacho kimekosekana katika mikataba ile kile kinachoeleza kwamba kama aliyebinafsishiwa akishindwa kukiendeleza Serikali inaweza kukichukua lakini haiwezi kuchukua mara moja. Sasa hivi wamiliki wengi wameipeleka

Serikali Mahakamani, kwa hiyo, inabidi warekebishe ili kuona kwamba wakati wanawekeza ule uwekezaji unatakiwa uwe wa makini lakini pia kipengele kiwepo ambacho kitasaidia endapo mwekezaji akishindwa Serikali iweze kuchukua kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, dakika moja, nawashukuru wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam, nakishukuru Chama changu cha Wananchi (CUF) kwa kunichagua kuwawakilisha kwa muda huu mfupi, lakini nawaahidi *In Shaa Allah*, wenzangu wametoa nia na mimi nitagombea Jimbo la Temeke kama Mbunge wao, nitarudi na nitashinda kwa kishindo. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zainab Mndolwa hilo Jimbo ulilotangaza nadhani kuna mtu atakuwa anajisikia kukupa taarifa sema umemaliza muda. (*Kicheko*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu atafuatiwa na Mheshimiwa Kanali Mst. Masoud Ali Khamis, Mheshimiwa Peter Lijualikali ajiandae.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ili nichangie Sekta ya Viwanda ambayo nina utaalim nayo, nimekuwa Waziri. Kwa hiyo, unaponipa nafasi kama hii lazima nikushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru sana Rais, Makamu wa Rais mama Samia na Waziri Mkuu kwa kukubali na kuamua kutoa kipaumbele kwa sekta hii. Sekta ya viwanda inaleta matumizi ya teknolojia ambayo inarahisisha maisha kwa ujumla. Sekta ya Viwanda inaongeza tija na thamani kwa malighafi hasa ya kilimo, mahali ambapo hata bei inapanda kwa sababu ya kuongeza thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahi sana kuona katika kipaumbele hiki viwanda haviishii mijini tu vinaenda mpaka Wilayani na Vijijini. Hili ni jambo ambalo litafanya

maendeleo ya nchi yaende kwa pamoja na kusiwe na eneo ambalo maendeleo hayatakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa Wilaya ya Hanang kwa wawekezaji waliojitokeza kuwekeza na kuweza kuendeleza chumvi. Badala ya kuuza chumvi ghafi, sasa wanaipitisha kwenye kiwanda na baadaye itakuwa na *quality* ama *standards* ambayo inatakiwa. Naomba sana tuanze kwa haraka na Serikali iweze kuwasukuma wale wawekezaji ili Wilaya ambayo haikuwa na viwanda sasa iwe na viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda kingine ambacho kitasaidia sana ni cha *cement*. Ukiangalia kule kwenye ukuta wa *Rift Valley* kuna malighafi zote za *cement*, ukienda Tanga, Dar es Salaam hata Mtwara malighafi nyingine ya *cement* inatoka kilomita nyingi lakini kwa Hanang malighafi zote zinatoka mahali pamoja. Kwa hiyo, *cement* ikizalishwa pale bei itakura rahisi. Naona kuna mwekezaji ambaye anataka kuwekeza lakini imechukua muda mrefu. Nakupongeza sana kuwa Waziri kijana na ambaye namfahamu sana, anaenda kwenye sekta ambayo kwa kweli ataiendeleza sana, tusaidie hiki kiwanda cha *cement* kiweze kuanza mapema ili kwanza tupate eneo ambalo litatoa *cement* kwa bei rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho nataka niungane na wenzangu ni kuanzisha kiwanda cha chuma na kiwanda cha mkaa kwasababu *that is basic industry* kiwanda cha msingi ambacho kitatumika kwenye kila sekta ya viwanda nisingependa kuongea sana kwasababu kwa kweli wenzangu wameongea na nimekuwa Waziri kwa hiyo, sina haja ya kurudia mambo mengi ambayo nimeyasema napenda kuungana na wenzangu kumshukuru sana Rais kutupa moyo wakati huu mgumu wa corona.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba na sisi tumuunge mkono tuliokubali kubali hapa Bungeni maana yake tumeona kwamba ni muhimu na bila kupitisha bajeti hii maana yake nguvu ya kupigana na corona itakuwa ndogo zaidi. Naona wale walioacha kuwa Bungeni watajijua

wenyewe wala hatuna haja ya kuwasema nataka kuwahakikishia watanzania sisi ambao tupo hapa Bungeni tuko na Rais wetu hapa Bungeni na nje ya Bunge kuona kwamba tunaomba Mungu lakini tunapigania vilevile suala la utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza wananchi wa Hanang tena kwa mimi kuwa Mbunge wao kwa mara ya tatu ninaamini mara ya nne hawataniacha na nitakuwa na nguvu zaidi, wameshirikiana na mimi tumetekeleza ilani yetu kwa kuwa pamoja tumeshikana mikono na ndiyo maana wananipenda na mimi nawapenda ninaomba sana ninaomba sana na Bunge letu lizidi kuendelea wote tulioko humu turudi kwasababu tumeshirikiana kupitisha mambo mengi na tumeshirikiana kuendelea maendeleo katika maeneo yetu na tumeshirikiana na uongozi wetu mzima ninawashukuru sana mungu awabariki. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Kanali Mstaafu Masoud Ally Hamis, atafatiwa na Mheshimiwa Peter Lijualikali Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke ajiandae.

**MHE. KANALI (MST) MASOUD ALLY KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa tena nafasi ya kusimama mbele ya Bunge lako ili kuchangia Wizara hii muhimu sana ya Viwanda na Biashara. Kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa azma yake kubwa ya kutaka kulipeleka taifa kwenye uchumi wa kati kupitia viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nimshukuru Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Rais wa Zanzibar na viongozi Mawaziri wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar kwa kazi kubwa wanayoifanya kulipeleka taifa letu kwenye maendeleo ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hiki ni kikao cha mwisho nianze kwanza pia kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa viongozi wote wa Jimbo la Mfenesini,

wanachama wa Chama cha Mapinduzi, viongozi wa Wilaya ya Mfenesini na familia yangu kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kunisaidia na kushirikiana nami katika kuleta maendeleo ya wananchi katika Jimbo hilo. Shukrani za pekee ziende kwa mke wangu Mziwanda ambaye ananisaidia sana kule Jimboni katika kufanya kazi za Jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Waziri, Naibu, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara hii. Kwa kweli katika muda mfupi mwenye macho haambiwi tazama yapo mabadiliko tayari yameanza kuonekana yanaendelea kutendeka hapa nchini ambayo yanawasababisha wawekezaji wetu na wafanyabiashara hivi sasa wafanye kazi kwa kujiamini sana naomba sana tuwape pongezi sana wenzetu hawa na waendeleo mungu awajaalie waendeleo kuimarika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais yeye anataka kuipeleka nchi kwenye uchumi wa kati kupitia viwanda. Lakini wapo wananchi na hata viongozi baadhi yao wanadhani kwamba Rais akisema leo tu basi kesho nchi itabadilika hakuna mwenye uwezo wa kubadilisha hivyo, mwenye uwezo wa kubadilisha mambo kama hayo ni Mwenyezi Mungu tu. Rais ana uwono wa mbali wa kuhakikisha kwamba kwa hizi *step* anazokwenda ikifika kipindi fulani nchi itakuwa imebadilika, na mimi naamini kwa mwendo huu tunaokwenda Mheshimiwa Rais na kushirikiana na Mawaziri hawa waliopo nchi itabadilika siyo muda mrefu. Namuomba sana dua Mheshimiwa Rais mungu ampe afya na kuendelea kutuongoza vizuri kulipeleka taifa hili kwenye uchumi wa kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako machangamoto yanayotokea katika utekelezaji wa miradi mbalimbali hapa nchini au ujenzi wa viwanda kutokana na sisi wenyewe kutokujipanga vizuri, yako mambo tukijipanga vizuri ninahakika tutafika mbali. Mfano viwanda vinavyozalisha tunaambiwa Wizara ya Kilimo na Wizara ya Biashara waendeleo kusaidiana kupata mali ghafi ni sawa, lakini pia Wizara hizi pia zisaidiane na Wizara ya Viwanda kununua

hizi bidhaa ambazo zinazalishwa hapa nchini. Yako mambo yanatokea lazima tuseme ukweli hayafurahishi sana tunapojenga kiwanda mfano kiwanda cha Tanzania *Bio Tech Product*. Kiwanda hiki kimejengwa miaka mitano iliyopita kimefanya kazi miaka mitano iliyopita na kwa ushirikiano na wenzetu wa Cuba kazi yake kubwa ni kuzalisha viudadu na sisi tunasema tuna ugonjwa malaria kwa hiyo wanazalisha dawa za kuuu vimelea vya malaria lakini tunashindwa kuzinunua sisi wenyewe hapa ndani na tunasema malaria bado tunayo kwanini tusizinunue kwa wingi tukaondosha malaria ili kusudi hawa wenzetu sasa wanapotaka kwenda kuuza nje wapate soko la kuuza dawa hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Biashara valia njuga hili uhakikishe kwamba Wizara yetu ya Afya inanunua madawa haya na kuyapeleka kwenye sehemu zinazohusika na halmashauri zetu nazo tuzihamashe zichukue madawa kuuu ili kuondosha hii malaria hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuwaomba watanania wote sizungumzii tena leo corona lakini nasema nazungumzia kupeleka nchi yetu kwenye uchumi wa kati ili tufike malengo hayo tuliyoyakusudia ni kila mmoja kwa nafasi yake atekeleze wajibu wake wa kuwajibika kuchapa kazi ili kulipeleka Taifa tulikokusudia taifa hili halitopelekwa kwa maneno tu au kwa kuonyesheana vidole au kupelekana matusi halipelekwi huko katika maendeleo. Maendeleo yatapatikana kwa kila mmoja kwa nafasi yake afanye kazi ya kujituma na kuhakikisha anatekeleze wajibu wake aliopangiwa kwa weledi na umakini zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya mimi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kanali Masoud nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Peter Lijualikali,



atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mheshimiwa Mussa Rashid Ntimizi ajiandae.

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru nianze kwa kusema Mheshimiwa Waziri Mkuu atakumbuka mwaka jana tulikuwa na ziara kule Kilombero mpaka Mlimba, tukafika Kiwanda cha Sukari cha Kilombero llovo na pale nakumbuka Mheshimiwa Waziri Mkuu yeye mwenyewe baada ya kupokea ripoti ya llovo akaona kwamba gawio la llovo ni dogo sana ukilinganisha na viwanda vingine, japokuwa llovo inazalisha kiasi kikubwa sana akawauliza kwanini mna gawio dogo kuliko viwanda vingine sasa nilikuwa natamani nijue kama hiyo tayari wameshaongeza pato hilo au bado ni vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili kwenye hii hoja pia ya hiki kiwanda tulizungumza pale kwasababu kiwanda kinaongeza uzalishaji mimi nikaomba basi pia na maslahi ya wafanyakazi pia yaongezeke sasa nilikuwa natamani pia nifahamu kama hilo pia limeshaka sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Tano, ilitoa ahadi ya kufufua viwanda ambavyo vimekufa tangu kwenye kampeni. Kule kwangu kuna kiwanda cha MMT - Mang'ula Mashen *Tools* ambacho kilikuwa ni kiwanda kikubwa sana kinachozalisha *spear* za karibu kila mashine kwenye nchi yetu, hiki kiwanda Serikali ilikibinafsisha. Nataka nijue *status* kiwanda hiki kimesharudi Serikalini au bado kipo kwa mwekezaji ni kwanini hakifanyi kazi iliyokusudiwa? Kwasababu kiwanda hiki kilikuwa kinafanyakazi hizi kwa ajili ya nchi nzima siyo tu Kilombero.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lijualikali kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Omary Mgumba Naibu Waziri wa Kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana nilikuwa nataka kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge anayezungumza kuhusu kama alivyosema kwamba kwenye ziara ya Mheshimiwa

Waziri Mkuu kwamba Waziri Mkuu ni kweli aliwauliza Kilombero kwamba gawio ni dogo walikuwa wanatoa milioni 700 nataka nimpe taarifa sasa hivi wanatoa bilioni 6 mwaka jana wametupa Serikali kama gawio.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lijualikali unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijamsikia vizuri amesema bilioni sita?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Bilioni sita.

**NAIBU SPIKA:** Bilioni sita.

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** *Ooh that is nice!* Nikupongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hilo sasa nilikuwa ninahitaji kama wanafanya hivyo basi fedha *service levy* inayokuja kwenye Halmashauri ya Kilombero pia iongezeke, kwasababu siyo tu mpate kwenye Serikali halafu sisi kwetu kule kwenye *service levy* ambayo inakwenda kwenye maji, kwenye barabara za mitaa, inakwenda kwenye huduma za afya inabaki palepale. Sasa niombe Serikali kama wameongeza kwenye Serikali Kuu tupambane mtusaidie watuongeze na kwenye halmashauri yetu sisi tunapata kama milioni 200 hivi kwa mwaka ambayo ni ndogo mno. Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri mmefanya kazi nzuri tunaomba na sisi kwenye halmashauri yetu basi fedha hizi ziongezeke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye hoja yetu ya MMT nataka nifahamu sasa maana yake Bunge ndiyo linaisha hoja ilikuwa ni ya kwenu Serikali mlitoa ahadi na mkasema mnafanyia kazi mmefikia wapi? Kile kiwanda ilikuwa ni injini ya Tanzania reli unayoiona hii ya *TAZARA* imejengwa *from* pale kwa hiyo hicho kiwanda ndiyo kilikuwa kinatengeneza mataruma na mashine zote za ile reli watu walikuwa wakikosa *spear* wanapata MMT vijana wa Mang'ula, wa Ifakara, wa Kidatu walikuwa wanapata kazi

pale leo kimekufa. Sasa nataka nijue mna mpango wowote au hakuna ili kiwanda hiki kiweze kufanya kazi na watu wa kilombero wapate pia ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba nifahamu tupo kwenye corona sijamsikia hata Waziri hapa akija na *analysis* ni kwa kiasi gani corona inaathiri uchumi wetu sisi kama nchi tumejipangaje kupambana na athari za kiuchumi tunafahamu biashara zinafungwa watu ambao walikuwa wanafanya biashara hizi za kwa mfano kwenye sekta ya maliasili watu wanafunga biashara sasa tunawasaidiaje wale watu kiuchumi tunaongea vipi na benki zetu wenzetu Kenya wameongea na benki angalau riba zipungue, na hata ule muda wa watu kutoa haya marejesho basi kidogo uongezeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi kwetu mbona kama kimya hivi yaani ina maana kweli sisi hakuna athari za kiuchumi kweli? Mbona kama vile tunaacha watu! Mheshimiwa Rais anahitaji nchi isongembele anataka mapato sasa biashara zinafungwa watu hawa biashara hizi zikifungwa hiyo kodi tunapata wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hizi shule zetu hizi hawa walimu hawapati tena mishahara nasikia wengine wanalalamika kwamba mishahara wamefungiwa hizi shule tunawasaidiaje wenye shule ambao wengine huenda walikopa kwenye mabenki waweze kulinda mitaji yao, ili *corona* itakapokwisha waweze ku-*maintain* biashara yao ambayo pia ni ajira. Sasa sisi kama Serikali sisi kama wawakilishi wa wananchi naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri ambao uko hapa utusaidie kwenye uchumi tunatatua vipi hizi changamoto? Watu kule wanakosa biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia leo kwenye *clip* huko sijui ni wapi kwenye mpaka watanzania hawaruhusiwi kuingia kwenye nchi zingine ile ni biashara maana yake ila wao wanakuja mpaka watu wengine wamegoma kwamba na nyie kama kwetu mnakuja basi

msiingie watu wanaathirika. Kwa hiyo, nawaomba Mheshimiwa Waziri utusaidie wenzetu wana-*package* wameomba fedha *IMF* na wamepewa fedha kwa ajili ya ku-*stimulate* uchumi wao sisi sijasikia hata kama kuna huo mkakati hata kuusikia tu kwamba tumefikiria kuomba fedha kwenye benki ya dunia kwa ajili ya ku-*stimulate* biashara za nchi hii sijasikia. Sijasikia hata kitu chochote cha kupambana kwenye *issue* ya kiuchumi kwenye hii corona.

Mheshimiwa Naibu Spika, *corona* itaisha tupo wazima Mungu ni mwema tutajikuta hoi, sasa maana yake ni nini? Nikuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu niwaombe viongozi ambao mko hapa *corona* si jambo la CCM, *corona* si ilani yenu, corona ni janga la kidunia tusione aibu kulifanyia mambo ambayo yanastahili kufanyika tunaelewa haikuwa kwenye ilani yenu fateni wenzenu ambacho wanakifanya ambacho ni kizuri tuwasaidie wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme niwaombe watanania niombe Serikali *corona is real*, corona inaathari jana nilisema kuhusiana na *social distance* na leo ninasema tena tusikilize utaalumu tuheshimu utaalumu tujaribu kuweka siasa kando angalau kwenye hili tuna mengi ya kuzungumza kwenye siasa hili tuliache, tuna mengi ya kufanya kwenye siasa hili tuliache na Bunge hili nimeona ratiba linaisha keshokutwa tu hapa maana yake baada ya keshokutwa inabaki Serikali peke yake Wabunge hapa hatupo mtabaki Serikali na Mheshimiwa Rais. Kama hapa hivi ndiyo tuko hivi kesho itakuwaje mko peke yenu tunaomba msikilize ya kwetu leo, ahsante sana Mungu awabariki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana labda Mheshimiwa Bashungwa hapo atachagua yeye hoja zinazomhusu hizo zingine Waziri wa Fedha wakati wake utakapofika nadhani atatueleza kama Taifa tunaelekea wapi. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke atafatiwa na Mheshimiwa Mussa Rashid Ntimizi, Mheshimiwa Eng. Gerson Hosea Lwenge ajiandae.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii kwanza kabisa napenda nimshukuru mwenyezi mungu kwa kunipa kibali cha kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpungeze Waziri Mheshimiwa Bashungwa pamoja na watendaji wote katika Wizara ya Biashara nawapongeza sana. Nitaongelea mambo matatu, nitaongelea kilimo, nitaongelea vitambulisho vya wajasiriamali na nitamalizia na janga la corona.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme yafuatayo ili tuweze kuwekeza viwanda katika nchi yetu ni lazima tuhakikishe tunawekeza katika kilimo, mifugo na uvuvi. Tukiwekeza katika maeneo haya tutaweza kufanya vizuri katika viwanda vyetu, kwasababu malighafi itatoka katika nchi yetu. Kwa mfano katika nchi yetu tumejaaliwa kuwa na mazingira mazuri ya kilimo mfano halisi ni mwaka huu tumepata mvua ya kutosha kwa maana hiyo mazao mengi yaliyopandwa katika mwaka huu yameweza kustawi. Natokea mkoa wa Kigoma nitaongelea kuhusu kilimo cha mchikichi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Dkt John Pombe Magufuli, lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuweza kulivalia njuga zao la mchikichi ndani ya Mkoa wa Kigoma. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru sana kwa kuhamasisha zao la mchikichi ndani ya Mkoa wa Kigoma umeshakuja mara nyingi na ninaomba nikutaarifu kwamba kazi yako imeshaanza kuzaa matunda tayari mbegu zimeshazalishwa na wakulima wameshachukua mbegu wameshaanza kwenda kupanda mbegu katika mashamba yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaamini ndani ya muda mfupi matokeo yataonekana. Niombe tu Mheshimiwa Waziri Mkuu ulipokuja Kigoma ulijionea hali halisi

kwenye kituo kile cha utafiti Kihinga. Ninaomba kituo hicho kipewe pesa ili kiweze kufanya utafiti vizuri hatimaye kiweze kuzalisha miche na wananchi waweze kuendelea kulima kilimo chenye tija. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuweza kuja na suala hili la vitambulisho kwa wajasiriamali. Kwa kweli tangu wameleta vitambulisho kwa wajasiriamali akinamama wengi wauza mboga mboga, akinamama ntilie, wanaofanya biashara ndogo ndogo sokoni wanapomaliza kulipia vile vitambulisho vyao wanafanyabiashara vizuri bila usumbufu wowote na wanaweza kujikimu wao wenyewe na kuweza kuchangia Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendeleo kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuweza kuja na suala hili la vitambulisho kuwapatia akina mama, vijana na wafanyabiashara wadogo wadogo. Kwa kweli baada ya kupewa vitambulisho hivi, wanafanyabiashara katika maeneo mbalimbali bila kubughudhiwa. Kwa hiyo, nina kila sababu ya kuishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuweza kubuni kitu cha namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, niendeleo kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyoendelea kupambana na nimtie moyo kwa sababu kila mara anatumia kumtanguliza Mungu. Nasi tuna kila sababu ya kuendelea kumuunga mkono kwa kumtanguliza Mwenyenzi Mungu. Mimi watoto wangu ni waombaji sana; wananiambia mama omba sana janga la *Corona* litaondoka na tutabaki salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu maeneo ya mipakani uongezwe ulinzi. Sisi tunatokea Kigoma, tunapakana na Burundi na Kongo na mara nyingi wageni wanakuja hata kwa kutotumia barabara, wanatumia njia za maji. Kwa hiyo, wakati mwingine wanaweza kuingia watu bila kujua. Naomba tu wale walinzi, maaskari na wote

ambao wapo mipakani kwanza wawe waaminifu. Wakishakuwa waaminifu wageni watakapoingia kwa kupitia njia za panya wataweza kudhibitiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilitaka nihamasishe hili la kuendelea kulinda mipaka yetu ili wageni wasiweze kuingia na kuleta magonjwa katika nchi yetu. Ninaamini tupo kwa yeye atutiaye nguvu na Mungu wetu atutushindia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimentaja Mheshimiwa Musa Rashid Ntimizi, atafutiwa na Mheshimiwa Eng. Gerson Hosea Lwenge na Mheshimiwa Janeth Zebedayo Mbene ajiandae.

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie katika hotuba ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Kwanza kabisa, nianze kwa kupongeza kazi nzuri sana inayofanyika katika kipindi hiki chini ya mdogo wangu Mheshimiwa Bashungwa. Amedhihirisha vijana kwamba wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile mama yangu Mheshimiwa Eng. Manyanya amekuwa ni msaada mkubwa sana kwa ndugu yetu, kijana mwenzetu Mheshimiwa Bashungwa kwa kazi nzuri ambazo kwa kweli zinafanyika sasa katika Wizara yetu ya Viwanda na Biashara. Pia napongeza timu ya watendaji ikiongozwa na Katibu Mkuu ambaye amekuja sasa. Kazi imefanyika vizuri na Watendaji wote walio chini Wizara hii vya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa leo ni siku ya kuzaliwa Mheshimiwa Bashungwa, Mungu azidi kumpa maisha marefu sana. Ameiweka vizuri Wizara, ameituliza, anaitendea haki kwa kiasi kikubwa kazi aliyopewa na Mheshimiwa Rais. Mungu azidi kumbariki na afanye kazi nzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yetu ya Viwanda na Biashara ilitembelea maeneo mengi wakati wa ziara na kujionea kwa vitendo kabisa yale ambayo yanasemwa na Wizara hii ya Viwanda na Biashara. Tumetembelea eneo *TAMCO*, tumekuta hekta zaidi ya 200 zimepimwa, vinajengwa viwanda, ukifika pale huwezi kuamini. Sasa hivi kuna kinatengenezwa cha ku-*assemble* magari hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya maeneo Watanzania wengi hawafahamu, lakini kiwanda hiki kipo pale *TAMCO* Kibaha na kipo katika hatua za mwisho katika kukamilika. Kuna viwanda vingi vya *tiles* vipo pale, lakini kuna viwanda vya kutengeneza madawa vinatengenezwa pale, viwanda vya kutengeneza vifungashio vipo pale. Kwa kweli kazi kubwa inafanyika. Waswahili wanasema tembea uone. Kwa kweli kuna haja ya kutembea kuona kazi kubwa ya uchumi wa viwanda inayokwenda kama azma ya Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Bashungwa na Wizara yako mnaitendea haki kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Bashungwa wakati anaingia, alikutana na shida na changamoto ya korosho. Walikwenda wakapambana, soko la korosho likapatikana. Kwa kweli ni kazi kubwa ambayo wameifanya na Watanzania wanaiona kwa sababu wananufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niseme kwenye korosho lakini Mheshimiwa Waziri umenidokeza hapa dakika mbili zilizopita, Kamati ilikwambia upambane na shida ya wanunuzi wa Tumbaku iweze kwisha. *FCC* na Wizara yako ilisimamia vizuri, leo umeniambia kesi imekwisha. Sasa wanunuzi wa Tumbaku wapo tayari kwenda kununua Tumbaku Mkoa wa Tabora. Nataka nikuhakikishie kwa hili ulilolifanya wana Tabora wataendelea kukuombea Mungu azidi kukubariki wewe na wasaidizi wako.

**MBUNGE FULANI:** Amina.



**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Tumbaku ni zao ambalo kwanza linaingiza pato kubwa kwa nchi, lakini la pili linaingiza kipato kikubwa kwa wakazi wa Mkoa wa Tabora na mwisho wa siku wa hili lililofanyika tunashukuru sana kwa kazi kubwa ambayo imeweza kufanyika. Nilitaka nishauri mambo mawili tu kwa kifupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napongeza kwa *Blue Print*. Unajua katika Kamati nilikuwa ni msemaji mkubwa wa *Blue Print*. Kwanza Serikali imetumia muda mrefu kuitengeneza, lakini imetumia gharama nyingi sana. Madhumini yake na malengo yake ni makubwa sana. La kwanza ilikuwa ni kurahisisha ufanyaji wa biashara nchini; la pili, kuondoa kero za uwekezaji; la tatu, kuongeza ufanisi; na la nne, kuongeza mapato kwa nchi. Wafanyabishara walikuwa wanakutana na vikwazo vingi katika uwekezaji, katika ufanyaji wa biashara. Hii *Blue Print* imekuja kutusaidia kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaloliomba ni kwamba, pamoja na kwamba *documents* iko katika hatua za mwisho, nashauri Watendaji wa Serikali waisome vizuri *Blue Print* na kuitafisiri kwa sababu *Blue Print is just a change of mindset*.

**MHE. BHAGWANJI M. MEISURIA:** *Thank you.*

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama hatubadilisha *mindset* za Watendaji wa Serikali yetu, hata ile *document* haitakuja kusaidia. Nitoe mfano mmoja ambao upo sasa. Sasa hivi wawekezaji wanakuja na teknolojia mpya, wanakuja na *equipments* mpya, wanahitaji kuleta watalaam kwa sababu ya kufunga zile teknolojia mpya na kuendesha ile mitambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Sheria ya Kazi inahitaji kufuatwa, lakini pia kuna sheria zinakinzana katika kutoa vibali vya hawa katika kufanya kazi katika vile viwanda. Maeneo mengi wafanyakazi wanakosa vibali kwa sababu ya sheria hizi mbili ambazo tunaomba mziangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, bado yapo malalamiko kwa baadhi ya wafanyabiashara kwenye suala la *18 percent ya VAT refund*, lakini pia kuwa *15 percent ya refundable import of industrial sugar*, amezungumza kidogo Mheshimwa Zainabu. Kuna makampuni ambayo yameshafanyiwa uhakiki wa mahesabu, lakini bado hawajalipwa *18 percent* yao ya *VAT refund*. Hawa ambao wametoa *15 percent ya import duty of industrial sugar*, mpaka sasa wanakaribia mwaka mzima hawajapewa ile *refund* yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hesabu zimeshafanyika lakini bado hawajapewa zile fedha. Jambo hili hupunguza mtaji wa wafanyabiashara, hupunguza uwezo wa kujiendesha kwa wafanyabiashara wetu, hupunguza uwezo wa kuajiri wafanyakazi katika maeneo yao mbalimbali. Naomba Wizara hizi mbili ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Fedha ilianganalie hili ili mwisho wa siku ilete ufanisi katika ufanyaji wa biashara nchini kwetu Tanzania na isaidie kuongeza mapato kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa aliyofanya...

**MBUNGE FULANI:** Amen.

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri waendeleo kufanya kazi, kwa sababu Wizara hii ndiyo nguzo ya uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Eng. Gerson Hosea Lwenge atafuatiwa na Mheshimiwa Janeth Zebedayo Mbene na Mheshimiwa David Ernest Silinde ajiandae.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza, namshukuru

Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema niweze kuongea leo katika Bunge lako. Kwanza nianze kutoa pole nyingi sana kwa misiba mitatu ya Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliotutangulia mbele za haki. Naomba Mwenyezi Mungu aweke roho za Marehemu mahala pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye hoja hii ya Viwanda na Biashara nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, kwa kazi nzuri ambayo anaifanya. Kwa kweli katika kipindi hiki cha Awamu ya Tano ya Serikali tumeona mapinduzi makubwa sana katika ujenzi wa viwanda katika nchi yetu. Nina imani kabisa azma ya Taifa kufikia uchumi wa kati mwaka, 2025 inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimshirikisha Mheshimiwa Bashungwa katika ujenzi wa kiwanda kimoja pale Njombe, kiwanda cha *Avocado* cha kuchakata parachichi kwa zaidi ya mwaka mzima kwa kupitia *EPZA*. Alizungushwa sana kupata kibali na leseni. Ninaamini kwa utaratibu huu wa kupitia *EPZA* wanapata unafuu fulani wa kodi ili kusaidia wananchi. Maana zao la parachichi kwa Mkoa wa Njombe lilifikisha bei ya kilo moja shilingi 1,500/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilisukuma sana kiwanda kile kiweze kuanzishwa na Mheshimiwa Waziri alisaidia na kweli kimeanza, lakini kimekuja kutoa kitu ambacho wananchi kwa kweli hawakihitaji kiwanda cha namna hiyo. Kwa sababu kutoka kilo moja ya parachichi ya shilingi 1,500/= kiwanda kinanunua kwa shilingi 250/= kwa kilo kwa kisingizio kwamba wao wanatafuta maparachichi yale ambayo ni *left overs* ambayo hayana thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kweli tunaagiza kiwanda kwa ajili ya kuchakacha *left overs*, halafu unaweka kigezo kipi cha kuonyesha hili parachichi ni *grade one* au hili ni *left overs*, lile ambalo wameacha kununua wengine? Kwa hiyo, wakulima wanalalamika kwamba wanapunjwa. Naomba sana Wizara iende ikaangalie undani wa biashara ya kiwanda kile kama kweli kimewekeza kwa manufaa ya

wananchi au wanafanya ujanja ili kusudi iwanunulie wananchi kwa bei ambayo kwa kweli inakatisha tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninataka nichangie, ni kweli tumeshafikisha viwanda 8,477, nimeona kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri na mpaka sasa tunachangia 8.5% kwenye pato la Taifa. Kwa kweli hili ni jambo la kupongezwa. Sasa nilitaka niseme kwamba katika viwanda hivi ili uwe na uhakika endelevu kabisa wa viwanda ni lazima uwe na vile viwanda mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kiwanda cha kutengeneza *Iron Ore*; kiwanda kile tulichokuwa tumekizungumza miaka zaidi ya 10 cha Liganga na Mchuchuma, kilikuwa ni kiwanda mama kwamba hata sasa unasema una viwanda vinne vya chuma lakini *Iron Ore* wanaagiza toka nje. Ingefaa sana tuwe na *Iron Ore* ambayo inatoka ndani ya nchi ndiyo tungefaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kweli nafikiri ni muhimu sana Mheshimiwa Waziri ukivalie njuga hata ikibidi mara nyingine kufanya maamuzi magumu, kama kuna mwekezaji ambaye anaonekana kwamba hatufai tutafute mwingine. Wananchi wale wana miaka zaidi 10 ardhi yao wameitoa kwa Serikali. Nimeambiwa kumbe hata fidia bado hatujalipwa, basi angalau tulipe fidia ili tuwe na uhakika lile eneo ni la kwetu sasa, tutafute wawekezaji kwenye *cooperative bases* kwamba waje washindane na masharti ya Serikali. *Of course* kwanza tutaweka maslahi mapana mazuri ya Serikali, hiyo iwe kitu cha kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna mwekezaji ambaye anaweka maslahi kwake, huyo hatumhitaji. Hilo halihitaji tuchukue miaka 10. Kwa hiyo, naomba sana Serikali kwenye hili kwa kweli hebu tuweke *speed* kidogo. Kiwanda kile cha kuchakata Liganga na Mchuchuma ni kipaumbele chetu kwa sasa na kwa uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nilitaka nizungumzie kwenye eneo la biashara. Ni kweli kama

alivyosema Mheshimiwa Waziri eneo la biashara linaingiza zaidi ya 35% ya pato la Taifa, ni jambo nzuri. Kutokana na ugonjwa huu ulioingia sasa hivi, inaonekana kwamba itashuka. Kuna eneo moja niliongea kwenye bajeti ya mwaka 2019, kwenye Sekta ya Huduma, kwa mfano kwenye uendeshaji wa hoteli, wanalalamika kwamba pamoja na kwamba wanalipa mapato, lakini kuna eneo moja linaitwa *service levy* ambazo zinatolewa na Manispaa, Sheria Ndogo, lakini ile *service levy* wanaoi-charge 10% ya mauzo, hivi ni faida gani utapata zaidi ya 10% anayochukua Manispaa au Jiji? Sasa huyo mfiyabiasha anapata nini? Baadaye tunafika mahali maana TRA huwa wanakokotoa kodi kutokana na namna faida ambayo ameipata huyu mwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba sana, najua Mheshimiwa Waziri ni mchapa kazi, hebu hilo aliangalie. Sawa tumewaruhusu waweke sheria ndogo, lakini sheria ndogo ziwe zinawapa unafuu wawekezaji wanaofanya kazi za namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada yakusema hayo, naomba niseme naunga mkono hoja hii na ninakutakia kila kheri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi.  
(Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Janeth Zebedayo Mbene atafuatiwa na Mheshimiwa David Ernest Silinde na Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula ajiandae.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru sana kwa kunipatia fursa ya kuchangia katika bajeti hii. Nianze kwanza kwa mkumshukuru Mwenyenzi Mungu na ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli kwa kuonyesha *free will* kama Kiongozi wa Taifa huru la Tanzania, kwa kuamua mambo ambayo kwa kweli hata sisi wenyewe tunaona yamekuwa ya faida kubwa sana. Tunazidi kumwomba kwa Mungu kwa maono yake na kwa upendo wake kwa Watanzania kwa kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kuwa hakurukia *bandwagon* kama viongozi wengine walivyofanya na sasa hivi wanahangaika wafanyeje juu ya kurudisha tena uchumi pale ulipokuwa. Kwa kweli tumepata Rais wa kujivunia, tuendeleo kumwomba Mungu amjalie maisha marefu, afya njema na azidi kumlinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii vilevile kumpongeza sana Waziri, Mheshimiwa Bachugwa kwa hotuba nzuri sana iliyosheheni mambo mengi ya maendeleo pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Eng. Manyanya dada yangu na Watendaji wengine wa Wizara hii. Kwa kweli nashukuru sana kuona jinsi ambavyo hii Wizara imejikita katika maeneo muhimu ambayo tunahitaji kuyaona hasa tunapoelekeza kwenye uchumi wa viwanda. Nami nataka nichangie machache kama njia ya ushauri tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona jinsi ambavyo viwanda vinachangia kwa kiasi kikubwa 8.5% ya pato la Taifa. Tumeona vilevile Sekta ya Viwanda au biashara ndogo ndogo inavyochangia 35% ya pato la Taifa na kuchangia vilevile ajira milioni tisa. Tumeona kuwa biashara peke yake inachangia 8.8% ya pato la Taifa. Haya ni maeneo muhimu sana ni moja kwa moja tunaona jinsi Wizara hii ilivyokuwa na umuhimu katika uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nijikite sasa kwenye eneo la *SMZ* wanaochangia 35% la pato la Taifa. Huu ni uchangiaji mkubwa sana wa sekta ambayo inajumuisha wananchi wengi sana; wazalishaji wadogo kabisa na wakati ambao wanachangia pato kwa kiasi kikubwa namna hii. Hii inaonyesha moja kwa moja ni wapi Serikali yetu ijikite katika kuwekeza na huku ndiko ambako unakuta wale ambao wanataka kuondoa umasikini wapo. Kwa hiyo moja kwa moja unaona jinsi gani *segment* hii inaweza ikaisaidia Taifa letu kuondoa umasikini kwa kiasi kikubwa sana na vilevile kutengeneza ajira kwa Watanzania wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndiyo sekta ambayo kuna wakulima, kuna wazalishaji wadogo wadogo, kuna mafundi,

kuna wana sanaa na wazalishaji mbalimbali. Kwa jinsi ilivyo sasa hivi kwa kiasi kikubwa imeacha yenyewe kujiendesha. Napenda sana kuona Serikali ikijikita zaidi katika *segment* hii kuhakikisha kuwa hii sehemu inapatiwa uwezeshaji mkubwa hasa katika masuala ya elimu, katika masuala ya mitaji na katika masuala ya kuboresha huduma zao au mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna tatizo kubwa la ubora. Tuna tatizo kubwa sana la ushindani yaani kuweza kumudu ushindani wa soko kutokana na uzalishaji wetu. Haya ndiyo maeneo ambayo ningetemea Wizara ijikite katika kutumia zile taasisi muhimu ambazo zipo katika Wizara hii na hata zile ambazo zipo nje ya Wizara hii, kwa mfano, VETA, Vyuo vya Ufundi, taasisi mbalimbali ambazo zinasaidia wazalishaji wa aina mbalimbali kujiboresha katika uzalishaji wao ili kwa pamoja sasa waongeze pato la Taifa kupita hii *segment* ambayo ni watu wanaojajiri wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuona jinsi ambavyo kupitia *segment* hii wanawake wengi zaidi wanajikita katika eneo la viwanda na uzalishaji. Wanawake ndiyo wakulima kwa kiasi kikubwa sana, lakini wao wanaishia kwenye kulima tu. Sasa tungependa hata katika uboreshaji au uchakataji wa mazao na wao wawemo. Kwa hiyo tunapozungumzia kutoa mafunzo kwa wajasiriamali au wazalishaji tungependa sana kuona na wanawake ni kiasi gani na wao wanashirikishwa kwa sababu tunao wasichana, tunao vijana wanawake waliosoma na ambao pia wanaweza kufanya hizi kazi za ufundi au hata za uzalishaji kwenye viwanda vidogo na vya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni maeneo ambayo ningependa sana Serikali sana ijikite kwa sababu kwa wingi wao tunaweza tukaona wengi zaidi wakijikwamua kiuchumi. Kama mnavyojua mwanamke akijikwamua kiuchumi hata familia yake inakuwa bora zaidi, lakini vilevile hata unyanyasaji wa kijinsia unapungua kwa sababu anakuwa hana ule utegemezi wa moja kwa moja mpaka anakuwa kero nyumbani kwa mumewe au kwa wazazi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia suala la *EPZA*; *EPZA* ilivyoanzishwa ilianzishwa ili kuharakisha mapinduzi ya viwanda nchini, lakini mpaka sasa hivi tunaona kuwa kuna mikwamo mingi kwenye *EPZA* hasa kwenye masuala ya ardhi. Kuna masuala ya kulipa fidia, kuna masuala ya miundombinu wezeshi katika maeneo haya ambayo yamesababisha yale maeneo ambayo yametengwa hayajaweza kufanya kazi ilivyotegemewa. Tumesikia maeneo mengine mpaka watu wanafikiria warudishiwe, maeneo ambayo yalikuwa yameshatengwa kwa ajili ya *EPZA* ilhali tumepanga *EPZA* ziharakisha uzalishaji wa viwanda katika nchi yetu kwa kuondoa urasimu ule ambao umepitiliza katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapenda sana kuona haya maeneo ya *EPZA* yanafanyiwa uwekezaji mzuri, lakini vilevile na mitaji inatolewa sasa ili kuhakikisha kuwa tunawavutia wawekezaji katika maeneo haya. Nimefurahi sana kuona sasa *EPZA* inajikita katika maeneo ya kilimo kwa sababu huko ndiyo ambako kutakuwa na uzalishaji mkubwa wa viwanda zaidi kutokana na kuwa Taifa letu sisi ni zaidi ni la kilimo. Kwa hiyo wanapokwenda kuwekeza maeneo kama Songwe ambako kiasi kikubwa uzalishaji wetu sisi ni wa kilimo, basi moja kwa moja unajua kabisa viwanda vitajitokeza pale na uzalishaji utakuwa mkubwa, ajira zitapatikana lakini hata bidhaa zinazotoka pale zitakuwa na ubora ambao unahitajika kwenye soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia suala la *SIDO*...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja nakushukuru sana. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa David Ernest Silinde, atafutiwa na



Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma ajiandae.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii kuchangia Wizara ya Viwanda na Biashara. Huu ni mwaka wa fedha tunaotaka kupitisha hapa 2020/2021 na Mheshimiwa Waziri alipokuwa anaeleza hapa Bungeni awali amesema kwamba Wizara hii ndiyo iliyobeba Sera ya Awamu ya Tano ya viwanda, ndiyo iliyobeba na mimi siwezi kubishana naye, nakubaliana naye kwa asilimia 100. Hata hivyo, kuna vitu ambavyo nilikuwa nategemea kutoka kwake na ningependa kupata majibu baada ya maelezo haya nitakayokuwa nimeyatoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza amezungumzia kufungamanisha kilimo na viwanda. Ili uwe na viwanda lazima uwe na uzalishaji yaani unasema kuna *production, processing* halafu mwisho unakwenda kwenye *market*; uzalishaji, uchakataji kwa maana ya kuongeza thamani ya bidhaa pamoja na soko. Sasa hivi vitu vitatu ni lazima uvifungamanishe pamoja ndiyo sasa hapo tutakuwa tunazungumzia sera sahihi ya viwanda. Kwenye hili Wizara ya Fedha, Kilimo, pamoja na Viwanda na Biashara walipaswa kuja na mpango wa pamoja kwa maana ya *comprehensive report* ya namna gani ya kwenda pamoja. Tukiiacha hivi hivi kwamba viwanda anakuja na sera yake, Kilimo anazungumza lugha yake, Wizara ya Fedha nayo kwenye kusimamia sera anakwenda tofauti ndiyo maana unajikuta kila siku kumekuwa na hizi *contradiction* ambazo zimekuwa zikitokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano, kwa mfano wazalishaji wakubwa wa chai Kampuni ya *DL* anataka kuondoa mtaji wake ambaye ndiyo mzalishaji mkubwa, kwa sababu tu kuna masuala ya kikodi ambayo watu wa *TRA* na Wizara ya Fedha wameshindwa kumalizana kule. Ukienda kwenye tumbaku kuna mambo ya namna hiyo hiyo, ukiangalia *TLTC*, ana malalamiko ambayo yanahusiana na kodi lakini huyu anasimamiwa Wizara ya Viwanda, lakini wanaokwamisha wako upande mwingine. Kwa hiyo lazima

Serikali ije *comprehensive report* yaani ni lazima tu-*demand* sera ya kikodi na sera ya fedha kwa watu wa hizi Wizara tatu ili kusaidia hii sekta nzima ya viwanda. Ni kitu ambacho hakiwezi kuepukika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili niliona niliseme, ukienda *Uniliver* wana malalamiko yale yale. Hii ni kwa sababu hawa watu watatu kila mmoja anasema anasimamia sera yangu mwisho wa siku tunakuwa tunawaumiza wawekezaji wa ndani ya nchi. Kwa hiyo niliona niliseme ili Serikali iweze kuwa na *comprehensive report* ambayo iletwe ndani ya Bunge tu-*debate* tuwasaidie *way forward* ili pasiwe na huo mkanganyiko ambao umekuwa ukijitokeza mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ili nchi yetu twende kwenye viwanda, unajikuta kabisa inabidi uende *BoT* ukaangalie pale ni vitu gani ndani ya nchi hii tunaagiza zaidi? Sasa ukiangalia kwenye ripoti ya *BoT* utaona Tanzania tunaagiza zaidi mafuta, sasa kwa taarifa ya mwaka 2018 tuliagiza mafuta ya 1.5 *billion USD*. Sasa hii takwimu unazungumzia karibu trilioni tatu na kitu za Kitanzania, hiyo ni uagizaji wa bidhaa nje. *Substitute* yake ni nini, ni gesi. Serikali ina wawekezaji kwenye viwanda vya gesi ili kusaidia kupunguza kupeleka fedha nje. Kuna vifaa vya viwandani, tulitumia milioni 600 dola, sawa sawa na trilioni mbili. Ukienda vifaa vya magari pamoja na uagizaji wa magari, vifaa vya umeme, hivi kila kimoja tulitumia zaidi ya milioni 600 dola sawa sawa na trilioni 1.8 kwa kila mojawapo, utakwenda kwenye madawa na kadhalika. Sasa ukiangalia ile takwimu ya vitu tunavyoagiza nje ndiyo majibu sahihi ambayo Serikali ya Viwanda ilipaswa ijikite. Sasa kwenye vifaa vya viwanda, uagizaji wa *parts* za magari na magari yenyewe maana yake tunatakiwa tuwekeze kwenye chuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye takwimu chini utaona namba nane *imports* tulizoleta zaidi utaona ni vifaa vya chuma maana yake hizi *aluminiums* ni *imported*. Mabati haya yanayoitwa *M-south* ni *imported from China*. Hii yote ni kama mtu ambaye hataki kufikiri sawa sawa ndiyo anaweza kuona kuiacha hii lakini hii *imports* ndiyo ilikuwa

inapaswa kuwa kipaumbele, *major major, I don't know* niseme nini, lakini ilitakiwa niseme ni *priority number one* za Serikali kuangalia sasa tuwekeze kwenye viwanda vya chuma ili tupunguze hii *imports*. Tuwekeze kwenye gesi ili tupunguze tupunguze uagizaji wa mafuta mkubwa kwa sababu fedha nyingi inapotea kwenye hizi *major imports*.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nieleze tu kidogo kuhusu athari za *corona* na biashara mipakani. Tumeona kwenye *clip* zinatembea; niliona moja ya Ngara, Watanzania sasa wanazuia magari ya nje yasingie nchini kwa sababu zile nchi zinazuia madereva wa malori Watanzania kupeleka nchi kwao. Tumeiona hiyo, tunaona *clip* zinavyotembea, sasa hapa kuna vitu vinavyopaswa vifanyike. Lazima Serikali ikubali kuwa na *coordinated approach* ya nchi za EAC kwa sababu hili janga la *corona* ni kama vita ya Idd Amini lazima tujifunge mkanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye *world analysis* wanakuambia *corona* itakwisha mwakani *mid of 2021* na itakwenda *far economic impacts* zake mpaka mwaka 2023. Kwa hiyo sasa na sisi lazima kwenye suala la kiuchumi kulinda biashara zetu, lazima na sisi tuangalie, yaani hatuwezi kuwa peke yetu kwamba sisi kama kisiwa tunajifunga kwamba tunaweza tukapambana sisi wenyewe, *no* haiwezekani. Kwa hiyo lazima sisi kama nchi tukubali kutumia hii *coordinated approach* ya kushirikiana na nchi jirani kuona tunawezaje kusaidia biashara yetu ikafanyika huko nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, ni kutumia dirisha hili la *World Bank* pamoja na *IMF* ambao wametoa fursa sasa hivi kwa nchi zote ambazo zinaathirika na uchumi kujaribu, mnaweza mkaenda ku-*restructure* mikopo yetu kwa maana ya deni la Taifa. Tunaweza tukaenda kukopa kwa bei nafuu ili kuweza kusaidia ku-*support* uchumi wetu. Sasa hizi ndiyo fursa ambazo hatupaswi kuacha kuzitumia. Ukiangalia kwenye uchumi moja ya athari kubwa ya *corona* ni pamoja na kushuka kwa bei ya mafuta, sasa hivi bei ya mafuta imefika mpaka dola kumi na kitu. Sasa ni wakati

mzuri kwa Serikali kutumia fursa hii kuagiza mafuta mengi ndani ya nchi ili wakati *price* ya mafuta inakwenda juu maana yake biashara ya mafuta tutakuwa tumewasaidia watu wetu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo utaona kabisa pamoja na hili janga ni tatizo, lakini vilevile lina fursa zake ikiwemo kuagiza chakula na tunaweza tukauza chakula kwa sababu watu wengi hawajazalisha kutokana na hili janga. Kwa hiyo ni vizuri Wizara ya Viwanda na Biashara ikajaribu kuyaangalia hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Stanslau Shing'oma Mabula, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba ajiandae.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi, lakini nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye anaendelea kutupa nafasi ya kuendelea kuishi na pili niishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa namna ambavyo imeendelea kuwa Serikali sikivu, Serikali ambayo inatambua zaidi maisha ya Watanzania na namna halisi ya kuweza kuwahifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kidogo juu ya Wizara ya Viwanda na Biashara, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na hongera kwa kuzaliwa najua leo ni siku yake muhimu na imekuwa bahati pia anawasilisha bajeti yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nizungumze suala la viwanda. Kule Mwanza tuna viwanda vya samaki takribani saba, kati ya hivi viwili vimefungwa na siyo vimefungwa kwa bahati mbaya. Tuna viwanda ambayo vimekuwepo na sasa hivi havifanyi kazi kabisa kama Kiwanda cha *TANNERIES* na vingine vinafanya kazi kwa uzalishaji wa

kawaida. Natambua Mheshimiwa Waziri amefanya kazi kubwa amepita kwenye viwanda hivi kikiwemo cha *MWATEX*, amekagua *TANNERIES* na yako mambo ambayo aliahidi kuyashughulikia na hakika tumeona amefanya hivyo, hii ni pongezi kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu nifahamu na niombe Mheshimiwa Waziri ni jambo la busara sana kama ambavyo wamendelea kufanya kwenye maeneo mengine. Sasa hivi Wizara ya Uvuvi imefanya nafasi yake kwenye kudhibiti uvuvi haramu ili viwanda hivi sasa vinapofanya kazi, vifanye kazi kulingana na matakwa ya kisheria, lakini na uhalisia ule ambao Watanzania tunataka tuuone. Kwa nini nasema haya, natamani sana kuona viwanda hivi vimeshuka sana uzalishaji wake. Sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri pengine apate muda kuvitembelea hivi viwanda vya samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua Mheshimiwa Waziri alikwenda Musoma, lakini ni kiwanda kidogo kulinganisha na viwanda vikubwa tulivyonyavyo Mwanza. Yeye kama Waziri wa Biashara atagundua biashara ime-*drop* kwa kiasi gani kwenye kiwanda cha samaki na atatumia maneno yao na matatizo yao waliyonayo akiunganisha na changamoto ambazo Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeshughulika nazo, tunaweza kupata jambo zuri sana la kusaidia viwanda hivi na tukaboresha kwenye sekta ya ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunazungumza viwanda ambavyo Mwanza vilikuwa vinazalisha, vilikuwa vina watumishi zaidi ya 6,000, leo tunaongelea watumishi wasiozidi 1,800 mpaka 3,000. Wengi wameenda kujiajiri, ni jambo zuri, lakini tunatamani sasa kwa sababu tumefufua vyombo vyetu vya usafiri, sasa hivi Victoria itakapoanza kazi, na *MV Butiama*, tunagetegemea kuwa na uzalishaji wa hali ya juu. Vyombo hivi sasa vika-*connect* kwenye shughuli ya uzalishaji na usafirishaji ili tuone matunda yanayotokana na shughuli hii kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANNERIES* tujue sasa leo ni lini watakuwa tayari kuhakikisha mashine zinapatikana, Chuo

cha *DIT* kiko pale, watoto wako pale wanajifunza, lakini hawana sehemu ya kwenda kufanya mazoezi. Kuanzishwa kwa kiwanda hiki cha *Mwanza TANNERIES* kutawasaidia sana wao, lakini kutasaidia kama ninavyosema kwa sababu kiwanda hiki ni kiwanda ambacho kinazalisha mazao yake kwa kutumia ngozi. Ni wakati gani ngozi zetu sasa zitapata thamani, ni kuhakikisha kwamba kiwanda hiki kinafanya kazi na tunaendelea mbele kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili Mheshimiwa Waziri ambalo ningependa niliongelee, ni juu ya mfumo wa *online business*. Huu mfumo kwa sasa unafanyiwa majaribio kule kwenye Manispaa ya Ilala na Jiji la Mwanza. Mfumo huu tunatamani sana tuone unaondolewa changamoto nyingi ulizonazo. Leo mtu anaweza kuingia akapata namba ambayo itamsaidia kwenda kulipia, akipata namba ya kwenda kulipa anaweza kuchukua siku tatu mpaka wiki mbili matokeo yake analipa lakini hataonekana kwenye mfumo kama amelipa. Sasa hii inaweka changamoto nyingi na ni mfumo ambao wafanya biashara wameanza kuufurahia, lakini unaonekana una changamoto ambazo ni lazima zifanyiwe kazi haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ukiangalia vizuri unaweza kuona mfumo huu huu sisi hapa tunayo *Finance Act* lakini haiendani na *bill* zilizowekwa kwenye mfumo. Kwa mfano, ukichukua leseni ya *hardware* kwenye *Finance Act* inasoma Sh.200,000 lakini kwenye mfumo imewekwa Sh.300,000. Ukichukua kwa mfano kwenye vifaa vya simu na simu huku kwenye *Finance Act* inasema Sh.200,000 kule kwenye mfumo inasema Sh.80,000. Kwa hiyo pengine kuna fedha nyingi tunapoteza kulingana na namna ambavyo mfumo wenyewe umekuwa *treated*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tuangalie mfumo huu na wataalam wetu wajikite sana katika kuhakikisha kwamba wanawasaidia wafanyabiashara ili waende sambamba na mabadiliko ambayo tunayataka. Mabadiliko haya yanatusaidia sana kulinda upotevu wa fedha nyingi

ambazo leo Mheshimiwa Rais pamoja na mambo mengine yote amejikita katika kuhakikisha tunasaidia jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, niseme kidogo kuhusiana na janga la *corona*. Ni lazima wenzetu wafahamu na sasa hivi kila mmoja kwenye nchi hii amekuwa ni mtaalam wa kuzungumza tafsiri za *corona*. Ni lazima kama Watanzania, kama nchi tubadilike. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu amezingatia utaalim na watu alionao wanaomshauri kuanzia Baraza la Mawaziri chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Rais mwenyewe. Kuna kitu kinaitwa *security analysis*, kwa watu waliobobea kwenye majukumu na kwenye kazi hizi wanafahamu. Hivi leo tukisema tuna-*lockdown* ni wakati gani tutaruhusu watu wangapi ambao watakuja kutoka kama bomu kwa ajili ya kutafuta riziki? Faida yake na hasara zitakuwa ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumza masuala haya, ni lazima tuangalie, ni vizuri tukasema sana kwa sababu Watanzania tunapenda kusema sana, lakini tunaposema ni lazima tujitambue kwamba hili ni janga na janga hili wataalam waliopo wamelifanyia utafiti na wakaona. Jambo zuri sisi tunao wataalam bora kabisa hata pengine kuzidi walioko Ulaya, wanapofanya *analysis* ya jambo wanatoa jambo ambalo linakwenda kutusaidia. Leo tunaona zipo baadhi ya nchi bila kuzitaja majina zilizokuwa zimefanya *lockdown*, masaa 16 baada ya *lockdown* watu waliokwenda kule na maambukizi yaliyotokana na mkusanyiko ule wa ghafla imekuwa ni mara dufu ya lile la kawaida. Sasa ni lazima tujue hizi ndizo zinazoitwa *security analysis*, lazima tuziangalie kabla ya kufanya maamuzi. Mheshimiwa Rais wetu amezingatia hili na anastahili pongezi na heshima ya kuwalinda Watanzania kwa mfumo ambao ameona unafaa kulingana na vyombo vyake ambavyo vimemshauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naomba niunge hoja mkono kwa asilimia mia moja na kazi iendeleo kuchapwa kama kawaida. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba na Mheshimiwa Injinia Stella Manyanya ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Kwanza kabisa nimpongeze Waziri Mheshimiwa Bashungwa. Kwa muda mchache ambao umeshika nafasi hii kwa kweli ameitendea haki na ameonesha kabisa kwamba vijana wakipewa nafasi wanaweza kufanya kazi nzuri, hongera sana. Nimwahidi mjomba wangu kwa moyo alioonesha kwa wafanyabiashara, tuko na yeye na Jimboni kwake tutahakikisha anarudi tena na rafiki zangu wa Karagwe wananisikia, wasikupingepinge, wakusaidie upite bila kupingwa ili uendelee kuchapa kazi zako kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumze kuhusiana na suala lile ambalo linaonekana mitandaoni, mimi nafanya biashara ya usafirishaji. Mheshimiwa Waziri au Serikali ione ni namna gani wanaweza kukutana na hizi nchi hasa mbili Rwanda na Uganda. Kuna tatizo kubwa sana yaani madereva wa Tanzania na magari ya Kitanzania kwenda kwenye hizi nchi, inaonekana kama sisi ndio tunaongoza kuwa na *corona* dunia nzima, lakini wao kuja Tanzania hakuna masharti. Ndiyo maana jana kama uliona *clip* inafika mahali watu wanaona labda wajichukulie sheria mkononi kwa sababu yaani Watanzania kuingia kwenye zile nchi wana *Corona* ila wao kuja kukaa hata mwezi wanasubiria makontena hawana madhara ya *Corona* hata wakirudi kwao hakuna tatizo. Kwa hiyo, ni vizuri watu wa diplomasia na Wizara ya Viwanda na Biashara muangalie namna nzuri mliweke hili suala vizuri ili tuendelee kufanya biashara kama tulivyokuwa na upendo kama zamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napenda kumshauri Mheshimiwa Waziri, najua dhamira ya Rais ilikuwa ni nzuri sana kusema tunyang'anye watu viwanda, ilikuwa ni nzuri. Pia ugonjwa huu wa *Corona* umetuonyesha dhamira



ya Rais alikuwa anataka tuwe na viwanda vyetu hata ikitokea tatizo tuwe na uwezo wa kujiendesha wenyewe angalau hata kwa miezi mitatu bila kuagiza vitu mataifa ya nje. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya Rais najjuliza ni kwa nini mnakuwa na kigugumizi kwenye kutafsiri. Najua tumenyang'anya watu viwanda leo miaka inaenda mitatu, minne maamuzi hayatoki. Ni mambo mepesi tu, tuseme ukweli tu kwamba Serikali iliyopita haikuwa na mfumo wa kukuzi viwanda vya Tanzania kila kitu tulikuwa tunaagiza nje hata kama wewe ungekuwa na kiwanda usingeweza kukiendesha ni lazima angalau ukope hela ukalete *material* kutoka nje uweze kuuza upate faida hata kulipa riba za benki. Kwa Serikali hii Mheshimiwa Waziri chukueni maamuzi, waiteni wale watu mliowanyang'anya viwanda wale ambao wanaweza kuendesha viwanda wafungulieni kuliko kufunga kwa sababu Serikali yetu ya Awamu ya Tano inataka viwanda vifanye kazi. Leo viwanda labda hata 10, 15 wangekuwa wameonyesha nia na wakavifungua haya matatizo tuliyonayo yakidumu miezi mitatu tutaagiza wapi vitu na viwanda vyetu vimefungwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nakuomba Mheshimiwa Waziri ukisaidiana na Waziri wa Uwekezaji hebu fikieni maamuzi mnaweza kuwaita, kama Rais alishaonyesha nia tunyang'anye viwanda basi waiteni wale walio na nia ya kuweza kufanya kazi na walio na uwezo wa kuviendesha wapewe mikataba mipya waendeshe kuliko kufunga tu mago-down vitu vya watu kule ndani vinaharibika na Serikali haichukui hatua yoyote. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri utakaposimama sijui kama umejipanga vizuri lakini ni kwa nia nzuri tu na wafanyabiashara wako tayari kuunga mkono Serikali ya Awamu ya Tano ni vizuri ukatoa majibu hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwenye Jimbo langu tunalima sana mananasi. Wakati wa Mheshimiwa Mwijage tulikuwa tumefikia hatua nzuri ambapo alikuwa ametutafutia watu kutoka India kwa ajili ya kuja kuwekeza. Sasa sijui Ofisini

kwako mmefikia wapi Mheshimiwa Waziri. Tuko vizuri na mananasi yanaoza tu, tutafutie masoko watu wangu waweze kulima na wapate sehemu ya kuuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme kidogo kuhusiana na hili suala la *Corona* kwa sababu muda ni mchache. Kwa kweli nachelea kusema, najua wataalam tumekuwa tukiwapitishia bajeti mara nyingi tu, mambo ya utafiti, Maprofesa na kadhalika lakini *term* hii inaonekana wamefeli kabisa 100% kwa kuwatizama tu hata mpaka leo hakuna anayeonyesha dalili yoyote ya kutusaidia. Sasa nafikiria tuangalie uwezekano wa jinsi gani hata tiba mbadala hizi tuzikuze yaani kiwe kama kiwanda kwa sababu watu wana mawazo mazuri. Leo angalia kitu kilichoshusha *Corona* Tanzania hapa si ni kujifukiza, imani kubwa imerudi kwenye kujifukiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani kama wiki moja, mbili, tatu kabla ya *Corona* kulikuwa na operesheni kubwa sana ya waganga wa kienyeji. Mungu saidia imekuja leo hii *Corona* hata Polisi wenyewe wanafukuzwa. Akifika kwenye msako anauliza vipi unajua kufukuzwa, anakula ubani kwanza halafu ndiyo anaanza kuuliza mambo mengine. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara, tuone namna ya kuwakuzwa hawa watu, tusiwaone kama watu ambao hawana mawazo. Wana uwezo mkubwa kabisa kama tutaweza kuwasaidia, wala msipuuze. Kama mnapuuza leo nyungu hizi tukizigeuza humu watu hamtatoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri azingatie hilo hasa la wafanyabiashara ambao Serikali imewanyang'anya viwanda. Mheshimwia Waziri wako tayari hata kesho na kwa kuwa tunaamini na tutakusaidia wewe unapita bila kupingwa chapa kazi, waite uwape *direction* nini unataka. Kama walikosea kule nyuma watu wanapewa maonyo, kaeni nao. Mbona kuna wahujumu uchumi walikuwa magereza mmekaa nao kwa

DPP mambo yanaenda vizuri, kuna tatizo gani kukaa na hawa wafanyabiashara?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja na mimi nakuombea sana Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Waziri ambaye ulitokana na kutumbuliwa kwa mtu umeonyesha akitumbuliwa mtu akija mpya watu wanakusifu. Hakuna hata mmoja amekuponda, chapa kazi Mungu akubariki sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

### MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu kwa hotuba nzuri na kwa jinsi mnavyofanya kazi nzuri kwenye Wizara hii. Kweli kuna mabadiliko makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nawapongeza kwa namna ambavyo Serikali inaendelea kuyaendeleza mazao ya kimkakati. Kahawa ni zao mojawapo ya mazao ya kimkakati. Ili kuweza kumpatia mkulima bei nzuri ni lazima Wizara ya Viwanda na biashara watanue wigo wa Masoko, waendeleo kutafuta Masoko ndani na nje. Mwaka jana kwenye mijadala tulitoa mapendekezo haya. Je kwa sasa kuna Masoko mapya ya zao la kahawa ili mkulima wa kahawa aweze kupatiwa bei nzuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, mkoa wa Kagera umepakana na Uganda, Kenya, Rwanda, Burundi. It is strategically placed. Ili kufungua Mkoa kiuchumi na kukuza mapato ya nchi ni vema kujenga Masoko mazuri, makubwa ya kileo ya kimkakati pale Mtukula, Murongo Kabanga na Rusumo yakiwa kwenye mipaka na Uganda, Uganda, Burundi na Rwanda respectively. Ni lini Masoko hayo yatajengwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipatia fursa hii kuweza kutoa mchango wangu katika Wizara hii ambayo ni miongoni mwa Wizara muhimu sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wake wote kwa kutayarisha na hatimae kuwasilisha kwa utaalum wa hali ya juu katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia Wizara hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni umuhimu wa kuimarisha Viwanda Vidogo. Napenda kuipongeza Serikali yetu kwa azma nzuri sana ya kuulekeza uchumi wa nchi katika maeneo ya Viwanda nchini. Viwanda ni eneo/sekta kubwa katika nchi. Viwanda vinaweza kuongeza ajira za watu wa rika na ujuzi tofauti. Ili kulifikia rika la watu wa chini kijira nashauri Serikali iongeze juhudi za makusudi kuimarisha Viwanda vidogo vidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Viwanda vidogo ndio sekta muhimu sana katika kuwapatia wananchi wajasiriamali ambalo ni kundi kubwa sana katika nchi hii. Hivyo kufanikiwa katika kuimarisha mpango wa viwanda vidogo Serikali itakuwa imeweza kufanikiwa kutoa ajira kwa kundi kubwa sana la vijana wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassimu Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waziri, Manaibu Waziri na Viongozi wote wa

Wizara ya Viwanda na Biashara, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Uongozi Wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza Mhimili wa Bunge hasa katika kipindi hiki tunapopambana na janga la COVID-19.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka minne, Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara, imetekeleza miradi mingi ya viwanda na pia kuboresha mazingira ya biashara (*Blueprint*) kwa kuondoa tozo, ada na kodi ambazo zimekuwa kikwazo katika shughuli za uchumi. Kupitia *Blueprint*, Serikali inatambua umuhimu wa kuweka mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji ili kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato. Pamoja na jitihada za Serikali, bado kuna changamoto za viwanda vya kuongeza thamani ya mazao yetu vijijini na pia kuna changamoto za uhakika wa masoko ya mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali iendelee na msukumo wa kujenga viwanda vya mazao ili kuweza kuongeza thamani hapa nchini na pia kuzalisha ajira. Kutokana na neema ya kijografia, nchi yetu inazalisha zao la pareto bora Afrika, pia ni wa pili duniani, lakini Wakulima wa pareto bado wanakosa soko la uhakika na lenye ushindani. Serikali ichukue hatua za kutafuta wawekezaji wa viwanda vya viatilifu ambavyo mahitaji yake ni makubwa hapa nchini na hata soko la nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, pPia nchi yetu ina neema ya madini adimu duniani kama vile *NIObium* ya Pandahill Mbeya, ambayo kuna fursa ya kujenga kiwanda cha kuchakata hayo madini ili kutengeza *FERRONIObium* ambayo mahitajika yake ni makubwa hapa nchini na pia nje ya Tanzania. Hii ni fursa ya kuwa kiwanda cha kwanza Afrika na cha nne duniani na pamoja na fursa za kichumi, kutakuwa na fursa kubwa ya kuongeza ajira na nchi yetu kuwa kiini

cha viwanda hivi duniani kutokana na uwepo kwa uwingi madini ya *NIOBIUM* na CHUMA hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki tunapopambana na janga la *coronavirus (covid-19)*, tumejifunza umuhimu wa kuwepo kwa mikakati mbadala kama vile kufanya kazi kwa kutumia TEHAMA. Pia napongeza mkakati wa Serikali kwa kuanzisha Soko la Bidhaa, 'The *Tanzania Mercantile Exchange (TMX)*'. Wizara ya Viwanda na Biashara iwe mstari wa mbele kuimarisha hili Soko la bidhaa ambapo wauzaji na wanunuzi wanakutana na kubadhilishana bidhaa na fedha katika mtindo wenye mpangilio na utaratibu maalumu. Kuanzishwa kwa soko la bidhaa kutamwezesha mkulima kuweza kuuza mazao yake katika utaratibu unaoeleweka bila kulanguuliwa. Pia soko la bidhaa linatupa mwanga na mwanzo mzuri wa kuboresha Soko la Madini kuwa sehemu ya TMX.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sina budi kumshukuru sana Allah kwa kuniwezesha kuchangia Wizara hii, pamoja na hayo napenda kuchangia zaidi kwenye Viwanda vya mazao ya Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni Nchi ya tatu (3) katika nchi za Afrika zenye Mifugo mingi , nilitegemea kutakuwa na ufafanuzi mzuri juu ya kufanya kazi Viwanda vilivyotajwa katika ukurasa wa 12 wa hotuba hii kwamba kuna Viwanda 145 vya usindikaji wa mazao ya kilimo (mifugo). Nilitaka kujua ni tani ngapi za nyama nchini zimeweza kupatikana na jee uzalishaji huo unaweza kutosheleza mahitaji ya soko. Kutaja idadi ya viwanda tu haitoshi ni vyema wakulima wa nyama waone ni kwa kiasi gani wanauza Mifugo yao , wakati huo huo Serikali imeweka idadi maalum ya ufugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningengezeza ni suala la mazao. Kama unavyojua kwamba yako Mazao yanaonekana barabarani yanazagaa

bila ya kuwa na soko , mfano mananasi, maembe, nyanya, mboga za majani, ni vizuri sana Serikali ielekeze zaidi nguvu zake maeneo hayo kuweka Viwanda ili wakulima waweze kusindika mazao yao bila ya usumbufu mkubwa unaopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuweka *record* sahihi za mauzo ni vyema Wizara ingetueleza ni zao gani linaongoza kwa mauzo ndani na nje ya Nchi ili wakulima waweze kufanya mlinganisho.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pamoja na mambo mengine kuwapongeza kwa utendaji mzuri. Nina ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Umilikishwaji wa ardhi kupitia TIC. Bado mlolongo ni mreefu sana, mwaka jana ilinibidi kuingilia kati Hati ya kiwanda cha kugema gundi cha ATY kule Mafinga baada ya suala hilo kuchukua zaidi ya mwaka. Ushauri wangu ikiwa umiliki ni kwa mfumo wa derivative rights na tayari vyombo vyote vinakuwa vimepitisha jambo husika je do we need national land allocation committee ambayo inakaa quarterly? Ushauri wangu ikiwa mwekezaji amepitishwa na ngazi zote za kisheria, tupunguze mlolongo ili Hati zitoke kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu masuala ya ardhi yapo Wizara ya Ardhi lakini ninyi ndo machampion wa kuelekea uchumi wa viwanda, you are the Engine.

Mheshimiwa Naibu Spika, linafanana na hili ni umiliki kwa hati za kimila, ikiwa mwekezaji anahitaji eneo lakini wamiliki wanalimiliki kwa hati ya kimila, sheria zinakinzana na hivyo kuchelewesha maamuzi, mfano Kampuni ya kuzalisha umeme ya Mwenga Hydro ya Mufindi toka mwaka 2015 wanafuatilia Hati kwa ajili ya kuwekeza uzalishaji wa Umeme wa upepo katika kijiji cha Nundwe lakini mpaka leo hawajapata, hizi ni cases ambazo ninafahamu kwa sababu ni wawekezaji ambao wapo kwetu, nashauri katika mambo ambayo Blueprint inapaswa kuyashughulikia ni suala la

upatikanaji wa Hati kwa wakati kwa wawekezaji, TIC ipo kwa Waziri Mkuu lakini *you are the engine*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sukari. Wakati wa mapendekezo ya mpango niliwasilisha mapendekezo na baadae nikamuandikia Mheshimiwa Waziri barua na *paper* nikishauri namna ambayo tutaondokana na kero ya sukari kupanda bei kila mwaka kwa ujanja ujanja wa wafanyabiashara, bado naamini ushauri wangu ambao kila bajeti nimekuwa nikiutoa, unaweza kusaidia sana, kwa sababu kwa mfano Mkulazi mwaka wa nne sasa, ndo maana nikashauri tuwekeze katika *factories* za *capacity* ya tano 5000 na 10000 ambazo ujenzi wake ni muda mfupi na vinaweza kujengwa maeneo tofauti tofauti ya nchi, naomba kuwasilisha.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuiona siku ya leo nikiwa na afya njema. Na kuniwezesha kuandika mchango wangu kwenye Wizara hii. Pili nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Bashungwa kwa kazi kubwa anayo ifanya katika kusimamia Wizara hii pamoja na changamoto mbalimbali. Nampongeza kwa kuweza kumdhahirishia Mheshimiwa Rais kuwa vijana wakiaminiwa wanaweza.

Mheshimiwa Spika, kwa leo mchango wangu kwanza naomba kuungana na ushauri wa kamati ya viwanda na biashara katika kuisimamia serikali na kuishauri kwa manufaa ya Taifa letu. Kwa kuwa lengo la Taifa letu ni kuelekea kwenye uchumi wa viwanda na uchumi wa kati, hivyo basi Serikali ni lazima ihakikishe Wizara hii inakuwa na bajeti ya kutosha hasa kwenye miradi ya mendeleo. Sambamba na kuiwezesha Wizara kulipa fidia kwa yale maeneo yaliyo twaliwa na Serikali kwa lengo la uwekezaji (EPZA).

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi kikubwa Wizara hii hushughulika sana na uwekezaji wa watu binafsi yaani wawekezaji katika sekta za Viwanda. Hivyo utaona kuna umuhimu mkubwa sana wa kuweko kwa mazingira mazuri



ya uwekezaji nchini. Napenda kuishauri Serikali kushirikiana na Wizara ya uwekezaji ili kuona ni kwa namna gani tunawasaidia wenye Viwanda nchini, kwani bado kuna watendaji wachache Serikalini wana tabia ya urasimu usio kuwa na lazima wa njoo kesho, njoo kesho.

Mheshimiwa Spika, Suala la bei ya sukari bado linaoneka kwa upande wa Serikali limeshashindikana, kwani sasa limezidisha tatizo baada ya wafanya biashara hasa wa mikoani kuacha kuagiza sukari, kwa kuogopa bei elekezi kwenye mikozi yao ambapo bei hiyo haina uhalisia wa mazingira ya maeneo yao. Bei ya jumla ya sukari kwa mkoa wa Dar es salam bado iko juu, hivyo si rahisi kwa mikoani kuwa na bei elekezi na ikatekelezeka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubinafsishaji wa viwanda na urejeshwaji wa viwanda vya umma nchini. Jambo hili limezingirwa na changamoto nyingi sana hivyo basi Serikali ni lazima ije na mkakati maalumu wa kukabiliana na changamoto hizo. Hizi ni kama:-

1. Changamoto za kimikataba zilizo ingiwa na wanunuzi wa viwanda hivyo.
2. Kupitwa na wakati kiteknolojiwa kwa baadhi ya viwanda hivyo.
3. Hali ya miundombinu ya viwanda hivyo kwa majengo, mashine, na miundombinu zingine mbali mbali.
4. Utaalamu na ujuzi unao hitajika kwa watumishi ili kuendesha viwanda hivyo. Kwa muktadha huo utaona ugumu uliopo katika kufufua viwanda hivyo.

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na viwanda nchini tunahitaji pia kuwepo kwa nguvu kazi ya kutosha na yenye ujuzi mahususi kwa Viwanda hivyo. Hivyo naiomba Serikali kufungamanisha uwepo na Viwanda na wataalamu wa uendeshaji wa Viwanda hivyo, hapa nazungumzia uwepo wa mafundi sadifu na mafundi mchundo. Hapa Serikali ni

lazima ione umuhimu wa kuwa na Chuo cha VETA kila Wilaya ili kuzalisha nguvu kazi ya kutosha kuhudumia Viwanda vyetu vidogo na vikubwa. Mfano Wilaya ya Liwale inayozalisha kwa wingi zao la korosho na ufuta, lakini iko mbali sana na Makao Makuu ya Mkoa ambako kuna Chuo cha VETA. Hivyo vijana wengi wanakosa ajira kwa kukosa ujuzi na elimu ya VETA.

Mheshimiwa Spika, changamoto za maghala katika Halmashauri nyingi nchini ni kubwa sana, kiasi cha wakulima kupoteza kwa kiasi kikubwa kwa mazao yao. Halmashauri ya Liwale ni miongoni mwa Halmashauri zenye uhitaji mkubwa sana wa maghala. Jukumu la ujenzi wa maghala nchini kuachiwa Halmashauri sio jambo jema sana kwani Halmashauri nyingi nchini hazina uwezo huo. Mfano Halmashauri ya Liwale kila mwaka zao la korosho linakubwa na changa moto hii ya uhaba wa maghala. Hivyo naiomba Wizara kushirikiana na Wizara ya Kilimo kutupatia fedha Halmashauri ya Liwale kwa ajili ya ujenzi wa maghala.

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikupongeze kwa uendeshaji bora wa Bunge lako Tukufu na kwamba umelijengea heshima Bunge letu katika kipindi chote cha miaka mitano. Aidha nampongeza sana kwa moyo mkunjufu Mheshimiwa Rais wetu kwa uongozi wake imara ambao umeipandisha nchi yetu kuakaribia uchumi wa kati na kujenga heshima kubwa ya nchi yetu. Pia nakupongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri na kubwa unayoifanya ya kusimamia sekta ya Viwandq na Biashara katika nchi yetu. Chapa kazi kijana tuko pamoja.

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Serikali yangu ya CCM katika mambo mawili tu kwa umuhimu wa kipekee. Jambo la kwanza niishauri Wizara kuanzisha kitengo maalum katika Wizara kitakachoratibu na kuwaunganisha wakulima na Asasi za Fedha ili kupata mikopo kutoka mabenki ya biashara kwa kutumia mazao yao kama dhamana. Nje ya kuwa na mfumo rasmi wa uratibu wa kuwaunganisha wakulima na mabenki itakuwa vigumu sana kwa wakulima

wa vijijini kupata mikopo kwani wengi hawana dhamana zinazokubalika.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili niishauri Serikali kuanzisha au kuweka mfumo rasmi wa taarifa za masoko katika kila ilipo Ofisi ya Kata ili wakulima waweze kupata taarifa zinazohusu mazao yao ya kilimo, mifugo, uvuvi, na kadhalika. Mathalani Mfumo wa Taarifa za Masoko ya Mifugo (*Livestock Information Network and Knowledge System - LINKS*) ipelekwe moja kwa moja katika ofisi za kata ambako kuna wakulima wengi hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Spika, awali nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri. Pia nawapongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa utekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi wa CCM.

Mheshimiwa Spika, pili, katika mchango wangu wa mwaka jana nilipongeza Serikali kwa Mkakati wa Ujenzi wa Viwanda ili kufikia Uchumi wa Kati mwaka 2025. Narudia tena kuipongeza Serikali kwa Mkakati huo. Naishauri Wizara iweke mkazo katika uwekezaji wa Viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana ndani ya nchi. Mfano jasi, makaa ya mawe, mazao ya chakula, mazao ya biashara na kadhalika. Vipatikane viwanda vya saruji, vigae, viwanda vya wanga, minofu ya samaki na kadhalika. Uwekezaji wa viwanda vinavyotumia malighafi za ndani utatupa tija maradufu; ajira viwandani na uzalishaji wa malighafi.

Mheshimiwa Spika, tatu, katika Jimbo la Bagamoyo kuna maeneo ya *EPZ* ambayo hayajalipiwa fidia sasa miaka 12. Mheshimiwa Rais alipokuja Bagamoyo kufungua Kiwanda cha matunda Elven Mapinga, aliagiza kuwa wale wananchi wote ambao maeneo yao hayajalipiwa fidia warudi katika maeneo yao na wayaendeleze. Ila maagizo hayo ya Mheshimiwa Rais hayatekelezwi kwa vile Halmashauri ya

Wilaya inawazuia wananchi kupima maeneo yao. Pia wale ambao wangependa kuyauza maeneo yao pia wanakatazwa kwa hoja kuwa *GN* ya Serikali bado inayatambua maeneo hayo kuwa ni ya *EPZ*. Namuomba Mheshimiwa Waziri aondoshe kikwazo hiki kwenye utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Rais. Ni miaka minne sasa tangu Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri asimamie *GN* itoke kuondoa toka *EPZ* maeneo ambayo hayajalipiwa fidia katika vijiji vya Zinga, Kondo, Mlingotini na Kiromo. Pia *GN* iondoshe katika *EPZ* maeneo yaliyo katika Mradi wa *EPZ II* (hekta 3,338), ili wananchi waendeleze maeneo yao kwa amani na kwa wale watakaopenda kuuza maeneo yao, basi wauze bila buguza. *EPZ II* inajumisha maeneo yenye makazi ya watu wengi ikiwemo Zinga kwa Awdhi, Zinga kwa Mtoro, Mlingotini, Kondo na Kiromo.

Mheshimiwa Spika, nne, kuna suala la mapunjo ya fidia kwa wananchi wanaopisha Mradi wa Bandari katika vijiji vya Pande na sehemu ya Mlingotini. Wananchi 687 wamehakikiwa na Mthamini Mkuu wa Serikali kuhusu mapunjo ya fidia zao tangu Januari 2017. Naiomba Serikali iwalipe wananchi hawa fidia zao stahiki kufuatana na maelekezo ya Mthamini Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, tano, kuna suala la makazi mbadala kwa wananchi wanaopisha mradi wa Bandari Bagamoyo. Wananchi wa Pande na Mlingotini waliahidiwa makazi mbadala katika Shamba la Kidagoni Bagamoyo kwa barua ya Mkurugenzi Mkuu wa *EPZA* ya tarehe 20.01.2014. Vijiji hivyo vina jumla ya kaya 460 zenye wakazi takriban 1,670. Wananchi hawa wanapoamriwa kuondoka wanaenda wapi? Naiomba Serikali yetu adhimu iwapatie makazi mbadala wananchi hawa kama vile walivyoahidiwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu

wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri mno ambayo amekuwa akiifanya katika nchi hii. Niendeleo kumpongeza Waziri Mheshimiwa Bashungwa, Naibu Waziri Mhe. Eng. Stella Manyanya, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri sana katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sera ya Viwanda. Kwa kuwa Serikali hii ya awamu ya Tano imeamua kuwa na Sera ya ujenzi wa viwanda vya kati na vidogo kwa ajili ya kujenga uchumi wetu. Nipongeze Serikali kwa kuanza kupunguza changamoto zilizokuwa zinajitokeza katika viwanda vyetu, ikiwapo na tozo nyingi zilizokuwa ni kero kubwa katika biashara ya viwanda Nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu ilipofanya ziara kutembelea baadhi ya viwanda katika Mkoa wa kagera, tulikumbana na baadhi ya changamoto ambazo ni vyema Serikali ikajaribu kuchukua hatua, kwa viwanda vya samaki.

Mheshimiwa Spika, kwanza, Selikari ianze kuangalia suala la sheria zile za maziwa ili ikiwezekana ziwe sasa kwa sababu sheria zetu zimekuwa zikiwabana wavuvi wetu na wenye viwanda na kusababisha baadhi ya wafanyabiashara kuhamia nchi za jirani.

Mheshimiwa Spika, pili, baadhi ya viwanda bado kuna tatizo kubwa la umeme kuwa mdogo na kushindwa kusukuma mtambo.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuwe na mkakati wa kuwa na Ndege ya kusafirisha bidhaa zetu nje ya nchi, hii pia ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Spika, nne, vifungashio. Hii changamoto pia ni kubwa ni vyema Serikali ihamasishe wawekezaji wa vifungashio kwani wafanyabiashara wengi wanafuata nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa hivi nchi imekumbwa na hili gonjwa la *corona* nikupongeze sana

Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri sana unayoifanya kuhamasisha wenye viwanda Nchini kufanya kazi kwa ufanisi na kwa kutoa bei elekezi kwa bidhaa za barakoa na sanitizer. Pia kwa bidhaa hii ya sukari katika mwezi huu mtukufu.

Mheshimiwa Spika, niendeleo kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kutoa Houston katika kipindi hiki kigumu cha ugonjwa huu wa *corona* na jinsi anavyoendelea kutoa miongozo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu zaidi kumlinda kwa yote.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wa Viwanda na Watumishi kwa jitihada zao za kuendesha sekta hii muhimu. Naunga kwa moyo wa dhati hoja ya Sekta ya Viwanda. Tuweke nguvu zetu pamoja kwa ushirikiano mkubwa kuendeleza viwanda na biashara, sekta muhimu. Mungu Awabariki.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru sana kunipa nafasi ya kuchangia kwa maandishi kuhusu hoja ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza sana mheshimiwa Rais kwa kusimamia vyema agenda ya Tanzania ya viwanda kuelekea uchumi wa kati ifikapo 2025. Mpaka sasa tuna viwanda vipya vinavyozalisha bidhaa mpya kama ville Viwanda vya Marumaru (*Ceramics*), hizi bidhaa zilikuwa zikiagizwa toka nje hapo nyuma. Sasa hivi zinazalishwa hapa nchini na ajira zimetengenezwa. Lakini pia viwanda vya kuzalisha bidhaa tulizokuwa tunazalisha hapa nchini vimeongezeka na uzalishaji wenyewe umeongezeka. Ni imani yangu kwamba Mheshimiwa Rais ataendelea kuuwasha moto wa Tanzania ya viwanda na nchi lazima itasonga mbele.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana pia Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara pamoja na Naibu wake kwa uchapakazi wao na hivyo kumsaidia Mheshimiwa Rais ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, nitoe ushauri wangu kwa Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara hii haipati pesa kama tunavyopitisha pesa za bajeti yake kwenye Bunge lako Tukufu. Ukirejea taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge juu ya Wizara hii, utaona fedha zinazopangwa ni kidogo sana na bado zinazopelekwa kutoka Hazina nazo ni kidogo pia. Kwa mwaka wa fedha 2019/20 Wizara ilitengewa bajeti ya Tshs 100.38 bilioni, lakini mpaka Machi 2020, ilipelekwa Tshs 26.02 bilioni tu ambapo ni sawa na 25% ya bajeti iliyoidhinishwa. Ni kweli kwamba hii Wizara ni Wizara wezeshi, haijengi viwanda isipokuwa wadau wengine na wawekezaji toka nje ndio wanaofanya kazi ya kujenga viwanda.

Mheshimiwa Spika, kazi yao ya kuratibu na kujenga mazingira wezeshi haiwezi kufanyika bila Wizara kupata pesa za kutosha kufanya kazi hiyo. Naishauri Serikali ione umuhimu wa kupeleka fedha zote zinazotengwa na Bunge lako Tukufu ili Wizara iweze kusukuma mbele agenda ya Mheshimiwa Rais na Watanzania ya Tanzania ya Viwanda na Uchumi wa Kati ifikapo 2025.

Mheshimiwa Spika, pili, naipongeze Serikali kwa *Blueprint*. Lakini *Blueprint* peke yake haiwezi kufanya biashara iwe rahisi mpaka tutakapobadilisha baadhi ya sheria ambazo zinakwaza utekelezaji wa *Blueprint*. Naelewa zipo baadhi ya sheria zilizobadilishwa ili ziendane na *Blueprint*, lakini bado ziko sheria ambazo zinahitajika kuondolewa au kufanyiwa marekebisho. Serikali iliahidi kuwa ingeleta Bungeni sheria ya *Business Facilitation*, sheria hiyo mbona inakawia kuletwa Bungeni? Naiomba sana Serikali yangu sikivu ikamilishe haraka mchakato wa kuleta sheria hiyo ili sasa tuweze kuweka mazingira yetu ya biashara na uwekezaji kuwa ni bora zaidi,

na hivyo kuvutia wafanyabiashara na wawekezaji wengi zaidi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba kuishauri Serikali kuwaajiri Maafisa biashara sita katika kila Halmashauri zetu nchini.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali iweke mpango wa kuhamasisha *Blueprint* kwa wawekezaji ili kufikia malengo mahususi ya kuandaliwa kwake.

Mheshimiwa Spika, tatu, Serikali itoe maelekezo kwa Viwanda vya sukari kuwa na mawakala wakubwa wa sukari kwa kila Wilaya kama wanachofanya TBL, TCC, SBL, POPCORN, na kadhalika ili kukomesha ulanguzi wa sukari unaofanywa na menejimenti ya Viwanda vya sukari na mawakala wakubwa kikanda wa bidhaa hiyo. Mchezo huu nchini wa kuficha sukari umedumu kwa zaidi ya miaka saba sasa.

Mheshimiwa Spika, nne, naipongeza sana Serikali ya awamu ya tano kwa kuja na mpango wa kitambulisho cha Wajasiriamali hivyo basi ni wakati muhimu wa kufanya tathimini kubaini changamoto, faida, hasara, ili kuleta ufumbuzi wa kupata mafanikio zaidi.

Mheshimiwa Spika, tano, Serikali ione utaratibu wa kuweka kalenda ya vikao vya wafanyabiashara kwa ngazi ya Mkoa afanye Waziri, ngazi za Wilaya Mkuu wa Mkoa, kama alichofanya Mheshimiwa Rais mwaka jana kule Ikulu.

Mheshimiwa Spika, sita, Serikali ifanye tathimini ya maendeleo ya Viwanda vidogo 100 katika Halmashauri zetu nchini ili kubaini changamoto kwa kuwa ndiyo fursa ya ajira zilizo karibu kwa vijana ngazi za wilaya.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja 100%.



**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, Serikali itajenga lini kiwanda cha kuchakata zao la Tumbaku Mkoa wa Tabora Ili kuinua uchumi wa wakulima wa tumbaku, uchumi wa Mkoa na Taifa kwa ujumla?

Mheshimiwa Spika, Serikali ni lini itafufua kiwanda cha nyuzi Mkoa wa Tabora ambacho kinaendelea kuuza pale ili kusaidia kuchakata pamba inayolimwa kwa wingi Mkoa wa Tabora na Wilaya ya Kaliua.

Mheshimiwa Spika, nini mkakati wa Serikali kuokoa kiwanda cha Tanzania Biotech Production Ltd kinachotengeneza viadudu vya malaria kisifungwe kutokana na kukosa soko la kile kinachozalishwa.?? Hata makubaliano yake na Wizara ya Afya kununua *products*zake wameshindwa kutekeleza kati ya lita 676,000 zilizozalishwa tangu 2015 ni lita 96 tu zimechukuliwa tena kwa mkopo hii ni hatari sana kwa uhai wa kiwanda hiki muhimu sana.

**NAIBU SPIKA:** Sasa tunaenda upande wa Serikali. Tunaanza na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba atafuatiwa na Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, mtoa hoja ajiandae.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru sana kwa kunupa fursa hii. Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza, naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuniamini kwa mara nyingine na kunitewa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Nakushukuru sana Mheshimiwa Rais, wewe ni Rais, wewe ni baba, wewe ni mlezi na wewe ni kiongozi unatufundisha na nikuahidi kwamba sitakuangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nimshukuru sana nimpongeze ndugu yangu Waziri wa Viwanda na Biashara kwa hotuba yake nzuri ambayo kwa kweli imejitambulisha yenyewe na imejitosheleza na ndiyo maana unaweza ukaona kwamba mashambulizi si mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa leo kufuatia hotuba ya Waziri wa Viwanda nitajikita katika mambo mawili ambayo sisi kama Serikali wenzetu wamekuwa wakijitahidi kuonesha kama kuna jambo tunalikosea. Kuna kauli zimekuwa zikisemwa na kurudiwarudiwa kwamba Serikali inajali zaidi uchumi kuliko maisha ya watu na kwamba kipaumbele cha Serikali ni kulinda uchumi kuliko maisha ya watu. Niwaombe Watanzania walielewe jambo hili kwa mapana yake kwamba hata bila *Corona* kungetokea njaa peke yake dunia nzima ama nchi nzima ingekuwa janga linalotosha kuyumbisha dunia na ujumla wake. Njaa peke yake hata bila ugonjwa mwingine wa aina yoyote ilikuwa inatosha kuwa janga. Ukienda kusoma kwenye majanga ambayo yanajitokeza janga la njaa na leyewe lipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo wenzetu wanaoona kwamba Serikali inajali uchumi kuliko maisha ya watu wajue kwamba wanaongelea kitu kilekile kwa pande mbili tofauti, kwamba huwezi ukashughulika na janga kwa kutengeneza janga lingine. Huwezi ukatengeneza majanga mawili kwa mpigo ukaanza kuhangaika nayo yote kwa wakati mmoja. Wale ambao wamejaribisha kufanya kinyume cha jinsi ambavyo Rais wetu aliamua tangu mwanzo umeona jinsi ambavyo wanatengeneza majanga mengine na watu wamefariki si kwa *Corona* bali kwa sababu ya majanga waliyoyatengeneza. Kweli wale waliotengeneza majanga mengine wanastahili wafike vyombo vya kisheria kwa sababu wametengeneza majanga ya kujitakia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Rais wetu ameona mbali, ameona tuzingatie taratibu ambazo zinaweza zikatusaidia tukajihami na janga hili lakini bila kutengeza janga lingine. Leo hii mtu anaibuka tu na Watanzania wanaona kama hoja imetolewa, anaibuka tu mtandaoni anasema Dar es Saalam wamefungiwe na walipwe, hafafanui wakishafungiwa kazi zote zikasimama, kikakosekana kinachokusanywa na bila kukadiria kwamba hili jambo haujui mwisho wake ni lini kama Mheshimiwa Rais alivyosema hivi majuzi kwamba huenda tukaishi nalo; yeye anasema tu wafungiwe na walipwe, ukishawafungia na

ukaacha kukusanya akiba iliyopo ukasema ndiyo itakayolipa, haya sasa hebu fikiria ukifungia Jiji moja tu kama Dar es Salaam hivi unahitaji si chini ya trilioni 2.5 kwa mwezi kuwalipa watu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya weka na Majiji mengine kwa sababu ulishaona inaanza kudokoadokoa, utahitaji si chini ya trilioni 5 kwa mwezi kulipa, uone kwamba hawa ni watu wanaongea vitu vya ndotoni wanataka wavilete kwenye maisha ya kawaida ya kila siku. Ndiyo maana hata wao wenyewe hawajajifungia, hata wale waliosema Wabunge wao wasiingie humu, nawashukuru wale waliojiongeza wakaamua kuingia, hata wale ambao walisema wamewafungua hawajajifungia wapo tu kutii maelekezo yale wako wanadhura tu. Wanavyodhurura vile hata yale masharti ambayo tunayazingatia maeneo mengine yote wao hawayazingatii. Kwa maana hiyo hata watakaposema wanarudi kwa sababu hawakuwa karantini utatakiwa Kiti chako kiwakarantini kwa angalau wiki tatu hivi ili watuhakikishie usalama humu ndani kwa sababu kwa kweli hawajajikarantini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Spika alisema Wabunge wake wakae katika mazingira haya, mmelirudia mara nyingi sana jambo hili lakini hawa ambao hawako hata hapa na hawajajikarantini na hakuna mtu anayehakiki wako wapi, leo hii wakirudi wanasema walikuwa wamejikarantini, ni jambo la hatari sana kwa sababu wako wanadhura. Ukiangalia kwamba hata kwenye lile waliloliamua hawajaweza kutekeleza na wako chini ya 50 sijui wako wangapi hawajaweza kuji-*lockdown*. Hebu fikiria sasa namna unavyoweza ku-*lockdown* watu milioni 60, hawa ni watu ambao wanajua kile wanachokifanya na mimi naamini walikuwa wana mpango mahususi kabisa wa kutengeneza *crisis* kwenye nchi yetu na linalolengwa mimi naamini si lingine ni kutengeneza *crisis* kinachoumiza zaidi ni uchaguzi unaokuja, hilo ndiyo kubwa zaidi wanaloliwaza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa sababu Rais wetu ameona mbali mimi niwaombe Watanzania wasiwe

wanasikiliza miluzi mingine ambayo ina nia ya kupotosha taifa na hatujui mizizi yake imetoka wapi na hatuwezi tukakadiria kwamba imetoka wapi huenda ni watu wale wale ambao mara zote wamekuwa wakifeli kwenye vita vya uchumi ambavyo Mheshimiwa Rais alivianzisha. Lazima tuwe *focused*, tuzingatie yale ambayo tumeelekezwa ambayo yanaweza yakatusaidia kujihami kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiweza kufanya tathmini ndogo tu, nchi yetu *informal sector* ni zaidi ya asilimia 55; watu hawa hawana akiba, kile wanachozungusha ndicho wanachotumia. Leo hii ukitumia tu mifano ya maeneo mengine ambayo walishafika hatua ya kuwaweka wazee katika majengo ya kuwalelea, walishafika hatua ya kuwalipa hata watu ambao hawana ajira ukalinganisha kwamba na hapa unaweza ukafanya kitu cha aina hiyo ambacho mataifa mengine fedha zao wanazokusanya ni za kukuza mitaji utakuwa umekosea hesabu hiyo na utakuwa umekosea kuiga kitu sawa na wale watu ambao walikuwa wanaangalia mtihami mpaka anaangalizia jina la yule aliyekuwa anamwangelizia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuende na maelekezo aliyoyotoa Rais na ndugu yangu hapa alikuwa anachangia ameshatoka anasema igeni sijui mataifa gani, mataifa gani mimi nina rafiki zangu wako Kenya, Uganda, Rwanda, wao kule kwenye mijadala yao wanaambiwa viongozi wao waige anachofanya Rais Magufuli, huyu mwenzetu anasema tuige kule. Sasa kama vitu vingi mataifa mengi wanataka waige huku tuna lipi sisi la kuiga kule? Tuende na utaratibu wetu. Bahati nzuri sana hata ambayo tumeona tukiyatekeleza yanaleta mantiki na tumeona ambavyo yanaweza yakatusaidia. Tuhakikishe tunajihami bila kutengeneza janga lingine na tuhakikishe kwamba janga halikimbiwi. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika maeneo mengine...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele imegonga.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja na nakutakia kila la kheri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Engineer Stella Manyanya.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali yote, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia kuwa salama. Pia tunamshukuru kwa maamuzi yake kwa wale waliotangulia Mwenyezi Mungu aweze kuwarehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane sana na Waziri wangu wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Innocent Bashungwa kwa salama zote za shukrani ambazo amezitoa kwa wadau wote ambao wameorodheshwa. Itoshe mimi nisirudie badala yake niseme wote Wizara ya Viwanda na Biashara tuko pamoja naye na hayo ametuwakilisha sisi sote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa jitihada kubwa anayofanya kwa Watanzania lakini vilevile kwa imani aliyoweza kunipa katika kipindi cha miaka mitano. Nadhani kati ya Manaibu Waziri walioweza kukaa na Mawaziri wengi zaidi humu ndani na mimi ni mmojawapo; kuanzia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na sasa kwenye Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ile kukaa na hawa Mawaziri imekuwa kwangu ni elimu tosha ya kujifunza kila Waziri na utendaji wake. Ukifuatilia kwa ujumla wake unakuita kwamba wote wana nia ya kuhakikisha kwamba

wanatekeleza vizuri yale majukumu ambayo walikuwa wamekabidhiwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Innocent Bashungwa, kama ambavyo imezungumzwa ni kijana, kweli ni kijana wa umri lakini ni mzee wa hekima, ni mzee wa kazi. Kitu kikubwa ambacho leo nafurahi nikisimama hapa siku ambayo tunarudisha hesabu kwa tajiri wetu Mheshimiwa Rais, tajiri wetu Chama cha Mapinduzi juu ya utekelezaji wa Ilani kupitia ujenzi wa uchumi wa viwanda ni hapa leo tunafarijika kwa mara ya kwanza Bunge zima linasema kwamba Ilani yetu tumeitekeleza vizuri, ahsanteni sana. Wanasema mgaagaa na upwa hali wali mkavu, basi na sisi hatimaye kila tulipokuwa tunaambiwa hatukuchukua kwamba Wabunge wanatusema, tulikuchukua kwamba wanataka kuhakikisha kwamba Ilani inatekelezwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuliyaifanyia kazi mambo yote yaliyokuwa yanashauriwa, tuliongeza ushirikiano baina yetu sisi wenyewe kwenye Wizara, kuweka uwazi, kuhakikisha kwamba wote tunafanya kama timu na leo naamini hata wenzetu ambao wanatuangalia kupitia vyombo vya habari, lakini wengine wamejifungua tu huku wanasikiliza hali itakuwaje, leo Wizara ya Viwanda na Biashara inafuraha kubwa sana. Tunasema ahsanteni sana, ahsate sana Naibu Spika na utupeleke pia salama na kwa Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini haya yote yamewezekana pia kwa sababu ya usimamizi madhubuti kutoka kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais, mama yetu Samia Suluhu, Mheshimiwa Jemedari wetu, kule Ruvuma sisi tunamuita *lidoda*, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana kwa kutuweka pamoja, kutuunganisha kati ya Wizara na Wizara kwa sababu Wizara hii haiwezi kufanikiwa kama Wizara nyingine hazitatoa mchango wake katika kuhakikisha kwamba inawezesha Sekta ya Viwanda na Biashara kufanya vizuri. Tunasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi kwa hawa ndugu zetu ambao leo hapa hawapo, nawapongeza kwanza wale wa upande wa pili walioweza kushiriki nasi mpaka mwisho kwenye bajeti hii lakini niseme tu kwamba katika vita woga ni adui namba moja, woga ni kushindwa mara mbili, lakini unapokuwa na askari ambaye anakimbia vita huyo askari hafai kabisa. Huyo askari akikimbia vita anapelekea wale askari wengine wapate woga washindwe kutekeleza majukumu yao inavyopaswa matokeo yake na huko anakoenda anaweza akakamatwa na adui na akatoa hata siri za wale ambao ni askari wenzake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wenzetu CHADEMA kutoendelea na bajeti safari hii eti kwa sababu ya kisingizio cha *Corona*, wapi hakuna *Corona*, kila mahali ipo. Ni tabia zao wala hilo suala la ajabu, wala siyo mara ya kwanza, wameshazoea kufanya hivyo. Sisi hatutakimbia vita hii tutaendelea kupambana nayo na kumuomba sana Mwenyezi Mungu atunusuru lakini wakati huu tuhakikishe kwamba Watanzania wanaweza kuishi na kufanikiwa kupitia bajeti hizi tunazozipitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengi yameshaelezwa vizuri kwenye hotuba ya bajeti ambayo Mheshimiwa Waziri amewasilisha vizuri sana labda nichangie maeneo machache. Kama ambavyo imezungumzwa kupitia bajeti yetu hii, ukweli ni kwamba Tanzania tumepiga hatua kubwa katika kujitosheleza kwenye bidhaa zetu mbalimbali zinazozalishwa hapa nchini. Kwa hali iliyopo sasa hivi kama tusingekuwa tumejipanga vizuri, kama tusingekuwa tumeijenga sekta binafsi kuwa na uthubutu, kama tusingekuwa tumewezesha hawa wajasiriamali wadogo wadogo katika kujifunza masuala ya uzalishaji wa bidhaa za aina mbalimbali leo *Corona* hii ilikuwa ni mfano wa kututia aibu, sasa hivi tungekuwa tumeshasambaratika lakini tumeweza kufanya mambo mengi. Vitakasa tumetengeneza wenyewe lakini barakoa hizi tumeendelea kutengeneza, hali ya upatikanaji wa bidhaa mbalimbali nchini umeendelea kuwa mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi Viwanda kama vya Saruji, unajua unapozungumzia umejenga kwenye nchi hii Vituo vya Afya zaidi ya 250, hospitali zaidi ya 67 ukiacha Hospitali za Rufaa na miundombinu mingi ikiwemo hiyo *Stiegler's Gorge* ikiwemo hiyo reli na mambo mengi hata uwekezaji binafsi. Hakuna simenti hata mfuko mmoja unaotoka nje ya nchi na bei ya simenti wala haijapanda ikaleta tofauti kubwa sana hii ni kuonesha kwamba viwanda vyetu vimeendelea kuimarika na tumeweza kujitosheleza sisi wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika kwenye nondo, halikadhalika kwenye mambo mbalimbali ya msingi, jamani Mwenyezi Mungu atupe nini? Gunia la chawa watuwashe au kitu gani?. Kwa hiyo, nasema kimsingi tumejitahidi kadri ilivyowezekana kama Watanzania na hapa napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza sana Sekta binafsi iliyoenda bega kwa bega na Serikali yao katika uzalishaji uliokuwa unatarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Sekta binafsi imeimarika kutokana na kuwa na nidhamu katika utendaji wake. Kwa siku za nyuma sekta binafsi imejikuta baadhi yao wanakwepa kodi, wengine hawana hesabu vizuri. Matokeo yake wengi walipata changamoto hasa tulipoanza uhibititi. Lakini sasa hivi karibu kila mmoja wetu anafanya shughuli zake kwa unadhifu na maadili yanayotakiwa kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ni jambo jema sana. Tumeendelea kujenga mazingira wezeshi ya kuondoa hizo kodi na vikwazo mbalimbali, lakini tumeendelea kuleta hali ya watu kutokusumbuka kuweza hata kufanya usajili wa biashara yake popote pale alipo kupitia *BRELA*. Lakini vilevile kukaa pamoja kumpongezana, kupeana moyo pale ambapo tumeona tunaenda labda pengine kuna changamoto na kuweza kuzitatua kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nasema kwamba hii ndio mikakati sasa tutakayoendelea nayo na kama ambavyo ilivyoorodheshwa hapo kwenye muelekeo, Wizara



yetu itaendelea kuhakikisha kwamba inazingatia na kupokea mawazo mema yanayotolewa na kila Mtanzania au mdau katika ujenzi wa uchumi wetu wa Viwanda. Ili kuhakikisha kwamba Tanzania inakuwa ni kati ya nchi zitakazoweza kujitegemea kiuchumi. Lakini vilevile kuhakikisha kwamba rasilimali za nchi zinatumiwa kwa manufaa ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo kwenye katiba yetu, siasa yetu ya ujamaa na kujitegemea. Maana yake ule ujamaa ni kwamba watu wachache kupitia sekta binafsi waweze kutumia rasilimali zetu kuzichakata lakini mwisho wa yote ile faida inayopatikana wao waitumie. Lakini pia kupitia kodi waweze kulipa kwenye Mfuko Mkuu wa Taifa na kuweza kutoa huduma kwa wananchi wote. Kwa hiyo, naamini kabisa kwamba nchi yetu ina muelekeo mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kuwashukuru sana Wananchi wa Jimbo la Nyasa kwa imani waliyoendelea kuwa nami wakati wote. Nawashukuru sana sana kwa upendo nawahakikishia dada yao Kagauni nipo pamoja nao wakati wote na nitahakikisha naendelea kufanya kazi kwa unadhifu na kwa heshima na kwa hekima kuhakikisha kwamba utu ndio silaha kubwa katika kulijenga Jimbo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe waendeleo kuiunga mkono Serikali yao ambayo ipo chini ya Chama Cha Mapinduzi. Chama bora kuliko Chama chochote Tanzania. Chama bora ambacho kina upendo, Chama bora ambacho kinajali maslahi mapana ya Wananchi wake. Mwenyezi Mungu azidi kuwabariki wananchi wa Nyasa. Mwenyezi Mungu awabariki sana Watanzania na niseme tu kwamba katika misingi hiyo ya Utaifa na upamoja sisi tutakuwa pamoja wakati wote kama Serikali lakini na wananchi watoe mkono wao kwa upande wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la *General Tyre*. *General Tyre* lilikuwemo katika Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi, hatujakimbia lakini Waheshimiwa Wabunge

mmekuwa mkishauri kwamba embu tuanze na miradi michache inayoweza kutekelezeka. Hiyo inayoonekana pengine haina uwezekano wa kutekelezwa kwa sasa hivi basi tunaendelea kuifanyia utaratibu wa kiutafiti wakati huo tunaanza kwanza na ile ambayo inaweza kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sema unaanza na matunda ambayo yananing'inia. Tumefanya hivi kuna miradi ambayo miaka nenda rudi ilikuwa haiwezi kutekelezeka, sasa hivi inatekelezwa. Tumeongeza nguvu za uzalishaji katika baadhi ya maeneo ambayo tuliona kwamba hayako vizuri. Lakini tumefanya ufuatiliaji wa viwanda hivi vilivyo binafsishwa. Kuna baadhi ya viwanda hata wakati tunavifuatilia walikuwa wanatushangaa, nyie mmetoka wapi? Mbona sisi toka tumbinafsishiwa kiwanda hiki hatujawahi kumuona mtu akija kutuuliza. Lakini sisi wakati wetu tumevijua viwanda vyote na kuhakikisha kwamba vinakaa katika utaratibu sahihi wa kuona ni namna gani *either* virejeshwe au viweze kufanyiwa taratibu zozote zinazofaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa nizidi kuwashukuru na ninasema asante sana Mwenyezi Mungu awabariki sana. Ahsante naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Waziri wa Viwanda na Biashara Mtoa hoja uhitimisha hoja yako.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kushukuru, nakushukuru sana kwa kutuendeshea kikao vizuri kama ilivyo ada yako nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote walichangia kwa kweli tunachoweza kuwaahidi mimi, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na Wizara nzima. Maoni na ushauri ambao mmetupatia tunawaahidi

tutazingatia na wote waliochangia tutahakikisha tunaleta majibu ya ufasaha kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawashukuru sana kwa pongezi, tunawashukuru sana kwa kuunga mkono jitihada za Wizara yetu. Jitihada za utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambapo bajeti hii inakamilisha utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika kujenga uchumi wa Viwanda kwa mujibu wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015/2020. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa maono yaani utadhani unaweza ukafikiri Malaika wakati wa kampeni walimpa maono haya Mheshimiwa Rais wetu kwa kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kujenga uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi hiki ambacho tunapambana na janga la *Corona* nimetafakari sana na kuona jinsi Mheshimiwa Rais wetu alivyokuwa na maoni na *Vision* ya kuona mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge hivi sasa wakati wa mapambano ya *Corona*. Kila nchi inaangalia *inward* kwamba sisi na Wananchi wetu. Je, hivi leo kama tungekuwa hatuna mkakati wa kujenga uchumi wa Viwanda ambapo hizi *PPE*, Barakoa, Vitakasa mikono vinatengenezwa na viwanda vyetu. Kwa kweli nchi yetu ingekuwa katika hali nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwasababu uelekeo wa utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na *Vision* ya Rais wetu janga hili la *Corona* limetukuka tupo katika safari nzuri ya kujenga uchumi wa viwanda. Kwa hiyo, tunavyozungumza ukiangalia hata Waheshimiwa Wabunge barakoa tunazovivaa unachagua kama unataka ile *surgical mask* zinatengenezwa hapa hapa nchini. Kama unataka barakoa ya nguo kama Mheshimiwa Naibu Waziri aliyovaa

amependeza na vazi la kijani zinatengenezwa hapa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunampongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa *vision* hiyo na sisi kama Wizara tunawaahidi tutaendelea kutekeleza maono haya na hatutamuangusha Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutusukuma sisi Wizara hii ambayo inasimamia mambo mtambuka ya ujenzi wa uchumi wa Viwanda na kwa maelekezo ambayo unaendelea kutupatia Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru sana boshi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wenzangu Wizara ya Viwanda na Biashara ni Wizara mtambuka. Sisi kazi yetu ni kuratibu mikakati ya Serikali ya Watanzania ya kujenga uchumi wa viwanda na katika hili hata zile pongezi na mafanikio ambayo mmetupongeza. Kwa kweli tusingeweza kufanikiwa kama sio ushirikiano wa Waheshimiwa Mawaziri wenzangu. Nawashukuruni sana pamoja na Waheshimiwa Manaibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa kunitakia siku ya kuzaliwa leo *(Birthday Wishes)* lakini nawaomba keki yangu na zawadi yangu naomba mnipitishie bajeti ya Wizara yangu ndio itakuwa keki ya kwangu. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa *Birthday wishes* na ili msiweze ku-*ruin* siku yangu pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri na Timu ya Wizara nzima basi mtusaidie mtupitishie bajeti yetu. Lakini nawashukuru sana kwa *birthday wishes*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na jambo la jumla, Waheshimiwa Wabunge katika michango yao ukiangalia changamoto za ufanyaji biashara na ujenzi wa uchumi wa viwanda, wamezizungumza lakini ukiangalia kwa ujumla

wake walikuwa wanatuambia kwamba tuwahishe *blue print* na sheria ije Bungeni ili iweze kupitishwa iweze kusaidia kurahisisha ufanyaji biashara na ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Waheshimiwa Wabunge niwape taarifa kwamba tumefikia hatua nzuri. Hatua zote zimeshafanyika za kuandaa sheria ya kuratibu na kuleta ufanisi katika ujenzi wa uchumi wa viwanda pamoja na kufanya biashara na hivi sasa iko katika hatua ya kufanyiwa maamuzi na Serikali kwenye Baraza la Mawaziri. Kwa hiyo, tumefikia hatua nzuri na najua sheria hii itarahisisha na kuleta ufanisi mkubwa katika kuwasaidia wafanyabiashara na kujenga uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mkakati wa Wizara yetu kama Waheshimiwa Wabunge mlivyoona kwenye hotuba. Sisi tumejikita katika kuhakikisha tunafungamanisha kilimo na viwanda na ukiangalia mkakati wa SVP2 tunapozungumzia kilimo. Hata *blue economy* ya uvuvi imo kwenye SVP2. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tutaendelea kusaidiana na Wizara hizi za uzalishaji, Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Hasunga nakushukuru kwa ushirikiano tunaopeana. Mheshimiwa Mpina nae ni *Birthday*yake leo nae alizaliwa Mei, 5 kwa hiyo, namtakia *Happy Birthday*, tutashirikiana hizi sekta zinazozalisha ziungane na sekta wezeshi za miundombinu na kazi nzuri tayari imeshafanywa na Serikali. Ili sasa tunapozalisha iwe ni mazao ya kilimo, yawe ni mazao ya mifugo, yawe ni mazao ya *blue economy* kutoka kwenye bahari ya Hindi na maziwa yetu. Basi tuwe na *platform* nzuri ya kufanya *agro processing* na ndio maana kwenye hotuba yetu tumesisitiza ile *model* ya *SIDO* ya kushirikiana na *NSSF* na *AZANIA Bank* kutengeneza *platform* kupitia *SIDO* inapojenga zile *shade* maeneo ya wafanyabiashara kwenda na kuzalisha basi hata kwenye masuala ya mikopo ya bei nafuu, kupeleka wataalam kuwafundisha jinsi ya kufanya ujasiriamali vizuri, kufanya *processing* vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwa na *platform* hizo katika Mkoa yetu yote nchini, tukafungamanisha hizi sekta tunazozalisha na mikakati tuliyoitaja ya muelekeo wa Wizara yetu. Tunahakika kabisa tutawasaidia Watanzania katika kuendelea kutoa mchango mkubwa wa kujenga uchumi wa viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na mkakati huo tunapitia sera za SMEZ kwa sababu tunatambua Watanzania wengi wakina mama na vijana tutaweza kuendelea kutengeneza ajira nyingi zaidi. Kama tutaweza kusaidia biashara na viwanda vidogo, biashara na viwanda vya kati kuweza kukua na kustawi ili tuweze kutengeneza ajira nyingi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kutambua hilo, Wizara yetu ipo katika hatua ya kukamilisha mapitio ya sera za *SME* lakini pia kusaidia Kampuni na Viwanda vikubwa ambayo tayari vinazalisha kwa ajili ya soko la Tanzania na nchi za jirani. Basi sera tutakayoboresha iweze kusaidia hata kampuni kubwa kuweza kuzalisha zaidi na kuweza kuchukua *market share* kubwa kwenye *SADC* na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ila pia tunaangalia wigo mpya. Nikitolea mfano tu wa bia na *whisk* ambazo tuna – *import*, ukiangalia kwenye upande wa bia tuna *choice* yaani mtu anaweza akaamua anywe bia inayozalishwa hapa hapa nchini au anywe bia ambayo ni *import*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kuongeza wigo wa biashara na viwanda. Lazima hata zile *nontraditional methods* za wajasiriamali wetu ifike mahali Bunge tushikamane na Serikali kufungua ukurasa mpya. Kwa mfano nilimuona Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Mtwara akizungumzia ile *whisk* ya kienyeji. Lakini kule Jimboni kwangu Karagwe Mheshimiwa DC ameomba na Wizara tumempelekea *SIDO*, *TIRDO* na Taasisi zote kwenda kukaa nao wale wajasiriamali kuangalia ni namna gani tunaweza

tuka-*standardize* hii *local whisk* iweze kuwa kama wenzetu Uganda walivyofanya na ile *Waragi (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ku-*formalized waragi* kule Uganda, Kampuni ya Bia ya kimataifa ilinunua *waragi* sasa hivi ni sehemu ya kinywaji ambacho ni rasmi. Kwa hiyo, Wizara yetu na muelekeo mpya ambao tumeutoa tunaangalia hata *informal sector* ni namna gani zinaweza tukazipa mazingira wezeshi ya kisera, ya kisheria. Ili waweze kuingia kwenye *formal sector* kuweza kuongeza wigo wa kikodi na wigo wa kimapato, wigo wa ajira ili tuweze kuwasaidia Watanzania wengi kupata ajira na kuchangia kwenye uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mahsusi ambayo Waheshimiwa wamechangia. Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa amegusia mambo ya fidia Bagamoyo, na nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Kawambwa kwa namna umekuwa ukifuatilia hili jambo. Ni kweli Mheshimiwa Rais alishatoa maelekezo na Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi kaka yangu Mheshimiwa Lukuvi hili jambo tumelifikia katika hatua nzuri. Tunaangalia ni namna gani yale maeneo ambayo tayari yameshafidiwa *demarcation* yake tunaporudisha maeneo ambayo hayajafidiwa kwa wananchi iweze kufanyika katika namna ambayo haitakuwa kero kwa wananchi wetu na haitakuwa kero kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza kwa namna unavyolifuatilia jambo hili kwa karibu sana na nakupongeza kwa namna unavyowapambania wananchi wa Bagamoyo, nakupongeza sana. Sina shaka watakurudisha kwenye Bunge hili ili tuweze kushirikiana kulifikisha hili mwisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wizara yetu tunapitia mikataba ambayo ilikuwa na maeneo hasi. Katika hili lipo suala la Liganga na Mchuchuma. Nimpongeze Mheshimiwa Sixtus Mapunda amelielezea vizuri, zile sheria za *natural resource* za mwaka 2017 zimetupa fursa ya kupitia mkataba huu vizuri ili utakapoteklezwa uweze kuwa na tija kwa nchi

yetu, uwe na tija katika Mkoa wa Ruvuma na uweze kuchangia kwenye mapato ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wanaotoka kwenye maeneo haya najua jambo hili mmekuwa mkilifuatilia kwa karibu na mmekuwa mkitusukuma. Tutajitahidi ili tuweze kwenda kwa kasi lakini tusifanye maamuzi ya haraka halafu baadaye tukajuta kama tulivyoona kwenye mikataba ya madini. Tulienda kwenye kasi kuukaribisha uwekezaji lakini baadae tukakuta tulipoteza kama nchi. Katika hili nampongeza Mheshimiwa Dotto Biteko amesimamia Wizara hiyo vizuri na sasa tunaenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kwenye Liganga na Mchuchuma tungependa hiyo *review* ya kimkataba ifanyike vizuri ili iweze kutoa tija kwa nchi yetu. Lakini sambamba na hili tunapitia mkataba wa TAMCO na wenyewe una maeneo hasi ambayo hayana faida kwa nchi yetu tunapitia mkataba wa Kiwanda cha Viua Wadudu Kibaha, na Serikali ya Cuba imekubali kwamba kuna maeneo ambayo baada ya mapitio tutaweza kunufaika zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili tunapitia mkataba wa Matrekta wa Ususi. Kampuni ya Ususi ilifilisika kule Poland, lakini sisi tulishapeleka *advance* ya fedha kwa ajili kuletwa matrekta. Baada ya kufilisika kwa hiyo, Kampuni tumeona ni fursa kwa nchi yetu ku-*negotiate* na Serikali ya Poland. Uzuri wamekubali kwa hiyo, matarajio yetu, matokeo ya *renegotiation* yatasaidia sana kwenye mkakati wetu wa kufungamanisha kilimo na viwanda. Ili isiwe matrekta peke yake lakini hata zile zana ndogo za kusaidia Wakulima wetu kuongeza tija mashambani itakuwa ni sehemu ya matokeo ya mkataba mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia viwanda vilivyobinafsishwa, hili jambo Waheshimiwa Wabunge mmelisubiri kwa muda mrefu lakini pia Serikali tunafanya uchambuzi ili viwanda hivi tutakavyopata wawekezaji.



Uwekezaji huo uwe na tija kwa Taifa letu. Tusiwe na *white elephant investment* ambazo hazileti tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Shemeji yangu Anjela Kairuki, tunavyoshirikiana katika kuyapitia maeneo ya viwanda hivi vilivyo binafsishwa kwa muongozo mzuri wa Mheshimiwa *Attorney General* na naamini hatua tuliyofikia kilichobaki si kikubwa sana miezi ya mbeleni huko Mwenyezi Mungu atusaidie wote turudi naamini tutakapoanza Bunge Iijalo, tutaleta habari njema sana kuhusu viwanda vilivyo binafsishwa na mapendekezo ambayo Serikali inayatoa juu ya muelekeo mpya ambao unaendana na mkakati wa kujenga uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, limezungumziwa suala la viwanda vya samaki, kama nilivyosema *blue economy* ni *potential* mpya ambayo sisi Serikali tunaiangalia kama ni fursa mpya ukiondoa kilimo pamoja na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutembelea viwanda hivi vya samaki nikubaliane na Mheshimiwa Stanslaus Mabula kwamba bado tuna fursa kubwa ya kufufua viwanda hivi kwa sababu ukiangalia Tanzania tuna asilimia 53 ya Ziwa Victoria. Mapato kwenye upande wa majirani zetu yamekuwa ni madogo lakini ukiangalia *by absolute value* ya *revenue* tutasema tunapata zaidi. Kiukweli kwa asilimia 53 ya Ziwa tuliyonayo tunaweza kupata hata zaidi ya mara 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwenye jambo hili nashirikiana na Mheshimiwa Waziri kuangalia tozo na mambo ya kisheria, tumeshafanya uchambuzi Mheshimiwa Waziri Mpango tutakuletea uchambuzi huo ili tuangalie jinsi ya ku-*realign* kodi zetu na tozo zetu tuweze kushindana na majirani zetu kuvutia uweke na usindikaji uweze kufanyika katika mikoa yetu inayozunguka hili Ziwa Victoria.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijui ni kengele ya mwisho au ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wizara ya Viwanda na Biashara zipo Taasisi ambazo kwa *design* yake zimejikita katika kutoa huduma kwa Watanzania wafanyabiashara na wenye viwanda. Taasisi ya *BRELA*, Taasisi ya *TBS*, Wakala wa vipimo tunaendelea kuziboresha ili ziweze kuwa na hiyo *Approach* ya *customer care* ziwe na *approach* ya kuondoa urasimu ili mikakati yote tunayoipanga ya kusaidia wafanyabiashara na wenye viwanda, wajasiliamali wetu nchini. Tutengeneze *platform* za wao kuzalisha kupitia *SIDO Modal* kuhakikisha wanapofanya biashara na nchi za jirani kupitia mipakani; kwa mfano, sasa hivi tuna orodha ya watumishi wote wa Taasisi za Serikali ambao wapo mipakani; ili mfanyabiashara anapoenda mpakani kwenda kufanya biashara na nchi jirani, anapokwazwa na mtumishi yeyote, anaweza kupiga simu, Wizara tukachukua hatua hapo hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaendelea kufanya *reform* ya hali ya juu kwa wafanyabiashara ambao wanafuatilia *reform* ambayo tunafanya ndani ya *BRELA*. Kwenye miaka inayokuja, tuseme kufika mwaka huu mwishoni ufanisi utakuwa umeongezeka kwa kiasi kikubwa. Tunafanya hivyo kwenye *TBS*, Wakala wa Vipimo na taasisi zile ambazo zinasaidia mkakati wa kujenga uchumi wa viwanda; *SIDO*, *TIRDO*, *TEMDO*, *CAMATEC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapitia Taasisi hizi na kuangalia kama kuunganishwa kwao kwa mfano *TEMDO* na *CAMATEC*, zikiunganishwa zikawa sehemu ya *TIRDO*, lengo la Wizara baada ya uchambuzi kukamilika ni kuangalia tunaongeza tija katika *research and involvement* ambayo itasaidia sekta za uzalishaji, wafanyabiashara wa kati na wadogo. Wenye viwanda wa kati na wadogo wanapokuwa katika zile *platforms* ambazo tutajenga mikoa yote kupitia *modal* ya *SIDO*, basi taasisi hizi zijikite katika kuwasaidia kupata teknolojia ambayo itawasaidia kuweza kusindika na kupata katika namna ambayo itakuwa ni ya viwango kwa

ajili ya soko letu la ndani ya nchi lakini na pia kwenda kwenye mauzo ya nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mtakapotupitishia bajeti hii ambayo imeelezea kwa kina vipaumbele hivi ambavyo nimevizungumzia, niwaahidi kwamba haya niliyoyasema mtayaona katika matokeo ya vitendo. Kwa hiyo, nakushukuru, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge kwa namna mlivyotupa ushauri na nimshukuru sana Mheshimiwa Suleiman Saddiq, Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kwa namna wanavyozidi kutupa ushirikiano na kutupa maoni na ushauri ili tuweze kufanya vizuri katika maeneo ambayo Bunge linaendelea kutushauri na kutusimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba Bunge lako lipitishie Makadirio ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono ahsanteni sana. Ninayo majina hapa ya Waheshimiwa Wabunge wanaohitaji ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri. Tutaanza na Mheshimiwa Pauline Gekul, atauliza kutoka Msekwa.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nipate kuuliza jambo moja la ufafanuzi. Kabla sijauliza jambo hilo, Mheshimiwa Waziri ni vizuri sasa Serikali ikatoa kauli juu ya wafanyabiashara wenye kumbi ambao wanakatazwa kuendelea na kazi baada ya Mheshimiwa Rais wetu kusema tuendeleee kuchapa kazi tukichukua tahadhari.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la ufafanuzi kwao, Mheshimiwa Waziri kwanza naipongeza Serikali yetu kutoa bei elekezi ya sukari, lakini sisi Babati tunanunua kilo moja kwa shilingi 2,900/= wakati sukari hii tunaichukua Dar es Salaam. Hapa Dodoma nafikiri ni kama shilingi 2,700/= . Mheshimiwa Waziri sisi tupo mbali na Dar es Salaam ukilinganisha na Dodoma. Naomba nifahamu kwa sababu wafanyabiashara wa sukari Babati wanakwama wauze kwa bei ipi kwa sababu wanaifuata Dar es Salaam na hatuna sukari inayojitoshesheleza katika Mkoa wetu wa Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nifahamu ni vigezo gani vimetumika? kwa sababu nafikiri *transportation cost* pia ni sehemu ya vigezo. Naiomba Serikali iangalie hili kwa upya kwa wafanyabiashara wa sukari ili mwone pia jinsi gani ambavyo wanaweza wakawa *considered* kwenye gharama za usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi kwenye hili la pili kwa sababu hilo la kwanza sitaki kukuweka katika mazingira ya kuanza kutoa matamko saa hizi wakati hujajitayarisha. Hilo la pili linahitaji ufafanuzi wa bei elekezi katika maeneo mbalimbali ambayo katika kupiga ile hesabu mnazingatia umbali wa eneo.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nianze kwa kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Gekul kwa *concern* yake ambayo ni ya Watanzania. Katika hili Waheshimiwa Wabunge Serikali tumeamua kutoa ukomo wa bei ya sukari baada ya kuona wafanyabiashara pamoja na mazingira mengine ambayo nitayaelezea muda mfupi, wamekuwa wakifanya ujanja wa kuhodhi sukari na wakati ipo kwenye magodauni yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwenye jitihada hiyo Serikali kupitia vyombo vya ulinzi na usalama, Wakuu wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya tunaendelea kulifanyia kazi ili wafanyabiashara hawa wachukuliwe hatua. Pia kwenya

upande wa changamoto hii ya bei kama mnavyojua janga la *Corona* ni la dunia, kwenye mambo ya *shipping* kumekuwa na changamoto pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilishatoa vibali ilishatoa vibali ili tani 40,000 ziweze kuingia nchini na tulitoa vibali hivyo baada ya kujua *gap sugar* huwa inatokea kuanzia mwezi wa Tatu mpaka mwezi Juni ambapo viwanda vyetu vya sukari vinaanza kuzalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya changamoto za *shipping*, wakati mwingine meli ambayo tumeshai-*book* ina-*cancel*. Kwa hiyo, Serikali inachokifanya ni kutafufa kila njia meli ambazo zina *cancel* tunatafuta namna yoyote ile ili sukari iweze kuja. Hata hivyo jitihada hizo wakati zinaendelea sukari ambayo ipo na wafanyabiashara baada ya kujua hizi changamoto za *Corona* wanahodhi ili waweze kupata faida maradufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hatulali, tunaendelea kuifanyia kazi. Mheshimiwa Gekul nakuhakikishia, hata kwenye Jimbo lako tutakaa tuangalie changamoto zilizopo na namna ya kuhakikisha kadri sukari inavyoingia inapakuliwa bandarini, hata wananchi wako wanapata huduma ya hii sukari bila shida yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zainab Mndolwa, ulisema unataka ufafanuzi.

**MHE. ZAINAB M. AMIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ni azma ya Mheshimiwa Rais wetu na Serikali kwa ujumla kuiona nchi yetu inakuwa ni nchi ya viwanda na Serikali ina wajibu ya kuweka mazingira rafiki kusaidia wenye viwanda kuzalisha kwa tija, pia kuweza kuleta ajira katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, wale wenye viwanda wanaomiliki

viwanda ambao wanatumia sukari ya viwandani, kuna ile *withholding tax* ya 15% inayochukuliwa na wengine wameshafanyiwa hesabu zao, lakini kunakuwa kuna kusuasua sasa kwa ulipaji. Nini kinachopelekea sasa kusuasua huko kwa ulipaji na wakati wengine wameshafanyiwa hesabu zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, naona umesimama.

**NAIBU WAZIRI VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba nitoe ufafanuzi kwa Mheshimiwa Mndolwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kumekuwa na malalamiko kwa upande wa wafanyabiashara wakidai kwamba hawajapewa hizo *VAT returns*, lakini pia kwa upande wa Serikali kama ambavyo tumekuwa tukijieleza siku za mwisho siku zote ni kwamba kilichopelekea kuleta hizi changamoto za ucheweleshaji wa kurejesha hizo *VAT returns* ilikuwa ni pamoja na baadhi ya hawa wafanyabiashara kutokuwa na hesabu ambazo ni sahihi na nyingine kupelekea kuwa na madai makubwa sana ikilinganishwa na hali halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yenyewe baada ya kuona hivyo kwa kweli pamoja na kutambua umuhimu wa viwanda vyetu kuendelea kukua na kuzalisha ilibidi lazima ijiridhishe na katika kujiridhisha ndipo ilipogundulika kwamba kuna watu ambao baadhi yao walikuwa na hesabu ambazo ni za kiuongo kabisa. Hata hivyo, Serikali inaendelea kufanyia kazi na ni nia ya Serikali kuhakikisha kwamba kwa yule ambaye ana madai halali anapata haki yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unikubalie kwa ufafanuzi huo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Venance Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, lakini swali langu kimsingi limeshajibiwa kwa sababu lilikuwa linahusu sukari.

**NAIBU SPIKA:** Haya, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri ameshahitimisha hoja lakini pia waliotaka ufafanuzi wameshaupata.

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020 – Wizara ya Viwanda na Biashara yaliidhinishwa na Bunge kama ifuatavyo:-**

#### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

Fungu 44 – Viwanda, Biashara na  
Uwekezaji.....Sh. 27,726,509,000/=

Fungu 60 – Biashara na Uwekezaji.....Sh. 23,952,507,000/=

#### **MIPANGO YA MAENDELEO**

Fungu 44 – Viwanda, Biashara na  
Uwekezaji.....Sh. 29,687,886,000/=

Fungu 60 – Biashara na Uwekezaji.....Sh. 0

**NAIBU SPIKA:** Nichukue fursa hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wanaofanya kazi chini yenu. Tunawapongeza kwa kazi nzuri, kwenye maeneo mbalimbali mmepongezwa na Kamati yetu ya Bunge, lakini pia Waheshimiwa Wabunge mbalimbali waliochangia hapa wameonesha namna ambavyo mmefanya kazi vizuri, mmesikiliza maoni yao. Kwa hiyo, tunawapongeza sana kwa huo usikivu na tunawatakia kila la heri kwenye utekelezaji wa yale ambayo mmeahidi kwamba mnaenda kuyafanya.

Pia Bunge sasa limeridhia hayo mliyokuwa mmeleta kama maombi, tunaamini kwamba mtaenda kuyatekeleza

na kwa sifa mlizopewa naamini hakuna shaka katika hilo, tunawatakia kila la kheri. *(Makofi)*

Vile vile nichukue fursa hii kuwashukuru sana Kamati yetu kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa niaba yetu sisi sote Waheshimiwa Wabunge kuchambua yaliyopita na haya ambayo yanakuja, tunawashukuru sana na tunawapongeza na ninyi kwa kazi nzuri na kwa kuipa Wizara ushirikiano ambao na wao wamekiri mmeshirikiana nao vizuri sana. Wale Waheshimiwa Wabunge waliopata fursa ya kuchangia hapa ndani, wengine kwa maandishi, pia tunawashukuru kwa sababu katika hayo mawazo yao yatawasaidia upande wa Wizara kuendelea kuboresha utendaji kazi wao.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 8.00 mchana.

*(Saa 11.54 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 6 Mei, 2020, Saa Nane Mchana)*